MWONGOZO WA MSHIRIKI

# KUSAIDIA BILA KUUMIZA BARANI AFRIKA

JONNY KABISWA KYAZZE NA ANTHONY SYTSMA
PAMOJA NA BRIAN FIKKERT

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

## Mwongozo wa Mshiriki

Jonny Kabiswa Kyazze *na* Anthony Sytsma *pamoja na* Brian Fikkert

Sio cha kuuzwa

The Chalmers Center

Sio cha kuuzwa

# Yaliyomo

Somo la 1: Utangulizi - - - - - - - - - 3

Somo la 2: Yesu Alikuja Duniani kwa Nini? - - - - 13

Somo la 3: Umaskini ni Nini? - - - - - - - 23

Somo la 4: Mahusiano Yaliyovunjika Barani Afrika - - 35

Somo la 5: Kupambana na Umaskini kupitia Upatanisho 50

Somo la 6: Usaidizi,Urekebishaji na Maendeleo - - 59

Somo la 7: Maendeleo ya Kijamii yenye Msingi wa Mali 72

Somo la 8: Tathmini ya Zoezi la Ufunguzi - - - - 82

Somo la 9: Kufanya Kazi kwa Utukufu wa Mungu - - 89

Somo la 10: Mabadiliko ya Mtazamo wa Ulimwengu - 104

Somo la 11: Mifumo Iliyovunjika - - - - - - 118

Somo la 12: Injili ya Mafanikio - - - - - - - 135

Somo la 13: Utamaduni wa Kiafrika na Pesa - - - 149

Somo la 14: Mabadiliko Katika Maisha ya Mtu
Husababishwa na Nini? - - - - - - - - 159

Somo la 15: Ushiriki wa Jamii - - - - - - - 168

Somo la 16: Huduma ya Ukarimu ya Kanisa- - - - 177

Somo la 17: Huduma ya Mijini: Fursa na Changamoto - 196

Sio cha kuuzwa

**Somo la 18: Safari za Misheni ndani ya Afrika - - - 210**

**Somo la 19: Wageni, Wamisionari na Wafadhili- - - 217**

**Somo la 20: Miradi ya Mbegu na Rasilimali Zaidi - - 230**

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



## Somo la 1: Utangulizi

# Utangulizi

Sikia maneno haya ya Mwanaharakati wa Mazingira wa Kenya Wangari Maathai:

> *Afrika imekuwa ikipiga magoti kwa muda mrefu sana, iwe wakati wa biashara ya utumwa inayodhalilisha utu, wakati ilipokuwa chini ya nira ya ukoloni, ikiomba msaada kutoka kwa jamii ya kimataifa, wakati inapolipa madeni ambayo sasa si halali, au wakati inapoombea miujiza. Waafrika wote wa tabaka za juu na chini, lazima wabadili mtazamo unaoathiri watu wengi waliotawaliwa na wakoloni kila mahali. Ni lazima wajiamini tena; kuwa wana uwezo wa kujitengenezea njia yao wenyewe na kutengeneza utambulisho wao wenyewe; kuwa wana haki ya kutawaliwa kwa haki, kwa uwajibikaji, na kwa uwazi; kuwa wanaweza kuheshimu na kutekeleza tamaduni zao na kuzifanya ziwe zinafaa kwa mahitaji ya sasa; na kuwa hawahitaji tena kuwa na madeni – ya kifedha, kiakili, na kiroho – kwa wale ambao wakati mmoja waliwatawala. Ni lazima wainuke na watembee…*
>
> *Haiwezi kusisitizwa zaidi: Lazima Waafrika waamue kusimamia maliasili zao kwa busara na kwa kuwajibika, wakubali kuzigawa maliasili hizo kwa usawa zaidi, na kuzitumia kwa manufaa ya Waafrika wenzao. Vinginevyo, wataendelea kuruhusu mataifa ya kigeni kushawishi au kulazimisha serikali zikubali mipango inayoruhusu rasilimali hizo kuhamishwa nje ya ya bara hili kwa malipo haba sana. Ni jukumu la Waafrika kuamua ikiwa watafanya kazi kwa bidii ili kujenga talanta na uwezo wao wenyewe, kuimarisha demokrasia na taasisi zao za utawala, na kukuza ubunifu na tasnia ya watu wao. Au, badala yake, ikiwa wataendelea kukuza utamaduni wa utegemezi.*[1]

Tunaamini kuwa kile ambacho Maathai alikuwa akihamasisha kwa shauku kinaweza kutimizwa tu na Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye anaokoa watu kutoka kwa dhambi zao, na sasa hivi anatekeleza utawala na Ufalme Wake mzuri katika ulimwengu huu. Ni katika Yesu pekee ndipo tunapoweza kuwa na tumaini la Waafrika kumjua Mungu kibinafsi na kupata upendo Wake na uzima wa milele. Ni kupitia kwa kazi ya Yesu pekee ndipo tunaweza kuwa na tumaini kuwa Waafrika watatambua kuwa wameumbwa kwa mfano wa Mungu, na wamepewa ujuzi, rasilimali, na ubunifu na Mungu ambao wanaweza kuutumia kujiendeleza wao wenyewe na jamii zao bila kujihisi duni na wanyonge. Ni kupitia kwa kazi ya Yesu pekee ndipo tunaweza kuwa na tumaini la mafanikio mengi katika hatua zetu za kupambana dhidi ya vita, ufisadi, uharibifu wa mazingira, na changamoto zingine nyingi ambazo zinakabili bara la Afrika sasa. Mafunzo haya yatasaidia makanisa na viongozi kukumbatia wito wao wa kuhubiri injili na kuishi kama raia wa ufalme wa Yesu katika ulimwengu huu uliovunjika.

Sio cha kuuza

# Ufunguzi wa Mafunzo

## Maombi ya Ufunguzi na Utambulisho wa Washiriki

## Maelekezo ya Warsha

Mwongozo huu wa Mshiriki unaweza kunakiliwa kwa ajili ya washiriki, lakini Mwongozo wa Kiongozi unaweza kununuliwa tu na hauwezi kunakiliwa. **Hupaswi** kujaribu kuongoza mafunzo haya bila Mwongozo wa Kiongozi. Mwongozo wa Kiongozi unaweza kununuliwa kupitia Amazon.com kama nakala iliyochapishwa au katika maduka maalum ya vitabu barani Afrika. Muone kiongozi wako kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kupata Mwongozo wa Kiongozi. Wakati wa mafunzo, fuata Mwongozo wako wa Mshiriki na uandike vidokezo katika mihadhara na mijadala ya kikundi.

- Kozi hii inatumia Biblia kama msingi wa juhudi zetu zote za kupambana na umaskini na kukuza maendeleo ya jamii zetu. Kwa hivyo kila mshiriki anahimizwa kuja na Biblia yake, daftari, na kalamu.

- Washiriki wote wanatarajiwa kufika kwenye warsha kwa wakati, wakiwa tayari kushiriki kikamilifu katika majadiliano wakati wote wa warsha. Washiriki wanatarajiwa pia kuweka sahihi zao kwenye karatasi za mahudhurio kila siku.

## Malengo ya Mafunzo

Lengo la mafunzo haya ni kubadilisha mitazamo ya viongozi wa Kikristo wa Afrika kama wewe, na kukuandaa kuwasaidia kwa busara watu maskini katika makanisa na jamii zenu. Hii si kazi rahisi. Kama vile Nelson Mandela, rais wa zamani wa Afrika Kusini, alivyosema, "Mojawapo ya mambo magumu zaidi si kubadili jamii bali ni kujibadilisha mwenyewe."[2]

# Matokeo Yanayotarajiwa Kutokana na Mafunzo

Kutokana na kupitia mafunzo ya kozi hii, tunatumai mtaweza:

- Kukua katika mahusiano yenu na Mungu, watu wengine, nafsi, na uumbaji wote.
- Kupata mtazamo mpya kuhusiana na ufalme wa Mungu katika huduma zenu.
- Kuamsha upendo na huruma zenu kwa wale walio maskini wa mali.
- Kupata ujuzi kuhusu jinsi ya kuwasaidia kwa busara watu na jamii zilizo maskini wa mali.
- Kutayarishwa kwenda na kufundisha kanuni hizi za maendeleo kwa makanisa na jamii zenu.
- Kuenda nyumbani baada ya mafunzo kukamilika, na kufanya shughuli za "Kufanya baada ya Somo" za kila somo.
- Kuanza kufanya kazi ya maendeleo yenu wenyewe na makanisa na jamii zenu, kwa kutumia rasilimali zenu wenyewe, hata kabla ya kupokea usaidizi kutoka kwa wamisionari, wafadhili wa kigeni, au Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Tunatumai kuwa baada ya kupokea mafunzo, baadhi yenu mtaenda kuongoza mafunzo zaidi ya *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika* ili kuwanufaisha viongozi na jamii zingine. Si kila mtu atakuwa na uwezo wa kutoa mafunzo haya, lakini kila mshiriki atapata fursa ya kwenda nyumbani na kufundisha kanuni na shughuli za utekelezaji kwa makanisa yao, timu na familia kupitia shughuli za kufanya baada ya somo.

Sio cha kuuzwa

# Muda wa Kozi

Utapewa cheti mwishoni mwa mafunzo ikiwa utakamilisha masomo yote katika mtaala huu. Mara tu utakapopokea cheti, utaruhusiwa kuwa kiongozi na kutoa mafunzo kwa kikundi kingine.

## Muhtasari wa Mtaala

**Somo la 1: Utangulizi** — Saa 1.75

**Somo la 2: Yesu Alikuja Duniani kwa Nini?** — Saa 2
Somo hili litatupa msingi wa kibiblia na wa kitheolojia wa jinsi ya kufikiria kuhusu wajibu wa Kanisa katika maendeleo na kupambana na umaskini.

**Somo la 3: Umaskini ni Nini?** — Saa 3
Somo hili litatupa ufahamu zaidi wa kujua umaskini ni nini hasa, na tutajifunza kuhusu aina mbalimbali za umaskini.

**Somo la 4: Mahusiano Yaliyovunjika Barani Afrika** — Saa 2
Katika somo hili, tutaangazia jinsi aina mbalimbali za umaskini zilivyo barani Afrika na jinsi zinavyozipa changamoto jamii zetu leo.

**Somo la 5: Kupambana na Umaskini kupitia Upatanisho** — Saa 1.75
Somo hili litaangazia maana ya mafanikio katika kupambana na umaskini, kile tunacholenga. Tutaanza kuona kile tunachopaswa kufanya ili kupambana na umaskini.

**Somo la 6: Usaidizi,Urekebishaji na Maendeleo** — Saa 2.5
Somo hili litaangazia aina mbalimbali za suluhu tunazopaswa kutoa kwa aina mbalimbali za mahitaji. Hasa, tutajifunza wakati wa kutoa pesa na wakati wa kutotoa.

**Somo la 7: Maendeleo ya Kijamii yenye Msingi wa Mali** — Saa 1.75
Katika somo hili, tutajifunza jinsi ya kuwatia moyo watu kuona rasilimali na uwezo ambao Mungu amewapa.

**Somo la 8: Tathmini ya Zoezi la Ufunguzi** — Saa 1
Somo hili litaangazia zoezi ambalo tunakaribia kufanya hapa katika utangulizi.

**Maoni, Shuhuda, Tathmini na Maombi** — Dakika 30

**Somo la 9: Kufanya Kazi kwa Utukufu wa Mungu** — Saa 2
Somo hili litaangazia umuhimu wa kazi na biashara katika kushinda umaskini.

**Somo la 10: Mabadiliko ya Mtazamo wa Ulimwengu** — Saa 2
Somo hili litachunguza umuhimu wa imani na mitazamo yetu katika kushinda umaskini.

**Somo la 11: Mifumo Iliyovunjika** — Saa 2.5
Katika somo hili, tutajadili jinsi ya kubadilisha mifumo iliyovunjika ambayo inawaweka watu kwenye mtego wa umaskini.

**Somo la 12: Injili ya Mafanikio** — Saa 2
Somo hili litaeleza kwa nini injili ya mafanikio ni uongo na litaelezea jinsi inavyowadhuru watu walio maskini wa mali.

Sio cha kuuzwa

**Somo la 13: Utamaduni wa Kiafrika na Pesa** **Saa 2.5**
Katika somo hili, tutalinganisha jinsi tamaduni zetu zinavyoona na kutumia pesa na kanuni ambazo tumejifunza katika mtaala huu.

**Somo la 14: Mabadiliko Katika Maisha ya Mtu Husababishwa na Nini?** **Saa 1.5**
Somo hili litachunguza kile kinachofanya mtu kufanya mabadiliko katika maisha yake. Tutajifunza pia vifungu vya Biblia na kubaini ikiwa ni sawa kumnyima pesa mtu anayeomba.

**Somo la 15: Ushiriki wa Jamii** **Saa 1.5**
Somo hili litaelezea umuhimu wa ushiriki wa jamii katika mchakato wa maendeleo.

**Somo la 16: Huduma ya Ukarimu ya Kanisa** **Saa 2**
Katika somo hili, tutajifunza jinsi ya kuanzisha huduma ya ukarimu katika makanisa yetu, na sera tunazopaswa kuweka ili kuwasaidia watu maskini katika kanisa na jamii yetu.

**Somo la 17: Huduma ya Mijini: Fursa na Changamoto** **Saa 2.5**
Katika somo hili, tutaangazia ukuaji wa miji barani Afrika sasa na fursa na changamoto ambazo ukuaji huu unaleta kwa huduma zetu za kanisa.

**Somo la 18: Safari za Misheni ndani ya Afrika** **Saa 1.5**
Somo hili litachunguza jinsi ya kusaidia bila kuumiza wakati makanisa yetu yanapotuma timu kwa jamii zingine ili kuhubiri injili na/au kutoa suluhu kwa mahitaji ya watu maskini.

**Somo la 19: Wageni, Wamisionari na Wafadhili** **Saa 2**
Katika somo hili, tutajadili utata na kutoelewana kunakotokana na mahusiano yetu na wageni barani Afrika, hasa wageni ambao ni wafadhili wa serikali zetu, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali au makanisa.

**Somo la 20: Miradi ya Mbegu na Rasilimali Zaidi** **Saa 1**
Somo hili la mwisho litatuhimiza kuchukua hatua kwa vitendo ili kutumia mafunzo tuliyojifunza kutoka kwenye mtaala huu katika jamii zetu. Hatua na mipango inayofuata itapendekezwa.

**Maoni, Shuhuda, Tathmini na Maombi** **Dakika 30**

**Jumla = Saa 38.5**

Sio cha kuuzwa

# Takwimu kuhusu Umaskini Barani Afrika

Mungu amekuwa akifanya kazi kupitia kwa watu Wake na mabadiliko yamekuwa yakitokea. Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka wa 2016[3], ilibainika kuwa kulikuwa na kupungua kwa idadi ya watu walio na umaskini uliokithiri barani Afrika, kutoka asilimia 57 mnamo mwaka wa 1990 hadi asilimia 43 mnamo mwaka wa 2012. Hayo ni maendeleo ya ajabu!
Hasa, tunaweza kuona:

- Pato la Kitaifa barani Afrika linaongezeka kwa takriban asilimia 4 kwa mwaka, kiwango kilicho juu ya wastani wa dunia wa takriban asilimia 3 kwa mwaka.[4]

- Umri wa kuishi umeongezeka barani Afrika. Katika mwaka wa 2013 ikilinganishwa na mwaka wa 2000, umri wa kuishi uliongezeka kwa wastani wa miaka 6.2 kwa kila mtu.[5]

- Kati ya mwaka wa 1995 na 2012, viwango vya watu wazima wanaojua kusoma na kuandika barani Afrika viliongezeka kwa asilimia 4.[6]

- Sote tunaweza kuona jinsi Waafrika wanavyotumia teknolojia mpya za Mtandao na simu za rununu kwa elimu, mawasiliano na maendeleo.

- Hata hivyo, licha ya mabadiliko hayo yote mazuri, umaskini ungali unakithiri barani Afrika. Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara linasalia kuwa eneo maskini zaidi duniani.[7] Haikubaliki kuwa asilimia 43 ya watu wote wanaishi katika umaskini uliokithiri, ambao unapimwa kwa msingi wa kuishi kwa chini ya dola 1.90 kwa kila mtu kwa siku.[8]

- Inasikitisha pia kuwa umaskini huu ungali upo licha ya zaidi ya dola trilioni 1 za msaada wa maendeleo kuhamishiwa hadi Bara la Afrika kutoka nchi tajiri katika kipindi cha miaka hamsini iliyopita.[9] Ingawa usaidizi huu umesaidia sana katika hali fulani, haujatolewa kwa busara wala kutumika kwa busara kila mara.

- Ni asilimia 25 tu ya Waafrika ndio wanaoweza kufikia chanzo bora cha maji.[10]

- Kuna ukosefu mkubwa wa usawa barani Afrika. Watu 10 matajiri zaidi barani Afrika wana utajiri unaolingana na utajiri wa nusu ya idadi ya watu maskini zaidi.[11]

- VVU bado ni tatizo sugu barani Afrika. Mnamo mwaka wa 2012, watu milioni 1.1 katika eneo hili walikufa kutokana na UKIMWI – takriban mara nne ya idadi ya ulimwengu wote kwa pamoja (takriban 300,000).[12]

- Malaria ni tatizo lingine sugu. Mradi wa Milenia wa Umoja wa Mataifa umekokotoa kuwa barani Afrika mtoto hufa kutokana na malaria kila baada ya sekunde 30, au takriban vifo 3,000 kila siku.[13]

- Tangu mwaka wa 2010, ghasia zimekuwa zikiongezeka barani Afrika, kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe, ugaidi na machafuko ya kisiasa. Kuna matukio ya vurugu mara nne zaidi kwa sasa kuliko miaka ya 1990.[14]

- Kwa bahati mbaya, vurugu na vita vyote hivi havijapunguzwa sana na misaada kutoka nchi zingine. Takriban asilimia 40 ya matumizi ya kijeshi barani Afrika yanafadhiliwa na misaada inayotumiwa vibaya.[15]

- Mataifa mengi ya Afrika yanateseka pia kwa sababu ya mizigo mikubwa ya madeni ambayo yanadaiwa na mataifa tajiri. Kwa sababu ya riba ya madeni, na kwa sababu ya watawala fisadi katika hali fulani, linakuwa jambo gumu kwa mataifa mengi ya Kiafrika kulipa mikopo hii.

- Katika miaka 50 iliyopita, kumekuwa na mabadiliko halisi barani Afrika. Kutokana na hatua fulani zilizochukuliwa, kumekuwa na kupungua kwa umaskini. Lakini bado kuna changamoto nyingi. Kungali na kazi nyingi zaidi ya kufanya, na tunahitaji kuifanya kazi hiyo kwa njia bora na zenye ufanisi zaidi kuliko tulivyofanya hapo awali.

Sio cha kuuza

### Maswali ya Majadiliano ya Washirika

1) *Je, ni mambo gani mazuri yanayofanyika katika jamii yako? Je, watu wanapiga hatua za maendeleo au kuushinda umaskini vipi?*

---

*2) Je, ni changamoto gani za umaskini zimesalia katika jamii yako?*

---

*3) Je, unadhani wewe na kanisa lako mnafanya vya kutosha kuwasaidia watu maskini kanisani na katika jamii?*

---

# Zoezi la Ufunguzi – Vikundi Vidogo (Dakika 30-45)

**Maagizo**: Katika vikundi vyenu vidogo, mjadili hali iliyochaguliwa na kiongozi na mjibu maswali yanayofuata. Fikiria kuwa washiriki wote wa kikundi chako wanatoka kanisa moja. Andikeni mpango wa huduma wa kanisa lenu kama mnavyoongozwa na maswali. Andikeni majibu yenu kwenye karatasi kubwa na muandike majina yenu juu ya karatasi. Mzihifadhi mahali salama, au mpe kiongozi wenu. Inaweza kuwa vyema kurekodi majibu na vidokezo vyako binafsi katika mwongozo wako ili uwe pia na nakala ya majibu ya kikundi chako.

## Hali

**Hali ya 1** – Lazima mpange jinsi ya kuwasaidia **ombaomba** katika jiji lenu. Hivi majuzi, mmoja wa wachungaji katika jiji lenu alihubiri kuhusu kutoa kwa maskini, na watu wengi katika kanisa waliguswa na walitaka kufanya zaidi kuwasaidia maskini. Hasa, washirika wa kanisa lako wamepata mzigo wa kuwasaidia ombaomba ambao huwa sokoni kila wakati. Hapo awali, washirika wa kanisa wamewapuuza zaidi ombaomba na kuwaepuka, lakini wakati mwingine washirika wachache wa kanisa huwapa sarafu chache. Ombaomba huomba chakula wakiwa wamekaa chini. Wengine wana ulemavu wa kimwili ilhali wengine wanaonekana kuwa na afya. Wengi wao ni wazee. Kanisa lenu lingependa sana kutoa kwa ukarimu na kuwasaidia.

**Hali ya 2** – Lazima mpange jinsi ya kuwasaidia **wajane** katika jamii ya kijiji chenu. Hivi majuzi, mshirika wa kanisa alitoa maoni yake kuwa kanisa lenu linapaswa kufanya zaidi kuwasaidia wajane kanisani. Washirika wengine wa kanisa walikubali, na kuongeza kuwa kanisa linapaswa pia kuwasaidia wajane wasiokuwa washirika wa kanisa katika jamii pana zaidi. Wengi wa wajane katika jamii wanataabika, ingawa matarajio ya kitamaduni ni kwamba watoto wao na jamaa zao wanapaswa kuwatunza. Baadhi ya wajane ambao ni wazee sana wanataabika, na baadhi ya wajane wenye watoto wadogo walipoteza waume zao wakiwa na umri mdogo.

Sio cha kuuzwa

**Hali ya 3 –** Lazima mpange jinsi ya kuwasaidia **watoto wanaorandaranda mitaani** katika jiji lenu. Watoto wanaorandaranda mitaani wamekuwa wakitumia muda wao mwingi karibu na kanisa lenu. Siku ya Jumapili, watu wanapokuja kanisani, wanaomba pesa na chakula kutoka kwa washirika wa kanisa wanaotembea kwa miguu au kuendesha magari kwenda kanisani. Jambo hili huwaudhi sana washirika wa kanisa. Wakati mwingine, watoto wanaorandaranda mitaani hata wamechorachora michoro na kuandika maneno kwenye kuta za jengo la kanisa. Washirika wote wa kanisa wamekubaliana kuwa watoto wanaorandaranda mitaani wamekuwa tatizo, kwa hivyo lazima hatua ichukuliwe. Viongozi wa kanisa wamependekeza kuwa kanisa lijaribu kuwapenda na kuwajali badala ya kuwataka polisi kuingilia kati. Washirika wa kanisa walikubali kujaribu kufanya hivyo.

**1)** *Je,* ***mtapanga na kujiandaa*** *vipi, kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu hatua ya kuchukua?*

**2)** *Je, mtatoa* ***pesa au rasilimali*** *gani?*

**3)** *Kando na kutoa rasilimali,* ***mtafanya mambo gani mengine*** *kama sehemu ya huduma hii?*

**4)** *Je,* ***watu*** *gani kutoka kanisa lenu watashiriki katika huduma hii?*

**5)** *Je,* ***mtatekelezaje*** *mipango yenu ya huduma?*

Sio cha kuuzwa

# Kichwa – *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika*

***Simulizi ya Jonny***

---

**Majadiliano** – Shiriki wakati ambao wewe au kanisa lako lilijaribu kusaidia mtu au jamii ya watu maskini, lakini baadaye mkagundua kuwa mlifanya hali yao kuwa mbaya zaidi.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

*Msiruhusu wasiwasi wa kufanya makosa uwazuie kuwasaidia maskini. Tunahitaji kufanya hata zaidi ili kusaidia na kutoa kwa ukarimu zaidi, lakini tunahitaji kufanya hivyo kwa busara.

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na picha iliyopigwa na Tabitha Kapic.

[1] Wangari Maathai, *The Challenge for Africa* (New York: Pantheon Books, 2009). Kindle, ed., Loc. 248-53.

[2] John Battersby, "Mandela", *Science Monitor*, (Februari 10, 2000), 92, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://www.csmonitor.com/2000/0210/p15s1.html.

[3] Kathleen Beegle, Luc Christaensen, Andrew Dabalen, and Isis Gaddis, *Poverty in a Rising Africa* (Washington D.C., World Bank, 2016), xi, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://www.worldbank.org/en/region/afr/publication/poverty-rising-africa-poverty-report.

[4] "Recent Economic and Social Developments in Africa", *Economic Report on Africa 2016* (New York, United Nations, 2016), 3, accessed online: https://www.uneca.org/economic-report-africa-2016

[5] Beegle, et al, *Poverty in a Rising Africa*, 88.

[6] Ibid., 11.

[7] Dambisa Moyo, *Dead Aid: Why Aid is Not Working and How There Is a Better Way for Africa* (New York, Farrar, Straus, na Giroux, 2009), Kindle ed., Loc. 240-241.

[8] Amy Frykholm, "Ending Extreme Poverty", *Christian Century* (Juni 8, 2016), 133, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.christiancentury.org/article/2016-05/ending-extremepoverty?CID=POV_TT_worldbank_EN_EXT.

[9] Moyo, *Dead Aid*, Kindle ed., Loc. 248-50.

[10] *Economic Report on Africa 2016*, 26.

Sio cha kuuzwa

[11] Beegle, et al., *Poverty in a Rising Africa*, 136.

[12] Ibid., 92.

[13] https://borgenproject.org/10-quick-facts-about-poverty-in-africa/.

[14] Beegle, et al, *Poverty in a Rising Africa*, 12.

[15] Paul Collier, *The Bottom Billion: Why the Poorest Countries Are Failing and What Can Be Done about It* (Oxford University Press, 2007), Kindle ed., Loc. 1700-1701.

Sio cha kuuzwa

Kusaidia Bila

Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki

Sio cha Kuuzwa



# Somo la 2: Yesu Alikuja Duniani kwa Nini?

# Swali la Majadiliano la Ufunguzi

*Je, washirika wa kanisa lako nyumbani wangejibu vipi ikiwa ungewauliza swali hili:*
*Je, Yesu alikuja duniani kwa nini?*

________________________________________________

## Huduma ya Yesu

Majibu yetu tofauti kwa swali hilo yanaweza kuwa na uhusiano na jinsi kila mmoja wetu anavyoitikia maskini kwa namna tofauti.

________________________________________________

________________________________________________

**Luka 4:16-21; Luka 7:18-23; Luka 4:43**
Yesu alikuja duniani kuhubiri habari njema ya ufalme wa Mungu, na alionyesha pia habari njema ya ufalme wa Mungu kupitia kwa matendo yake.

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

Yesu, akiwa Mfalme wa wafalme, anatumia uwezo wake kurekebisha kila kitu katika ulimwengu huu ambacho dhambi yetu imeharibu. Hakuja kuokoa roho zetu tu, bali pia kuponya magonjwa yetu, kuleta amani, kuanzisha ufalme wake, na kutufanya wapya.

Ikiwa tunafikiria kuwa Yesu alikuja tu kutuokoa ili twende Mbinguni, tutajaribu tu kuokoa nafsi. Lakini ikiwa tuna mtazamo wa ufalme, tutaishi kama raia wa ufalme, watu wanaohubiri injili na kuonyesha upendo na kujali wengine katika maisha yao ya kila siku. Tutatimiza mwito wa Kanisa wa kuhubiri habari njema, lakini tunapoendelea kufanya hivyo, kama raia wa ufalme tutawaombea wagonjwa wapone, tutawasaidia maskini, tutawashauri waliovunjika moyo, tutawapa haki walioonewa, na kuwapa matumaini wasio na matumaini.

________________________________________________

## Wokovu na Kuhesabiwa Haki kwa Imani Pekee

Sio cha kuuzwa

Tunahitaji kuelewa jinsi mtu anavyoweza kuwa sehemu ya Ufalme wa Mungu. Mara tunapopokea wokovu, tunakuwa raia wa ufalme wa Mungu, tukifurahia baraka za ufalme na kutenda mema kama raia wa ufalme. Lakini maisha na kifo cha Yesu hutuokoaje?

## Swali la Majadiliano:

*Je, Yesu anatuokoaje? Je, tunawezaje kujiunga na ufalme wake?*

**Warumi 3:10-12, 23**

**Waefeso 2:8-9; Warumi 3:21-24**

Tunapounganishwa na Kristo, tunahesabiwa haki machoni pa Mungu. Anatuona kama watu ambao ni waadilifu kikamilifu, kwa kuwa tumepewa haki kamilifu ya Yesu kama karama.
**Warumi 5:17-19**

Hatuwezi kamwe kuwa "wazuri vya kutosha" kiasi cha kujiokoa. Tunaokolewa kwa haki na matendo mema ya Yesu, si yetu wenyewe. Mungu anaona haki kamilifu ya Kristo ndani yetu. Kwa hiyo hatupaswi kuishi kwa hofu ya Siku ya Hukumu. Tunaokolewa kwa imani katika Kristo. Mafundisho haya yanaitwa **kuhesabiwa haki kwa imani**.

Lakini bado tunahitaji kufanya matendo mazuri. Hatutakuwa wakamilifu, lakini wale walio na imani ya kweli katika Kristo watajitahidi kuishi kwa ajili ya Mungu, kuungama na kutubu dhambi, na kuzaa matunda mema.
**Warumi 6:1-2, 15; Waefeso 2:10; Mathayo 7:17; Yakobo 2:17-18; 1 Yohana 1:8-10.**

Sio cha kuuzwa

## Maswali ya Majadiliano:

*Je, watu wengi katika nchini mwenu wanakuwa Wakristo ili kuhesabiwa haki kwa imani katika Kristo na kuingia katika ufalme Wake, au wanakuwa Wakristo kwa sababu wanataka Mungu awape chakula, fedha, au uponyaji wa kimwili?*

*Eleza jibu lako.*

Tunapewa uwezo wa kuwa wana wa Mungu na kufurahia baraka za kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu kwa kuhesabiwa haki kwa imani katika Kristo tu. Habari njema ya ufalme ni nzuri tu kwa wale wanaohesabiwa haki kwa imani katika Kristo. Kwa wengine ambao hawamtumaini Kristo kwa wokovu, lakini wanataka tu vitu kutoka kwa Mungu, ufalme wa Mungu huleta hukumu na adhabu.

Iwapo tungependa kufurahia kuwa na Mungu kama Baba yetu mwenye upendo na anayetujali kama watoto wake kwa kutupa vitu vizuri, ni lazima kwanza tupatanishwe na Mungu na kusamehewa dhambi zetu, kupitia kuhesabiwa haki kwa imani katika Kristo.

Sio cha kuuzwa

# Ufalme wa Mungu na Wajibu wa Kanisa

## Swali la Majadiliano:

*Tumekuwa tukizungumza kuhusu ufalme wa Mungu, lakini, je, ufalme wa Mungu ni nini? Je, uko hapa sasa hivi, au bado tunausubiri?*
*Eleza.*

**Wakolosai 1:15-20.** Tunajifunza kutoka kwa kifungu hiki kuwa Yesu ndiye Muumba, Mdumishaji, na Mpatanishi wa **KILA KITU.** Yesu alikufa ili kutuokoa, lakini alikufa pia ili kupatanisha vitu vyote alivyoviumba. Hii ina maana kuwa anataka kuweka **KILA KITU** katika uhusiano sahihi na Yeye na kila mmoja. Yesu anayafanya mambo yote kuwa mapya!

Tunapaswa kuelewa kuwa Ufalme **tayari uko hapa, lakini bado haujafika kikamilifu.** Ufalme wa Mungu ambao Yesu aliuhubiri upo hapa ***tayari.*** Ulikuja kwa mara ya kwanza wakati Yesu alipokuja na kufa na kufufuka tena. Tunapata baraka za ufalme wa Yesu ***tayari*. Ufunuo 21:1-4.**

**Kwa kuwa ufalme wa Mungu uko hapa tayari na Roho Mtakatifu anafanya kazi**, tunaweza kuwa na matumaini kuwa Mungu atatutumia kuleta mabadiliko na kuwatoa watu kutoka kwenye umaskini na kuendeleza jamii zetu. Yesu alikuja kuhubiri habari njema kwa maskini. Lakini **kwa kuwa ufalme wa Mungu bado haujafika hapa kikamilifu**, tunaweza kuwa na uhalisia na kujua kuwa tutakuwa na watu maskini siku zote na umaskini kiasi fulani sisi wenyewe hadi Yesu atakaporudi.
**Mathayo 6:9-10**

Nukuu kutoka kwa Desmond Tutu, Askofu Mkuu wa zamani nchini Afrika Kusini:

> *Mpendwa Mtoto wa Mungu, ninaandika maneno haya kwa sababu sisi sote hupitia huzuni, sote hupitia nyakati fulani za kuhisi kukata tamaa, na sote hupoteza matumaini ya kwamba mateso maishani mwetu na katika ulimwengu yataisha. Ningependa kushiriki nanyi imani yangu na ufahamu wangu kwamba mateso haya yanaweza kubadilishwa na kukombolewa. Hakuna kitu kama hali ya kukosa matumaini kabisa. Mungu wetu ni mtaalamu wa kushughulikia machafuko, kuvunjika moyo, na mabaya yote ambayo tunaweza kufikiria. Mungu aliumba utaratibu kutokana na hali ya ukosefu wa utaratibu, aliumba ulimwengu kutokana na machafuko, na Mungu anaweza kufanya hivyo daima, anaweza kufanya hivyo hata sasa – katika maisha yetu binafsi na katika maisha yetu kama mataifa, duniani kote… Kwa hakika, Mungu anabadilisha ulimwengu sasa – kupitia kwetu sisi – kwa sababu Mungu anatupenda.*[1]

Mfalme Yesu anatawala vitu vyote – watu, viumbe, mifumo ya kitamaduni, na nguvu za kiroho.

Tunapaswa kufanya mahubiri yetu, kazi zetu za kila siku, kazi zetu za familia, na vitu vingine vyote maishani mwetu kama raia wa ufalme wa Mungu, na tufanye mambo haya kwa utukufu wa Mungu.

## Swali la Majadiliano:

***Je, Wakristo Waafrika wanafundishwa vyema kuhusu ufalme wa Mungu na wajibu wa Kanisa katika ufalme wa Yesu? Eleza.***

Sio cha kuuzwa

Yesu alihubiri habari njema ya ufalme na alionyesha habari njema hiyo kupitia kwa matendo Yake. Kanisa linahitaji kufuata mfano wa Yesu. Kanisa barani Afrika linapaswa pia kujiuliza: "*Je, tunaweza kufanya nini ili kuwasaidia watu kuondoka katika mateso wanayopitia hivi sasa*?"

---

Makosa Mawili ya Kuepuka:

1. ______________________________

2. ______________________________

Tunapaswa kulenga kuwa zaidi kama Kanisa la Hapo Mwanzoni. **Matendo 4:32-35.**

---

## Swali la Majadiliano:

***Eleza ikiwa Wakristo Waafrika leo hii wanaabudu pamoja na kushughulikia mahitaji ya kimwili ya kila mmoja wao kama vile Wakristo wa hapo mwanzoni walivyokuwa wakifanya?***

______________________________

______________________________

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zitajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii yenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Kulingana na kile kinachoendana na hali na nafasi yako, chagua mojawapo ya shughuli hizi mbili za kufanya kama itikio lako kwa yale uliyojifunza katika somo hili.

1. Hubiri katika kanisa lako kuhusu mojawapo ya vifungu vya Biblia kutoka katika somo hili kuhusu kuhesabiwa haki kwa imani au ufalme wa Mungu. Au, hubiri kuhusu mojawapo ya vifungu vya Biblia kutokana na maswali ya majadiliano ya kikundi kidogo.
2. Fanya mazungumzo na familia yako, wafanyakazi wenzako, au kikundi cha jamii kuhusu yale uliyojifunza katika somo hili kuhusu ufalme wa Mungu. Ikiwa wanataka na wako tayari, jaribu kupanga funzo la Biblia pamoja nao ili muweze kusoma baadhi ya vifungu muhimu vya Biblia vilivyotajwa katika somo hili na kuvijadili pamoja.

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

**Soma vifungu vifuatavyo vya Maandiko (vinaendelea kwenye ukurasa unaofuata). Jadilini pamoja kile ambacho Mungu anatufundisha katika vifungu hivi kuhusu jinsi ya kuwapenda na kuwajali maskini.** Muda usipotosha kujadili vifungu vyote, soma vifungu vilivyosalia nyumbani peke yako.

**Je, vifungu hivi vinafundisha kanuni gani za jumla? Je, ingekuwaje kama tungejaribu kutumia kanuni hizi leo katika wakati na utamaduni wetu?**
Amosi 2:6-7 na Amosi 5:21-24

---

Mambo ya Walawi 19:9-10

---

Kumbukumbu la Torati 14:28-29

---

Mithali 19:17

---

Mithali 21:13

---

Isaya 58:1-10

---

Luka 12:32-34

---

Yakobo 1:27

---

1 Yohana 3:16-18

---

**2. Je, wewe na kanisa lako mnaweza kubadilisha nini ili kumzingatia zaidi Yesu na ufalme Wake?**
Baada ya kujadiliana kuhusu jinsi mtakavyobadilika, ombeni pamoja kama kikundi mkimwomba Mungu awasaidie kubadilika.

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Kuhesabiwa Haki kwa Imani

Mwanatheolojia wa Kiafrika Matthew Michael anadai kuwa mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani pekee, ndiyo mafundisho yasiyohubiriwa sana katika makanisa ya Kiafrika.[2] **Je, unadhani ni kwa nini baadhi ya wachungaji wa Kiafrika hawahubiri kuhusu mafundisho haya?** Jadili hili na rafiki yako.

Wakati mwingine wachungaji wanaogopa kuwa ikiwa Wakristo wataamini mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani, watatoa visingizio vya dhambi zao. Lakini ikiwa watu kweli wataelewa mafundisho haya ya kuhesabiwa haki kwa imani, hawataweza kutoa kisingizio cha namna hii kwa ajili ya dhambi zao. Mtu ambaye ameokoka kikweli anatamani kumpendeza Mungu na kumtii. Mti mzuri huzaa matunda mazuri. Matendo mema ni ushahidi wa imani ya kweli. Mtu aliye na imani ya kweli katika Kristo hatatumia kuhesabiwa haki kwa imani kama kisingizio cha kufanya dhambi. Mkristo wa kweli hatakuwa mkamilifu, lakini hatatembea katika dhambi. Ataendelea kutubu, kuungama, na kujaribu kuishi kwa ajili ya Kristo.

Fikiria kuhusu maswali haya na uyajadili na wengine ikiwa unaweza:

**1. Je, wewe au mchungaji wako mnaweza kusema nini wakati wa mahubiri ili kuhakikisha kuwa watu hawaelewi vibaya mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani?**
**2. Je, unawezaje kumshauri mtu katika kanisa lako ambaye amekuwa akitumia mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani na msamaha wa Mungu wa dhambi kama kisingizio cha kutomtii Mungu? Je, ungeshiriki na mtu huyo vifungu gani vya maandiko ?**

---

## Ufalme wa Mungu

Ifuatayo ni mifano mingine inayoonyesha jinsi ambavyo tayari tumepata kuwa katika ufalme wa Mungu sasa, lakini bado hatujapata ukamilifu wa ufalme wa Mungu hadi Yesu atakaporudi. Tafakari juu ya mifano hii.

1. Kabla ya Yesu kuja, watu waliteseka kutokana na magonjwa mengi. Baada ya Yesu kuja na ufalme, watu wengi waliponywa magonjwa na hata leo hii anatuponya. Kwa sababu ufalme bado haujafika kikamilifu, hata hivyo, hatuponywi kimuujiza kila wakati tunapougua. Kwa kweli, sisi sote tunakufa hatimaye. Lakini Yesu atakaporudi mara ya pili, na ufalme utakapokamilika, hakutakuwa na magonjwa tena. Na kifo hakitakuwapo tena. Tutaishi naye milele.

2. Yesu alipokuja, alituweka huru kutokana na utumwa wa dhambi. Kwa hivyo sasa tuna uwezo wa "kukataa" dhambi katika maisha yetu, lakini bado tunapambana na dhambi kila siku. Mara nyingi tunafanya kile ambacho hatutaki kufanya. Yesu atakapokuja tena, ataondoa kabisa hamu na uwezo wetu wa kutenda dhambi.

3. Kabla ya Yesu kuja, watu hawakuhisi ukaribu wa uwepo wa Mungu kikamilifu kama tunavyohisi sasa. Baada ya Yesu kuja, alitutumia Roho Mtakatifu kuwa uwepo wa Mungu pamoja nasi, lakini bado hatumwoni Yesu uso kwa uso, jambo ambalo tutaweza kufanya atakapokuja tena.

***Je, unaweza kufikiria kuhusu mifano mingine inayoonyesha kipengele hiki cha ufalme wa Mungu?***

## Simulizi za Kutia Moyo

Soma na utafakari simulizi hizi za makanisa ambayo yalifundishwa kuhusu ufalme wa Mungu. Kwa mtazamo mpya unaozingatia ufalme wa Mungu, makanisa haya yalibadilisha sana jinsi walivyofanya huduma katika jamii zao. Tujifunze kutokana na mifano yao.

1. Mnamo mwaka wa 2005, katika kanisa la Mchungaji Emmanuel lililoko eneo la kati la Burundi, washirika wa kanisa walianza madarasa ya kujifunza kusoma na kuandika. Baada ya kujifunza kusoma, washirika hao walianza kusoma Biblia na kuitumia maishani mwao. Baada ya kujifunza kuhusu ufalme wa Mungu, na kwamba imani bila matendo imekufa, walianza kujihusisha zaidi katika huduma na kufikia jamii. Kanisa liliweza kuwafundisha watu si tu kusoma na kuandika, bali pia ujuzi wa kibiashara na jinsi ya kuunda vikundi vya kuweka akiba vya jamii. Kupitia kwa huduma hizi za mafunzo, kanisa limekua, likipata washirika wapya mara kwa mara. Shule yao ya Jumapili imekua na kuongezeka kutoka kwa watoto wachache hadi kuwa na zaidi ya washirika 200 kila wiki. Jamii ilipatwa na mshangao wakati kanisa lilipoanza kuwaelimisha wanawake na kuwafundisha jinsi ya kusimamia fedha, lakini sasa waume zao wanashukuru sana kwa sababu wameona manufaa ya mafunzo hayo. Familia kutoka katika kanisa lao zina matumaini mapya na umoja mpya.[3]

2. Mchungaji wa Kianglikana wa Naijeria, Canon Isaac, aliwahamasisha washirika wa kanisa lake pamoja na wanajumuiya kupata mafunzo kupitia kwa mpango ulioitwa Mabadiliko ya Kanisa na Jamii (Church and Community Transformation, CCT). Mpango huo ulibadilisha mawazo ya watu, na kuwapa mtazamo kamili zaidi wa huduma ya kanisa. Waliweza kufanya kazi pamoja kujenga kituo kidogo cha afya. Hapo awali, walilazimika kutembea kwa saa 1 ili kufikia kituo cha afya kilichokuwa karibu. Walijenga kituo kipya cha afya kwa rasilimali zao wenyewe. Kituo cha afya kimekuwa cha baraka kwa watu wengi sana hasa akina mama wajawazito 134 waliojifungua salama hapo kufikia sasa! Kanisa na jamii waliweza kujenga shule pia. Kutokana na kazi hii ya ajabu ya ufalme, kanisa la Isaac limekua kutoka washirika wachache hadi washirika 170![4]

3. Katika mwaka wa 2000, viongozi wa Kampala Pentecostal Church nchini Uganda walienda kwenye kongamano na wakafundishwa mtazamo wa kibiblia kuhusu huduma ya Yesu na ufalme wa Mungu. Katika kongamano hilo, Mungu aliweka shauku ndani ya viongozi kuifikia jamii yao kwa upendo wa Kristo. Mchungaji mkuu aliwapa changamoto washirika wa kanisa hilo kubaini mahitaji katika jamii zao na kuwajibikia matatizo yao. Washirika wa kanisa walitoka na kufanya matendo ya upendo sana katika jamii kama vile kutengeneza visima, kubadilisha mapaa ya nyumba za familia maskini, na kuwapa chakula mayatima. Wakati mmoja kanisa lilikuwa likiwatunza mayatima 1,200 na kuwajengea nyumba takriban nusu ya mayatima hao! Aidha, kila kikundi kidogo cha kanisa kiliombwa kutunza familia yenye angalau mtu mmoja anayeugua UKIMWI. Mara kwa mara washirika wa kanisa huenda kwa familia hizi, kuzungumza nao, kuwakumbatia, na kuwaombea. Ikiwa mtu anayeugua UKIMWI katika familia angefariki, kikundi cha washirika wa kanisa kingefanya ibada pamoja na familia. Hata serikali ya Uganda ilitambua kanisa hilo na kulitaja kuwa mojawapo ya mashirika kumi yenye ushawishi mkubwa katika kupambana na UKIMWI. Kupitia huduma hizi kanisa limekua na kufikia takriban washirika 12,000.[5]

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Justin Lonas.

[1] Desmond Tutu, *God Has a Dream: A Vision of Hope for Our Time* (New York, Doubleday, 2004), vii-viii.

[2] Matthew Michael, *Christian Theology and African Traditions* (Eugene, Ore., Resource Publications, 2013), Kindle ed., Loc. 5809-10.

[3] Imetolewa kutoka kwenye "The Kingdom in Action: A Case Study on Financial Education and Community Savings from Central Burundi", Cuba Parish, Gitega Diocese, Bugenyezi Commune, Five Talents. Imetumiwa kwa ruhusa.

[4] Ilishirikiwa na Chalmers Center na Richard Lister. Simulizi kutoka Nigeria ya Mpango wa Tearfund wa Mabadiliko ya Kanisa na Jamii.

[5] Scott Allen, Darrow L. Miller, and the African working group of Samaritan Strategy Africa, *Against All Hope: Hope for Africa* (Phoenix, Ariz., Disciple Nations Alliance, 2005), 49, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://disciplenations.org/resources/against-all-hope-hope-for-africa/

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki

Sio cha kuuzwa



## Somo la 3: Umaskini ni Nini?

# Maswali ya Majadiliano ya Ufunguzi

*1. Je, wewe ni maskini?*

*2. Je, kuna watu maskini katika kanisa lako?*

*3. Je, ungemwona mtu fulani katika kanisa lako kama maskini ikiwa yeye ni ________________ ?*

*Jaza nafasi iliyo wazi kwa majibu yako mwenyewe.*

Katika miaka ya 1990, Benki ya Dunia iliuliza maelfu ya watu maskini ulimwenguni kote swali hili: "*Umaskini ni nini*?" Andika maneno na mawazo muhimu uliyoyasikia katika majibu yao.

## Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kikubwa:

*Je, ulisikia maneno au vifungu vipi vya maneno ambavyo unadhani ni muhimu?*

*Je, kuna tofauti gani kati ya jinsi tulivyoelezea umaskini mwanzoni na jinsi watu hawa maskini walivyoelezea umaskini wao wenyewe?*

# Mhadhara wa Kiongozi: Kuelewa Umaskini

Tunapojaribu kuwasaidia maskini, tatizo kubwa ni kuwa mara nyingi tunafafanua umaskini kwa njia tofauti sana na jinsi watu maskini wenyewe wanavyoufafanua. **Jinsi tunavyofafanua umaskini huamua jinsi tunavyojaribu kuwasaidia watu walio katika umaskini.**

Sio cha kuuzwa

Tunapofanya kazi na watu maskini, tunahitaji kubaini kwa usahihi kile kinachosababisha umaskini wao kabla ya kujaribu kutoa suluhisho sahihi kwa tatizo lao.

**Kile tunachoamini kuwa sababu ya umaskini kitaamua suluhisho tutakalotoa.**

- Ikiwa tunafikiria kuwa umaskini unasababishwa na ukosefu wa rasilimali, tutawapa maskini rasilimali.
- Ikiwa tunafikiria kuwa umaskini unasababishwa na ukosefu wa maarifa, tutajaribu kuwaelimisha maskini.
- Ikiwa tunafikiria kuwa umaskini unasababishwa na ukandamizaji kutoka kwa watu wenye mamlaka, tutapambana na ufisadi.
- Ikiwa tunafikiria kuwa watu ni maskini kwa sababu ya dhambi zao za kibinafsi, tutajaribu kuhubiri injili na kuwafunza maskini.

## Visababishi vya Umaskini

Katika kupambana na umaskini, tunahitaji utambuzi sahihi na suluhisho sahihi, kwa hivyo tunapaswa kuchukua muda kutambua kisababishi halisi cha umaskini wa mtu.

## Maswali ya Majadiliano:

*Je, unadhani visababishi vikuu vya umaskini nchini mwenu ni vipi?*

*Je, visababishi vikuu vya umaskini kwa watu maskini katika kanisa lako na katika jamii yako ni vipi?*

## Fikiria kuhusu hali hii:

*Je, ikiwa mwanaume fulani atakuja kanisani kwenu na kuomba usaidizi wa kulipa karo ya shule ya watoto wake, mtafanyaje? Je, mnapaswa kumsaidia kwa kumpa pesa?*

Tunapowaona watu maskini duniani kote, dalili za watu maskini zinafanana kwa kiwango kikubwa. Wote hawana vitu wanavyohitaji. Lakini kile kinachosababisha ukosefu wa vitu kinaweza kuwa tofauti sana kwa kila mtu.

**Isaya 58:10 –** Kujitoa kwa ajili ya maskini.

Sio cha kuuzwa

Mifano ya visababishi vya umaskini ni pamoja na tabia ya dhambi – kama vile uvivu au uasherati, ukosefu wa elimu, kukandamizwa na watu, kukandamizwa na nguvu za pepo, kuwa na imani potofu, magonjwa, kukosa fursa, ukosefu wa rasilimali, majanga ya kiasili kama vile ukame au mafuriko, kujitenga kijamii, mifumo ya serikali na kiuchumi iliyovunjika, au ulemavu wa mwili au akili.

## Maigizo

Andika mafunzo yoyote uliyojifunza kutokana na maigizo.

**Maswali kutoka kwa Maigizo:**

1. *Je, kwa nini ni vigumu kutambua sababu halisi ya umaskini wa mtu?*
2. *Je, shangazi na mjomba wanaweza kufanya nini ili kusaidia familia hii kwa njia halisi?*
3. *Je, wanapaswa kutoa pesa au vitu vyovyote kwa familia hiyo? Kwa nini wafanye hivyo au wasifanye hivyo?*

## Je, Biblia Inafundisha Nini kuhusu Umaskini?

Kisababishi kikuu cha umaskini na matatizo yote katika ulimwengu huu ni **dhambi**, kuanzia wakati wa Anguko la Adamu na Eva.

Sio cha kuuzwa

Simulizi ya jumla ya Biblia inahusu Mungu na uhusiano wake na watu wake – **Uumbaji, Anguko, Ukombozi, na Ukamilifu.** Je, ni kitu gani kinachotokea katika kila sehemu ya hizi simulizi nne za Biblia?

**Uumbaji**

**Anguko**

**Ukombozi**

**Ukamilifu**

**Je, leo hii tuko katika sehemu gani ya simulizi hizi?**


Sio cha kuuzwa

## Uumbaji – Mahusiano Manne Muhimu

### Mwanzo 1-2

Biblia inatufundisha kuwa kuna Mungu mmoja ambaye ni Utatu – watu **watatu** wanaoshiriki kiini **kimoja** cha uungu. Hii ina maana kuwa Mungu ni Mungu wa uhusiano. Kwa kuwa wanadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu, tuliumbwa pia ili tuwe na mahusiano. Katika simulizi ya Uumbaji, tunaona mahusiano manne makuu ambayo Mungu alikusudia wanadamu wawe nayo.

# UUMBAJI




**Kielelezo cha 2.1**
Kimetolewa kwenye Bryant L. Myers, *Walking with the Poor: Principles and Practices of Transformational Development* (Maryknoll, N.Y.: Orbis Books, 1999), 27.

Sio cha kuuzwa

**1) Uhusiano na Mungu**

______________________________________________

______________________________________________

**2) Uhusiano na Wengine**

______________________________________________

______________________________________________

**3) Uhusiano na Uumbaji Wote –** Soma **Mwanzo 1:28-30.** Tunapaswa kuwa mawakili wa uumbaji wa Mungu. Tunafanya kazi katika ulimwengu wa Mungu, na tunabuni utamaduni. Mungu ametupa ulimwengu huu ili kuuelewa, kuulinda, kuutawala, na kuusimamia.

**4) Uhusiano na Nafsi Yetu –** Uhusiano huu unarejelea jinsi tunavyojifikiria sisi wenyewe. Mungu alituumba ili tuwe na amani na nafsi zetu na tutunze miili yetu na roho zetu. Watu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Hii ina maana kuwa kila mtu ana thamani na heshima.

**Wakati mahusiano haya manne yanapofanya kazi ipasavyo, watu wanaweza kufanya kile ambacho Mungu amewakusudia kufanya. Wanaweza kumtukuza Mungu kwa kufanya kazi na kujisaidia wao na familia zao.** Wakati mahusiano haya yote yanapofanya kazi vyema, tunasema kwamba kuna "**shalom**". Shalom ni neno la Kiebrania linalomaanisha kuwa kila kitu kina amani, jinsi kinavyopaswa kuwa. Kabla ya Adamu na Eva kutenda dhambi, kila kitu kilikuwa kizuri, hakukuwa na maumivu, matatizo, njaa, magonjwa, na umaskini.

# Anguko – Mahusiano Manne Muhimu

## Mwanzo 3

**Je, uhusiano kati ya Mungu na Adamu na Eva ulivunjwa au kuharibiwaje?**

**Je, uhusiano kati ya Adamu na Eva ulivunjwa au kuharibiwaje?**

**Je, uhusiano kati yao na uumbaji wote ulivunjwa au kuharibiwaje?**

**Je, mtazamo wao juu yao wenyewe uliharibiwaje?**

Sio cha kuuzwa

Umaskini ni matokeo ya dhambi ya wanadamu waliomwasi Mungu. Umaskini ni matokeo ya kuvunjika kwa mahusiano haya manne muhimu. Na kwa kuwa sote tunapitia mahusiano yaliyovunjika, tutaona kuwa sote tuna umaskini katika maisha yetu.




**Kielelezo cha 2.2**
Kimetolewa kwenye Bryant L. Myers, *Walking with the Poor: Principles and Practices of Transformational Development* (Maryknoll, N.Y.: Orbis Books, 1999), 27.

## Aina Tano za Umaskini

Kwa kuwa umaskini unahusu mahusiano kutofanya kazi ipasavyo, basi kuna aina nne za umaskini kulingana na aina nne za mahusiano yaliyovunjika, pamoja na moja zaidi inayotokana na hili.

**1) Umaskini wa Uhusiano wa Karibu wa Kiroho**

____________________________________________

____________________________________________

**2) Umaskini wa Jamii**

____________________________________________

____________________________________________

**3) Umaskini wa Uwakili**
(**a.** Kutokuwa mawakili wazuri wa Uumbaji. **b.** Kutofanya kazi katika ulimwengu wa Mungu)

Sio cha kuuzwa

**4) Umaskini wa Nafsi**

**5) Umaskini wa Mali**

**Kwa hivyo, je, maskini ni nani**? Sisi sote ni maskini. Watu wote wanaweza kutatizwa na moja au zaidi ya mahusiano haya yaliyovunjika.

Tunapomjua Yesu, tunasamehewa dhambi zetu na kuwa na amani na Mungu, na kuanza kupata nafuu kutokana na umaskini wetu wa uhusiano wa karibu wa kiroho. Kisha Yesu anaanza kubadilisha mioyo na tabia zetu ili umaskini wetu upungue katika zile sehemu zingine tatu.

Kwa baadhi ya watu, kuvunjika kwao katika mahusiano haya manne husababisha umaskini wa mali. **Umaskini wa mali** ni kile ambacho watu humaanisha kwa kawaida wanapotumia neno "*umaskini*". Umaskini wa mali unarejelea watu kukosa pesa au vitu ambavyo wanahitaji ili kuishi, kama vile chakula, makazi, au huduma za afya.

Sio cha kuuzwa

# Mfano: Simulizi ya Mary

*Mary anaishi katika kitongoji duni nchini Kenya na anakabiliwa na umaskini. Alikulia katika jamii iliyo na mtazamo kuwa wanaume ni bora kuliko wanawake. Wazazi wake hawakumthamini sana kama ndugu zake, kwa hivyo hawakumpeleka shule kwa miaka mingi sana. Hatimaye alipoolewa, alikuwa mmoja wa wake za mume wake. Mume wake alimpiga mara kwa mara hadi hatimaye akatoroka na kuishi peke yake. Baada ya kutoroka, akawa anaishi katika umaskini wa mali. Alijiona kuwa duni sana akijilinganisha na wengine kiasi kwamba hakuwa na ujasiri wa kuomba kazi. Badala yake, katika hali yake ya kutamausha, aliamua kujiajiri. Alihitaji mkopo ili kuanza.*

*Alipata mkopo kutoka kwa muuzaji fulani wa eneo hilo, lakini alimtoza riba isiyo ya haki ya asilimia 300. Alianza biashara ya kuuza makaa ya kujitengenezea nyumbani katika soko la eneo hilo, lakini kulikuwa na mamia ya watu wengine waliokuwa wakiuza makaa hivyo bei ilibaki chini sana. Mary hakufikiria hata kufanya aina nyingine ya kazi yenye mapato zaidi kwa sababu alihisi kuwa alipaswa kufanya kile ambacho kila mtu alikuwa akifanya. Akiwa amefadhaishwa na kushindwa kulipa mkopo huo, Mary alienda kwa mganga kutafuta usaidizi. Mganga huyo alisema kuwa matatizo yake ya umaskini yalisababishwa na Mary kuwakasirisha mizimu ya mababu. Alimwambia Mary anunue fahali na kuwatolea dhabihu. Kwa hivyo Mary alitumia takriban pesa zake zote zilizosalia kutoka kwa mkopo kununua fahali. Mwishowe, alikuwa maskini zaidi wa mali kuliko alivyokuwa hapo mwanzoni, na hata alifadhaika zaidi na kukosa matumaini.*[1]

## Maswali ya Majadiliano:

***1) Je, Mary alikuwa na aina gani za umaskini kando na umaskini wa mali?***

____________________________________________________________

____________________________________________________________

***2) Je, aina hizo zingine za umaskini zilichangiaje Mary kuwa na umaskini mbaya zaidi wa mali?***

____________________________________________________________

____________________________________________________________

***3) Ikiwa tungetaka kumsaidia Mary na tukampa pesa tu, je, zingemsaidia kutoka katika hali yake ya kutamausha?***

____________________________________________________________

***4) Je, tungeweza kufanya nini ili kumsaidia Mary kwa njia halisi, si tu katika umaskini wake wa mali, bali katika aina zake zote za umaskini?***

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii yako, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza.

Fikiria kuhusu angalau mtu mmoja unayemjua katika kanisa au jamii yako anayehitaji usaidizi. Jaribu kumsaidia mtu huyu kwa ujumla, katika mahusiano yake yote manne muhimu. Jitolee kumsaidia mtu huyo kwa muda mrefu. Julisha familia yako kuhusu kile unachopanga kufanya na uone kama watajitolea kumsaidia mtu huyo pamoja nawe. Unaweza kufikiria kuanza kwa kumwalika mtu huyo nyumbani kwako kwa chakula, ili muweze kujenga uhusiano na kufahamiana. Muombee mtu huyo kila siku. Mara moja kwa mwezi, chukua muda wa kufikiria kuhusu mtu huyo na mahusiano yake manne muhimu, na uhakiki jinsi umekuwa ukimsaidia, na mambo mengine zaidi unayoweza kufanya. Haya ni maswali ambayo unaweza kujiuliza mara kwa mara:

- **Je, nimekuwa nikimsaidiaje mtu huyu kukua katika uhusiano wake na Mungu?**
- **Je, nimekuwa nikimsaidiaje mtu huyu kuwa na tumaini, na asijihisi kuwa duni au asiye na thamani?**
- **Je, nimekuwa nikimsaidiaje mtu huyu kuwa na uhusiano bora na familia yake, marafiki, na majirani zake?**
- **Je, nimekuwa nikimsaidiaje mtu huyu kupata kazi ya maana ya kufanya ili kujikimu?**

Sio cha kuuzwa

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

**1) Fikiria kuhusu maisha yako mwenyewe. Je, ni kwa njia gani ambazo mahusiano yako na Mungu, nafsi yako, wengine, na uumbaji wote yanahitaji uponyaji? Je, ni mambo gani mahususi unayoweza kufanya ili kutafuta uponyaji wa Mungu katika mahusiano haya katika wiki mbili zijazo?**

______________________________

______________________________

**2) Je, kuna uhusiano wowote kati ya mahusiano manne yaliyovunjika ambao umechangia umaskini wa mali katika maisha yako au katika maisha ya mmoja wa wanafamilia wako? Ni upi?** Ikiwa unaweza, shiriki jibu lako na wanachama wa kikundi chako. Ikiwa tatizo linaendelea, jadilini pamoja jinsi uhusiano uliovunjika unaweza kushughulikiwa.

______________________________

______________________________

*(Maswali yanaendelea kwenye ukurasa wa 34)*

**3a) Kwa ufupi, waambie washiriki wa kikundi chako simulizi ya kibinafsi kuhusu wakati ambao ulimsaidia maskini.** (**Mfano:** Naweza kusema, "Wiki iliyopita, nilikutana na ombaomba sokoni na nikampa njugu karanga.") Kamilisha sehemu ya a. na b. kikamilifu kwa simulizi moja, kabla ya mtu mwingine kushiriki simulizi yake. Hakutakuwa na wakati wa kutosha kwa kila mtu kwenye kikundi kushiriki simulizi yake.

______________________________________________

______________________________________________

**3b) Chambua kila simulizi ambayo inashirikiwa katika kikundi chako. Kosoa simulizi za watu wengine kwa upendo na upole.**

- **Je, mshiriki wa kikundi alimsaidia maskini huyo kupunguza kiwango chake cha umaskini wa mali? Eleza.**
  - (**Mfano:** "Ndiyo – nilimpa ombaomba chakula ili kukidhi hitaji lake.")
- **Je, alimsaidia maskini huyo kupunguza kiwango chake cha umaskini wa uhusiano wa karibu wa kiroho? Eleza.**
  - (**Mfano:** "Hapana – sikumsaidia ombaomba huyo kukua katika uhusiano wake na Mungu.")
- **Je, alimsaidia maskini huyo kupunguza umaskini wake wa nafsi? Eleza.**
  - (**Mfano:** "Ndiyo – nilimsalimia kwa kumpa mkono na kuzungumza naye, nikijaribu kumwonyesha kuwa ana heshima na thamani.")
- **Je, alimsaidia maskini huyo kupunguza umaskini wake wa jamii? Eleza.**
  - (**Mfano:** "Hapana – sikumsaidia kukutana na watu wapya au kushiriki kanisani.")
- **Je, alimsaidia maskini huyo kupunguza umaskini wake wa uwakili? Eleza.**
  - (**Mfano:** "Hapana – sikumsaidia kupata kazi ya maana katika ulimwengu wa Mungu.")

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

Sio cha kuuzwa

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na Picha ya Adobe Stock.

[1] Steve Corbett and Brian Fikkert, *When Helping Hurts, 2e* (Chicago: Moody Publishers, 2012), 60.

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

## Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 4: Mahusiano Yaliyovunjika Barani Afrika

# Maswali ya Majadiliano ya Ufunguzi

*1) Shiriki baadhi ya mifano ya umaskini wa uhusiano wa karibu wa kiroho katika kanisa, jamii, au eneo lako.*

---

*2) Shiriki baadhi ya mifano ya umaskini wa jamii katika kanisa, jamii, au eneo lako.*

---

*3) Shiriki baadhi ya mifano ya umaskini wa uwakili katika kanisa, jamii, au eneo lako.*

---

*4) Shiriki baadhi ya mifano ya umaskini wa nafsi katika kanisa, jamii, au eneo lako.*

---

Sio cha kuuzwa

## Mhadhara wa Kiongozi


Katika somo hili, tutaangazia jinsi aina mbalimbali za umaskini zilivyo barani Afrika na jinsi zinavyoathiri jamii zetu leo.

## Umaskini wa Mali

Kuvunjika kwa mahusiano hayo manne husababisha umaskini wa mali kwa baadhi ya watu. Umaskini wa mali ni ukosefu wa mapato ya kutosha na mahitaji mengine muhimu, kama vile chakula, mavazi, malazi, huduma za afya na hata elimu ya msingi. Vipengele mbalimbali vya umaskini wa mali vinaweza kufanya kazi pamoja ili kuwafanya watu wajihisi wamenaswa.

Mchoro ulio juu ya ukurasa unaofuata unatupa mifano ya kawaida ya aina zingine nne za umaskini:

# MAHUSIANO YALIYOVUNJIKA




**Umaskini wa Uhusiano wa Karibu wa Kiroho**
- Kuabudu Sanamu
- Kufurahisha Mizimu au Mababu
- Uchawi na Hirizi
- Kukosa Matumaini
- Kupenda Mali
- Dhambi

**Umaskini wa Nafsi**
- Kutojistahi
- Kujiona kama Mungu

**Umaskini wa Uwakili**
- Uchafuzi na Takataka
- Ukataji Miti
- Uvivu
- Kuishi kwa Hofu ya Mizimu

**Umaskini wa Jumuiya**
- Ukabila, Migogoro, na Vita
- Ukosefu wa Usawa wa Kijinsia na Unyanyasaji wa Kinyumbani
- Unyanyasaji wa Watoto
- Ufisadi
- Migogoro ya Ardhi

**Umaskini wa Mali**

**Kielelezo cha 3.1**
Kimetolewa kwenye Bryant L. Myers, *Walking with the Poor: Principles and Practices of Transformational Development* (Maryknoll, N.Y.: Orbis Books, 1999), 27.

Sio cha kuuzwa

## Umaskini wa Uhusiano wa Karibu wa Kiroho

**1) Kuabudu Sanamu.** Sanamu ni **kitu chochote** kinachopewa nafasi au umuhimu zaidi kuliko Mungu mmoja wa kweli. Inaweza kujumuisha kuabudu miungu ya uwongo kama vile mbao, miti, mawe, mito, milima, wanyama, mizimu na sanamu.

---

*Je, umaskini wa aina hii wa uhusiano wa karibu wa kiroho unaweza kusababisha umaskini wa mali kwa njia gani?*

---

**Kutoka 20:1-6.** Tukichukua kitu chochote maishani mwetu na kukifanya kuwa cha maana zaidi kuliko Mungu, hiyo ni kuabudu sanamu.

*Je, tunaona aina hii ya kuabudu sanamu katika jamii zetu leo? Katika makanisa yetu? Eleza.*

**2. Kufurahisha mizimu na mababu.** Katika sehemu nyingi barani Afrika, watu hutoa sadaka na dhabihu ili kufurahisha mizimu au mababu. **Kumbukumbu 18:10-11** na **1 Timotheo 2:5.** Ni jambo la kawaida kutoa dhabihu kwa mizimu, miungu, au mababu ili kujaribu kupata ulinzi wa kiroho, kupata pesa, kuponywa magonjwa, au kupata uteuzi au kazi mahususi ya kisiasa. Jambo la kusikitisha ni kwamba watu wanaofanya vitendo hivi mara nyingi ni maskini wanaoshawishika kwa urahisi na waliotamauka ambao wanahisi kwamba hawana mahali pengine pa kugeukia.

*Je, kuabudu mababu au mizimu ni tatizo katika jamii zetu?*

*Je, umaskini wa aina hii wa uhusiano wa karibu wa kiroho unaweza kusababisha umaskini wa mali kwa njia gani?*

**3. Uchawi na Hirizi.** Kupitia matendo hayo, watu wanajaribu kutumia nguvu za ulimwengu wa kiroho kupata vitu wanavyotaka, badala ya kutumaini nguvu za Mungu pekee. **Ufunuo 21:8.**

*Je, Wakristo wanapaswa kuogopa watu wengine wanaotumia uchawi au hirizi dhidi yao?*

Soma **Waefeso 6:10-18** na **1 Yohana 4:4.**

**4. Kukosa Matumaini.** Bila msamaha na tumaini la uzima wa milele, bila kuamini kuwa Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha yao, watu yamkini hawatakuwa na matumaini ya siku zijazo, na hivyo wanaweza kufanya chochote kujaribu kubadilisha hali yao. Soma **Warumi 8:28** na **Wafilipi 1:4-6.**

*Je, kukosa matumaini ni tatizo katika jamii zetu?*

*Je, tunawezaje kuwapa watu matumaini?*

Sio cha kuuzwa

**5. Kupenda Mali.** Kupenda mali ni kuthamini mali na pesa kama njia kuu ya kupata kusudi la maisha na kuwa na furaha. **Luka 12:15** na **1 Timotheo 6:6-10.** Hata katika baadhi ya makanisa, lengo si kumtukuza Mungu na kumshukuru kwa msamaha, bali ni kumwabudu Mungu ili atupatie pesa zaidi.

*Je, umaskini wa aina hii wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho unaweza kusababisha umaskini wa mali kwa njia gani?*

______________________________

**6. Dhambi.** Hata sisi Wakristo, bado tunatenda dhambi wakati mwingine. Ikiwa tumeokoka kweli, tutaungama dhambi zetu na kutubu na kuendelea kupigana dhidi ya dhambi. Lakini tunapotenda dhambi, haimpendezi Mungu, na tunapata pia matokeo ya kawaida kwa kuishi katika njia ya upumbavu ambayo Mungu hataki tuishi. Hivyo kwa namna fulani, Wakristo wanapotenda dhambi tunapata kiasi kidogo cha umaskini wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho. Lakini mfano unaofahamika zaidi wa umaskini wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho ni watu wasiokuwa Wakristo wanaoishi katika dhambi. Dhambi, bila shaka, ni za aina nyingi lakini kuna mifano inayofahamika ya dhambi ambayo haisababishi tu umaskini wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho, bali husababisha pia umaskini wa mali. Dhambi hizi ni pamoja na ulevi, uraibu wa dawa za kulevya, wizi, uraibu wa kucheza kamari, na uasherati. Janga la VVU linaenea kote Afrika kwa kiasi kikubwa (ingawa si njia pekee) kupitia dhambi za zinaa za uzinzi na uasherati.

*Je, kuna dhambi yoyote kati ya hizi inayosababisha umaskini mwingi wa mali katika jamii zetu?*

*Katika makanisa yetu?*

______________________________

# Umaskini wa Jamii

**1. Ukabila, Migogoro, na Vita.** Nchi nyingi barani Afrika zina historia ndefu ya vita, mapinduzi, vikundi vya waasi, ujambazi, migogoro ya kikabila, na hata mauaji ya halaiki. Kila siku, watu 9,500 kwa wastani wanahamishwa kutoka kwa makazi yao barani Afrika, hasa kutokana na migogoro na vurugu.[1] Mwishoni mwa mwaka wa 2015, takriban watu milioni 12.4 barani Afrika walikuwa wakiishi kama wakimbizi au watu waliohamishwa.[2]

*Je, ukabila au migogoro ni tatizo katika eneo lako?*

*Je, Kanisa linazungumza kuhusu tatizo hilo?*

______________________________

Mungu anajali makabila yote na anataka watu wa mataifa na lugha zote wawe katika Ufalme wake. **Ufunuo 7:9-10**

"Kuwepo kwa makabila mengi kunapaswa kututajirisha; kunapaswa kutufanya kuwa watu wa kipekee katika utofauti wetu na hakupaswi kutumiwa kutugawanya." – Ellen Johnson Sirleaf, aliyekuwa rais wa Liberia.[3]

"Tunaweza kuwa na dini tofauti, lugha tofauti, ngozi za rangi tofauti, lakini sote ni wa jamii moja ya wanadamu." – Kofi Annan, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.[4]

**2. Mahusiano Yaliyovunjika kati ya Wanaume na Wanawake.** Hii inarejelea mahusiano yaliyovunjika kati ya wanaume na wanawake. Katika jamii, yanaweza kudhihirika kwa kupendelea wavulana kuelimishwa kuliko wasichana. Katika sehemu ya ndoa, uhusiano uliovunjika kati ya mwanaume na mwanamke unaweza kudhihirika katika ubakaji, kuoa wake wengi, kutokuwa mwaminifu katika ndoa, au talaka. Takriban theluthi moja ya wanawake wa Kiafrika waliripoti kukumbwa na unyanyasaji wa nyumbani (kimwili au kingono), bila kuhesabu wale wanaoogopa sana kiasi cha kukosa kuripoti.[5] Suala lingine katika ndoa za Kiafrika ni kwamba baadhi ya watu wanaamini kuwa jukumu la wanaume ni kuketi huku wanawake wakifanya kazi nyingi.

*Katika makanisa yetu, je, baadhi ya watu wanadhani ni jambo linalokubalika kwa waume kuwapiga wake zao?*

**Mwanzo 1:27.** Ni lazima tukumbuke kuwa wanaume na wanawake wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Ingawa waliumbwa na miili tofauti na majukumu tofauti, wote waliumbwa kuwa na utu na thamani. Wanawake waliumbwa ili kuwasaidia wanaume kwa kazi zao, lakini si kufanya kazi zote. **Waefeso 5:28-29.** Waume wanapaswa kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Kupiga mwili wako mwenyewe ni unyama.

**3. Unyanyasaji wa watoto.** Watoto wengi wamekuwa wakifanyishwa kazi kama vijakazi wa nyumbani, wakilima kwenye bustani za watu. Zaidi ya asilimia 40 ya watoto wote walio na umri wa miaka 5–14 hufanya kazi ili kujikimu barani Afrika.[6] Kupigwa kupita kiasi mara nyingi hutumiwa kama aina ya adhabu na wazazi.

*Je, ulidhulumiwa kwa njia gani ulipokuwa mtoto?*

*Je, hilo lilikuathiri kwa njia gani?*

**4. Ufisadi.**

*Tutarejelea mada hii katika somo lingine.*

**5. Migogoro ya ardhi.** Mifano inajumuisha mabishano kati ya majirani kuhusu mipaka ya mashamba, mabishano kati ya familia kuhusu masuala ya urithi, migogoro kati ya wafugaji na wakulima, migogoro kati ya serikali na wazawa, na mabishano kati ya kampuni na wakazi wa eneo fulani kuhusu haki za kuchimba na kutumia madini, maji, au rasilimali zinginezo.

*Je, kuna migogoro ya ardhi katika jamii yako? Eleza.*

*Je, Kanisa linafanya nini ili kusaidia kutatua migogoro kama hiyo?*

Sio cha kuuzwa

# Umaskini wa Uwakili

Hii inaweza kuchukua namna ya utunzaji usiofaa wa mazingira, au kutofanya kazi na kuwa mwenye tija.
**Zaburi 8**

**1. Uchafuzi na Takataka.** Maji, hewa na ardhi zinachafuliwa na kemikali zinazovuja, mafusho hewani, na takataka za plastiki. Matokeo yake ni udongo usiokuwa na rutuba, kuzaliana kwa wadudu na magonjwa, na kuondoa uzuri wa uumbaji wa Mungu.

---

Tunapokosa kutii amri za Mungu za kutunza uumbaji wake, tunapata matokeo mabaya ya kawaida kutokana na matendo yetu.

Nukuu kutoka kwa Mwanaharakati wa Mazingira wa Kenya, Wangari Maathai:

> Changamoto zinazokabili jamii za wakulima kote nchini Kenya zinafanana na zile zinazoonekana kote barani Afrika na katika nchi nyingi maskini katika maeneo ambayo hayajakua kiuchumi. Katika maeneo haya, kujali masuala ya mazingira huchukuliwa kama anasa. Lakini sivyo: kulinda na kurejesha mifumo ya ikolojia, na kupunguza au kurekebisha ongezeko la joto duniani, ni masuala yanayotishia maisha. Mlinganyo ni rahisi: chochote tunachofanya, kinaathiri mazingira; tukiyaharibu, tutadhoofisha njia zetu za maisha na hatimaye kujiua. Hii ndiyo sababu mazingira yanahitaji kuwa kiini cha sera na utekelezaji katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.[7]

**2. Ukataji miti.** Ukataji miti unamaanisha uharibifu wa miti na misitu bila kupanda tena miti. Ukataji miti barani Afrika umesababisha njaa, kuenea kwa jangwa, uhaba wa maji, ukame, mgawanyiko mkubwa wa kiuchumi na kijamii, na migogoro iliyoenea yenye msingi wa rasilimali. Asilimia 80 ya kaya barani Afrika zinategemea kuni au makaa kama chanzo kikuu cha nishati.[8] Kiwango cha ukataji miti barani Afrika ni mara nne ya wastani wa dunia.[9]

---

*Je, ni matatizo gani ya kimazingira kati ya haya unayoona katika jamii yako?*

*Je, Kanisa au serikali inashughulikia masuala haya? Eleza.*

---

**3. Uvivu.** Inaweza kuhusisha kutumia njia za mkato, kutofanya kazi wakati meneja hayupo, kuchelewa kufika kazini, au kutokamilisha kazi kwa muda uliokubaliwa. Ni jambo la kawaida, hasa kwa wafanyakazi wa ofisini, kufika kazini lakini kisha wanatumia saa nyingi wakijadiliana kuhusu siasa, kupokea simu za kibinafsi, kununua vitu, au kusoma magazeti ya kitaifa.

---

*Je, umaskini wa aina hii wa uwakili unasababisha umaskini zaidi wa mali kwa njia gani katika jamii yako?*

---

Sio cha kuuzwa

**4. Kuishi kwa hofu ya mizimu.** Kuna imani iliyoenea miongoni mwa baadhi ya watu kuwa mizimu hutawala ardhi, mito, au misitu fulani barani Afrika. Kutokana na woga, watu hawa huepuka kutumia rasilimali ambazo Mungu amewapa. Huenda watu wengine wasifanye kazi fulani mahususi au wasifanye kazi kabisa, wakidai kuwa mizimu haiwaruhusu. Watu hawa hawatambui kuwa Mungu ametupa uwezo na wajibu wa kuwa mawakili wa ardhi. Soma **Yakobo 4:7.**

*Je, kuna watu wenye hofu ya aina hii katika jamii yako?*

*Je, Kanisa linaweza kufanya nini ili kuwasaidia?*

## Umaskini wa Nafsi

Umaskini wa nafsi unarejelea kuwa na uhusiano uliovunjika na sisi wenyewe. Tutakita mjadala wetu kwa aina mbili tu za umaskini wa nafsi. Kimsingi, watu wanaweza 1) kujiona kuwa duni sana na wasione thamani yao kama watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu, au 2) wanaweza kujiona kuwa watu wa hadhi ya juu sana, kama miungu wenyewe, badala ya kuwa watumishi wa Mungu.

## Umaskini wa Nafsi 1: Kutojistahi

Watu wanakuwa na umaskini wa aina hii wanapojihisi kuwa duni sana. Inaweza kujumuisha kujiona duni, kuwa huna thamani, kutokuwa na uwezo, kutokuwa na ujuzi, kuona aibu, kuwa na hofu, kuhisi kudhalilishwa, kutokuwa na uwezo wa kuchangia maoni, na kutegemea wengine. Kwa ujumla, ni kuwa na mtazamo hasi kujihusu. Ni jambo la kawaida sana (ingawa si kweli kwa wote) kwa watu maskini wa mali kutojistahi na kuhisi mambo hayo yote.

Hii ni Simulizi kutoka kwa Bryant Myers, Mmarekani ambaye ni profesa katika seminari na mwandishi. Bryant alikuwa ameketi karibu na moto katika Jangwa la Kalahari akizungumza na mwanamke kutoka kabila la wenyeji. Alimwambia kuwa Mwana wa Mungu alikufa kwa ajili ya dhambi zake. Kwa kujibu hilo, alisema angeweza kuamini kuwa Mungu angemtoa Mwanawe afe kwa ajili ya mtu mweupe au mzungu, na labda hata mtu mweusi, lakini hangeweza kamwe kukubali wazo kuwa Mungu angemtoa Mwanawe afe kwa ajili ya mwanamke, hasa mmoja kutoka kwa kabila lake. Unaweza kuona kuwa alikuwa na umaskini wa nafsi. Umaskini wa nafsi hauchangii tu umaskini wa mali, bali katika hali hii, alijiona asiyefaa na duni, kiasi kwamba alikataa kukubali hata habari njema ya injili. Umaskini wake wa nafsi ulikuwa unamfanya pia awe na umaskini wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho. Anahitaji usaidizi ili kupata tena utambulisho wake kama mtoto wa Mungu, aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu. Anahitaji kufundishwa kuwa jukumu lake halisi maishani ni kuishi na kufanya kazi kama mtoto wa Mungu katika ulimwengu ambao Mungu aliuumba kwa ajili yake.[10]

Sio cha kuuzwa

*1) Je, nini husababisha kutojistahi katika familia yako, jamii na eneo lako?*

*2) Unaweza kuwashauri vipi watu walio maskini wa mali katika kanisa lako ambao wanaona aibu na wasiojiweza kutokana na umaskini wao?*

**Historia ya biashara ya utumwa na ukoloni.** Katika kipindi chote cha ukoloni, Waafrika walijifunza kuogopa watu wa nchi za magharibi, walijifunza kuwa na aibu kuhusu tamaduni zao wenyewe, na walijifunza kujinyenyekeza na kujiona duni.

- Agostiine Musopole, kasisi na mwandishi kutoka Malawi, alisema, “Hapa ndipo Mwafrika anahisi umaskini wake zaidi: Umaskini wa nafsi, ambapo Waafrika maskini wameamini kuwa wao si wema na hawawezi kufanya mambo kwa njia sawa.”[11]

- Tunapaswa kujifunza na kuhubiri kuwa Waafrika si watu wa hadhi ya chini, kwamba si lazima wawategemee wageni siku zote. Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu na Mungu anaweza kututumia kubadilisha jamii zetu.

*Je, unapomwona mgeni katika nchi yako, unajiona kuwa sawa na yeye kwa hadhi na thamani au unajiona duni?*

*Kwa nini?*

## Maswali ya Majadiliano:

*Je, wanawake katika kanisa na jamii yako wanajiona kuwa duni kuliko wanaume au wenye thamani sawa na wao mbele za Mungu?*

*Je, watu wenye ulemavu au uzeruzeru katika kanisa lako wanahisi kuwa muhimu na wa thamani kwa huduma ya kanisa kama kila mtu mwingine? Eleza.*

*Ikiwa watu hawa hawako katika kanisa lako, hali hiyo huenda imesababishwa na nini?*

Sio cha kuuzwa

Ni lazima tuhubiri na tukumbuke kuwa sisi sote tumeumbwa kwa usawa kwa mfano wa Mungu, tumebarikiwa na talanta na karama, bila kujali rangi ya ngozi yetu au mahali tulipotoka. **Zaburi 139:13-16.**

# Umaskini wa Nafsi 2: Kujiona kama Mungu

Watu walio na hali ya "kujiona kama mungu" wanajiona kuwa bora zaidi kuliko inavyopaswa, wanajiona kuwa bora kuliko wengine. Tunaiita hali ya kujiona kama mungu kwa sababu watu hawa wanajiweka karibu na nafasi ya Mungu. Wanataka kupokea utukufu na heshima. Wanajiona kuwa wa muhimu sana. Mara nyingi ni wale walio matajiri wa mali ndio wanaohisi hivyo.

---

***Unapotembea mjini na kumwona ombaomba akiomba pesa, je, unajiona kuwa bora kuliko mtu huyo? Je, unahisi kuwa wa muhimu sana?***

______________________________________________

Mojawapo ya nyakati ambazo tunajifikiria kuwa wa muhimu sana, tukiwa na hali ya kujiona kama mungu, ni wakati tunapojaribu kusaidia maskini wa mali. Tunadhania kuwa tunawasaidia kwa upendo, lakini ni lazima tuchunguze nia zetu. Je, tunawasaidia ili kusifiwa kuwa sisi ni wakombozi wao? Je, tunawasaidia ili tujihisi vizuri zaidi? Je, tunapowasaidia, tunawalaumu kwa umasikini wao, tukijiona kuwa sisi ni bora kuliko wao na wanastahili umaskini wao? Je, tunafikiri kuwa sisi ni wenye akili zaidi na tuna mawazo bora zaidi tukijilinganisha na watu maskini wa mali?

***Je, kuna mtu ambaye yuko tayari kukiri makosa yake na kushiriki simulizi yake kuhusu wakati ambapo yeye mwenyewe alijiona kama mungu alipokuwa akisaidia watu wenye umaskini wa mali?***

______________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Kuwaumiza Maskini

**Mlinganyo wa madhara katika kupambana na umaskini:**

**1)** Matajiri ambao wanajaribu kusaidia wana hali ya kujiona kama mungu.

**2)** Maskini wa mali wanaosaidiwa hawajistahi.

**1 + 2 = 3**

**3)** Baada ya kusaidiwa, maskini wa mali huona aibu hata zaidi na kusalia watu wasioweza kujisaidia huku wakiendelea kubaki katika umaskini, na matajiri wanahisi kuwa bora zaidi. Maskini wa mali na matajiri wa mali ambao walijaribu kusaidia wanaishia *kuwa na kinyongo wao kwa wao*.

**Uchunguzi Kifani kuhusu Vichujio vya Maji:**

*1) Je, tunajifunza nini kutokana na simulizi hii?*

*2) Je, kuna mtu yeyote anayetaka kushiriki simulizi kama hiyo ili kuelezea mlinganyo huu ambao umesikia au kuona? Unaposhiriki, usitaje majina au mashirika mahususi.*

Kwa hivyo tunaweza kufanya nini ili kuepuka kufanya makosa hayo tunapowasaidia watu? Je, tunawezaje kuondoa hali yetu ya kujiona kama mungu?

**Kwanza,** tunahitaji kubadili ufafanuzi wetu wa umaskini. Ni lazima tutubu kwa kufikiria tu kuhusu pesa, na kuelewa kuwa kuna aina nyingi za umaskini.

**Pili,** tunapaswa kukumbuka kuwa sote tuna umaskini kwa njia fulani (katika mahusiano manne muhimu), na hivyo sote tunamhitaji Yesu.

**Tatu,** tunahitaji kuwa wanyenyekevu na kuendelea kuwatia moyo maskini wa mali kwa kuwaambia kuwa wameumbwa kwa mfano wa Mungu na wako sawa na sisi.

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi hapa chini.

**1)** Panga ibada inayozingatia mahusiano hayo manne. Fundisha kanisa kuyahusu kwa ufupi. Fikiria kuwa na wakati wa toba na maungamo, ukiangazia jinsi sisi sote tumekosea kwa njia mbalimbali katika mahusiano yetu manne muhimu. Chukua muda hasa kukiri jinsi tunavyochangia kuwafanya maskini wajihisi kutojistahi. Wakati wa ibada, hubiri mahubiri kuhusu jinsi watu wote walivyoumbwa kwa mfano wa Mungu, na wanavyostahili heshima na upendo wetu.

**2)** Shughuli mbadala kwa wasiokuwa wachungaji – Fundisha familia yako kuhusu mahusiano hayo manne. Kisha, kwa pamoja kama familia, fanyeni mpango wa jinsi mtakavyojaribu kuboresha kila uhusiano kati ya mahusiano hayo manne.

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

**1)** Ukizingatia uhusiano wako na Mungu, nafsi yako, watu wengine, na uumbaji wote, unaweza kufanya nini ili kuboresha mahusiano hayo?

Uhusiano na Mungu

______________________________

Na nafsi

______________________________

Na watu wengine

______________________________

Na uumbaji wote

______________________________

**2)** Soma **Zaburi 19:1-4.** Uumbaji unapaswa kudhihirisha utukufu wa Mungu. Je, kanisa lako linaweza kufanya nini ili kufanya mazingira ya kimaumbile ya jamii yako kuwa mahali pazuri zaidi na penye afya panapodhihirisha utukufu wa Mungu vyema zaidi?

______________________________

______________________________

**3)** Tunapowaangalia maskini wa mali, je, tunawaona kama watu walio sawa nasi na walioumbwa kwa mfano wa Mungu? Eleza.

______________________________

**4)** Soma vifungu hivi vya Biblia kuhusu kiburi. Jadili jinsi ya kuondoa hali yako ya kujiona kama mungu. **Warumi 12:3, Warumi 12:16, Mathayo 23:12, na Mithali 26:12.**

______________________________

______________________________

**5)** Je, wewe mwenyewe huwa unajiona duni kuliko wale walio na pesa nyingi kuliko wewe? Eleza.

______________________________

**6)** Ombeni pamoja kama kikundi. Chukua muda wa kutubu, omba unyenyekevu, na umwombe Mungu ayabadilishe mahusiano yako na Yeye, nafsi yako, wengine na uumbaji wote.

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Kuelewa Mfano wa Mungu

Soma na utafakari kuhusu Mwanzo sura ya 1-3.
*Je, kuumbwa kwa mfano wa Mungu kunamaanisha nini hasa?*

Siku ya sita ya uumbaji, Mungu aliumba viumbe Vyake vya ajabu na vya kipekee, wanadamu. Soma **Mwanzo 1:26–27.** Mungu alimaliza kazi Yake ya uumbaji kwa "mguso wa kibinafsi". Mungu alimuumba Adamu kutoka kwa mavumbi na kumpa uhai kwa kushiriki naye pumzi Yake mwenyewe (**Mwanzo 2:7**). Kwa hiyo, binadamu ni wa kipekee kati ya viumbe vyote vya Mungu, akiwa ameumbwa kuwa na mwili unaoonekana na pia nafsi isiyoonekana (ambayo tunaweza pia kuiita roho yetu).

Kuwa na "sura" au "mfano" wa Mungu kunamaanisha kuwa tuliumbwa tufanane na Mungu. Lakini hatupaswi kufikiri kuwa huku kufanana na Mungu ni sawa na jinsi tunavyoangalia kwenye kioo na kuona sura zetu. Adamu hakufanana kimwili na Mungu. Mungu, katika asili Yake ya uungu, hana mwili; bali Yeye ni Roho. Soma **Yohana 4:24.** Biblia inazungumza kuhusu mikono, masikio au macho ya Mungu kwa njia ya sitiari ili kutusaidia kumwelewa vizuri zaidi. Kwa hivyo mfano wa Mungu lazima uwe unarejelea kitu kingine kando na mwonekano wa kimwili. Katika historia yote ya kanisa, Wakristo wamefikiria kwa kina kuhusu maana ya mfano wa Mungu na kuhitimisha kuwa kuumbwa kwa mfano wa Mungu kunarejelea njia ambazo tuliumbwa ili tufanane na Mungu. Na tuliumbwa tufanane naye kwa njia nyingi:

1. Hatukuumbwa tu kama viumbe wa kimwili, bali pia kama viumbe wa kiroho, ili tufanane na Mungu ambaye ni Roho.

2. Tuliumbwa kuwa watakatifu na wenye haki kama alivyo Mungu. Hii inaweza kuitwa "mfano wa kimaadili wa Mungu."

3. Tuliumbwa tofauti na wanyama ili tuwe na akili, lugha, hisia, na uhuru wa kimaadili.

4. Mungu wetu ni Mungu wa Utatu. Kama vile nafsi tatu daima zimekuwa katika uhusiano mkamilifu wa upendo kati yao wenyewe, ndivyo tulivyoumbwa pia kuwa katika uhusiano wa upendo na Mungu, na sisi wenyewe, na wengine, na uumbaji wote.

5. Mungu alituumba tuwe mawakili Wake na kufanya kazi Yake katika ulimwengu huu. Kwa kuwa Mungu anatawala uumbaji, alituumba kwa mfano Wake ili tushiriki katika kuutawala uumbaji. Soma **Mwanzo 1:28–30.** Tunapaswa kusimamia uumbaji, kuutunza kwa upendo, na kufanya kazi ndani yake ili kuukuza na kuufanya uwe na matunda na umaridadi. Tutajadili zaidi kuhusu kazi hii katika somo la baadaye.

Mfano wa Mungu ni kitu ambacho kinashirikiwa na watu wote. Dhambi zetu zinatia doa mfano wa Mungu ndani yetu, lakini sisi sote bado ni watu wenye mfano wa Mungu. Hata watu wabaya zaidi ulimwenguni bado wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Tunapaswa kukumbuka kuwa kila mtu ameumbwa kwa mfano wa Mungu, ikiwa ni pamoja na watu wasiokuwa Wakristo, wale wenye ulemavu wa kimwili, wale ambao wana ulemavu wa kiakili na wale ambao bado wako ndani ya matumbo ya mama zao – kila mtu. Hili linapaswa kutufanya tuwe na heshima kwa watu wote, hata wale ambao hawajasoma na wenye umaskini mkubwa wa mali. Maisha ya kila mtu yana thamani. Kwa kuwa sisi sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, kumdhuru mtu mwingine si kumkosea mtu huyo tu bali pia ni dhambi dhidi ya Mungu wetu mweza yote. Ni lazima tuwatendee watu wote kwa heshima, kwa kujali, na kwa upendo.

Sio cha kuuzwa

Lengo ni kwamba sisi sote tunapaswa kuwa na maoni ya kweli na mazuri juu yetu wenyewe kama watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu. Lakini tunaweza kusahau ukweli huu muhimu haraka sana. Watu wengine hawajawahi kamwe kufundishwa ukweli huu hata kidogo. Tunapokuwa na mtazamo usiofaa kujihusu, tunakuwa na umaskini wa nafsi. Tunahitaji kuepuka kutojistahi na kujiona kama mungu.

## Mfano wa Kimaadili wa Mungu

Ni vizuri kutafakari kwa undani zaidi kuhusu mfano wa kimaadili wa Mungu (maana ya pili ya mfano wa Mungu katika orodha iliyo hapo juu). Adamu na Eva waliumbwa kwa mfano wa Mungu, lakini walipomwasi Mungu, Dhambi iliingia ulimwenguni. Adamu alikuwa mwakilishi wetu wa wanadamu, kwa hivyo tunabeba matokeo ya dhambi yake pamoja na yeye (**Warumi 5:12**). Sasa watu wote wanazaliwa na asili ya dhambi na watu wote wanamtenda Mungu dhambi kama vile Adamu na Eva walivyofanya.

Dhambi imepotosha mfano wa Mungu ndani ya watu. Tumetumia mantiki yetu kubuni uwongo changamano. Tumetumia mahusiano yetu kuhadaa na kutumia watu wengine vibaya. Na badala ya kutumia mamlaka yetu juu ya dunia kuwakilisha utawala wenye upendo wa Mungu, tumepotosha na kuharibu sehemu kubwa ya uumbaji unaotuzunguka. Je, tutaondokaje katika machafuko na uharibifu ambao tumesababisha? Tunahitaji kuwa na mfano wa Mungu uliorejeshwa ndani yetu. Lakini hili ni jambo ambalo hatuwezi kufanya peke yetu. Tunahitaji Adamu mpya, mwakilishi mpya ambaye mfano wake haujatiwa doa na dhambi, mtu ambaye anafanana kikamilifu na Mungu na anamtii Mungu kikamilifu.

Tunamhitaji Yesu! Yesu ndiye mfano kamili wa Mungu. Yeye ni Mungu mwenyewe. Tafakari **2 Wakorintho 4:4, Wakolosai 1:15** na **Waebrania 1:3.** Alipochukua mwili wa binadamu, Yesu alitufunulia Mungu kwa njia yenye nguvu zaidi. Kama binadamu, alitembea na kuzungumza na watu uso kwa uso. Na Yesu aliishi maisha makamilifu ya utiifu na uadilifu. Tunapokuwa na imani katika Yesu na kuunganishwa na yeye, anaturejeshea sura ya kimaadili ya Mungu. Tunahesabiwa haki kwa imani na kupokea haki kamilifu ya Kristo kama karama. Sasa Mungu anapotuona, anaona mfano mkamilifu wa kimaadili wa Mungu kwa sababu anamwona Kristo ndani yetu. Soma na utafakari **Wakolosai 3:9-10, 2 Wakorintho 3:18, Waefeso 4:22-24, 1 Wakorintho 15:49,** na **Warumi 8:28-30** ili uone jinsi Mungu anavyorejesha mfano wa Mungu ndani yetu kupitia kwa Kristo.

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na picha iliyopigwa na Musa Tukurah.

[1] Ellie Kemp, ed., "Africa Report on Internal Displacement" (Oslo, Norwegian Refugee Council, 2016), 5, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.internal-displacement.org/publications/2016-africa-report-on-internal-displacement/

[2] Ibid.

[3] Imenukuliwa katika Joe McCarthy, "It's Time for a Woman to Lead the UN: Here Are 5 Candidates" (Global Citizen, Agosti 24, 2015), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.globalcitizen.org/en/content/its-time-for-a-woman-to-lead-the-un-here-are-5-can/.

[4] Imenukuliwa katika Shirley A. Jones, ed., *Simply Living: The Spirit of the Indigenous People* (Novato, Calif., New World Library, 1999).

[5] Luc Christensen, "Domestic Violence and Poverty in Africa: When the Husband's Beating Stick is Like Butter" (World Bank, Africa Can End Poverty blog, Januari 18, 2016), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://blogs.worldbank.org/africacan/domestic-violence-and- poverty-in-africa-when-the-husbands-beating-stick-is-like-butter.

[6] "Child Labour in Africa" (International Labour Office, 2002), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/--- ed_norm/---declaration/documents/publication/wcms_decl_fs_37_en.pdf.

Sio cha kuuzwa

[7] Wangari Maathai, *The Challenge for Africa*, (New York: Pantheon Books, 2009) Kindle, ed., Loc. 3482-93.

[8] John-Paul Iwuoha, "Africa's Addiction to Charcoal – Everything You Need to Know about This Billion-Dollar Business!" (Smallstarter, 15 Septemba, 2013), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.globalcitizen.org/en/content/charcoal-africa-power-good-bad/.

[9] "Deforestation 'Faster in Africa'", (BBC News, Mei 26, 2009), accessed online: http://news.bbc.co.uk/2/hi/africa/8066871.stm.

[10] Bryant L. Myers, *Walking with the Poor: Principles and Practices of Transformational Development* (Maryknoll, N.Y.: Orbis Books, 1999), 129.

[11] Ibid., 127.

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 5: Kupambana na Umaskini kupitia Upatanisho

# Swali la Majadiliano la Ufunguzi

*Neno "upatanisho" linamaanisha nini?*

______________________________

______________________________

# Mhadhara wa Kiongozi

Katika masomo ya awali, tuliangazia kwa kina asili ya umaskini na mahusiano manne yaliyovunjika. Somo hili linaangazia suluhisho la matatizo hayo ya umaskini. Na suluhisho ni upatanisho.

**Ukombozi**

______________________________

**Wakolosai 1:19–20**

______________________________

**Warumi 5:10**

______________________________

**Ukamilifu**

______________________________

______________________________

**Suluhisho la umaskini ni**

______________________________

# Huduma ya Upatanisho

**2 Wakorintho 5:17-21**

______________________________

Sio cha kuuzwa

***Je, tunaweza kutarajia maendeleo kiasi gani katika kazi ya upatanisho?***

***Je, inawezekana kwa Mungu kututumia kuondoa umaskini kabisa? Eleza.***

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

Tunaweza kukubali ukweli halisi kuwa hatutatatua matatizo yote ya ulimwengu mwaka huu. Lakini wakati huo huo, tunaweza kupiga hatua kwa matumaini na ujasiri tukijua kuwa Yesu yuko kazini. Atatutumia kuleta urejesho fulani kwa mahusiano manne yaliyovunjika tunayoona ulimwenguni.

## Simulizi ya Jonny

*Kumbuka katika sehemu ya kwanza ya simulizi yangu, kwa bahati mbaya nilimsababishia madhara kaka yangu, familia yake na mimi mwenyewe nikiwa najaribu kumsaidia kwa njia yangu mwenyewe. Nilitamani sana kumsaidia lakini niliishia kufadhili uraibu wake wa pombe, jambo ambalo lilisababisha kuvunjika kwa mahusiano zaidi. Kwa kweli alinisikitisha sana lakini baadaye niligundua kuwa sehemu ya tatizo ilikuwa njia yangu ya kumsaidia. Kwa hivyo nikaomba kuhusu jambo hilo, kisha nikaenda kumuona tena. Niliomba msamaha kwa maneno makali niliyoyatumia kuhusu jinsi alivyonisikitisha kisha nikathibitisha tena heshima yangu kwake kama kaka yangu mkubwa. Aliomba msamaha pia kwa kutusikitisha mimi na familia yake na kwa tabia yake. Tulipatanishwa na tukafanya mazungumzo pamoja na familia yake.*

*Mimi na wanafamilia wengine tulithibitisha vipawa na uwezo wake, hasa ujuzi wake katika kilimo. Tulibaini pia kuwa kuna ardhi ya bure kijijini ambayo ina rutuba sana kwa kilimo. Nilimsifu Mungu kwa kipindi hiki kizuri cha upatanisho na tukafunga wakati wetu pamoja kwa maombi. Baadaye, nilimpa zana za kilimo alizohitaji. Niliendelea pia kumtia moyo kuwa anaweza kutoka katika hali yake na kumsihi aombe mwongozo na amrudie Mungu. Baada ya muda, kaka yangu alianza kuzunguka kijijini akitafuta kazi, na alilipwa kwa kufanya kazi katika mashamba ya watu wengine. Aliweka akiba na kuanza kulima shamba lake mwenyewe na anaendelea na kazi hiyo hadi leo.*

***Jonny alifanya nini vizuri?***

***Je, angefanya kitu gani kwa njia tofauti?***

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Kupatanisha Mahusiano manne

*1. Je, tunaweza kufanya nini ili tusaidie kuwapatanisha watu na Mungu?*

*2. Je, tunaweza kufanya nini ili tuwasaidie watu kuwa na mtazamo unaofaa kuhusu wao wenyewe?*

*3. Je, tunaweza kufanya nini ili tuwahimize watu wapatane?*

*4. Je, tunawezaje kuwa mawakili bora wa uumbaji wa Mungu?*

*5. Je, tunaweza kufanya nini ili tuwasaidie watu kupata kazi nzuri za kufanya katika ulimwengu wa Mungu?*

Sio cha kuuzwa

Shughuli hizi zote tulizoziorodhesha ni njia za kupambana na umaskini, ingawa mara nyingi hatuzioni hivyo.

Tunapaswa pia kuzingatia upatanisho tunapopima mafanikio yetu katika kazi yetu ya kupambana na umaskini. Tunataka kuona watu wanaomtukuza Mungu kwa kuishi katika uhusiano mzuri na yeye, na nafsi zao, na wengine, na uumbaji wote. Upatanisho huu utasababisha kupungua pia kwa umaskini wa mali.

**Kupambana na umaskini wa mali ni juhudi za kupatanisha mahusiano hayo manne ili watu waweze kutimiza wito wao wa kumtukuza Mungu kwa kufanya kazi na kukimu mahitaji yao na ya familia zao.** Kupambana na umaskini wa mali kunajumuisha juhudi nyingi zaidi za kuhakikisha kuwa watu wana mali na pesa za kutosha. Kunahusisha kazi ngumu zaidi ya kuwawezesha watu ***kupata mapato*** ya kutosha ili kukidhi mahitaji yao ya kimwili kupitia kwa kazi zao wenyewe za maana katika ulimwengu wa Mungu.

## Upatanisho na Mungu

Uhusiano wa mtu na Mungu ndio msingi wa mahusiano mengine yote. Kwa hivyo lengo muhimu zaidi ni kuwapatanisha watu na Mungu, na hapo ndipo tunapopaswa kuanzia.

**1 Petro 3:15-16**

*1. Je, unaweza kufikiria hali zozote ambapo lingekuwa jambo la hekima kuwasaidia watu wenye uhitaji wa kimwili kabla ya kuwahubiria injili?*

*2. Ikiwa watu watamkataa Yesu na kubaki katika umaskini wao wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho, je, kuna jambo lolote tunaloweza kufanya ili kuwasaidia kushinda aina zao zingine za umaskini?*

## Upatanisho na Nafsi

Upatanisho na nafsi unamaanisha mtu atakuwa na mtazamo sahihi kuhusu yeye mwenyewe, akijua kuwa ameumbwa kwa mfano wa Mungu, na kubarikiwa na karama na talanta.

## Upatanisho na Wengine

Tumeitwa kuwa na uhusiano wa upendo na majirani zetu kwa kufuata mfano wa upendo wa Mungu kwetu. Ni lazima tuonane kama watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu. Askofu Mkuu wa zamani wa Afrika Kusini Desmond Tutu aliwahi kusema – "Tunapowaona wengine kama adui, tunaingia kwenye hatari ya kuwa kile tunachochukia. Tunapowakandamiza wengine, tunaishia kujikandamiza wenyewe. Ubinadamu wetu wote unategemea kutambua ubinadamu ndani ya wengine."[1]

**Mathayo 5:9 na Warumi 12:17–21**

Kupitia kwa huduma ya Kanisa ya upatanisho na upendo kwa majirani, makanisa hujenga pia imani katika jamii. Umaskini unatawala pale ambapo hakuna imani katika jamii.

Sio tha kuuzwa

*Je, kanisa la kieneo hujenga imani katika jamii kwa njia gani?*

______________________________________________

## Upatanisho na Uumabji Wote

Upatanisho na uumbaji una sehemu mbili. Kwanza, inamaanisha kufanya kazi nzuri ulimwenguni kwa utukufu wa Mungu na kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya familia zetu. Tutasubiri na kuzungumzia hilo katika somo linalofuata. Pili, inamaanisha kutunza uumbaji wa Mungu kwa kuwa mawakili wazuri.

______________________________________________

______________________________________________

## Simulizi ya Anthony

Hii ni simulizi kutoka kwa mwandishi mwingine, Anthony, alipokuwa akijaribu kumsaidia ombaomba katika soko moja nchini Uganda.

> Kuna ombaomba ambaye nilimuona mara nyingi sokoni. Alionekana kuwa na uhitaji mkubwa. Nilikuwa nimempa chakula mara chache. Lakini siku moja niliamua kuzungumza naye. Nilimpata mfanyabiashara mmoja anifanyie ukalimani. Nilimsalimu ombaomba huyo kwa mkono, nikajitambulisha na tukawa na mazungumzo mafupi. Niligundua kuwa ana uwezo wa kutengeneza kamba kutokana na mifuko chakavu jambo ambalo mimi mwenyewe sikuwa najua kufanya. Nilimhakikishia kuwa ameumbwa kwa mfano wa Mungu na Mungu ndiye aliyempa karama na ujuzi wake. Kwa hivyo nilimnunulia mifuko iliyotumika kwa shilingi 3000. Kutokana na mifuko niliyompa, angetengeneza kamba za kutosha kupata kiasi cha shilingi 18000. Niliona kuwa ni bora kumsaidia afanye kazi ili apate chakula kuliko kumpa chakula ambacho kingemfanya awe katika hali ya kuombaomba. Nilizungumza naye kuhusu Mungu na nikagundua kuwa alikuwa Mkristo mwenzangu. Nilimhakikishia kuwa ana vipawa na hadhi, na kumtia moyo kurudi kufanya kazi kwa mikono yake. Nilijivunia kutumia saa moja kumsaidia mtu huyu badala ya kumpa kitu kidogo tu. Mara nyingine nilipoenda kwenye soko hilo sikumkuta na mfanyabiashara mmoja aliniambia kuwa aliacha kuwa ombaomba na alikuwa ameenda kuuza kamba. Lakini la kusikitisha ni kwamba, baada ya wiki chache alirudi kuombaomba tena. Sasa ninatambua kuwa ingawa kile nilichofanya kilikuwa bora zaidi kuliko kumpa kitu kidogo tu, haikutosha, na kulikuwa na mengi ambayo nilipaswa kufanya.

*1. Je, katika simulizi hii Anthony alifanya kitu gani vizuri?*

______________________________________________

*2. Je, Anthony alijaribu kusaidia kupatanisha mahusiano yote manne ya ombaomba huyo? Eleza.*

______________________________________________

*3. Je, Anthony alikosea wapi, au angefanya nini zaidi?*

______________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Kuzingatia Watu

Kwa vile tumeona kuwa kazi kuu ya kupambana na umaskini kwa hakika ni kazi ya upatanisho, basi hii ina maana kuwa kupambana na umaskini hakuhusu sana vitu vya kimwili, bali kunahusu watu.

---

**Isaya 58:10**

---

Mara nyingi, tunazingatia mipango badala ya watu. Tunatengeneza mipango kwa ajili ya watu masikini bila kuwashirikisha.

---

Ni lazima tuwashirikishe watu walio maskini wa mali. Ni lazima tujitahadhari na hali ya kujiona kama Mungu na tukumbuke kuwa sisi sote ni maskini, kwa njia tofauti. Sisi na maskini wa mali tunahitaji kumwendea Mungu pamoja ili kumwomba aturekebishe sote. Badala ya kutoa mipango yetu kwa watu maskini wa mali, tunahitaji kuwa pamoja nao tukimwomba Mungu atubadilishe sote.

Si ya kuuzwa

## Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Jaribu kufanya shughuli zote nne zilizo hapa chini, lakini chagua angalau shughuli mbili ambazo utahakikisha kuwa umezifanya.

1. **Kariri Isaya 58:10 peke yako. Ikiwa wewe ni kiongozi wa kanisa, tathmini na uone ikiwa kanisa lako lote litakuwa tayari kukariri pamoja nawe. Eleza kusanyiko kuwa tunahitaji kuzingatia kujenga mahusiano na maskini wa mali badala ya kuwatengenezea mipango ya haraka kila wakati.**
2. **Ili uweze kuwa na mtazamo mzuri zaidi, soma Zaburi 139 na utafakari kuhusu jinsi Mungu alivyokuumba kwa uangalifu na jinsi anavyokuthamini. Andika mambo matano ambayo unathamini kukuhusu, kuhusu mtu ambaye Mungu alikuumba uwe. Kisha mwambie mwanandoa mwenzako au rafiki yako mambo matano ambayo unathamini, kuhusu mtu ambaye Mungu alimuumba awe.**
3. **Ili kuboresha uhusiano wako na uumbaji wa Mungu, panda mti mahali fulani katika jamii yako au katika kanisa lako, hasa mahali ambapo patawanufaisha wengine zaidi kuliko wewe. Hakikisha kuwa umejengea ua mti huo ili usiharibiwe na wanyama.**
4. **Shiriki injili na angalau rafiki mmoja ambaye si Mkristo au mtu unayemfahamu ambaye si rafiki wa karibu.**

## Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

**Je, vifungu hivi vinatufundisha nini kuhusu kujenga mahusiano na maskini wa mali?**

**a. Mathayo 25:31–46**

---

**b. Luka 14:12–14**

---

**Je, unajenga mahusiano ya karibu na maskini wa mali katika kanisa au huduma yako au unazingatia mipango ya haraka tu? Eleza.**

---

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Msamaha

Msamaha ni mojawapo ya vipengele muhimu vya upatanisho. Msamaha ni muhimu sana katika kukabiliana na umaskini wa jamii na mahusiano yaliyovunjika.

**Tafakari kuhusu swali hili.** ***Je, inamaanisha nini hasa kumsamehe mtu?***

1. Msamaha unahusu moyo wako na hisia zako kwa mtu mwingine na si jinsi mtu mwingine anavyoitikia. Kwa hivyo, unaweza kumsamehe mtu hata ikiwa upatanisho kamili hauwezekani. Hatuwezi kudhibiti jinsi mtu mwingine anavyoitikia, lakini tunaweza kudhibiti itikio letu.
2. Msamaha unamaanisha kuwa tunajaribu kuwa na fikira nzuri kumhusu mtu mwingine. Tunamwachia Mungu hukumu ya mtu huyo, na tunamwomba Mungu ambariki mtu huyo. Tafakari kuhusu **Warumi 12:19-20.**
3. Tunakumbuka kuwa sisi ni wenye dhambi vilevile mbele za Mungu pamoja na mtu huyo mwingine. Tunasamehe kwa sababu tumesamehewa na Mungu. Kama vile Mungu ametuhurumia, tunawahurumia wengine pia. Soma **Waefeso 4:32.**
4. Mtu anaweza kuwa amesamehewa kweli lakini bado apate matokeo mabaya kwa matendo yake. Kwa mfano, muuaji anaweza kufungwa gerezani, lakini familia ya mwathiriwa inaweza kumsamehe muuaji kutoka mioyoni mwao huku muuaji akilazimika kubaki gerezani.

5. Tunaposamehe, tunapaswa kujaribu kusahau, ingawa hilo haliwezekani nyakati zote. Tunapaswa kujaribu kutoendelea kufikiria kuhusu kosa hilo na hatupaswi kulizungumzia tena na tena. Hatupaswi kushikilia uchungu wetu.
6. Msamaha unaweza kuwa mchakato mrefu ambapo tunaendelea kumwomba Mungu abadili moyo na hisia zetu juu ya mtu ambaye ametukosea.
7. Ikiwa sisi ni Wakristo wa kweli, tutawasamehe wengine. Mungu anasema kuwa ikiwa hatutawasamehe wengine, hatutasamehewa. Soma **Mathayo 6:14-15.**

Je, kuna mtu yeyote katika maisha yako ambaye unahitaji kumsamehe? Chukua muda wa kuomba sasa hivi. Muombe Mungu aubadilishe moyo wako umpende mtu huyo. Muombe Mungu akupe nguvu ya kumsamehe. Muombe Mungu ambariki mtu huyo na ampe neema na amani.

## Kuzingatia Watu na Upatanisho: Simulizi ya Hamida [2]

Hii hapa ni simulizi ya kutia moyo ambayo inatukumbusha kuzingatia watu na mahusiano badala ya mipango ya haraka.

> *Hamida anaishi nchini Malawi. Yeye na ndugu zake saba walihama ili wakae na nyanya yao baada ya wazazi wao kufariki. Hamida alimsaidia nyanyake katika biashara yake ya kukusanya na kuuza kuni. Ingawa Hamida alifanya kazi kwa bidii, walikuwa hawapati pesa za kutosha kwa ajili ya familia. Ndugu zake walilazimika kuacha shule. Wanaume walipoanza kumshawishi Hamida wakitaka kufanya naye mapenzi, alikataa mwanzoni. Lakini familia ilipozidi kuhitaji pesa, aliamua kujaribu ukahaba. Kwa zaidi ya miaka minne, Hamida aliutoa mwili wake utumiwe na wanaume kwa ajili ya kulisha familia yake.*
>
> *Shirika linaloitwa Word Alive lilitaka kumsaidia Hamida na wasichana wengine kama yeye katika jamii. Word Alive ilibuni kikundi cha wasichana ili wasaidiane wenyewe kwa wenyewe. Mwanzoni Hamida alikuwa na shaka. Lakini alijiunga na kikundi hicho na alifurahi kukutana na wasichana wengine ambao walikuwa wamepitia hali kama yake. Kikundi kikawa mahali salama pa kuuliza maswali na kujifunza mambo mapya. Walikuza uhusiano wa karibu sana. Kikundi hicho kilimhimiza Hamida kupimwa VVU na kumsaidia katika uamuzi wake wa kuacha kushiriki biashara ya ngono. Alipokea mafunzo zaidi na kujifunza jinsi ya kuongoza vikundi vidogo. Alianza kuwafundisha wasichana wengine kuhusu afya ya uzazi na mila za kitamaduni ambazo ni hatari kwa wasichana. Sasa Hamida ni mshauri wa rika na anaongoza kikundi cha wasichana 17. Amekuwa akiwasaidia wasichana wengine kuacha kushiriki biashara ya ngono na kutafuta kazi zingine za kufanya. Anapokea posho kidogo kutoka kwa Word Alive huku akitumia muda wake kuwashauri wasichana wengine. Yeye na wenzake wanapata mafunzo ya biashara na wanapanga kuanzisha biashara pamoja ili kujikimu wenyewe na familia zao.*

Tunaweza kujifunza kutokana na simulizi ya Hamida jinsi mahusiano ni muhimu. Ni lazima tuzingatie watu. Ingawa huduma ya Word Alive inahusisha mipango, kiini cha huduma yake ni kuhusu watu. Imewekea mkazo mahusiano kati ya washauri na wanarika. Mahusiano hayo ndiyo yaliyompa Hamida usaidizi aliyouhitaji ili kuwa na matumaini na kuona mabadiliko katika maisha yake.

Sio cha kuuzwa

---


Uchoraji wa mistari ulifanywa na Justin Lonas kutokana na picha iliyopigwa na Anthony Sytsma.

[1] Desmond Tutu, *God Has a Dream: A Vision of Hope for Our Time* (New York, Doubleday, 2004), 49-50.

[2] Taylor Smith, “Together Doing More: Breaking Barriers to End Hunger” (The Banner, Octoba 2017), 23-24, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.thebanner.org/issue/2017-10-01-000000

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

## Mwongozo wa Mshiriki




# Somo la 6: Usaidizi, Urekebishaji na Maendeleo

# Maswali ya Majadiliano ya Ufunguzi

*1. Je, ni katika hali gani ambapo tunapaswa kuwapa pesa watu wanaoomba msaada katika jamii zetu?*

---

*2. Je, ni katika hali gani ambapo mgeni kutoka nchi ya kigeni anapaswa kutoa pesa kwa watu katika nchi yetu?*

---

---

# Mhadhara wa Kiongozi

Hatua ya kwanza ni kuelewa hali hiyo na kubaini ikiwa inahitaji ***usaidizi***, ***urekebishaji***, au ***maendeleo.***

**Usaidizi** – Huu ni usaidizi wa dharura wa muda mfupi unaotolewa ili kupunguza mateso ya wakati huo kutokana na tatizo la asili au linalosababishwa na binadamu. Usaidizi hujaribu "*kukomesha kutokwa na damu*".

---

**Urekebishaji** – Urekebishaji huanza mara tu "damu" inapoacha kutoka. Hili ni jaribio la kuwarejesha watu na jamii zao katika hali ile ile waliyokuwa nayo kabla ya janga au dharura fulani.

---

---


***Maendeleo*** – Maendeleo ni mchakato wa mabadiliko unaowatoa watu kutoka kwenye hali waliokuwa hadi kwenye njia bora ya maisha kuliko walivyowahi kuwa hapo awali. Maendeleo ya Kikristo hayapaswi kuhusika tu na kuinua kiwango cha mapato ya watu, lakini yanapaswa kuzingatia hasa kusogeza watu karibu na kuwa katika uhusiano sahihi na Mungu, nafsi, watu wengine, na uumbaji wote. Kama ilivyo katika urekebishaji, maendeleo hayafanywi *kwa* watu, na hayafanywi *kwa ajili* ya watu, bali yanafanywa *kwa kushirikiana na* watu.

---

---

Sio cha Kuuzwa

## Mchoro[1]




Lakini maendeleo yanaweza pia kuwa njia ya kumsaidia mtu binafsi au jamii ambayo iko katika hali yao ya kawaida na haijapatwa na janga. Hakika, tunapotaka kuwasaidia watu wanaokabiliwa na umaskini, mara nyingi mbinu iliyo sahihi ni maendeleo, na katika hali nyingi, haitakuwa baada ya janga.

*Je, ni usaidizi, urekebishaji, au maendeleo:*

- *Tunapowafundisha watu mbinu mpya za usafi wa mazingira?*
- *Tunapompeleka mtu aliyeumwa na nyoka hospitalini?*
- *Tunapomsaidia mtu kujenga upya nyumba yake baada ya mafuriko?*
- *Tunapomtuma mmishonari kwa jamii kuhubiri injili?*
- *Mtoto mdogo ambaye alikuwa amelazimishwa kuingia jeshini anapotoroka na kurudi nyumbani, na tunampa ushauri nasaha?*
- *Tunapompata mtoto aliyetelekezwa akiwa na njaa na tukampa chakula?*
- *Tunapowapa wakulima sampuli ya mashina mapya ya muhogo ili wajaribu kuyapanda?*

Kati ya maitikio hayo matatu, usaidizi ni ule ambao kwa kawaida unahitaji kutolewa kwa rasilimali na pesa. Pesa na rasilimali zinaweza kutolewa au kutumika katika urekebishaji au maendeleo, lakini hii inapaswa kufanywa tu kwa njia ambayo inaenda sambamba na jinsi watu hao wanavyotumia mali zao wenyewe. Ikiwa pesa zitatumika katika urekebishaji na maendeleo, zitatumika kwa ushirikiano, wananchi wakisaidiwa pia kuchangia kile wanachoweza.

*Je, watu wasiokuwa na makazi katika mji wenu mkuu wanahitaji usaidizi, urekebishaji, au maendeleo? Jadili.*

________________________________________

________________________________________

# Kutoa Usaidizi, Kufanya Urekebishaji na Maendeleo Vizuri

## Usaidizi

**1. Usaidizi haupatikani mara kwa mara.** Kuna hali chache sana ambazo watu wanahitaji usaidizi.

**2. Usaidizi unapaswa kutolewa haraka.** Ikiwa watu hawawezi kujisaidia, basi hatua ya haraka ni muhimu. Ni vyema kupanga mapema. Shauri kanisa au shirika lako lifikirie kuhusu aina za majanga na matatizo ambayo watu katika jamii yenu wanaweza kukumbana nayo.

**3. Usaidizi ni wa muda mfupi.** Usaidizi hutolewa tu wakati ambapo watu hawawezi kujisaidia. Haitakuwa vyema kusitisha usaidizi wetu mapema sana. Lakini tukitoa usaidizi kwa muda mrefu sana, tunaweza kujenga utegemezi usiofaa ambao ni hatari. Sisi sote tunategemea watu wengine kwa mahitaji fulani. Hakuna ubaya katika hilo. Lakini utegemezi usiofaa ni wakati ambapo watu wanawategemea wengine kwa mahitaji ya kimsingi ambayo wanapaswa kuwa na uwezo wa kuyapata wao wenyewe. Wanaishia kuhisi kana kwamba hawawezi kuishi bila yule anayewapa rasilimali.

***Shiriki simulizi fupi kuhusu jamii au mtu ambaye alisalia katika utegemezi kwa sababu usaidizi ulitolewa kwa muda mrefu sana.***

## Urekebishaji

**1. Urekebishaji unafanywa *pamoja na* watu si *kwa ajili ya* watu.** Watu wanaosaidiwa wanapaswa kushirikishwa katika kubuni na kuendesha mpango.

**2. Fanya tathmini mwanzoni ili kupata ufahamu wa hali ya janga.**

**3. Chukua hatua wakati watu wenye uhitaji hawajasaidiwa tayari na wenyeji na mashirika ya eneo husika.** Hii ina maana kuwa tunasaidia tu wakati kuna hitaji na mashirika ya eneo husika hayawezi kusaidia au yanakataa kusaidia. Mashirika ya kieneo yanaposaidia, yanaweza kujenga mahusiano mazuri, umoja, na nia njema katika jamii. Ikiwa tutajaribu kusaidia kama watu wa nje wakati mashirika ya kieneo yana uwezo wa kusaidia, tunaweza kuwa kizuizi au, wakati mwingine, kukandamiza juhudi za kusaidia za

Sio cha kuuzwa


mashirika ya kieneo.

Tunaweza kuona kutokana na baadhi ya maandiko ya Biblia kuwa watu wa kwanza kuwajibika kumsaidia mtu ni wale watu wake wa karibu naye zaidi katika uhusiano wa kifamilia, kanisa, au eneo.

**1 Timotheo 5:8**

**Wagalatia 6:10**

## Miduara ya Kipaumbele




Wazo la miduara ya kipaumbele pia ni muhimu kwa sababu sote tuna muda na rasilimali adimu. Ikiwa hatuna mwelekeo wowote lakini tukajaribu kusaidia mara moja watu wote na shida zote tunazosikia, tutalemewa na kushindwa kabisa. Lakini miduara ya kipaumbele inatuonyesha pale ambapo majukumu yetu makubwa zaidi yapo. Bila shaka, tunapokuwa na uwezo, upendo wa Kristo bado unatulazimisha kujitoa kwa ajili ya kuwasaidia wengine walio mbali nasi.

## Simulizi Kuhusu Kutoa Kwa Furaha

Katika mwaka wa 2010, takriban nusu ya wakazi wa Nijeri walikuwa na uhaba wa chakula na walihitaji misaada fulani. Shirika la kimataifa la Kikristo lilitoa nafaka na kushirikiana na kikundi cha Kikristo cha kieneo, SEL, kuuza nafaka hiyo kwa watu wenye uhitaji katika jamii kadhaa kwa bei iliyopunguzwa sana. Hapo awali, wakati wa uhaba wa chakula, shirika la kimataifa lilikuwa limetoa nafaka ambazo zingetolewa

bila malipo kwa watu wenye uhitaji zaidi, kwa mfano watu wenye ulemavu au magonjwa sugu. Lakini wakati huu, wafanyakazi wa kimataifa walitoa changamoto kwa SEL kufikiria kuchangisha pesa ndani ya nchi kutoka kwa makanisa ili kununua nafaka ambayo ingetolewa kwa watu bila malipo. Mwanzoni, wanachama wa SEL walikuwa na shaka, wakifikiria kuwa hakuna chochote ambacho wao kama Wakristo maskini wangeweza kufanya wao wenyewe ili kuwasaidia wengine. Lakini Wakristo walitoa kwa ukarimu na waliweza kununua nafaka kwa ajili ya watu 98 ambao walikuwa na uhitaji mkubwa katika jamii kadhaa zilizosaidiwa na shirika la kimataifa. Mwishowe, SEL ilishukuru shirika hilo kwa kuwahimiza kuwasaidia wanajamii wao wenyewe. Walisema, "Ilikuwa ni fursa nzuri sana kusaidia, kujua kuwa hatukuwa tunasambaza msaada wa mtu mwingine tu, bali ulitoka mifukoni mwetu, na kutoka kwa mioyo yetu wenyewe. Kila mtu kijijini alijua kuwa msaada huo ulitoka kwetu."[2]

***Je, unadhani jamii hii ilibadilika vipi kwa sababu watu 98 walipewa nafaka na majirani badala ya wafadhili wa kigeni?***

______________________________________________

## Maendeleo

Maendeleo ni mchakato wa kuwahamisha watu kwenye njia bora ya maisha ambapo wanaweza kujikimu wenyewe na familia zao kwa kufanya kazi, na kuhakikisha kuwa wanakua katika uhusiano wao na Mungu, nafsi zao, watu wengine, na uumbaji. Tutaangazia kanuni za maendeleo katika somo linalofuata, na unaweza kusoma zaidi kuhusu maendeleo katika sehemu ya "Tafakari Zaidi" mwishoni mwa somo hili.

## Shughuli ya Kikundi Kikubwa – Mifano ya Usaidizi, Urekebishaji, na Maendeleo

Mifano ya Usaidizi:

______________________________________________

______________________________________________

Mifano ya Urekebishaji:

______________________________________________

______________________________________________

Mifano ya Maendeleo:

______________________________________________

______________________________________________

Sio cha kuuzwa

## Makosa ya Kawaida

Mojawapo ya makosa makubwa tunayofanya katika kupambana na umaskini ni kutoa usaidizi katika hali ambazo zinahitaji urekebishaji au maendeleo. Kutoa usaidizi kwa wale ambao hawauhitaji kunaweza kuwafanya wajihisi kutokuwa na uwezo na kuona aibu. Katika hali fulani, watakuwa wategemezi, wataacha kutafuta kazi ya kufanya, na kwa hiyo hawatatimiza kusudi la Mungu kwa maisha yao.

---

Kuna mambo kadhaa tunayohitaji kuzingatia kabla ya kumpa mtu usaidizi.

**1. Je, kuna dharura kweli?**

---

**2. Je, mtu huyo hajiwezi, au anaweza kuchangia katika uboreshaji wake wenyewe?**

---

**3. Je, mtu huyo alichangia vipi kwa hali yake?** Ikiwa watu hawajiwezi, basi tunapaswa kutoa usaidizi, iwe alichangia kwa kiasi fulani kuwa katika hali hiyo au la. Lakini ikiwa anajiweza, basi namna tunavyofanya urekebishaji au maendeleo inaweza kuamuliwa kwa kiasi fulani na kiwango ambacho mtu huyo alichangia kuwa katika hali yake. Kuwa na mazungumzo na watu ambao tabia zao za kutowajibika zimesababisha maumivu yao kunaweza kuwafanya watambue makosa yao na kujirekebisha.

---

*Je, kuna yeyote anayeweza kushiriki mfano wa wakati alipokataa kumpa mtu pesa ili mtu huyo ajionee matokeo ya kitendo chake kisicho cha busara na kujifunza kutokana na kitendo hicho?*

---

**4. Je, mtu huyo amekuwa akipokea usaidizi wa kiasi gani kutoka kwako au kutoka kwa wengine hapo awali?** Je, kuna uwezekano gani kwamba atapata usaidizi huo katika siku za baadaye?

---

Wageni wengi wanaozuru Afrika hutoa usaidizi katika nyakati zisizofaa, hivyo wanachangia matatizo ya aibu na utegemezi barani Afrika. Hii inaweza kuharibu kwa urahisi mipango na miradi ya wenyeji. Ikiwa Shirika Lisilo la Kiserikali litaamua kumpa kila mtu neti za kuzuia mbu bila malipo, inakuwaje kwa mtu wa eneo hilo ambaye anapokea mapato yake kutokana na kutengeneza na kuuza neti za kuzuia mbu? Kama Waafrika, tunahitaji kuwa tayari kuzungumza na kuwakabili wageni kwa upole tunapowaona wakitoa kwa njia isiyofaa na yenye madhara.

Ni muhimu kwa kanisa lenu kuwa na sera kuhusu wakati na jinsi ya kuwasaidia maskini wanaoomba usaidizi. Kwa njia hii kanisa halitashutumiwa kwa upendeleo kwa sababu ya kusaidia watu fulani na si wengine.

Si cha kuuzwa

## Majadiliano ya Kikundi Kikubwa

*Je, ni watu wa aina gani wanaohitaji kuendelea kupata misaada ya kifedha na rasilimali?*

Lakini watu wengi si wanyonge kabisa, kwa hiyo hawahitaji kuendelea kupata usaidizi. Na tunapowachukulia watu kuwa wanyonge, tunawadhuru zaidi kuliko kuwasaidia. Hata watu wengi katika kategoria tulizozungumzia wanaweza kufanya jambo fulani katika ulimwengu huu na kuwasaidia wengine, hata kama hawawezi kufanya hivyo ili kupata pesa.

## Simulizi ya Ombaomba Anayeitwa Eddy

# Kuepuka Ubaba

Kanuni ni: ***Tunapaswa kuepuka ubaba.***

Ubaba unamaanisha "kuwa kama baba". Kwa hivyo ubaba unamaanisha kutenda kana kwamba wewe ni mzazi na kuwachukulia watu unaowasaidia kama watoto wanaokutegemea.

Usiwafanyie watu ***mara kwa mara*** mambo ambayo wanaweza kujifanyia wenyewe. Katika kujaribu kutatua masuala ya umaskini, kuwafanyia watu maskini mambo mara kwa mara ambayo wanaweza kujifanyia wenyewe hujenga utegemezi, hupunguza kujistahi kwa watu, na hudumisha umaskini wao.

## Maigizo kuhusu Ubaba

***Unafikiri mtu aliyekuwa akisaidiwa alihisi vipi?***

sio cha kuuzwa

## Aina za Ubaba

**1) Ubaba wa rasilimali –** Huku ni kutoa rasilimali au pesa kwa watu wakati wanapata rasilimali zao wenyewe.

---

Wakati mwingine ni vizuri kuwapa watu kitu mara moja, hata kama wangeweza kujinunulia wenyewe. Ubaba wa rasilimali unamaanisha kuwa tunawapa watu rasilimali ***mara kwa mara*** ambazo wangeweza kupata wao wenyewe. Robert Lupton aliueleza vyema ubaba katika kitabu chake Toxic Charity (Uhisani Unaodhuru)[3] akisema: "*Mpe mtu usaidizi mara moja na atakushukuru; mpe mara mbili na ataanza kuutazamia; mpe mara tatu na ataanza kuwa na matarajio; mpe mara nne na ataanza kuhisi kuwa ni haki yake; mpe mara tano na utakuwa umejenga utegemezi*."

Njia moja rahisi ya kuepuka ubaba na kuepuka kujenga utegemezi ni kutoza ada ndogo kwa rasilimali ambazo ungependa watu maskini wapokee. Watachukua umiliki zaidi, watakuwa na heshima zaidi, na maoni yao yatasikilizwa.

**2) Ubaba wa kiroho –** Hapa ni pale tunapofikiri kuwa sisi tumekomaa zaidi kiroho kuliko watu maskini na kwa hivyo tunapaswa kuwa wenye kuhubiri au kuongoza maombi. Katika makanisa na mipango yetu, hatupaswi kuonyesha upendeleo kwa kuwapa nafasi za uongozi wale walio matajiri pekee. Mtu aliye maskini wa mali lakini tajiri wa imani, bado ana uwezo wa kuhubiri, kuongoza ibada, au kueneza injili.

---

**3) Ubaba wa maarifa –** Hapa ni pale tunapofikiri kuwa tuna mawazo bora zaidi kuhusu jinsi ya kufanya mambo. Wakati mwingine tuna maarifa muhimu tunayohitaji kushiriki na watu maskini wa mali, lakini tunapofanya hivyo, tuwe wazi kupokea mawazo yao pia.

---

**Simulizi kuhusu Ubaba wa Maarifa**

---

---

**4) Ubaba wa kazi –** Hapa ni pale tunapofanya kazi kwa ajili ya watu ambao wanaweza kujifanyia kazi wenyewe.

---

**5) Ubaba wa usimamizi –** Hapa ni pale tunapanga, kudhibiti, na kuelekeza shughuli za kusaidia jamii maskini wakati watu katika jamii hizo wangeweza kufanya mambo hayo wao wenyewe.

---

Sio cha kuuzwe

*Je, kuna yeyote aliye na simulizi kuhusu ubaba ambazo ungependa kushiriki, iwe katika familia yako, kanisa lako, jamii yako, au nchi yako?*

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi.

**1) Kwa Viongozi wa Kanisa**
Pamoja na viongozi wako wengine wa kanisa, mashemasi, na wafanyakazi, andika majina ya mashirika na makanisa yote unayoweza kufikiria katika jamii yenu ambayo yanajaribu kuwasaidia maskini. Je, wanatoa usaidizi, kufanya urekebishaji, au maendeleo? Je, watu katika jamii yenu wanahitaji usaidizi, urekebishaji au maendeleo? Je, kuna kutolingana kati ya kile ambacho mashirika yanafanya na kile ambacho watu wanahitaji? Je, kanisa lenu linawezaje kushughulikia kutolingana huku? Andaa mpango wa kile ambacho kanisa lako litafanya. Kisha shauri viongozi wako waeleze kanisa zima kuhusu mpango wako na lengo lako. Omba usaidizi na mwongozo wa Mungu katika huduma hiyo.

**2) Shughuli Mbadala kwa ajili ya Maendeleo au Wafanyakazi wa Serikali**
Fanya shughuli sawa katika #1, lakini na wafanyakazi wenzako. Jadili kile ambacho mashirika mengine yanafanya.

**3) Shughuli Mbadala kwa ajili ya Watu Wengine**
Chunguza mahusiano yako ya watu wa ukoo. Baini ikiwa wewe au wanafamilia wengine mna ubaba katika mahusiano yenu na wanafamilia wengine. Andaa mpango wa jinsi ya kushughulikia suala hili ili mabadiliko yaweze kufanywa.

Sio cha kuuza

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

1) Je, umewahi kujaribu kumsaidia mtu maskini bila kusikiliza kikweli maoni yake kwa sababu ulifikiri kuwa una ujuzi na masuluhisho yote? Eleza.

______________________________

2) Je, kanisa lenu lina ubaba katika huduma zenu zozote? Eleza.

______________________________

3) Je, unafahamu mipango yoyote ya serikali kwa ajili ya maskini ambayo inatumia hatua zisizofaa (kwa mfano – kutoa usaidizi wakati kile kinachohitajika ni maendeleo)? Je, unaweza kufanya vitendo gani mahususi ambavyo vinaweza kuanza kuleta mabadiliko fulani katika mipango hii?

______________________________

______________________________

4) Fikiria kuhusu maskini wa mali katika jamii yako. Je, watu hawa wanahitaji usaidizi, urekebishaji au maendeleo? Je, kanisa lenu limekuwa likisaidia kwa njia ifaayo?

______________________________

5) Je, wewe binafsi unatoa pesa zozote kwa mashirika katika jamii yenu ambayo yanafanya kazi nzuri kusaidia maskini? Ikiwa umejibu "hapana", basi kwa nini hutoi?

______________________________

______________________________

6) Ombeni pamoja. Tubu ubaba wowote na umwombe Mungu akuongoze na akupe uwezo wa kusaidia kwa njia sahihi.

______________________________

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Kanuni za Maendeleo Mazuri

**1. Maendeleo yanahusu aina zote tano za umaskini.** Usisahau kuwa maendeleo si kupunguza umaskini wa mali tu kwa kujenga barabara mpya, majengo mapya, na kuongeza mapato ya watu. Lengo halisi la maendeleo linapaswa kujumuisha watu kukua katika uhusiano wao na Mungu, nafsi

zao, watu wengine, na uumbaji. Lengo si kufanya nchi yetu iwe tajiri huku watu wakikosa maadili, wasio na furaha na wasiomcha Mungu. Lengo ni kumtukuza Mungu na kuwa na mahusiano mazuri.

**2. Ushiriki unaanzia mwanzo.** Kama ilivyo katika urekebishaji, maendeleo hufanywa ***pamoja na*** watu lakini ***si kwa ajili ya*** watu. Wananchi wanapaswa kushirikishwa katika kila sehemu ya mchakato huo. Usiingie tu kwenye jamii na uanzishe mradi. Kwanza wajue watu. Baini pamoja nao jinsi mradi unapaswa kuwa na kile wanachoweza kuchangia kwa mradi (fedha, wakati, talanta, vifaa, nk).

**3. Anza hatua kwa hatua.** Hakikisha kuwa mradi unaweza kusimamiwa zaidi na jamii wakiwa peke yao. Usifanye mradi wa maendeleo kuwa mkubwa kiasi kwamba hauwezi kuendelea peke yake bila kuendelea kupata usaidizi kutoka nje. Haitakuwa vyema kutegemea sana rasilimali za nje au watu wa nje. Itakuwa vyema kwa mradi uwe endelevu na uendelee hata baada ya ufadhili kutoka nje kukomeshwa.

**4. Wasaidie watu kujifunza jinsi ya kujifunza.** Badala ya kuwafundisha watu teknolojia moja mpya au mbinu mpya, wafundishe watu jinsi ya kujifunza na kufanya majaribio. Ni rahisi kumwambia mkulima atumie aina mpya ya mahindi, na anaweza kuitumia na kupata mafanikio. Lakini nini kitatokea ikiwa ugonjwa utaharibu mahindi hayo? Kisha mkulima anaweza kukusubiri tu urudi na kumwambia cha kufanya. Badala yake, tunataka kuwafundisha watu jinsi ya kufanya majaribio, kuwa wabunifu, jinsi ya kujifunza na kudhibiti hali tofauti. Kwa njia hiyo ugonjwa ukiharibu aina moja ya mmea, mkulima anaweza kujaribu mimea mpya peke yake bila kukusubiri urudi tena.

**5. Himiza jamii kuchangisha rasilimali zake yenyewe.** Jamii haiwezi kutegemea wafadhili kutoka nchi zingine au kutoka maeneo mengine ya nchi yenu kwa asilimia 100. Ikiwa pesa na rasilimali zote zinatoka maeneo mengine, watu wa eneo husika hawatahisi kushirikishwa katika mradi huo, hawatakuwa na hisia ya umiliki na hawatausimamia vizuri.

## Kubaini Wajibu Wako

Ni vigumu sana kwa mtu mmoja au kanisa moja kutekeleza hatua zote tatu za kukabiliana na umaskini katika jamii yenu – usaidizi, Urekebishaji na Maendeleo. Hatua zote tatu zinatofautiana sana na zinahitaji ujuzi na mipango tofauti, na zote huchukua muda. Ni vyema kulenga kundi moja au jamii moja ambayo unajaribu kusaidia. Kisha unapaswa kuzingatia kukidhi mahitaji ya usaidizi, mahitaji ya urekebishaji, au mahitaji ya maendeleo, lakini si yote matatu. Ikiwa kanisa lenu linajulikana kama mahali ambapo chakula cha bure hutolewa kwa wale wanaokihitaji sana (usaidizi), basi yamkini kanisa lenu si mahali ambapo juhudi zinafanywa ili kuwasaidia watu kupata kazi za maana (maendeleo). Ni bora kuzingatia suluhu moja na kuifanya vizuri. Makanisa na mashirika mengine yanaweza kuwa yanakidhi mahitaji mengine ambayo wewe huyakidhi. Kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Je, unawezaje kuamua kile ambacho kanisa lenu linafaa kufanya? Hatua ya kwanza ni kufahamu aina za huduma ambazo tayari zinatolewa na mashirika au makanisa mengine katika jamii yenu. Pili, fanya uchunguzi wa jamii yenu ili kubaini mahitaji ya maskini wa mali katika jamii yenu. Je, wako katika hatari ya kupoteza uhai wao kwa hivyo usaidizi unahitajika, au je, wanaweza kuchangia katika uboreshaji wao wenyewe? Mara nyingi watu katika jamii zetu hawahitaji usaidizi, bali wanahitaji maendeleo. Tunapendekeza uzingatie maendeleo baada ya kufanya kozi hii kwa sababu makanisa na mashirika mengi hayajafikiria kwa kina kuhusu masuala haya na mara nyingi hutoa usaidizi.

Sio cha kuuzwa

## Simulizi

1. Changanua simulizi hii na ufikirie jinsi inavyoonyesha umuhimu wa miduara ya kipaumbele uliyojifunza katika somo hili:

> Nchini Uganda, kulikuwa na makabila mawili yenye historia ya mgogoro. Kabila la Kaskazini Mashariki lilikuwa linaiba ng'ombe kila mara na kuua watu wakati wa mashambulizi dhidi ya kabila lililo magharibi mwa kabila hili la Kaskazini Mashariki. Baada ya miaka mingi ya serikali kuingilia kati na mipango ya kanisa, hatimaye amani ilipatikana, na upatanisho kati ya makabila hayo mawili ulipatikana. Mashambulizi yalikoma. Lakini muda mfupi baadaye, kulikuwa na njaa kali iliyokumba kabila la Mashariki. Baadhi ya makanisa ya kabila lililo magharibi mwa kabila hili la Kaskazini Mashariki yaliweka juhudi zao pamoja ili kuletea kabila la Kaskazini Mashariki chakula na rasilimali zingine. Walijua kuwa hatua hii ingeonyesha msamaha wao na upendo na kusaidia kuponya maumivu ya zamani. Hata hivyo, baada ya kukusanya rasilimali, usaidizi wa serikali ya Marekani ulifika haraka kabla ya wao kupeleka usaidizi wao. Marekani ilituma tani nyingi za chakula cha msaada, kiasi kwamba juhudi za kanisa la eneo hilo la Uganda zilikosa maana na kutohitajika. Wageni waliharibu fursa hii kwa kanisa la Uganda kutekeleza wajibu wao na uwakili mzuri, na kuharibu fursa hii ya kuonyesha upendo na msamaha na kujenga upatanisho zaidi kati ya makabila hayo mawili.[4]

2. Hii ni simulizi ya kutia moyo kuhusu upatanisho na huduma nzuri ya urekebishaji:

> Baada ya kuhudhuria Kongamano la Maono nchini Rwanda mnamo mwaka wa 1998, kasisi mmoja aliwapa changamoto waumini wa kanisa lake kuwasaidia wakimbizi waliokuwa wanarejea ambao walikuwa wamekimbia Rwanda kutokana na mauaji ya halaiki ya 1994. Washirika wa kanisa waliwakaribisha wakimbizi waliokuwa wakirejea, wakawasaidia kujenga upya nyumba zao, wakawaletea chakula na maji, na kuwasaidia watoto wao kurudi shuleni. Wakimbizi wa zamani walishangazwa na upendo wa kujitolea na ukarimu wa washirika wa kanisa. Washirika wengi walikuwa na marafiki au familia ambao waliuawa katika mauaji ya halaiki – na kulikuwa na uwezekano mkubwa kuwa wakimbizi waliokuwa wakirejea walijumuisha wahusika wa mauaji ya halaiki. Hata hivyo, Wakristo hao waliojitoa waliwakumbusha wale waliokuwa wakirejea kuwa upatanisho huja kwa kusikia Neno la Mungu na kuonyesha upendo wake kwa kuwapenda wale ambao hata wamewaua watu wa ukoo wetu.[5]

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na picha iliyopigwa na Chris Shiundu.

[1] Imetolewa kwenye Steve Corbett and Brian Fikkert, *When Helping Hurts: How to Alleviate Poverty Without Hurting the Poor... And Yourself*, 2nd edition (Chicago: Moody Publishers, 2012), 100.

[2] Simulizi hii imeshirikiwa katika mawasiliano ya kibinafsi, imetumiwa kwa ruhusa.

[3] Robert D. Lupton, *Toxic Charity: How the Church Hurts Those They Help and How to Reverse It* (San Francisco, Harper One, 2011), Kindle ed., Loc. 1438-43.

[4] Mawasiliano ya kibinafsi kutoka kwa Edward Etanu.

[5] Simulizi hii imesimuliwa na Simon Nizaramakena katika kitabu cha Scott Allen, Darrow L. Miller, and the African working group of Samaritan Strategy Africa, *Against All Hope: Hope for Africa* (Phoenix, Ariz., Disciple Nations Alliance, 2005), 52, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://disciplenations.org/resources/against-all-hope-hope-for-africa/.

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 7: Maendeleo ya Kijamii yenye Msingi wa Mali

# Maswali ya Majadiliano ya Ufunguzi

*Hebu fikiria mtu kutoka eneo au nchi nyingine anazuru na anataka kusaidia jamii yenu. Akikuuliza umwambie kuhusu jamii yenu, utasema nini?*

______________________________

______________________________

______________________________

# Maendeleo ya Kijamii yenye Msingi wa Mali

Sio cha kuuzwa

**Yenye Msingi wa Mali**

______________________________

**Jamii**

______________________________

**Maendeleo**

______________________________

**MJYMM** ni mchakato wa muda mrefu, unaoanzishwa na watu wa eneo husika katika jamii mahususi. Katika mchakato huu, wenyeji kwanza hutambua mali zao, kisha wanajaribu kutumia vyema mali zao kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe. Hii inasababisha mabadiliko makubwa katika jamii, ikijumuisha kupungua kwa umaskini wa mali, na kuboresha mahusiano na Mungu, nafsi, watu wengine, na uumbaji.

**Maendeleo Kulingana na Mahitaji**

______________________________

Tathmini ya mahitaji inaweza kuwa zana muhimu. Lakini ni muhimu kuzingatia mali za watu kwanza. Kisha, hatua inayofuata ni kuwauliza watu maswali haya: "Je, unaona matatizo gani ambayo lazima yatatuliwe? Je, unawezaje kutumia mali zako kushughulikia mahitaji hayo na kutatua matatizo hayo?"

Ikiwa sisi kama viongozi na wachungaji wa Kiafrika tunajaribu kusaidia jamii zetu wenyewe, tunahitaji kuanza kwa kutafuta mambo mazuri ambayo Mungu tayari anafanya katika jamii zetu. Na lazima tuangalie ili kutambua vipawa, rasilimali na fursa zaidi katika jamii, kisha kuwahimiza watu kuzitumia na kufanya kazi pamoja.

# Somo la Biblia – Mfano wa Talanta

*Je, tunajifunza nini kutokana na Mathayo 25:14-30? Je, kifungu hiki kinafundisha nini ambacho kinaweza kuhusiana na maendeleo ya jamii kwa namna fulani?*

## Simulizi ya Mchungaji Gideon

Kijana mmoja alimtembelea Mchungaji Gideon na kulalamika kuhusu umaskini wake. Alitaka mchungaji ampe pesa. Lakini Gideon alimuuliza kwanza, "Je, una nini?" Yule kijana akasema, "Sina chochote." Gideoni akasema, "Hapana, lazima una kitu hata kama ni kidogo. Je, una nini?" Kijana huyo akasema ana shilingi 1000 tu (takriban dola senti 30). Mchungaji alimwambia kijana huyo kwamba Mungu angeweza kumsaidia kutumia kiasi hicho kidogo cha shilingi 1000 kuleta maendeleo katika maisha yake, na hivyo mchungaji hakumpa pesa yoyote. Gideon alisema kuwa kijana huyo alikuwa na uwezo wa kununua na kuuza, alikuwa na afya nzuri ya kuweza kusafiri, hivyo anapaswa kwenda kununua asali katika eneo la kijijini kwao kisha asafiri kwa baiskeli umbali wa kilomita 15 hadi mji mkubwa ulio karibu ili kuuza asali kwa faida. Kwa hivyo kijana huyo alifanya hivyo. Alinunua asali kwa shilingi 1000, kisha akaiuza kwa shilingi 3500 mjini. Aligundua kuwa hii inaweza kuwa njia ya kuendelea kupata pesa, kwa hivyo aliendelea na baada ya safari kadhaa tu alikuwa amepata faida ya shilingi 35,000! Na alijihisi vizuri kupata pesa hizo kwa kutumia kile alichopewa na Mungu!

## Shughuli ya Kikundi Kikubwa – Hesabu ya Mali

Watu wengine hawatoi chochote kanisani au kwa watu wengine, na ukiwauliza sababu watajibu, "Sina cha kutoa." Au ikiwa tunataka mtu atambue mali zake ili tumsaidie, anaweza kusema, "Sina kitu na hakuna ninachoweza kufanya ili kubadili hali yangu. Unahitaji tu kunipa pesa." Kwa hivyo, mojawapo ya mambo muhimu tunayoweza kufanya ni kumsaidia mtu kuandaa kile kinachoitwa "**hesabu ya mali**", au watu wengine hukiita mchakato huo "**kufanya hesabu ya mali**". Tunaweza kufanya hivi na mtu binafsi, kanisa zima au jamii.

Sio kwa kuuzwa

*Tengeneza orodha ya mali katika jamii zetu:*

*Rasilimali za kifedha:*

*Mali tulizonazo:*

*Rasilimali watu:*

*Maliasili:*

*Maarifa na Ujuzi:*

*Taasisi na miundombinu ya eneo husika:*

*Rasilimali za kitamaduni na za kijamii:*

*Rasilimali za kiroho:*

*Eleza jinsi unavyohisi baada ya kuorodhesha mali hizi zote:*

*Je, ni mabadiliko gani yanaweza kutokea katika jamii yenu ikiwa utafanya zoezi hili pamoja na wanajamii wenu wote?*

Sio cha kuuzwa

# Kutafakari juu ya Maendeleo ya Kijamii yenye Msingi wa Mali

Si kweli watu wanaposema kuwa hawana chochote. Mungu ametupa sisi sote karama, rasilimali, na ujuzi mwingi. Kila mmoja wetu amebarikiwa na mambo tofauti.


Jukumu letu si kujilinganisha sisi kwa sisi, bali ni kuwa waaminifu na kile ambacho Mungu amempa kila mmoja wetu, na jamii zetu.

Ikiwa tutazingatia kile tulicho nacho badala ya kuzingatia kile ambacho hatuna, tutaweza kufanya mabadiliko na kukua. Ikiwa tutazingatia kile ambacho Mungu ametupa, maombi yetu yatajaa shukrani na furaha. Soma **1 Wathesalonike 5:16-18.**

Baada ya watu kutambua mali zao, hatua inayofuata, iliyo ngumu zaidi, ni kubaini jinsi ya kutumia rasilimali na ujuzi huo kuleta maendeleo na mabadiliko.

Simulizi ya John Mwangi jijini Nairobi:

***Tunahitaji mtazamo uliobadilika. Je, unaona nini?***



Sio cha kuuzwa

Utajiri na rasilimali si adimu wakati wote kama watu wanavyofikiria. Mtu mwingine akitajirika, haimaanishi kuwa lazima mimi niwe maskini. Si mashindano. Ikiwa tuna maparachichi mawili, si lazima tuyapiganie, lakini kila mmoja wetu anaweza kuchukua parachichi moja na kupata mti mzima wa maparachichi kutokana na hilo moja. Kupitia ubunifu, bidii, na ushirikiano sote tunaweza kuendeleza na kuzalisha mambo mapya zaidi. Kuna uwezekano wa uzalishaji wa ajabu wa utajiri kwa sababu ya jinsi uumbaji wa Mungu unavyofanya kazi.

***Je, hii ina maana gani?*** *"Unaweza kuhesabu idadi ya mbegu kwenye embe, lakini huwezi kuhesabu idadi ya maembe kwenye mbegu." – Methali ya Jadi ya Kenya.*

Tunahitaji kuwafundisha watu mtazamo mpya. Tambua ulichonacho, tumia mali ambazo Mungu amekupa, jenga juu ya rasilimali na ujuzi huo, na umtumainie Mungu kuzidisha juhudi zako kwa manufaa ya familia yako na ufalme wake.

# Kanuni za Maendeleo ya Kijamii yenye Msingi wa Rasilimali

**1) Tambua na utumie ujuzi na rasilimali za mtu binafsi au jamii.** Waangalie maskini wa mali kama watu wenye uwezo mkubwa waliopewa na Mungu. Wakati mwingine watu wana rasilimali na uwezo ambao wanaweza kuanza kutumia mara moja wakitiwa moyo. Lakini mara nyingi watu wanaweza kunufaika kutokana na mafundisho au mafunzo ya ujuzi ili kukuza uwezo wao waliopewa na Mungu.

---

**Simulizi ya Farida**

---

**2) Tafuta rasilimali na masuluhisho ya kutoka kwa mtu binafsi au jamii kadri uwezavyo, badala ya kutoka kwa watu wa nje.** Uliza maswali mazuri, na usikilize vyema watu na mawazo yao. Na uamini kuwa watu wanajali sana jamii zao na wanataka kuleta mabadiliko.

---

**3) Jaribu kujenga mahusiano kati ya watu binafsi, mashirika, makanisa, biashara, shule na serikali.** Mungu alikusudia watu binafsi na taasisi katika jamii zifanye kazi pamoja.

---

**4) Leta rasilimali kutoka nje ya jamii wakati rasilimali za ndani hazitoshi kutatua mahitaji muhimu.** Na uwe mwangalifu ili usilete rasilimali za nje mapema sana katika mchakato, na kuwa mwangalifu usilete nyingi sana. Ingawa usaidizi kutoka nje mara nyingi husaidia, ni lazima tuwe waangalifu ili tusidhoofishe juhudi za jamii za kutumia rasilimali na uwezo wao wenyewe.

---

**Simulizi kuhusu uchangishaji wa pikipiki huko Afrika Magharibi:**

---

Lao Tzu Mwanafalsafa wa Kichina wa Karne ya 6 alisema, "Nenda kwa watu. Ishi nao. Jifunze kutoka kwao. Wapende. Anza na wanachokijua. Jenga na walichonacho. Lakini tukiwa na viongozi bora zaidi, kazi itakapofanywa, kazi ikikamilika, watu watasema 'Tumefanya kazi hiisisi wenyewe.'"[1] Lakini tukiwa Wakristo, tunahitaji kuongeza, "Kwa usaidizi wa Mungu!"

Si pa cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi.

**1) Kwa Viongozi wa Kanisa**
Hubiri mahubiri kuhusu mfano wa talanta katika kanisa lenu. Kisha wakati wa ibada ya Jumapili au katika hafla tofauti ya kanisa, waagize washirika wote wa kanisa kutambua na kuandika mali na uwezo wa kanisa zima. Zungumza kuhusu rasilimali zinazoonekana na karama za kiroho. Jadilini pamoja jinsi ya kutumia vyema karama za kila mtu kwa manufaa ya kanisa na jamii.

**2) Kwa Watu Binafsi**
Fanya somo la kujifunza Biblia kuhusu mfano wa talanta pamoja na familia yako au na kikundi chako cha jamii. Tambua na uandike mali na uwezo wa familia yako, au mali na uwezo wa kikundi chako cha jamii. Jadilini jinsi mnavyoweza kuzitumia pamoja ili kushinda umaskini wa mali. Andaa mpango wa jinsi ya kushughulikia suala hili ili mabadiliko yaweze kufanywa.

# Zoezi la Kuchora la Kikundi Kidogo

*Katika vikundi vyenu, choreni picha ya jamii inayokua kimaendeleo. Msitumie maneno yoyote, tumieni picha pekee. Muwe wabunifu. Kumbukeni kuwa maendeleo yanapaswa kujumuisha kupunguza umaskini wa mali, na pia uboreshaji wa mahusiano yote manne.*

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Afrika Imebarikiwa

Sehemu ya kuwa na mtazamo uliobadilika ni kulitazama bara letu kwa njia tofauti. Kutokana na historia ya biashara ya utumwa, na kutokana na misaada yote kutoka kwa serikali za kigeni na wafadhili ambayo imetolewa kwa bara letu, wengi wetu wamekubali kabisa kuwa sisi ni maskini, hatujiwezi, na ni duni kuliko ulimwengu wote. Wengine tumewahi kujiuliza hata ikiwa Afrika imelaaniwa. Katika miaka iliyopita, baadhi ya wageni walidai kuwa Waafrika wamelaaniwa kwa kutumia Mwanzo 9:24-27, lakini huu ni uwongo. Waliiita "Laana ya Hamu". Lakini kwa kweli, laana katika kifungu hiki ilikuwa juu ya mwana wa Hamu, Kanaani, si Hamu. Kanaani alikuwa babu wa Wakanaani, kwa hivyo kifungu hiki hakiwahusu Waafrika. Ni kweli kwamba Hamu alikuwa na wana wengine ambao walikuwa mababu wa Waethiopia, Wamisri, na Walibia, lakini hawakuwa wamelaaniwa.[2] Na laana hiyo haikuhusu kabila, bali ilihusu jinsi Waisraeli wangewashinda Wakanaani waovu katika Nchi ya Ahadi.[3] Hatuko chini ya laana ya Kanaani, lakini hata kama tungekuwa chini la laana hiyo, tunapata baraka ambayo inashinda laana hiyo na laana nyingine yoyote mara tunapomjua Kristo. Yesu ana nguvu kuliko laana zote. Kifo na ufufuo wa Yesu hushinda hata laana ya asili ya kifo.

Ukweli ni kwamba Mungu amelibariki bara la Afrika sana. Baadhi ya mali ambazo Mungu amezipa Afrika ni pamoja na: turathi nyingi za kipekee za kitamaduni, idadi kubwa ya watu, maliasili kama vile mafuta na madini (kwa mfano – almasi, dhahabu, na koltani pia, madini adimu sana yanayotumiwa kutengenezea simu za mkononi), wanyama maridadi na mbuga za kitaifa, baadhi ya mito mikubwa zaidi ulimwenguni, kilimo chenye tija, na eneo kubwa la ardhi.

Afrika ni tajiri wa zawadi kutoka kwa Mungu. Jambo la kusikitisha ni kwamba wakati mwingine rasilimali hizi zimekuwa zikitumiwa vibaya na wageni, au kusimamiwa vibaya na viongozi fisadi wa Afrika. Lakini ni lazima tutambue kiasi ambacho Mungu amelibariki bara letu na kutumia vyema kile ambacho ametupa kwa kufanya kazi pamoja. Kufanya hivi ni tumaini letu bora zaidi la kushinda utegemezi wa bara letu kwa misaada kutoka kwa mataifa ya kigeni. Misaada inaweza kusaidia na bado tunaweza kushirikiana na nchi za nje tunapojaribu kusaidia watu wetu, lakini hatupaswi kubaki kutegemea misaada hiyo. Si suluhisho la muda mrefu na endelevu, wala misaada si kitu kinachojenga heshima ya watu wetu. Ikiwa tunataka kuwa watiifu kwa Mungu kwa kuwa mawakili wazuri, ni lazima tujifunze kuzingatia na kutumia zawadi ambazo Mungu ametupa. Ni lazima tuwajibike kwa maendeleo ya jamii na mataifa yetu wenyewe.

## Simulizi za Kutia Moyo Kuhusu Maendeleo yenye Msingi wa Mali

1. Nchini Uhabeshi, Kanisa la Kale Heywet katika eneo la Arba Minch lilipata njia ya kutumia rasilimali kidogo walizokuwa nazo kupata faida nzuri kwa kanisa. Hapo awali, walipewa ardhi ya kanisa na serikali. Serikali ilisema kuwa ardhi hiyo ilikuwa imejaa mawe na hakuna mtu ambaye angeweza kufanya chochote nayo. Kwa hivyo viongozi wa serikali waliona vyema kupeana ardhi hiyo. Ardhi hiyo ina ukubwa wa hekta 20 na juu yake imejaa miamba mikubwa. Lakini mmoja wa viongozi wa kanisa alitambua kuwa miamba hiyo inapaswa kuangaliwa kama mali, si kama laana. Aliona kuwa labda miamba hiyo inaweza kuuzwa kwa miradi ya ujenzi. Yeye na viongozi wengine walipanga na kutafiti jinsi jambo hilo lingeweza kufanywa. Hii leo magari ya ujenzi yanaweza kuonekana kwenye ardhi hiy ya kanisa yakivunja miamba ili kuuzwa. Sasa kanisa linafurahia faida ya mara kwa mara kutoka kwa miamba hiyo! Kwa mtazamo mpya, mambo ambayo baadhi ya watu wanaona kuwa hayana thamani yanaweza kuonekana kuwa ni mali iliyotolewa na Mungu.[4]

2. Hellen na mumewe wanaishi katika Kaunti ya Turkana nchini Kenya, mahali kame na penye joto na hakuna umeme. Yeye na mume wake wote ni vipofu kiasi lakini wanalisha watu kumi na watano katika nyumba yao kila siku. Je, wanawezaje kufanya hilo? Hellen alijiunga na VSLA (Muungano wa Akiba na Mikopo wa Kijijini) mnamo mwaka wa 2015. VSLA inaweza kuwa kama benki inayofadhiliwa na kusimamiwa na jamii. Wanachama huhimizana, kuweka akiba pamoja, na kupeana mikopo yenye riba nafuu. VSLA inawawezesha watu kutumia rasilimali kidogo walizo nazo, na kuzizidisha kwa kushirikiana pamoja. Hellen alitumia mkopo wake wa kwanza kununua mashine ya kunyoa na kuanza biashara ya kinyozi akipata takriban dola 4 za Marekani kwa siku. Baada ya kulipa mkopo huo aliendelea kuweka akiba. Kisha akachukua mikopo mingine miwili ili kununua sola, televisheni, mashine ya video, spika, kikuza sauti na betri, ambayo aliitumia haraka kufungua biashara ya kuonyesha video na biashara ya kuchaji simu, ambayo imeongeza dola 4-10 zingine kwa siku kwa mapato ya kaya yake. Baada ya kulipa mikopo hiyo, alichukua mkopo mwingine wa kununua mabomba ya maji ya kuleta maji nyumbani kwake ili familia yake ipate maji kila wakati. Sasa yeye huuza maji kwa majirani zake pia na hupata dola 1-2 kwa siku.

   Mume wa Hellen alichochewa na mafanikio hayo. Kwa vile VSLA ilikuwa imefika kikomo chake cha kutoa mikopo,, alichukua mkopo kutoka kwa benki na, pamoja na akiba ya Hellen, wamewekeza katika mradi mwingine wa biashara kwa kununua mashine ya kusaga mahindi. Usagaji wao huleta takriban dola 4-8 za Marekani, kwa siku. Biashara tano za Hellen zimeongeza dola 24 za Marekani kwa siku kwa mapato ya familia yake. Maisha yake yamebadilika. Anaweza kumudu kulisha, kuelimisha, na kuvisha familia yake kubwa, na kutoa kwa furaha kwa kanisa. Hellen anatiwa moyo na mafanikio yake na hayuko tayari kuacha kujitahidi; ana mipango ya kuwekeza kwenye tanki la maji. Simulizi hii inatuonyesha njia moja ya kuwasaidia watu kuzidisha rasilimali kidogo walizonazo ili waweze kujikimu. Tutaangazia VSLA katika somo lijalo.[5]

3. Dinnah, anayejulikana pia kama "Termite (Mchwa)", anaishi karibu na jiji la Soroti nchini Uganda. Kabla ya kumjua Kristo, alikuwa mlevi sana. Alitengeneza pombe na alikuwa akinywa na kuvuta sigara kwa hadi saa 12 kwa siku. Leo hii anaangalia nyuma na kuhisi maisha hayo hayakuwa na manufaa yoyote na yalikuwa yamejaa uchungu na ugomvi na watu wengine. Lakini katika mwaka wa 2010, alimjua Yesu kibinafsi. Maisha yake yakabadilika kabisa! Alijawa na furaha na amani, na akafanya amani na watu wa familia yake pia. Lakini aliendelea kuwa maskini wa mali, hasa kwa kuwa aliacha kutengeneza pombe. Baada ya kuhudhuria somo la kujifunza Biblia kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa mikono yake, alijua kuwa alihitaji kutafuta kazi itakayompa mapato. Alijaribu kufikiria sana kuhusu rasilimali na ujuzi ambao Mungu alikuwa amempa ambao angeweza kuutumia kujipatia mapato. Aliona vilima vya mchwa kote katika eneo la jamii yake, na alipokuwa mtoto alifunzwa jinsi ya kushika mchwa kutoka kwenye vilima. Aliamua kushika mchwa na kukaanga ili kuwauzia watu. Baadhi ya watu katika jamii yake hufikiria aina hiyo ya kazi kuwa ya aibu. Lakini maisha na mafanikio yake yanathibitisha kuwa mtazamo wa watu hao si sahihi. Dinnah alianza kupata pesa nyingi hasa kwa kuwa alikuwa na njia yake ya kipekee ya kupika: mchwa wa kukaanga na vitunguu na viungo. Ameweza kukidhi mahitaji yote ya familia yake kupitia kwa

Sio cha Kuuza

kuuza mchwa hao, na sasa ni biashara yake ya kawaida. Amejenga nyumba kutokana na mapato yake na kuwalipia watoto wake karo ya shule. Sasa watu katika kanisa na jamii yake wanamwita "mbarikiwa" na wanavutiwa naye kwa sababu ya mabadiliko katika maisha yake. Watu humwita "mchwa" kwa upendo katika lugha ya eneo hilo. Mwandishi, Anthony, ni mmoja wa wateja wake na anaweza kushuhudia kuwa anaweza kupika kweli kweli!

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na picha iliyopigwa na Tabitha Kapic.

[1] Traditional. Imenukuliwa katika "Transformation: An Asset-Based Approach to Engaging Church and Community", (New York, Episcopal Relief, 2015), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://calledtotransformation.org/team-building/called-to-facilitation/.

[2] Tokunboh Adeyemo, ed., *Africa Bible Commentary* (Nairobi, Grand Rapids, WordAlive/Zondervan, 2010), 25.

[3] See K. A. Matthews, *Genesis 1-11:26*, Vol. 1A, (Nashville, B&H Publishers, 1996), 423.

[4] Inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://reedsinthewind.blogspot.com/2018/08/when-life-gives-you-lemons.html.

[5] Muhtasari kutoka David Kangangi, "Entrepreneurial Spirit Activated", (World Renew, Desemba 2017), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://worldrenew.net/our-stories/team/entrepreneurial-spirit-activated.

Sio cha kuuzwa

## Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# MWONGOZO WA MSHIRIKI




# Somo la 8: Tathmini ya Zoezi la Ufunguzi

Sio cha Kuuzwa

# Tathmini

*Je, tunapaswa kuwa tayari kusikiliza watu wengine wanaokosoa na kutathmini huduma na mipango yetu kwa nini?*

________________________________________

________________________________________

**Mithali 12:15** na **Mithali 19:20:**

________________________________________

*Je, tunapaswa kuwa na mtazamo wa aina gani tunapotathmini huduma na mipango ya watu wengine?*

________________________________________

________________________________________

**Waefeso 4:29** na **1 Wakorintho 13:1-2:**

________________________________________

Si jambo la kawaida kwa Wakristo kuwajibishana kuhusu njia ifaayo ya kuwatunza maskini, lakini ni lazima tuseme ukweli kwa upendo na kwa unyenyekevu.

________________________________________

________________________________________

**Waefeso 4:2-3:**

________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Ukaguzi wa Tathmini ya Zoezi la Ufunguzi

Rejelea ukurasa wa 9 na 10 ili kuona hali inayozingatiwa.

## Maswali ya Tathmini

1) *Taja baadhi ya mambo mazuri unayoyaona kwenye mipango yako. Je, ulipanga vyema kwa njia gani?*

2a) *Je, ulishughulikia umaskini wa mali katika mipango yako? Eleza.*

2b) *Je, ulishughulikia umaskini wa kukosa uhusiano wa karibu wa kiroho katika mpango wako? Eleza.*

2c) *Je, ulishughulikia umaskini wa jamii katika mpango wako? Eleza.*

2d) *Je, ulishughulikia umaskini wa nafsi kwenye mpango wako? Eleza.*

2e) *Je, ulishughulikia umaskini wa uwakili katika mpango wako? Eleza.*

3) *Je, unaona ushahidi wowote wa hali ya kujiona kama mungu katika mpango wako, (kufikiri kuwa wewe ni bora au mwenye akili zaidi kuliko watu ambao ulikuwa unajaribu kuwasaidia)?*

4) *Je, katika mpango wako, ulizingatia watu, upatanisho, na kujenga mahusiano kwa muda mrefu? Au ulizingatia mipango mifupi tu ya kusaidia maskini haraka iwezekanavyo?*

5a) *Je, katika mpango wako ulikuwa unaitikia mahitaji ya watu kwa kuwapa usaidizi, urekebishaji au maendeleo?*

Sio cha kuuzwa

5b) *Baada ya yale uliyojifunza, unafikiri watu wanahitaji nini hasa – usaidizi, urekebishaji, au maendeleo?*

6) *Je, katika mpango wako unaona ubaba wowote (kuwafanyia watu mambo ambayo wangeweza kujifanyia wao wenyewe)?*

7a) *Je, uliwahimiza watu kutambua karama na mali zao?*

7b) *Ikiwa ulitoa rasilimali, je rasilimali hizo zilitoka kwa jamii ya eneo hilo au wafadhili kutoka nje?*

8) *Je, umejifunza nini kuhusu wewe mwenyewe au kuhusu kanisa lako kutokana na zoezi hili?*
Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Nenda nyumbani na mpango wako wa huduma ulioandikwa ambao ulitathmini wakati wa somo hili, pamoja na madokezo yako na majibu kwa maswali ya tathmini. Fanya mkutano na viongozi wenzako wa kanisa au wafanyakazi wenzako. Kwa kipindi cha miezi kadhaa ijayo, rekebisha mpango wako wa huduma na urekebishe makosa yoyote uliyofanya kwa kutumia yale ambayo umejifunza katika Somo la 1-7. Boresha mpango wako kisha nenda na ujaribu kuutekeleza katika kanisa lako na jamii.

Tafadhali usifanye hilo peke yako, bali hakikisha kuwa unashirikiana na jamii au kanisa lako. Mkabidhi Mungu mpango wako na uendelee kuomba mwongozo wake. Piga hatua kwa imani na ujasiri ukiamini kuwa Mungu wetu mwenye nguvu atakuwa pamoja nawe na kukutumia kwa njia kuu kuleta mabadiliko katika maisha ya watu katika jamii yako!

Sio cha kuuzwa

# Shuhuda, Tathmini, na Maombi

Unahimizwa kupanga muda na kiongozi wako ili kukamilisha masomo yaliyobaki. Hii itakusaidia kupata mafunzo ya kina zaidi kuhusu jinsi ya kupambana na umaskini katika maisha yako mwenyewe na katika makanisa na jamii zenu. Ni lazima ukamilishe masomo yote yaliyosalia ili uweze kufuzu kupata cheti cha ukamilisho. Cheti hicho kinahitajika ili uwe kiongozi wa *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika*.

Masomo Yaliyosalia:

Somo la 9: Kufanya Kazi kwa Utukufu wa Mungu
Somo la 10: Mabadiliko ya Mtazamo wa Ulimwengu
Somo la 11: Mifumo Iliyovunjika
Somo la 12: Injili ya Mafanikio
Somo la 13: Utamaduni wa Kiafrika na Pesa
Somo la 14: Mabadiliko Katika Maisha ya Mtu Husababishwa na Nini?
Somo la 15: Ushiriki wa Jamii
Somo la 16: Huduma ya Ukarimu ya Kanisa
Somo la 17: Huduma ya Mijini: Fursa na Changamoto
Somo la 18: Safari za Misheni ndani ya Afrika
Somo la 19: Wageni, Wamisionari na Wafadhili
Somo la 20: Miradi ya Mbegu na Rasilimali Zaidi

Kumbuka kwenda nyumbani na kutekeleza yale uliyojifunza, hasa **shughuli za Kufanya Baada ya Somo**! Mungu akubariki na kukutia nguvu katika shughuli hizo! Pia, chukua muda nyumbani kusoma sehemu za "**Tafakari Zaidi**" za kila somo. Endelea kukagua Somo la 1-7 hadi kipindi chetu kijacho cha mafunzo.

## Shuhuda

## Maswali ya Tathmini

**1)** ***Je, kuna jambo lolote ambalo tumelijadili ambalo limekukanganya? Je, una chochote unachotaka kusaidiwa kuelewa kabla hatujaondoka?***

**2)** ***Je, ulifurahia masomo au shughuli gani zaidi katika masomo hadi hapa tulipofika sasa?***

(*Maswali yanaendelea kwenye ukurasa wa 87*)

Sio cha kuuzwa

3) *Je, unapanga kukamilisha masomo yaliyosalia katika* Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika? *Kwa nini ufanye hivyo au kwa nini usifanye hivyo?*

---

4) *Je, ni nini kinaweza kuboreshwa katika mafunzo haya au katika uongozi wangu?*

---

5) *Je, unaweza kupendekeza mafunzo haya kwa rafiki? Kwa nini ufanye hivyo au kwa nini usifanye hivyo?*

---

## Maombi

***Tafadhali kuwa huru kutuma barua pepe moja kwa moja kwa waandishi ukiwa na maswali na ushuhuda:**

Jonny: jonny.kabiswa@chalmers.org Anthony: anthony.sytsma@chalmers.org

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na picha iliyopigwa na Tabitha Kapic.

Sio cha kuuzwa

# *LA HIARI* Ushuhuda wa Maandishi na Tathmini

(Mpe kiongozi wako ukurasa huu baada ya mafunzo)

Ushuhuda

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Tathmini

1) *Je, ulifurahia masomo au shughuli gani zaidi katika masomo hadi tulipofika sasa?*

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

2) *Je, unapanga kukamilisha masomo yaliyosalia katika* Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika? *Kwa nini au kwani sivyo?*

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3) *Je, ni nini kinaweza kuboreshwa katika mafunzo haya au katika uongozi wangu?*

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4) *Je, unaweza kupendekeza mafunzo haya kwa rafiki? Kwa nini au kwani sivyo?*

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Maoni ya Ziada

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

## Mwongozo wa mshiriki

Sio Cha Kuuzwa



# Somo la 9: Kufanya Kazi kwa Utukufu wa Mungu

# Maswali ya Majadiliano ya Ufunguzi

*Je "kazi" ni nini?*

*Je, kazi ni zawadi au adhabu?*

# Mhadhara wa Kiongozi

## Kazi katika kitabu cha Mwanzo

Kazi nyingi hufanywa ili kulipwa pesa lakini kazi zingine hufanywa bila malipo.

**Mwanzo 2:1-3**

**Mwanzo 1:31**

**Mwanzo 1:28, 2:15**

Kazi ilikuwa zawadi kutoka kwa Mungu ili Adamu na Eva wawe na maisha yenye kusudi. Kwa kuwa Mungu ndiye muumbaji, watu walioumbwa kwa mfano wake wanaendelea pia kuumba vitu vipya.

Tatizo la kazi zetu leo hii lilianza wakati wa Adamu na Eva katika bustani.

**Mwanzo 3:17–19**

Kazi ingali zawadi japo imekuwa ngumu. Kazi ni shughuli ya kiungu.

Sio cha kuuzwa

Utafiti wa hivi karibuni umeonyesha kuwa watu walio na kazi ya kufanya wana furaha zaidi kuliko wale wasio na kazi ya kufanya.[1] Tunahitaji kazi.

---

Tunaweza kuwa na matumaini katika kazi zetu. **Zaburi 104:10-14.**

---

Baadhi ya watu na tamaduni barani Afrika zimeona kazi kuwa laana au adhabu. Hii ni mojawapo ya imani inayosababisha watu wengi walio maskini wa mali kusalia katika umaskini wao.

*Je, unafahamu watu au jamii zozote zilizo na imani hii?*

---

Ili kuwasaidia maskini wa mali, tunahitaji kujaribu kupatanisha uhusiano wao na uumbaji wa Mungu. Hilo linamaanisha kuwa tunajaribu kuwasaidia maskini wa mali wapate kazi ya maana ya kufanya katika ulimwengu wa Mungu, kazi ambayo inaweza kuwasaidia kujikimu kifedha wao na familia zao. Tunataka wawe na kazi ya kufanya ili wawe watu ambao Mungu aliwakusudia wawe, watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu wanaofanya kazi jinsi Mungu afanyavyo.

---

Kuwasaidia watu kupata kazi kunaweza kujumuisha kuwatia moyo kutumia mali na ujuzi wao, na wakati mwingine kunamaanisha kuwaelimisha na kuwapa mafunzo ya ujuzi mpya.

## Kufanya Kazi kwa Utukufu wa Mungu

*Je, kufanya kazi kwa utukufu wa Mungu kunamaanisha nini?*

*Kiutendaji, sisi tukiwa Wakristo tunapaswa kufanyaje kazi tofauti na wengine, kwa njia inayomheshimu Mungu?*

---

---

**1 Wakorintho 10:31**

---

---

Sio cha kuuzwa

## Njia za kufanya kazi kwa Utukufu wa Mungu

1. Fanya kazi ili kumpendeza Mungu si watu. **Wakolosai 3:23-24.**

Mwanamageuzi Mjerumani Martin Luther akizungumzia kazi ya mzazi – "Mungu, pamoja na malaika wake na viumbe wote, wanatabasamu – si kwa sababu baba huyo anafua nepi, bali kwa sababu anafanya hivyo kwa imani ya Kikristo."[2]

*Je, Martin Luther anamaanisha nini kwa kauli hii?*

2. Mwangalie Yesu kama kielelezo chetu katika kazi. **Yohana 5:17.**

3. Mkabidhi Mungu kazi zako. **Mithali 16:3.**

4. Tufanye kazi ili kukidhi mahitaji yetu wenyewe na ya familia zetu. **Matendo 20:34** na **1 Timotheo 5:8.**

Mtume Paulo aliweka wazi kuwa si vizuri kwetu kuwategemea wengine, bali ni vyema kwetu kufanya kazi. **1 Wathesalonike 4:11-12**

5. Tufanye kazi ili tusijaribiwe kutenda dhambi. **Waefeso 4:28.**

*Je, baadhi ya sababu zinazofanya watu waibe katika jamii yenu ni zipi?*

Sio cha kuuzwa

6. Fanya kazi kwa bidii. **Mithali 10:4.**

7. Tutumie karama na ujuzi ambao Mungu ametupa. **1 Petro 4:10.**

8. Fanya kazi bora. Mungu ndiye Muumbaji ambaye aliita uumbaji "mzuri". Tunamheshimu tunapofanya kazi nzuri pia. Tunapaswa kufanya kila tufanyalo kwa bidii na vizuri.

***Fikiria kuwa wewe ni mmiliki wa duka. Je, ni hatua gani inayompa Mungu utukufu zaidi, kuendesha biashara yenye faida nzuri au kuliita duka hilo "Praise Jesus Supermarket (Duka Kubwa la Msifuni Yesu)", au zote mbili? Jadili.***

9. Usidharau aina fulani za kazi. Katika baadhi ya maeneo barani Afrika, kuna wazo kuwa kazi ya mkono ni duni kuliko kuwa na kazi ya ofisini. Katika kanisa, mara nyingi watu huwaona wachungaji kuwa watu wanaofanya kazi muhimu zaidi kuliko watu wote wengine. Usiwadharau wale ambao wana kazi iliyo tofauti na yako au wanaopata pesa kidogo.

***Je, ni aina gani ya kazi inayoonekana kuwa duni katika jamii yenu? Je, mtazamo huu unachangia umaskini wa mali?***

Sio cha kuuzwa

10. Fanya kazi kwa shukrani na uifurahie. **Mhubiri 2:24–25.**

11. Wapende watu wengine katika mahali pa kazi.

12. Tutunze vyema uumbaji wa Mungu tunapofanya kazi.

13. Fanya kazi kwa kufuata sheria. Ni lazima tutii hata kama hatuko kwenye hatari yoyote ya kupatikana, hata kama sheria hazitekelezwi, na hata kama kila mtu anakiuka sheria.

**Warumi 13:1-2**

Tukikosa kufanya kazi yetu kwa uadilifu, tunamkana Kristo kupitia kwa matendo yetu. **Tito 1:16.** Hakika tunakuwa wanafiki kwa kuwatangazia watu kuwa sisi ni Wakristo, lakini hatuishi kama Wakristo.

***Je, ni kanuni na sheria zipi ambazo hazifuatwi katika eneo lako la kazi na katika taifa lenu? Je, Wakristo wanazitii?***

14. Tuwabariki wengine kwa matunda ya kazi zetu. Mungu aliumba ulimwengu ili kazi zetu ziwafaidi watu na jamii kwa jumla. Mungu anatuita tuwe mawakili wazuri wa yale aliyotubariki nayo kwa kutoa msaada wa kifedha kwa wengine. **Matendo 20:35.**

15. Chukulia mahali pa kazi kama mahali pa misheni.

16. Pumzika kutoka kwa kazi. **Kutoka 20:8-11.** Sabato ilikuwa zawadi kutoka kwa Mungu kwa watu wa Israeli. Leo, tunaabudu Jumapili, Siku ya Bwana, badala ya Jumamosi, kwa sababu Jumapili ndiyo siku ambayo Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Lakini kanuni ya kupumzika siku ya Sabato inapaswa kutumika kwa siku ya Jumapili.

Baadhi yetu hatupumziki kwa sababu tunatafuta utajiri. Wakati mwingine, kufanya kazi kupita kiasi ni ishara ya dhambi ya kiburi. Tunapenda hisia ya kuwa muhimu na wenye kuhitajika.

Kupumzika kunaonyesha kuwa tunamwamini Mungu kutupa mahitaji yetu.

***Je, kufanya kazi kupita kiasi ni tatizo kwako? Je, tunapaswa kubadilika vipi?***

Sio cha kuuzwa

17. Fanya kazi kwa uaminifu na uadilifu. Ikiwa tutakosa kuwa waaminifu katika mambo madogo, tutakosa kuwa waaminifu katika mambo makubwa pia. **Luka 16:10-12.**

____________________________________________

Uadilifu na uaminifu wetu ni muhimu pia kwa sababu unaweza kuwafanya wengine kumjua Kristo. **1 Petro 2:12.**

____________________________________________

Kudumisha uadilifu wetu kunaweza kutuletea mateso. **1 Petro 4:12-16.**

____________________________________________

# Simulizi ya Daniel[3]

Daniel alilelewa katika familia maskini sana huko Ethiopia. Danieli aliokoka akiwa na umri wa miaka ishirini. Kwa kutia bidii shuleni akiwa kijana, aliweza kwenda chuo kikuu ambako alipata shahada ya Uhasibu. Baada ya kuhitimu, Daniel alituma maombi kadhaa ya kazi, lakini wakati wa mahojiano aliwaambia waajiri kuwa ikiwa watamwomba kubadili nambari "3" kuwa nambari "8", angekataa. Ilimchukua muda mrefu kabla ya kupata kazi.

Hatimaye alipata kazi katika kampuni ya mbegu ambayo iliagiza na kuuza mbegu nje ya nchi. Daniel alitazama kwa huzuni bosi wake akiwahonga maafisa ili waseme uwongo kwamba mbegu fulani zilikuwa za ubora ufaao. Bosi wa Daniel alipoenda kuendeleza masomo yake, Daniel alijua kuwa atalazimika kuchukua nafasi yake na kuchukua jukumu la kutoa hongo. Lakini Daniel hangeweza kuwazia kufanya hivyo kwa kuwa alikuwa Mkristo. Kwa hivyo badala ya kuchukua nafasi ya bosi na kupata pesa nyingi zaidi, aliacha kazi hiyo kabisa. Mmiliki wa kampuni alishtuka na kumwomba Daniel asiondoke. Daniel alisema kuwa hawezi kufanya jambo lolote lisilo la kimaadili kwa hiyo hangeweza kuchukua nafasi hiyo. Bosi huyo alithamini sana uadilifu wa Daniel hivi kwamba baada ya Daniel kuacha kazi hiyo, alimwajiri Daniel kuwa mwalimu wa watoto wake.

Baadaye, Daniel alirejea shuleni kupata mafunzo ya ujuzi fulani kando na uhasibu kwa sababu alihofia kuwa kazi yoyote ya uhasibu ingehusisha ufisadi. Alipata shahada katika kazi ya maabara ya matibabu. Akiwa shuleni, Daniel alikataa kudanganya katika mitihani na kazi za ziada, na kupitia uadilifu wake aliwafanya wanafunzi wenzake kadhaa kumpokea Kristo! Daniel alimaliza kama mwanafunzi bora katika darasa lake na kupata kazi mpya nzuri kama meneja wa maabara katika hospitali mpya ya serikali iliyofunguliwa. Jambo la kusikitisha ni kuwa, alikabiliwa tena na maswala ya ufisadi. Wasimamizi, hata walio Wakristo, walimpa pendekezo la kupata pesa za ziada kwa kununua vifaa vya bei nafuu na visivyo na ubora unaofaa, huku akiandika ankara zenye kiasi kikubwa zaidi ili aweze kujiwekea pesa zilizosalia. Daniel alikataa na akakabiliwa na changamoto nyingi, lakini alianzisha maabara bora. Kisha, madaktari wangeomba uchunguzi usio wa lazima kwa wagonjwa ambao walikuwa na pesa kidogo sana na wasio na bima ili kuongeza faida. Daniel aliwakashifu madaktari hao lakini hakukuwa na mabadiliko. Daniel alihisi vibaya sana jinsi wateja walivyokuwa wakidanganywa kiasi kwamba hatimaye aliacha kazi hiyo pia.

Baadaye Daniel alienda kufanya kazi kama msaidizi wa mmiliki wa biashara. Leo hii Daniel anafanya kazi kama meneja wa biashara hiyo na analipwa dola 100 kwa mwezi. Kwa mapato hayo anakimu mahitaji ya watoto wake kumi. Kuhusu maisha yake, hivi karibuni alisema, "Sitoi. Mungu pekee ndiye mtoaji. Ninashiriki tu kile ambacho Mungu ametoa. Ninajua kuwa kuna mtu mahali fulani ambaye ananitafuta ili nimuonyeshe Kristo. Kwa hivyo nasubiri Mungu anionyeshe hatua inayofuata."

## Maswali ya Majadiliano

*Je, Daniel alikabiliwa na changamoto gani kutokana na uadilifu wake?*

---

*Je, Daniel au watu wengine walipata baraka gani kutokana na uadilifu wake?*

---

*Je, utafanya nini kwa njia tofauti mahali pako pa kazi baada ya kusikia simulizi hii?*

---

## Kufanya Biashara kwa Utukufu wa Mungu

*Je, Kanisa lina mtazamo gani kuhusu ulimwengu wa biashara?*

---

*Je, ulimwengu wa biashara una mtazamo gani kuhusu Kanisa?*

---

*Je, inawezekana kwa Mkristo kufanikiwa sana katika biashara?*

---

Biashara inaweza kuwa kitu kizuri sana inapofanywa kwa njia inayomtukuza Mungu. Kwa kweli, biashara ni sehemu muhimu ya maendeleo.

---

Kimsingi, biashara inahusu kupata utajiri. Watu wengine hufikiria kwamba utajiri ni kama keki ndogo, na ya kwamba kuna vipande kiasi fulani tu vya kugawanya baina ya watu wote. Lakini utajiri hauna mipaka kwa namna hiyo. Mungu hututumia sisi watu Wake kuendeleza uumbaji na kupata utajiri.

---

Mungu ndiye anayetupa uwezo wa kupata utajiri na pesa. **Kumbukumbu la Torati 8:18.**

---

Sio cha kuuzwa

Kanuni kutoka kwa Wealth Creation Manifesto (Manifesto ya Uzalishaji wa Utajiri) iliyotengenezwa na Lausanne Global Mission Movement na BAM Global:[4]

1. Uzalishaji wa mali msingi wake ni Mungu Muumbaji, aliyeumba ulimwengu unaostawi kwa wingi na utofauti.
2. Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, ili kuumba pamoja Naye na kwa ajili Yake, kuzalisha bidhaa na huduma kwa manufaa ya wote.
3. Uzalishaji wa mali ni wito mtakatifu, na zawadi iliyotolewa na Mungu, ambayo inasifiwa katika Biblia.
4. Wazalishaji wa mali wanapaswa kutambuliwa na Kanisa, na kuwezeshwa na kutumwa kuhudumu mahali pa kazi kati ya watu na mataifa yote.
5. Uzalishaji wa mali kupitia kwa biashara una uwezo uliothibitishwa wa kuondoa watu na mataifa kutoka kwenye umaskini.

***Je, kuna kipengele chochote kati ya hivi kinachokushangaza? Na ikiwa ndiyo, ni kwa nini?***

Kuzalisha mali na kutilia maanani biashara ni bora zaidi kuliko kutilia maanani misaada kutoka kwa watu wengine au mataifa ya kigeni. Tunapaswa kutilia maanani kubuni nafasi za kazi. Kiwango cha ukosefu wa ajira ni cha zaidi ya asilimia 25 katika baadhi ya nchi za Kiafrika.[5] Kuanzisha biashara mpya kunaweza kuleta utajiri na kuwapa ajira watu wenye mahitaji.

---

George Ayittey, Mwanauchumi wa Ghana: "Kizazi cha Duma ni kizazi kipya cha Waafrika chenye hasira ambacho kinaweza kuona kuwa viongozi wao wamewaangusha kwa kukosa kutekeleza matarajio yao … Hawatatulia na kusubiri serikali zije kuwafanyia mambo. Hakika, hawatatulia na kuomba msaada kutoka nje, kwa sababu wanaweza kuona kuwa kila hitaji la kijamii barani Afrika ni fursa ya biashara. Kizazi cha Duma ni cha ujasiriamali."[6]

***Je, unaweza kufikiria mifano ya mahitaji ya kijamii ambayo Waafrika wabunifu waliigeuza kuwa fursa za biashara?***

Askofu wa Kianglikana kwa jina John Rucyahana nchini Rwanda alisema, "Badala ya kuwafunza watu watakaotafuta kazi, tunapaswa kutoa mafunzo kwa watu watakaobuni nafasi za kazi", alisema. "Tunahitaji kuwa na uwezo wa kuacha kutafuta misaada na kuanza kuwa wazalishaji."[7]

---

Wakati mwingine Wakristo wamekuwa na mtazamo hasi kuhusu biashara kwa sababu ya ushindani unaokuwepo. Lakini ushindani katika biashara huzalisha uvumbuzi, ubunifu, na bidhaa na huduma bora zaidi.

---

Si cha kuuzwa

Herman Chinery, mfanyabiashara nchini Ghana, aliyepewa lakabu ya Bill Gates wa Ghana alisema hivi, "Katika kila biashara unayofanya, lazima kuwe na hali ya kunufaisha kila mtu. Lazima mtu anayenunua huduma yako anufaike, na wewe unufaike vilevile. Vinginevyo, biashara yako haitakuwa endelevu."[8]

*Je, hali itakayomnufaisha mnunuzi na muuzaji ni hali gani?*

Biashara ni kazi inayomletea Mungu heshima kwa sababu hutumia kwa hekima vitu katika uumbaji wa Mungu na huvitumia kwa njia inayowasaidia watu. Papa Francis aliandika: "Biashara ni kazi nzuri, inayoelekezwa katika kuzalisha utajiri na kuboresha ulimwengu. Inaweza kuwa chanzo cha mafanikio katika eneo ambapo inaendeshwa, hasa ikiwa inaona uzalishaji wa ajira kama sehemu muhimu ya huduma yake kwa manufaa ya wote."[9]

Wakristo wanaweza pia kumheshimu Mungu katika biashara kwa kupata pesa zaidi za kusaidia huduma ya Kikristo na kuwasaidia maskini. John Wesley, mhubiri wa Uingereza, alisema kauli maarufu, "Pata chochote unachoweza! Toa yote uwezayo! Weka akiba yote uwezayo!"[10]

## Kutoa zaka na matunda ya kazi yetu

*Je, kutoa zaka kunamaanisha nini?*

*Je, Wakristo wameamriwa na Mungu kutoa zaka?*

**Luka 11:42**

Mtume Paulo aliweka wazi pia kuwa wachungaji na wainjilisti wanapaswa kupata usaidizi wa kukimu mahitaji yao kutokana na utoaji wa Wakristo, kama vile makuhani walivyopata usaidizi wa kukimu mahitaji yao kupitia kwa zaka (angalia 1 Wakorintho 9 baadaye kwa maelezo zaidi).

Sio cha kuuzwa

Kama Wakristo hatutoi kutokana na hisia ya hatia au kwa kutii mzigo mzito wa sheria, bali tunatoa kwa ajili ya kutoa shukrani. Hatupaswi kutoa ili kupata wokovu au kukubalika na Mungu. Badala yake, tunatoa kwa sababu ya kutoa shukrani baada ya kupokea msamaha na upendo kama zawadi bila malipo.
**2 Wakorintho 9:7**

---

Paulo alifundisha pia kuwa watu wanapaswa kutoa kulingana na kile wamepewa.

**2 Wakorintho 8:11-12**

---

**Baadhi ya Wakristo wanafundisha kuwa tunapaswa kutoa zaka na sadaka kwa Kanisa ili Mungu atubariki na kutuzawadia fedha nyingi zaidi. Tutajadili mada hii kwa urefu zaidi katika somo la Injili ya Mafanikio.*

Kutoa zaka ni njia mojawapo ya kumwabudu Mungu. Anataka tutumie rasilimali zote tulizo nazo kwa njia inayomtukuza, iwe ni kupitia kukimu mahitaji ya familia yetu, au kutoa kwa ajili ya huduma za Kanisa, au kuwaonyesha huruma watu walio maskini wa mali.

---

Hii leo, duniani kote, zaka na matoleo ya Wakristo yanatumika kusaidia huduma za kanisa na wachungaji, kutuma wamisionari, kutafsiri na kuchapisha Maandiko, kutunza wagonjwa na wafungwa, kuinua watu walio maskini wa mali, kuleta maendeleo ya jamii na mambo mengine mengi.

***Je, kanisa lako linatumia sehemu kubwa ya zaka na matoleo kwa ajili ya ujenzi wa kanisa? Je, asilimia ngapi ya pesa inatolewa kila mwezi kuwatunza watu maskini katika jamii?***

---

---

Utoaji wa zaka unatupa ukumbusho wa mara kwa mara kuwa tunamtegemea Mungu kama mpaji wetu.

---

***Wakristo wanapokosa kutoa zaka, hiyo inaonyesha nini kuhusu imani yao?***

---

***Je, Wakristo walio maskini wa mali wanapaswa kutoa zaka?***

---

---

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zitajumuisha kazi au shughuli ambazo washiriki watafanya katika jamii zao, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia mafunzo waliyopata. Chagua moja au shughuli zote mbili:

1. Hubiri mahubiri kuhusu umuhimu wa kazi na jinsi ya kufanya kazi yetu kwa utukufu wa Mungu.
2. Fikiria kuhimiza kanisa lako lianzishe mpango wa mafunzo ya kuwafunza watu katika jamii kuhusu ujuzi wa kazi na kuzalisha kipato kwa lengo la kwamba wataweza kupata kazi ya kufanya na kutunza familia zao. Mawazo machache:

    a. Mpango wa mafunzo ya ujuzi wa kimsingi wa kazi, maadili ya kazi, kutengeneza bajeti na kuweka akiba.

    b. Mpango wa mafunzo kuhusu mojawapo ya yafuatayo: umakanika, useremala, uokaji, kutengeneza nywele, biashara, utengenezaji wa matofali, Teknolojia ya Habari au IT (kompyuta), ushonaji, upigaji picha, n.k.

Sio cha kuuzwa

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo[11]

Tufunge somo hili kwa kujadili katika vikundi vidogo kuhusu hali ngumu za kimaadili tunazokabiliana nazo katika kazi zetu za kila siku na pia katika huduma ya kanisa. Tunapaswa kufuata sheria, kufanya kazi kwa uaminifu, na kufanya kazi kwa utukufu wa Mungu. Jadilini ikiwa tabia ya kila mtu ni sawa kimaadili au si sawa kimaadili.

<u>Matanziko ya Kimaadili katika Mahali pa Kazi</u>

1. Mwanamke muuza sukari anakulipisha kwa kilo 1 ya sukari na kuweka mizani yake ili kukupa kiasi kilicho chini ya kilo 1. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)
2. Ulikopa pesa kutoka kwa rafiki ili uanzishe biashara mpya. Uliahidi kulipa pesa hizo mwezi ambao ungefuata, lakini hukulipa wala kutaja mkopo tena. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili*)
3. Unadhani mwajiri wako hakulipi ujira unaostahili. Unapata majaribu ya kuchukua bidhaa za kazini wende nazo nyumbani ili kufidia upungufu huo. Badala yake, unamwomba mwajiri wako muwe na mkutano na mjadiliane kuhusu nyongeza ya mshahara wako. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)
4. Uliwaajiri wanaume wanne wavune mahindi shambani kwako na ukawaahidi kuwalipa kwa kazi yao mwisho wa siku. Mwisho wa siku, kiasi cha mahindi kilichovunwa kilikuwa kidogo sana kuliko ulivyotarajia. Unapompata mfanyakazi mmoja amelala shambani karibu saa sita mchana, unamwamsha na kumrudisha nyumbani na nusu ya malipo ya siku nzima. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*). Unawalipa wafanyikazi wale wengine watatu malipo kamili licha ya mavuno kidogo. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*).
5. Meneja wako alikupa shilingi 1,000 kununua baadhi ya vitu vya kazini mjini. Unatumia shilingi 950 kununua vitu hivyo na shilingi 50 nyingine zilizosalia kujinunulia kikombe cha chai. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

***(Maswali yanaendelea kwenye ukurasa wa 101)***

6. Jirani yako aliazima jembe lako ili afanyie kazi shambani mwake. Alipomaliza, alikurudishia likiwa limevunjika na kukuomba msamaha na kuahidi kukupa jembe jipya mwezi unaofuata. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*) Mwezi unaofuata ulipofika, alikuja kwako na kukuelezea matatizo yake ya kifedha. Kisha akaomba akupe kikapu cha mahindi kama malipo. Unakubali. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

7. Uliomba kampuni ya umeme ikuwekee nyaya hadi kwenye biashara yako kwa shilingi 6,000. Baada ya wao kukubali na kukuwekea nyaya, ukawapa shilingi 4,000 na kuwaeleza kuwa hizo ndizo pesa zote ulizokuwa nazo. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

<u>Matanziko ya Kimaadili katika Kanisa</u>

1. Mgeni kutoka sehemu nyingine anatoa zawadi kwa kanisa akisema kuwa itumike kwa ajili ya ujenzi wa kanisa, lakini kasisi anatumia matoleo hayo kununua vifaa vya kupaza sauti baada ya mgeni kuondoka. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

2. Mshirika anakopa pesa kutoka kwa mfuko wa kanisa ili kulipia ada ya hospitali lakini anakosa kuzirejesha kwa wakati unaofaa. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*) Kisha mchungaji anamwendea mshirika huyo na kupanga naye ratiba ya ulipaji. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

3. Mshirika mmoja anampata mchungaji akitembea kando ya barabara na kumpa pesa, akisema kwamba ni zawadi ya kanisa. Kwa kutumia pesa hizo, mchungaji huyo ananunua chai na gazeti akielekea nyumbani, akichukulia kuwa huo ni usaidizi wa kanisa kwa huduma yake. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

4. Mchungaji anawaambia washirika wa kanisa gharama ya kutengeneza sakafu ya saruji kanisani. Fedha zinachangwa na sakafu inatengenezwa, lakini gharama ni tofauti na vile mchungaji alivyotarajia na kuna pesa zilizobaki kutokana na fedha zilizokuwa zimechangwa. Mchungaji anawatangazia washirika kuhusu pesa zilizosalia na kwa pamoja washirika wanaamua jinsi ya kutumia pesa hizo. (*Sawa kimaadili au si sawa kimaadili?*)

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Simulizi za Kutia Moyo kuhusu Kazi

1. Grace, mwanamke mwenye umri mdogo nchini Tanzania, ni kielelezo cha mtu ambaye alisaidiwa kuondoka katika umaskini wa mali kwa kupata kazi yenye maana ya kufanya katika ulimwengu wa Mungu. Grace anaishi na wazazi wake wazee ambao ni maskini wa mali. Grace alimaliza elimu ya shule ya sekondari lakini jambo la kusikitisha ni kuwa hakuweza kwenda chuo kikuu kwa sababu wazazi wake hawakuwa na pesa za karo yake ya shule. Baada ya kurudi nyumbani, Grace hakujua namna ya kupata pesa za kukidhi mahitaji yake. Hatimaye, alikata tamaa na akaanza kazi ya ukahaba ili kukidhi mahitaji yake ya chakula na mavazi. Baadaye, alisikia kuhusu shirika linaloitwa ACHAMA ambalo huwasaidia wasichana wadogo wanaofanya kazi ya ukahaba. Wafanyakazi wa shirika hilo walikubali kumruhusu Grace aingie kwenye mpango wao na wakamfundisha ujuzi wa kiufundi. Grace alijifunza jinsi ya kutengeneza sabuni, vitambaa, vikapu, chaki, pochi, na kadhalika. Leo hii anatumia ujuzi wake mpya kutengeneza vikapu vinne kwa siku na anaviuza sokoni. Grace amesema – "Nimefurahishwa sana na ujuzi wangu mpya nilioupata kwa sababu unaniwezesha kukidhi mahitaji yangu. Nina furaha pia kwa sababu niliweza kuacha kazi ya ukahaba yenye hatari kubwa ya kuambukizwa VVU." Grace anawashauri wasichana wengine ambao bado wanategemea kazi ya ukahaba kuiacha, na kuwa kuna kazi nyingine ambayo wanaweza kufanya! [12]

2. Mtawa wa Kike Mkristo ambaye ni mfanyakazi mkuu wa serikali katika serikali ya Benin alihudhuria Kongamano la Maono ya Mkakati wa Msamaria Afrika. Wakati wa kongamano alijifunza kuwa Mungu alimtaka amtukuze na kumheshimu katika sehemu zote za maisha – si katika maisha yake ya kiroho tu. Hii ilianza kuwa na athari kubwa kwa maadili yake ya kikazi. Alianza kuwa mwenye bidii kazini na mwenye kufika kwa wakati. Mabadiliko haya yalimletea changamoto. Alikabiliwa na upinzani kutoka kwa wafanyakazi wenzake na wafanyakazi waliokuwa chini yake ambao walihisi kuwa na hatia kutokana na tabia zao za ulegevu wa kufanya kazi. Hata hivyo, bidii yake ilionekana na wakuu wake, na ndani ya miezi mitatu, alipandishwa cheo na kuwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Baadaye alishikilia wadhifa katika baraza la mawaziri katika serikali ya kitaifa, mwanamke wa kwanza kushikilia wadhifa huo. Anashukuru sana kwa kazi ya Mungu maishani mwake na kwa Kongamano la Maono.[13]

## Kuhusu Biashara na Kuzalisha Nafasi za Kazi

- **Tafakari kuhusu nukuu hii.** Waziri wa Fedha wa kwanza wa kike wa Nijeria, Ngozi Okonjo-Iweala alisema, "Njia bora ya kuwasaidia Waafrika leo ni kuwasaidia kusimama kwa miguu yao wenyewe. Na njia bora ya kufanya hivyo ni kuwasaidia kubuni nafasi za kazi." [14]

- **Soma pendekezo hili la Vuguvugu la Misheni la Lausanne:** "Tunatoa wito kwa Kanisa ulimwenguni kote kutambua, kuthibitisha, kuombea, kuagiza na kuwatuma wafanyabiashara na wajasiriamali kutumia karama na wito wao kama wafanyabiashara ulimwenguni – miongoni mwa watu wote na hata mwisho wa dunia. Tunatoa wito kwa wafanyabiashara ulimwenguni kote kupokea uthibitisho huu na kuzingatia jinsi karama na uzoefu wao unavyoweza kutumiwa kusaidia kukidhi mahitaji muhimu zaidi ya kiroho na kimwili ya ulimwengu kupitia biashara kama misheni." [15]

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Justin Lonas kutokana na picha iliyopigwa na Anthony Sytsma.

1 Jan-Emmanuel De Neve and George Ward, "Does Work Make You Happy? Evidence from the World Happiness Report", (Harvard Business Review, Machi 20, 2017), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://hbr.org/2017/03/does-work-make-you-happy-evidence- from-the-world-happiness-report.

2 Jeff Robison, "The Luther Family and the Reformation of Marriage", (the Gospel Coalition, Octoba 27, 2015), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.thegospelcoalition.org/reviews/katharina-and-martin-luther-radical-marriage/.

3 Muhtasari kutoka "Daring to be Daniel", (Reeds in the Wind, Mei 16, 2016), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://reedsinthewind.blogspot.com/2016/05/daring-to-be-daniel.html.

4 Kwa hoja zingine za manifesto tembelea - https://www.lausanne.org/content/wealth-creation-manifesto.

5 "Africa Statistics Flash", African Centre for Statistics of the Economic Commission for Africa, (United Nations Economic Commission for Africa, Juni 2017) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://repository.uneca.org/handle/10855/49802.

6 Video: "Maoni ya George Ayittey kuhusu Msaada wa Kigeni dhidi ya Ujasiriamali wa Afrika", (PovertyCure.Org, Machi 21, 2011), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://povertycure.org/learn/media/george-ayittey-foreign-aid-vs-african-entrepreneurship.

Sio cha kuuzwa

[7] Imenukuliwa katika "Education at the Sonrise School in Rwanda- Training Job Makers", inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://www.povertycure.org/learn/issues/human-person/education.

[8] "Africa's Dream: Ghana's Herman Chinery Hesse", (BBC, tarehe Septemba 6, 2011), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://www.bbc.com/news/world-africa-14793780.

[9] "Wealth Creation: A Godly Gift and Command", (Transformational SME, tarehe Agosti 23, 2016), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://web.archive.org/web/20170425170508/http://www.transformationalsme.org/tag/business-is-a-noble-vocation/.

[10] Nukuu kutoka kwa John Wesley, (Good Reads), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.goodreads.com/quotes/113423-earn-all-you-can- give-all-you-can-save-all.

[11] Zoezi hili limefupishwa na kuhaririwa kutokana na lile la asili, na kutumika kwa ruhusa kutoka kwa Leslie Mosher, kutoka kwenye mtaala wa – Entrepreneurship: Christ Centered Business Education, Session 1: "Preparing your Spirit and Mind", 14.

[12] Jim Zylstra, "Vocational Skills Training Changed my Life", (World Renew, Mei 11, 2017) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://worldrenew.net/our-stories/team/vocational-skills-training-changed-my-life.

[13] Scott Allen, Darrow L. Miller, and the African working group of Samaritan Strategy Africa, *Against All Hope: Hope for Africa,* (Phoenix, Ariz., Disciple Nations Alliance, 2005), 51, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://disciplenations.org/resources/against-all-hope-hope-for-africa/

[14] "Insights: The Need to Invest in Africa's Emerging Economies", (the Foresight Initiative, Desemba 1, 2014) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://medium.com/@hsiangyuchen/want-to-help-africa-c2c9d9e517de.

[15] "Business as Mission", *Lausanne Occasional Paper No. 59,* (Lausanne Committee for World Evangelization, Pattaya, Thailand 2004) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://web.archive.org/web/20240516022348/https://lausanne.org/docs/2004forum/LOP59_IG30.pdf

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa mshiriki

Sio cha Kuuzwa



## Somo la 10: Mabadiliko ya Mtazamo wa Ulimwengu

# Swali la Majadiliano la Ufunguzi

***Je, ukiona ng'ombe unaona nini?***

Watu huona ng'ombe kwa njia tofauti kwa sababu wana "mitazamo tofauti ya ulimwengu".

Je, mtazamo wa ulimwengu ni nini? Mtazamo wa ulimwengu ni imani zote alizo nazo mtu zinazoathiri jinsi anavyoishi na kutenda. Mitazamo yetu ya ulimwengu huathiri jinsi tunavyohusiana na Mungu, sisi wenyewe, watu wengine, na uumbaji. Mtazamo wetu wa ulimwengu unajumuisha imani zetu kuhusu maswali muhimu ya maisha.

***Je, kwa nini ni muhimu kwetu kuangazia mtazamo wa mtu tunapojaribu kumsaidia kuondoka katika umaskini?***

Sisi kama Wakristo tuna mtazamo wa Kikristo, au tunaweza kuuita mtazamo wa kibiblia. Kwa watu wengine, wanaweza kuwa na imani fulani za kweli, lakini pia wana imani potovu. Lakini tunapaswa kukumbuka kuwa inawezekana pia kwamba sisi Wakristo tuna imani fulani za uwongo, kwa hivyo tunapaswa kuendelea kusoma Neno la Mungu ili kujirekebisha. Soma **Warumi 12:2**.

Sehemu ya kazi yetu katika kupambana na umaskini ni kuwafundisha watu mtazamo wa Kikristo. Tunapaswa kujaribu pia kuwashawishi watu wasio Wakristo kuwa mtazamo wa Kikristo ndio sahihi. Watu wakishamwamini Yesu, wataweza kuwa na uhusiano mzuri na Mungu, nafsi zao, watu wengine na uumbaji.

# Mhadhara wa Kiongozi: Mitazamo ya ulimwengu

Huu hapa mfano wa imani potovu kuhusu uhusiano wa mwanadamu na uumbaji wa Mungu. Katika imani za kitamaduni za Basotho nchini Lesotho, imani ya jadi ni kwamba ikiwa wakulima watapalilia mashamba yao wakati wa mchana kati ya saa 4:00 asubuhi na saa 9:00 alasiri, basi kutakuwa na mvua ya mawe.

sio cha kuuzwa

Kwa hivyo wakulima hawapalilii wakati huo na muda wao mwingi wa kufanya kazi kwa bidii na kupanda mashamba yao unapotea. Imani nyingine waliyonayo ni kuwa wanawake wakifua nguo zao mchana au kuwanyonyesha watoto wao mchana, kutakuwa na mvua ya mawe. Kwa hivyo wanafanya shughuli hizi usiku.[1] Unaweza kuona jinsi imani hizi zinavyosababisha watu kutokuwa na tija. Hali hii inaweza kubadilika watu watakapofundishwa mtazamo wa kibiblia. Ni lazima tuwafundishe watu kwamba Mungu aliwaumba ili watawale uumbaji, si uumbaji kutawala watu. Pia, tunaweza kufundisha kwamba Mungu ndiye anayeongoza uumbaji wake na hali ya hewa, na ndiye aliyewaambia watu wafanye kazi kwa siku sita kila juma.

---

Watu wanaweza pia kuwa na imani potovu kumhusu Mungu zinazowaweka kwenye mtego wa umaskini. Ikiwa mtu anaamini kuwa uchawi una nguvu zaidi kuliko Mungu, anaweza kupoteza pesa zake nyingi kwa kafara na matambiko ya mganga. Matambiko na uchawi hazitaleta uponyaji au baraka, bali zitasababisha tu kupoteza rasilimali na umaskini wa mali.

---

***Katika jamii yenu, watu wana imani gani potovu zinazowaweka katika umaskini?***

______________________________

______________________________

Imani potovu zinaweza kuchangia watu kukumbwa na aina zote tano za umaskini. Hii ina maana kuwa mabadiliko ya mtazamo ni muhimu katika kupambana na umaskini! Kwa kweli, katika baadhi ya hali ni vigumu kuleta maendeleo yoyote hadi watu wabadili mtazamo wao wa ulimwengu. Hii inatufunulia, kwa mara nyingine tena, jinsi Kanisa lilivyo na jukumu la kipekee katika kupambana na umaskini. Ni Wakristo watakaoshiriki habari njema ya injili ndio watakaobadilisha kabisa mtazamo wetu wa ulimwengu!

---

## Imani potovu zinazowaweka watu katika umaskini[2]

***Shughuli.*** *Kwanza jadili njia ambazo kila imani inaweza kuchangia mojawapo ya aina tano za umaskini katika maisha ya watu. Pili, jadili ukweli kuhusu kila jambo, na ukiweza, jaribu kutaja yale ambayo Biblia inafundisha.*

***1. "Ikiwa wewe ni maskini, utakuwa maskini siku zote. Ikiwa wewe ni maskini, ni kwa sababu Mungu anataka uwe maskini. Ni hatima yako."***

______________________________

***2. "Familia yetu imelaaniwa." Au, "Jamii yetu imelaaniwa." Au, "Kabila letu limelaaniwa." Au, "Afrika imelaaniwa."***

______________________________

***3. "Mungu anajali mambo ya kiroho tu."***

______________________________

***4. "Sisi ni maskini sana kiasi cha kwamba hatuwezi kutoa kwa wengine. Watu wengine wanapaswa kutoa kwetu."***

______________________________

***(Maelezo yanaendelea kwenye ukurasa wa 107)***



Sio cha kuuzwa

*5. "Kuna tabaka tofauti za watu. Watu wetu ni wa tabaka la chini na tunastahili kiwango cha maisha tulicho nacho."*

---

*6. "Kazi ni adhabu. Tunapaswa kufanya kazi kidogo iwezekanavyo."*

---

*7. "Bidhaa kutoka nchi zingine ni bora kuliko bidhaa za nchini mwetu."*

---

*8. "Hakuna umaskini nchini Marekani, Ulaya na Uchina. Kuna rasilimali zisizo na kikomo huko. Ni jukumu lao kututunza."*

---

*9."Sina uwezo wa kubadili hali yangu."*

---

*10. "Wanawake ni duni kuliko wanaume."*

---

*11. "Kifo, ajali, na umaskini siku zote husababishwa na watu wengine, laana, mizimu, au uchawi."*

---

*12."Kufanya kazi kwa bidii na kutafuta pesa ni hatari. Watu wengine watanishambulia au kuniroga na mwishowe nitakuwa katika hali mbaya zaidi."*

---

Kwa nyingi ya imani hizi za uwongo, ni muhimu kufundisha kuhusu jinsi Mungu alivyowaumba watu wote kwa usawa na kwa mfano wake. Pia, fundisha kuwa Mungu amemuumba kila mtu akiwa na kusudi. Amempa kila mtu talanta; kila mtu ana ujuzi na karama mbalimbali za kutumia katika ulimwengu huu kumtukuza Mungu na kuwasaidia watu wengine.

Wakati mwingine sisi, tunaojaribu kuwasaidia maskini, pia tuna imani potovu. Imani hizi potovu si tu tatizo katika maisha yetu, bali pia imani hizi potovu zinaweza kutufanya tuwaumize watu tunaojaribu kuwasaidia.

# Shughuli Kuhusu Imani Potovu

*Utapewa kikundi kidogo na nambari fulani kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini ili kujadili pamoja. Jadilini kwa dakika 5-10 jinsi kila imani uliyopewa inaweza kusababisha sisi kuumiza watu. Kwa maneno mengine, imani hizi zinawezaje kuzuia juhudi zetu za kupambana na umaskini?*
*Chagua imani moja tu kati ya hizo potovu ya kuwasilisha kwa kikundi kikubwa. Mwakilishi kutoka kwa kikundi chako atachukua dakika moja tu kutoa muhtasari wa jibu lenu. Mwasilishaji huyu anapaswa pia kuelezea ikiwa tunaona imani hizi potovu ndani yetu.*

*Imani potovu zinazotufanya tuumize wengine wakati wa kusaidia:*[3]
*1. "Maskini hawana chochote. Wamekata tamaa sana. Inasikitisha na inatisha sana. Ni lazima tuwape rasilimali na pesa nyingi."*
*2. "Maskini hawana elimu na hawana ujuzi mwingi. Hakuna wanachoweza kufanya ili kujisaidia."*
*3. "Kile viongozi wanachosema ni sawa kila wakati."*

---

*4. "Maendeleo ya kweli yanahitaji pesa nyingi ili kuwa na athari kubwa."*
*5. "Mungu hafanyi kazi katika maisha ya watu masikini hadi tuwafikie kama suluhisho la shida zao."*
*6. "Maskini wengi wanamjua Yesu, lakini sisi tunaojaribu kusaidia tumekomaa zaidi kiroho kuliko wao."*

*7. "Watu hao wote ni wafisadi. Ni jambo gumu sana kuwasaidia au kufanya kazi nao."*
*8. "Ikiwa maskini wangesikiliza tu mawazo yetu yote mazuri, basi hali yao hatimaye ingebadilika. Tuna majibu yao yote."*
*9. "Wakati wetu ni muhimu zaidi kuliko wakati wa watu maskini katika jamii tunayotembelea na kujaribu kusaidia."*

*10. "Kanisa la kieneo haliwezi kuleta mabadiliko halisi katika mahitaji ya kimwili ya jamii. Wanaweza kutunza familia moja au mbili, lakini mabadiliko halisi hufanyika kupitia Mashirika makubwa Yasiyo ya Serikali au mipango ya serikali."*
*11. "Tuna rasilimali nyingi zaidi kwa sababu tumebarikiwa zaidi yao." Au "kwa sababu sisi ni bora zaidi kuliko wao." Au "kwa sababu tumefanya kazi kwa bidii zaidi na tunastahili kuwa na rasilimali nyingi."*

Baadhi ya imani hizi potovu zinatufanya tuhitaji kubadilisha mtazamo wetu. Ikiwa sisi ni wakweli, baadhi ya imani hizi potovu ni matokeo ya hali yetu ya kujiona kama Mungu, matokeo ya dhambi na kiburi katika mioyo yetu. Tunahitaji kuchukua muda wa kukiri dhambi hii na kutubu.

# Kulinganisha Mitazamo ya Ulimwengu

Katika somo hili tutaangazia mitazamo mitatu ya jumla ya ulimwengu: Mtazamo wa kidunia ambao unashikiliwa na watu katika nchi za Magharibi, dini za jadi za Kiafrika (DJK), na mtazamo wa kibiblia.

Mtazamo wa kidunia na DJK kama mitazamo ya ulimwengu zina ukweli fulani unaolingana na kile ambacho Biblia inafundisha. Kwa mfano, mojawapo ya imani za DJK ni kuwa kuna Mungu Muumbaji. Biblia inafundisha hivyo pia. Lakini kwa sehemu kubwa, mtazamo wa kidunia na DJK ni mitazamo inayokinzana na mtazamo wa kibiblia. Kuamini mtazamo wa kibiblia inamaanisha kwamba ni lazima tukatae imani na mitazamo mingi ya kidunia na DJK.

Tunahitaji kuelewa mitazamo hii ya ulimwengu na jinsi inavyohusiana na umaskini na maendeleo. Tutaanza kwa kuangazia imani tofauti za kila mtazamo kuhusu Mungu, kuhusu ubinadamu, na matatizo katika ulimwengu huu.[4]

Sio cha kuuzwa

## Mtazamo Kuhusiana na Mungu

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu wenye mtazamo wa kidunia hawaamini kuwa miungu au roho zipo. Au ikiwa wanaamini kuwa kuna mungu, wanamwona Mungu kama kiumbe asiyeweza kujulikana na aliye mbali sana na ulimwengu.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, watu wanaamini katika miungu na roho nyingi. Wanaamini pia kuwa kuna mungu mkuu ambaye ndiye muumbaji na mpaji. Lakini mara nyingi anaonekana kuwa mtakatifu sana, mwenye nguvu sana, au aliye mbali sana kiasi cha kwamba haiwezekani kuwasiliana naye. Hilo linafanya iwe muhimu kutumia viumbe wengine wa kiroho au mababu kama wapatanishi kati ya watu na Mungu. Viumbe wa kiroho mara nyingi huchukuliwa kuwa na mamlaka juu ya dunia na juu ya shughuli za watu. Ili kuepuka utumwa wa roho hizo, watu hujaribu kutumia vibaya nguvu zao, na kujaribu kuzitumia kwa manufaa yao. Watu wanaweza kujaribu pia kumhonga Mungu kupitia kwa kutoa sadaka na dhabihu ili kupata kile wanachotaka kutoka kwa Mungu.

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

_______________________________________________

_______________________________________________

## Mtazamo Kuhusiana na Wanadamu

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu walio na mtazamo wa kidunia huona wanadamu kama spishi iliyoibuka kwa bahati katika ulimwengu huu. Watu wengi wenye mtazamo wa kidunia hawaamini kuwa watu wana roho.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, watu wanaamini kuwa wanadamu waliumbwa na Mungu, lakini wanawaona wanadamu kama watu walio chini ya nguvu za kiroho. Mara nyingi watu huishi kwa hofu. Huenda wana mtazamo wa kuona kwamba hali yao haiwezi kubadilika wakafikiri kuwa hatima ya wanadamu ni utumwa na hakuna kitu ambacho wanadamu wanaweza kufanya ili kubadili hali yao. Wanaamini kwamba watu wanaathiriwa na miungu, roho, nguvu za asili, laana, na uchawi, na kwa hivyo hawawajibiki sana kwa hali yao wenyewe.

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

_______________________________________________

_______________________________________________

## Mtazamo Kuhuisiana na Dunia

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu walio na mtazamo wa kidunia wanafikiri kuwa tunahitaji kutumia rasilimali za dunia kwa manufaa yetu. Lakini watu wengi walio na mtazamo huo wa kidunia husema kuwa tunapaswa kuitunza dunia pia kwani tukiiharibu tutajiangamiza wenyewe.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, dunia inadhaniwa kuwa imeunganishwa kwa karibu na ulimwengu wa kiroho. Sehemu kubwa ya dunia huonwa kuwa makao ya roho ambazo zinadhibiti rasilimali fulani, milima, misitu, na mito. Wakati mwinginewatu huogopa roho hizo na hivyo hawatumii sehemu hizo za dunia.

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

_______________________________________________

_______________________________________________

Sio cha kuuzwa

## Mtazamo Kuhusiana na Kazi

**Mtazamo wa Kidunia:** Baadhi ya watu wenye mtazamo wa kidunia huabudu kazi na kupata utambulisho wao wa kimsingi, hadhi, na maana ya maisha kupitia kwa kazi zao. Wengine huona kazi kuwa uovu usioepukika ili kupata pesa na mali wanazotaka.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, watu huona kazi kama adhabu kutoka kwa Mungu au kutoka kwa roho. Kazi inafanywa kama uovu usioepukika, lakini kazi inaepukwa inapowezekana. Hata hivyo, mtazamo huu unabadilika polepole kwa vile sasa tunaona ushawishi fulani wa mtazamo wa kidunia katika bara la Afrika, ambapo watu wengine wameanza kuabudu kazi zao na kuona kazi kama aina fulani ya utambulisho na hadhi.

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

## Mtazamo Kuhusiana na Maadili na Dhambi

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu wenye mtazamo wa kidunia hawaamini kwamba kuna dhambi. Wanafikiri kwamba hakuna kiwango halisi cha kimaadili, bali kila mtu au kila utamaduni hujiamulia kile kilicho chema na kile kilicho kibaya. Wengine hutegemea mantiki ya kibinadamu ili kutufundisha kile kilicho chema na kile kilicho kibaya, lakini kwa sababu ya mabadiliko ya kitamaduni, maoni yao kuhusu maadili hubadilika kulingana na wakati na mahali.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, mema na mabaya huamuliwa na mila, au na kile kitakachowafurahisha watu wa kabila na ukoo. Matendo ni mema ikiwa yanaleta heshima, na ni mabaya ikiwa yanaleta aibu. Inaonekana kama usaliti mkubwa kutenda kinyume na matarajio ya jamii. Maadili pia yanaamuliwa na matokeo ya matendo. Watu hufanya kile "kinacholeta manufaa". *Matendo ni mema ikiwa yananiletea thawabu, na mabaya ikiwa yananiletea matatizo.*

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

## Mtazamo Kuhusiana na Watu Wengine

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu wengi wenye mtazamo wa kidunia hujaribu kuwajali watu wengine kwa sababu wanaamini kuwa hiyo ndiyo njia bora zaidi yetu sisi sote kuishi pamoja kwa amani. Lakini wengine huwatendea vibaya watu ili wasonge mbele maishani, kwa kuwa wanaamini kuwa jambo la muhimu zaidi maishani ni kufanikiwa kwa wenye nguvu zaidi. Tamaduni zingine zinachukuliwa kuwa bora kuliko zingine ambazo zinaweza kuonekana kama "za zamani" au "ambazo hazijaendelea".

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, watu wanaamini kuwa wameunganishwa kwa karibu na watu wengine, hata wafu ambao wamekuwa mababu wanaoheshimiwa. Wanaheshimu kabila na ukoo, na hofu ya kuwasumbua watu wengine, jamii, au ukoo hufanya iwe vigumu kufanya jambo lolote jipya hata kama litakuwa na manufaa kwa watu. Hii inaweza kufanya mabadiliko kuwa ya polepole na magumu. Wanadamu wote hawana usawa. Kabila la mtu linaonekana kuwa bora kuliko makabila mengine. Katika hali nyingi, waganga, machifu, na wazee huonekana kuwa watu wa kipekee au bora kuliko wengine. Mababu wanapaswa kuheshimiwa na kutiiwa. Wanaume kwa ujumla huonekana kuwa bora kuliko wanawake. Jamii huonekana kuwa muhimu zaidi kuliko mtu binafsi. Lakini watu walio nje ya tabaka zenye hadhi ya juu au zilizo bora zaidi wanatarajiwa kubaki sawa kwa pamoja. Kuna kile ambacho wengine wamekiita ugonjwa wa PHD – "Pull Him Down" yaani "Mvute Mwingine Chini".[5] Watu hawapaswi

Sio cha kuuzwa

kuwa mbele ya wengine, au kujiendeleza mbele ya wengine, na wakijaribu kufanya hivyo, jamii itajaribu kuwarudisha nyuma.

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

## Mtazamo Kuhusiana na Matatizo Duniani

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu wenye mtazamo wa kidunia hufikiria kwamba matatizo ya ulimwengu yanatokana na ujinga, ukosefu wa rasilimali, na ukosefu wa teknolojia. Wanafikiri kuwa, baada ya muda wa kutosha kupita, mantiki ya kibinadamu na teknolojia zitaweza kutatua matatizo mengi ya ulimwengu.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, matatizo katika ulimwengu yanasababishwa na miungu, roho, mababu, laana, na uchawi.

*Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?*

Wakristo wanaweza kutumia teknolojia na vitu vya asili kufanya maisha ya watu kuwa bora, lakini wanaona vitu hivyo kama zawadi kutoka kwa Mungu. Wakristo pia wanaona kwamba teknolojia inaweza kusababisha uovu mwingi sawa na mema, kwa sababu watu wote ni wenye dhambi, na watu ndio wanaotumia teknolojia. Wakristo wanajua kwamba pepo husababisha matatizo katika ulimwengu, lakini wanajua vilevile kuwa katika Kristo tuna nguvu juu ya pepo hao.

# Maswali ya Majadiliano

*1. Je, ni imani au mitazamo gani ya DJK unayoiona katika nchi yenu na je, mitazamo hiyo inachangia katika mojawapo ya aina tano za umaskini?*

*2. Je, ni imani au mitazamo gani ya mitazamo ya kidunia unayoiona katika nchi yenu na je, mitazamo hiyo inachangia katika mojawapo ya aina tano za umaskini?*

*(Maswali yanaendelea kwenye ukurasa wa 112)*

Sio cha kuuzwa

***3. Kuhusu majibu yako katika #1-2, je, kuwafundisha watu mtazamo wa kibiblia kutaleta mabadiliko na maendeleo kwa njia gani?***

# Utamaduni

Somo hili linatupatia changamoto kwa utamaduni wetu, kwa sababu mtazamo wetu wa ulimwengu una uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni na mila zetu. Kila utamaduni una vipengele vinavyompendeza Mungu na vipengele visivyompendeza Mungu. Kwa hiyo, bila kuzingatia utambulisho wetu, Neno la Mungu hutathmini utamaduni wetu kwa njia fulani. Ili kuwa mwanafunzi wa Yesu, si lazima tuache utamaduni wetu kabisa, bali tunapaswa kubadili desturi za kitamaduni na imani zozote ambazo hazilingani na Neno la Mungu.

Inaweza kuwa jambo gumu sana kwenda kinyume na matarajio na imani za utamaduni wetu. Ni vigumu kubadilika kibinafsi, na pia ni vigumu kukabiliwa na dhihaka na hasira kutoka kwa wengine katika familia au kabila letu.

Katika bara la Afrika, ni rahisi kuwahubiria watu na kuona watu wakiokoka. “Lakini kando na kuwa na mioyo ‘iliyookoka,’ Wakristo wanahitaji kuwa na akili ‘zilizookoka’.”[6]

***Je, kuna mtu mmoja ambaye angependa kushiriki ushuhuda wake mfupi kuhusu wakati alipochagua kumtii Kristo badala ya matarajio ya utamaduni wake? Je, uliteseka kwa ajili ya kufanya hivyo na Mungu alikusaidiaje katika mateso hayo?***

Kumfuata Kristo kunaweza kutuletea mateso. Tunakumbuka kuwa Yesu alituambia tuchukue misalaba yetu na kumfuata. Lakini tunajua kwamba Mungu hutumia mateso yetu kuzalisha mema (tazama **Warumi 8:28**). Kupitia kwa mateso, Mungu hutuvuta karibu na yeye, hutukuza katika subira na tabia zetu, na kututumia kama mashahidi kwa wengine. Tunajua pia kuwa Mungu atatupa nguvu za kustahimili mateso na atakuwa pamoja nasi tunapopita bondeni. Ni lazima tumweke Kristo katika nafasi ya kwanza na utamaduni wetu katika nafasi ya pili hata inapokuwa vigumu kufanya hivyo.

## Mabadiliko ya Mtazamo wa Ulimwengu

Kwa sababu kila utamaduni una mtazamo wa ulimwengu ambao hauendani kikamilifu na ukweli wa Neno la Mungu, sote tunahitaji mabadiliko ya mtazamo wa ulimwengu. Kwa baadhi yetu, labda tunahitaji kutubu imani na tabia fulani ambazo tulirithi kutoka kwa DJK ambazo haziendani na ukweli wa Neno la Mungu. Kwa wengine, ni sharti tutubu kuhusu baadhi ya mitazamo ambayo tumerithi bila kujua kutoka kwa mtazamo wa kidunia.

Sio cha kuuzwa

________________________________________

### Kufundisha Maarifa ya Kiufundi

Ni muhimu pia kufundisha watu maarifa ya jumla na maarifa ya kiufundi kama sehemu ya mbinu yetu ya kupambana na umaskini.

Nukuu kutoka kwa Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa, Kofi Annan:
"Maarifa ni nguvu. Maelezo hutukomboa. Elimu ndio msingi wa maendeleo, katika kila jamii, katika kila familia."[7]

Tunahitaji kuwafundisha watu maarifa na ujuzi mpya. Wakati mwingine tunahitaji kuwafundisha jinsi magonjwa yanavyoenezwa, jinsi ya kutibu VVU-UKIMWI, jinsi ya kuandaa bajeti, jinsi ya kutangaza biashara, na jinsi ya kutumia nishati ya jua. Lakini tunapofundisha mambo haya, ni muhimu kufundisha kuhusu mambo hayo kutokana na mtazamo wa kibiblia.
Mfano wa Dawa:

________________________________________

________________________________________

Iwe unafundisha kuhusu huduma za afya, biashara, kilimo, au mipango ya k uweka akiba, hakikisha kuwa unafundisha kuhusu mada hizi kwa mtazamo jumuishi wa Biblia.

***Je, umekuwa ukifundisha mtu yeyote maarifa ya kiufundi bila kujumuisha mtazamo wa kibiblia? Eleza.***

________________________________________

Sio cha kuuzwa

## Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisani au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi:

**1. Kwa viongozi wa kanisa:**

Hubiri mahubiri kuhusu mtazamo wa kibiblia kwa kutumia mojawapo ya vifungu vya Biblia vilivyotajwa katika somo au katika maswali ya majadiliano ya kikundi kidogo. Zungumza kuhusu umuhimu wa kuzaliwa mara ya pili akilini na mioyoni mwetu pia. Hakikisha umezungumza kuhusu jinsi tunavyohitaji kumpa Kristo nafasi ya kwanza, juu ya miungu mingine yote, ikiwa ni pamoja na kumweka mbele ya matarajio ya utamaduni wetu. Ni muhimu kuzungumza kuhusu ukweli kwamba kufanya hivyo kunaweza kusababisha mateso, lakini pia kwamba Mungu atakuwa pamoja nasi katika mateso haya.

**2. Kwa wengine:**

Panga kuwafundisha watu katika kanisa lako, au jamii yako, au katika familia yako kuhusu mada au ujuzi unaoufahamu. Ujuzi huo unaweza kuwa unahusiana na afya, biashara, kilimo, useremala, usafi wa mazingira, kupanga bajeti, kupika n.k. Lakini kabla ya kuanza kufundisha, hakikisha somo lako ulilotayarisha limejumuisha mtazamo wa kibiblia. Hii si kazi rahisi ya kufanya kila wakati. Huenda ukahitaji kutumia muda katika kutafakari kwa kina kuhusu mada yako na pia kutafakari kuhusu vifungu vya Biblia vinavyohusiana na mada yako. Ikiwa unatatizika kuunganisha mada yako na mtazamo wa kibiblia, zungumza na mchungaji, rafiki, au mtaalamu katika mada yako, ili kupata mawazo yao.

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

1. Je, vifungu vilivyo hapa chini vinatufundisha nini kuhusu umuhimu wa kuwa na mtazamo wa Kikristo?

   a. **Waefeso 4:17-24**

   ______________________________________________

   b. **Wakolosai 2:6-10**

   ______________________________________________

2. Someni na mjadili **1 Petro 3:14-16** na **1 Petro 4:12-16** kuhusu kazi ya mateso katika maisha ya Mkristo. Je, uko tayari kumpa Kristo nafasi ya kwanza, na kuishi kwa njia tofauti na watu wengine katika utamaduni wako, hata kama hiyo inamaanisha utateseka? Eleza.

   ______________________________________________

   ______________________________________________

3. TayariTumezungumza kuhusu imani za kidunia na DJK katika nchi yetu. Lakini unaona mtazamo wa kidunia au DJK una ushawishi ndani ya kanisa lako leo kwa njia gani?

   ______________________________________________

   ______________________________________________

4. Je, maarifa gani ya kiufundi yanaweza kunufaisha watu katika jamii yako? Je, ni nani katika kanisa lako au aliye pamoja nawe katika kikundi hiki cha mafunzo anayeweza kufundisha maarifa hayo?

   ______________________________________________

   ______________________________________________

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Maelezo zaidi kuhusu tofauti kati ya mtazamo wa kidunia, DJK, na mtazamo wa kibiblia:

1. **Mitazamo hii ina maoni tofauti kuhusu "maana ya maisha".**

**Mtazamo wa Kidunia**: Baadhi ya watu walio na mtazamo wa kidunia wanafikiri kwamba maisha hayana maana, kwamba wanadamu waliibuka tu kwa bahati kutoka katika hali ya utupu. Wengine wanadhani kuwa tunapaswa tu kujaribu kufurahia vitu vya kimwili na mali zetu kwa muda mrefu kadiri tuwezavyo, kwa sababu sote tutakufa. Wengine hujaribu kubuni maana ya maisha wenyewe kwa kujaribu kuona jinsi wanadamu wanavyoweza kufanya maendeleo na kujiendeleza kupitia kwa sayansi.

Wanataka kuwa wanadamu bora zaidi kadiri wanavyoweza. Watu walio na mtazamo wa kidunia hawaamini kwamba kuna maisha baada ya kifo kwa hivyo wanaishi kikamilifu kwa ajili ya maisha haya.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, watu wengi huzingatia nguvu kama kipengele muhimu zaidi maishani. Inahusu " – *uwezo wa babu kuwatawala watu wa ukoo wake, nguvu ya jicho baya kuua mtoto mchanga au kuharibu mavuno, nguvu za sayari kuathiri hatima ya mtu duniani, nguvu za kipepo kummiliki mtu anayewasiliana na roho, nguvu za uchawi kudhibiti matukio ya wanadamu, nguvu zisizo na nafsi kumponya mtoto au kumfanya mtu kuwa tajiri*."[8] Lengo ni kutumia nguvu za viumbe wa kiroho kwa manufaa yako na familia yako katika maisha haya. Kuna imani kwamba kuna maisha baada ya kifo. Lakini, kwa jumla katika DJK, watu wanajali zaidi kupata mahitaji ya kila siku, kutafuta chakula, uponyaji, n.k. ndipo wafikirie kuhusu maisha baada ya kifo.

***Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?***
Mtazamo wa kidunia na DJK huzingatia nguvu. Mtazamo wa kidunia hutazamia nguvu za wanadamu na DJK hutazamia kutumia nguvu za rohoi. "Watu wanaobudu uumbaji hulenga kutumia nguvu za kiroho kwa njia ya uchawi; watu wanaoshikilia mtazamo wa kidunia hudhibiti mazingira yao kwa kutumia teknolojia."[9] Lakini Biblia inafundisha kuwa maana ya maisha si kutafuta mamlaka, bali kutumia wakati wetu kuabudu Mungu na kufurahia upendo wake. Maisha haya na maisha ya baadaye yanamhusu Mungu na utukufu wake; tunaishi ili kumtumikia na tunapokea upendo wake. Ni tatizo pia kuzingatia nguvu kwa sababu kunaweza kuwa na nguvu bandia. Hebu fikiria kuhusu nguvu ambazo wachawi wa Farao walimwonyesha Musa. Nguvu haiwezi kuaminiwa kila wakati. Lakini ukweli hauwezi kuwa bandia.[10] Ni vyema kwetu kuzingatia ukweli wa Neno la Mungu, kisha tuamini nguvu.

2. **Mitazamo hii ina maoni tofauti kuhusu "roho".**

**Mtazamo wa Kidunia:** Watu walio na mtazamo wa kidunia hawaamini kwamba kuna ulimwengu wowote wa kiroho, kwa hivyo hawaishi kwa hofu ya roho wala hawajaribu kutumia nguvu za hizo roho.

**Dini za Jadi za Kiafrika (DJK):** Katika DJK, kuna imani kwamba kuna roho nyingi, zingine nzuri na zingine mbaya na zingine si nzuri wala si mbaya. Wanadamu sharti wajaribu kujua roho hizo na kisha kuzifurahisha ili kupata manufaa kutoka kwao. Mizimu hii inaweza kumsaidia mtu kupata kazi nzuri au kumponya kimuujiza kutokana na ugonjwa fulani. Watu wengi huishi kwa hofu ya roho hizo na kile ambacho watu wengine wanaweza kuwafanyia kwa kutumia roho hizo.

***Kinyume cha hayo, mtazamo wa kibiblia unafundisha nini?***
Biblia inatufundisha kuwa Mungu ni mwenye enzi kuu na mweza yote. Yeye ndiye aliyeziumba roho zote na anazitawala zote. Baadhi ya roho ni malaika wanaomwabudu Mungu na wanamtii. Baadhi ya roho ni pepo ambao wamemwasi Mungu. Mungu amewaruhusu waendelee kuwepo na kusababisha madhara katika ulimwengu huu, lakini amewaruhusu kufanya hivyo kwa muda mfupi tu. Siku inakuja ambapo Yesu atarudi, ambapo pepo yote watatupwa katika ziwa la moto (Mathayo 25:41). Tunapongojea, bado tunapaswa kupambana dhidi ya pepo, hata kama Wakristo, (Waefeso 6:12-13). Lakini hata sasa hivi, wale walio ndani ya Kristo hawahitaji kuishi wakiogopa pepo. Kristo amemshinda Shetani kupitia kwa kifo na ufufuo wake. Kupitia kwa Kristo anayeishi ndani yetu, tuna nguvu juu ya pepo (Wakolosai 2:15, Luka 10:18-19, 1 Yohana 3:8, na 1 Yohana 4:4). Hatupaswi kuogopa tena. (1 Yohana 4:18, Warumi 8:38-39).

Ni kweli kwamba umaskini kwa kiasi fulani unaweza kusababishwa na pepo. Pepo husababisha matatizo katika ulimwengu kwa watu binafsi, na hata hufanya kazi kupitia kwa vikundi na taasisi ili kufanya mifumo izidi kukosa ufanisi, izidi kuwa na ufisadi, na izidi kukosa haki. Ni lazima tutambue mamlaka na uwezo tulio nao Kristo akiwa ndani yetu, na kushinda pepo hawa. Hii ina maana kuwa sehemu ya kupambana na umaskini ni kuwakomboa watu kutokana na pepo kupitia kwa nguvu za Kristo. Ni lazima tuvae silaha za Mungu, ambazo ni ukweli, haki, injili, imani, wokovu, Biblia, na maombi (Waefeso 6:10-20).

Sio cha kuuza

Watu wengine huepuka kujaribu kujiendeleza kwa sababu wanaogopa kuwa watu wengine watawaangusha kupitia kwa uchawi au laana. Lakini hatuhitaji kuishi kwa hofu ya uchawi, roho au laana. Yesu ameshinda yote hayo. Yesu anatawala maisha yetu. Yesu ndiye mshindi. Yesu ni Mfalme!

Maelezo zaidi kuhusu mabadiliko ya mtazamo wa ulimwengu:

Mabadiliko ya mtazamo wa ulimwengu ni muhimu sana, na ndiyo sababu tuna somo zima kuhusu mada hii, lakini hatupaswi pia kufanya makosa ya kufikiria kwamba mradi tu tunawafundisha watu mtazamo wa kibiblia, basi kila kitu kitakuwa sawa, na watu watatoka kwenye umaskini mara moja. Hata kama mtu ana imani sahihi, bado anaweza kukabiliwa na umaskini. Zifuatazo ni baadhi ya sababu kwa nini inakuwa hivyo:

1. Biblia inafundisha kuwa Wakristo bado wataendelea kukabiliwa na mateso, ikiwemo umaskini, hata ikiwa wanampenda Mungu na wana imani sahihi.
2. Kuwa na mtazamo sahihi wa ulimwengu kuhusu jinsi mahusiano yanavyotakiwa kuwa haifanyi mahusiano hayo kufanya kazi vizuri moja kwa moja jinsi yanavyopaswa. Ninaweza kujua jinsi *ninavyopaswa* kuwa na mahusiano mazuri na majirani zangu, lakini hiyo haimaanishi kuwa hakutakuwa na migogoro.
3. Uumbaji wote umelaaniwa kwa sababu ya Anguko. Hiyo ina maana kuwa matetemeko ya ardhi,vimbunga, njaa na mafuriko bado hutokea na kutuathiri hata tunapokuwa na mitazamo sahihi ya ulimwengu.
4. Wakati mwingine watu wengine huhujumu juhudi za mtu maskini za kubadilisha hali yake, hata kama mtu huyo maskini ana mtazamo wa Kikristo.
5. Mifumo iliyovunjika inaweza kusababisha umaskini pia, hata kwa watu wenye mtazamo wa Kikristo. Ufisadi na mifumo iliyovunjika imejadiliwa katika Somo la 11.

Sio cha Kuuzwa

---

Uchoraji wa **mistari** ulifanywa na Lisa Brown kutokana na picha iliyopigwa na Tabitha Kapic.

[1] Mawasiliano ya kibinafsi kutoka kwa Joshua Ramatlali.

[2] Imehaririwa kutoka kwenye wasilisho la Anna Ho, “Truth-Centred Transformation”, Imetumika kwa Ruhusa.

[3] Ibid.

[4] Gayle Van Rheenen, “Animism, Secularism and Theism: Developing a Tripartite Model for Understanding World Cultures”, (IJFM, Octoba 1993) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://www.ijfm.org/PDFs_IJFM/10_4_PDFs/04_Van_Rheenen.pdf.

[5] Imetolewa kutoka kwenye vidokezo vilivyochukuliwa wakati wa uwasilishaji kuhusu mtazamo wa ulimwengu na Dennis Tongoi.

[6] Scott Allen, Darrow L. Miller, *Against All Hope: Hope for Africa,* 43, inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://disciplenations.org/resources/against-all-hope-hope-for-africa/.

[7] https://www.brainyquote.com/quotes/authors/k/kofi_annan.html.

[8] Van Rheenen, "Animism…", Ukurasa wa 1 (ukurasa wa 169).

[9] Ibid., Ukurasa wa 2 (ukurasa wa 170).

[10] Imetolewa kutoka kwenye vidokezo vilivyochukuliwa wakati wa uwasilishaji kuhusu mtazamo wa ulimwengu na Dennis Tongoi.


Sio cha kuuzwa

Kusaidia Bila

Kuumiza Barani Afrika

MWONGOZO WA MSHIRIKI

Sio cha kuuzwa



# Somo la 11: Mifumo Iliyovunjika

# Swali la Majadiliano la Ufunguzi

*Unaposikia neno "mifumo iliyovunjika", ni nini kinakuja akilini mwako?*

Mifumo iliyovunjika inarejelea miundo, sera, na mipango ambayo haiendelezi kwa ufanisi ustawi wa wanadamu: haisaidii watu kuishi katika uhusiano unaofaa na Mungu, nafsi zao, watu wengine na uumbaji. Mifumo inaweza kuvunjika kwa sababu haitimizi tena kusudi jema ambalo iliundwa kutimiza. Mifumo ya kisiasa inarejelea taasisi, sheria na sera zinazoongoza taifa. Katika kitengo hiki pia, tunajumuisha mfumo wa kupiga kura, kikosi cha polisi, elimu ya umma, na huduma za afya ya umma. Mifumo ya kiuchumi inarejelea mifumo ya ndani au ya kimataifa ya biashara, masoko, benki, mishahara, na usimamizi wa rasilimali katika nchi. Mifumo ya kijamii ni pamoja na familia, ukoo, kanisa, na mifumo mingine ya kitamaduni na matarajio yake.

Inapovunjika, mifumo hii inaweza kuwanasa watu kwenye umaskini ingawa si makosa yao wenyewe. Kama Wakristo lazima tujali mifumo iliyovunjika kwa sababu Mungu anaijali pia.
**Amosi 2:6-7**

**Amosi 5:24**

Sehemu kubwa ya kutia juhudi za kufanikisha haki ambayo Mungu anataka ni kujaribu kubadilisha na kurekebisha mifumo iliyovunjika.

# Shughuli ya kikundi kidogo

***Andaeni orodha rahisi ya mifumo iliyovunjika ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo mnaona katika nchi au jamii yenu ambayo inachangia kuwaweka baadhi ya watu katika umaskini. Zipangeni kwa mpangilio maalum, kuanzia ile inayochangia zaidi katika kuwaweka watu katika umaskini, hadi ile inayochangia kwa kiwango kidogo zaidi katika kuwaweka watu katika umaskini (#1 inapaswa kuwa mfumo mbaya zaidi uliovunjika katika nchi au jamii yenu).***

Sio cha kuuzwa

# Mhadhara wa Kiongozi: Mifumo Iliyovunjika ya Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii

## Mifumo ya kisiasa

Mifumo ya kisiasa iliyovunjika ni pamoja hali ya vita na ukosefu wa usalama kwa muda mrefu. Katika nchi nyingi za Kiafrika, tunakabiliwa pia na utawala mbovu, udikteta, na mamlaka kuwa mikononi mwa watu wachache au makabila machache. Mifano mingine ya mifumo ya kisiasa iliyovunjika ni pamoja na chaguzi zisizo za haki, na ukosefu wa uhuru wa kusema na uhuru wa vyombo vya habari. Mfumo unaweza kuwa umevunjika ikiwa utawanufaisha watu wachache tu au kuwatenga maskini.

---

### Huduma za Afya ya Umma

Huduma za afya ya umma zinapatikana katika nchi nyingi za Afrika lakini mara nyingi ni mfumo ambao haufanyi kazi kwa ufanisi au kwa haki. Wakati mwingine, matatizo ni pamoja na:

- Kiwango cha chini cha upatikanaji wa vituo vya afya hasa vijijini, na huduma duni za afya kutokana na vituo vya afya kuwa hafifu na visivyo na rasilimali za kutosha.
- Ukosefu wa dawa hospitalini. Kwa kuwa dawa hazipo, wagonjwa lazima walipie dawa kwenye kliniki za kibinafsi na maduka ya dawa.
- Ukosefu wa uwajibikaji na ufuatiliaji wa vituo vya afya na wafanyakazi. Hii inachochea utoro wa wafanyakazi wa afya na pia wizi wa dawa kutoka katika hospitali za umma. Zaidi ya hayo, hali hii inaruhusu ufisadi wakati wa ununuzi wa bidhaa za matibabu na kusababisha ununuzi wa dawa za ubora wa chini.
- Uwekezaji wa kiwango cha chini katika huduma za kiafya na utafiti wa afya unaofanywa na serikali.
- Wahudumu wa kiafya wanalipwa mishahara duni, kwa hivyo wakati mwingine wanatoza malipo ya ziada kwa huduma ambazo zinapaswa kuwa za bila malipo. Wanafanya kazi nyingi kupita kiasi pia kwa sababu ya ukosefu wa wafanyakazi wa matibabu. Na wengi huishia kwenda kufanya kazi katika nchi zingine ambako watalipwa vizuri zaidi na hawafanyishwi kazi nyingi kupita kiasi.

***Je, mfumo wa afya ya umma umevunjwa nchini mwetu katika njia yoyote kati ya hizo zilizotajwa? Gani? Je, matatizo haya yanawaathiri vipi maskini wa mali ikilinganishwa na matajiri?***

________________________________________

________________________________________

### Elimu ya Umma

Elimu kwa umma inapatikana katika nchi nyingi za Kiafrika, kwa kawaida kama huduma ya umma bila malipo,[1] lakini mara nyingi ni mfumo ambao haufanyi kazi vizuri. Wakati mwingine matatizo huwa ni pamoja na:[2]

- Ukosefu wa miundombinu ya shule na ukosefu wa vifaa vya kutosha, hasa katika maeneo ya vijijini.
- Ukosefu wa walimu wenye mafunzo. Katika mwaka wa 2012, wastani wa uwiano wa wanafunzi/mwalimu katika shule za msingi ulikuwa 42:1 barani Afrika. Takwimu hizo hazijabadilika tangu 1999.[3]

- Kukosa kutekeleza sera na viwango vya elimu. Shule nyingi ambazo hazikidhi viwango vinavyohitajika na zisizo na walimu waliohitimu zinaendelea kuanzishwa.

- Walimu wanalipwa mishahara duni, hivyo kusababisha migomo ya mara kwa mara katika ngazi zote kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Wakati mwingine walimu huhamia nchi zingine ambako wanalipwa vizuri zaidi.

- Ukosefu wa ufuatiliaji na usimamizi wa serikali unaosababisha ufisadi, pamoja na kutolewa kwa karatasi za mtihani kabla ya siku ya mtihani, na kughushi nakala za vyeti vya mitihani.

- Hakuna mfumo wa serikali wa mikopo ya kusaidia watu kugharamia elimu ya juu.

- Shule ambazo zinatakiwa kuwa za bila malipo wakati mwingine bado zinatoza ada kubwa ya chakula au vitabu, na kusababisha familia nyingi maskini kuendelea kushindwa kupeleka watoto shuleni.

- Familia zilizo na uwezo wa kifedha hupeleka watoto wao katika shule bora za kibinafsi, na hivyo kusababisha uwekezaji mdogo wa jamii katika shule za umma. Kwa kuwa shule za umma zimejaa watoto kutoka kwa familia zenye umaskini wa mali, familia hizo zenye uwezo mdogo ndizo zinazoachiwa jukumu la kutetea maendeleo ya shule hizo.

*Je, mfumo wa elimu ya umma umevunjika nchini mwetu kwa njia yoyote kati ya hizi zilizotajwa? Zipi? Je, matatizo haya yanawaathiri vipi maskini wa mali na watoto wao wakilinganishwa na matajiri?*

______________________________________________

______________________________________________

## Miundombinu

Katika nchi nyingi za Afrika, kuna ukosefu wa mtandao mzuri wa nguvu za umeme, mitandao mizuri ya mawasiliano ya simu kote nchini, maji safi na usafi wa mazingira, na mtandao mpana wa barabara unaokarabatiwa mara kwa mara. Wakati mwingine ni maeneo tajiri tu ya nchi ndiyo yanayopata manufaa ya miundombinu bora, huku maeneo ya vijijini na makazi duni ya jiji yakipuuzwa.

*Je, ni makabila au maeneo gani katika nchi yako ambayo yana matatizo zaidi yanayohusiana na ukosefu wa miundombinu?*

______________________________________________

______________________________________________

## Utawala wa Sheria

"Utawala wa sheria" unamaanisha kuwa kuna mamlaka na sheria zinazotekelezwa katika nchi. Watu hawawezi kufanya chochote wanachotaka na wale wanaovunja sheria wanaadhibiwa. Kila mwananchi sharti afuate sheria, awe tajiri au maskini, hata viongozi wa ngazi za juu serikalini. Sheria zinapaswa kuandikwa wazi na zijulikane na wananchi wote. Haki ya kumiliki mali inapaswa kuzingatiwa. Haki ya kupiga kura inapaswa kuzingatiwa na chaguzi zifanyike kwa uhuru na haki. Vikomo vya muhula wa uongozi vinapaswa kuheshimiwa. Hukumu za majaji zisishawishiwe na hongo au vitisho. Watu wanapaswa kutendewa haki na mahakama na viongozi wa serikali, bila kujali kabila.

Sio cha kuuzwa

***Je, katika maeneo ambayo sheria hazitekelezwi, watu walio maskini wa mali wanaathiriwaje zaidi ikilinganishwa na wale walio matajiri?***

## Urasimu

Urasimu ni shirika lililoundwa na idara na vitengo vingi ambavyo vinasimamiwa na watu wengi sana.[4] Mifumo ya urasimu ya Serikali ilianzishwa barani Afrika ili kukuza ufuatiliaji bora na ufanisi katika kutoa huduma kwa watu wa nchi zetu. Lakini urasimu unaweza kukosa kuwa na manufaa wakati utawala unakuwa changamano bila sababu na wenye fomu nyingi za kujaza, taratibu, na michakato isiyo na ufanisi, ambayo yote ni mambo yanayoweza kutoa fursa za ufisadi.

---

Fikiria kuhusu tatizo la urasimu na watu wanaotaka kuja kufanya kazi katika nchi yako. Nchi inaweza kusema kuwa inachukua siku 14 kupata kibali cha kufanya kazi, lakini kwa kweli, mchakato huo unaweza kuchukua zaidi ya mwaka mmoja. Fikiria kuhusu mfano huu: "Nchini Kamerun, inachukua mwekezaji ambaye anatafuta leseni ya biashara wastani wa siku 426 kutekeleza taratibu kumi na tano." Nchini Marekani, itachukua siku 40 tu kufanya taratibu 19.[5]

***Eleza jinsi miundombinu, utawala wa sheria, na urasimu unavyoweza kuathiri serikali za kigeni na kampuni za kigeni zinazotaka kuwekeza barani Afrika. Je, zitachaguaje nchi ambapo zitafanya kazi na kuwekeza?***

"Tume ya Afrika ilibaini kuwa uchumi wa Uganda ulikua kwa takriban asilimia 7 kati ya 1993 na 2002 wakati nchi hiyo ilipoboresha taratibu zake za udhibiti. Pia ilipunguza idadi ya watu wanaoishi chini ya dola moja kwa siku kutoka asilimia 56 katika mwaka wa 1998 hadi asilimia 32 katika mwaka wa 2002 baada ya serikali kuweka hatua za kuvutia wawekezaji."[6]

## Mifumo ya Kiuchumi

Mfumo wa kiuchumi unarejelea michakato na kazi za ndani za uzalishaji, ugawaji wa rasilimali na usambazaji wa bidhaa na huduma ndani ya jamii au eneo fulani la kijiografia.[7] Kwa maneno mengine, tunazingatia mifumo ya biashara, fedha, na usimamizi wa rasilimali.

---

Mifumo ya kiuchumi iliyovunjika inaweza kujumuisha:

- Mishahara midogo kwa wafanyakazi.
- Ukosefu wa huduma za benki, hasa katika maeneo ya vijijini.
- Mapato duni kwa serikali kutokana na wigo mdogo wa ukusanyaji wa ushuru.
- Ukosefu wa miundombinu, hasa barabara na aina zingine za usafiri, unamaanisha baadhi ya watu hawana uwezo wa kusafirisha mavuno na bidhaa zao hadi kwenye masoko ya ndani ya nchi au kuyasafirisha nje ya nchi.
- Ongezeko la idadi ya watu linazidi sana kasi ya kubuni nafasi za kazi katika nchi nyingi; hivyo, ukosefu wa ajira ni mkubwa sana.

Lakini baadhi ya mifumo ya kiuchumi iliyovunjika ni matokeo ya sera za nchi za nje au mikataba ya kimataifa. Kwa mfano:

Sio cha Kuuzwa

- Serikali za kigeni na kampuni za kigeni hujinufaisha na utayari wa Waafrika kufanya kazi kwa mishahara ya chini sana na kuuza maliasili kwa bei ya chini mno. Na wakati mwingine viongozi fisadi wa serikali barani Afrika pekee ndio wanaonufaika na uuzaji wa maliasili huku wenyeji wakitazama rasilimali zao zikichukuliwa. Kwa mfano, Nigeria imezalisha mafuta yenye thamani ya zaidi ya dola bilioni 400 tangu yalipogunduliwa huko katika miaka ya 1950, fedha zinazotosha kufuta madeni yote ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, zaidi ya asilimia 80 ya mapato ya mafuta yameenda kwa asilimia 1 tu ya watu, huku idadi kubwa ya watu ikizidi kuwa maskini, na kusababisha uasi wa kivita katika eneo la Niger Delta lenye utajiri wa mafuta.[8]

- Kuna ushiriki mdogo wa viongozi wa Afrika katika kuamua kanuni na masharti ya biashara ya kimataifa. Hii inaruhusu uwezekano wa nchi zingine kubuni sera na ushuru ambao ni kwa manufaa ya watu wao, lakini si kwa watu wa Afrika. Kwa mfano, "nchini Senegal, takriban nusu ya mashamba ya kuku yamefungwa kwa sababu ya ongezeko la asilimia 1,000 la uagizaji wa kuku kutoka Umoja wa Ulaya." "Uagizaji huu wa kuku kutoka nje unapata ruzuku wa kiasi kikubwa kutoka kwa Umoja wa Ulaya na kusababisha kusambaratika kwa uzalishaji wa ndani ya nchi."[9]

---

## Mikopo na Madeni
Mfumo mmoja wa uchumi wa kimataifa unaoathiri nchi za kiafrika ni mfumo wa mikopo na madeni. Nchi za Kiafrika zimepokea misaada na zimepokea pia kiasi kikubwa cha fedha za mikopo kutoka kwa serikali na benki za kigeni. Kutokana na viwango vya juu vya riba na fedha kidogo zinazokusanywa kwa njia ya kodi, nchi nyingi za kiafrika zinashindwa kulipa mikopo yao.

---

*Je, unafikiri suluhisho bora kwa mikopo hii isiyolipika ni nini? Je, nchi yako inafaa kuendelea kuchukua mikopo kutoka kwa mataifa ya nje?*

________________________________________

________________________________________

# Mifumo ya Kijamii Iliyovunjika

## Familia
Kuvunjika kwa mifumo ya kifamilia kunaweza kuonekana katika utengano na talaka katika ndoa, watoto wanaolelewa na mzazi mmoja, familia zinazoongozwa na watoto, kutelekezwa kwa watoto, unyanyasaji wa watoto na watoto kufanyishwa kazi,watoto wanaorandaranda mitaani na vijana wajeuri. Lazima kanisa lijaribu kusaidia familia zilizovunjika kupata amani na upatanisho unaopatikana katika Kristo pekee.

---

## Kanisa
Wakati fulani tunaendesha makanisa yetu kwa kufuata desturi, sera, na mifumo isiyompendeza Mungu. Baadhi ya desturi zetu hasa huwaathiri vibaya maskini wa mali.

Sio cha kuuzwa

Baadhi ya mifano inaweza kujumuisha:

- Nafasi nyingi za uongozi na fursa zinatolewa kwa matajiri wa mali, na kuwanyima maskini wa mali fursa ya kuhudumu.
- Makanisa mara nyingi huwakaribisha matajiri au watu wanaojulikana sana wakati wa ibada za Jumapili. Watu hawa hupewa viti vizuri vya kuketi na nafasi ya kuongea. Watu masikini hawatendewi kwa njia hiyo kila wakati.
- Watu wanaotoa kiasi kikubwa cha pesa za matoleo au michango ya kanisani wanatambuliwa na kupewa shukrani sana, huku maskini wanaotoa kiasi kidogo lakini kwa ukarimu mkubwa hawatambuliwi.
- Viongozi wa kanisa na washirika huungamkono na kuhudhuria mazishi na karamu za matajiri wa kutoka kanisani badala ya watu walio maskini wa mali.
- Harusi kanisani zinatarajiwa kuwa sherehe kubwa ambazo kila mtu anaweza kufurahia. Kwa hivyo, Wakristo maskini wanaweza kusubiri miaka mingi kabla ya kufunga ndoa kanisani huku wakijaribu kuweka akiba ya pesa ili kukidhi matarajio mengi ya kila mtu.
- Mara nyingi, kanisa huona ni rahisi kuwaadhibu watu walio maskini wa mali, lakini kwa matajiri wanaotoa pesa kanisani, nidhamu ya kanisani haitolewi. Dhambi zao zinavumiliwa.
- Baadhi ya wachungaji wanapendelea kuwatembelea, kuwashauri na kuwatunza matajiri kuliko maskini katika makanisa yao. Wanajua kuwa wanaweza kupokea zawadi za kifedha au chakula kutoka kwa nyumba ya tajiri, lakini maskini wa mali kutoka kanisani mwao wanaweza kukosa kutoa chochote.

*Eleza jinsi matendo haya yanavyochangia aina tano za umaskini kwa watu maskini katika makanisa yetu?*

## Utamaduni wa Jadi

Kuna thamani kubwa katika tamaduni zetu za jadi. Ni jambo zuri kujifunza hekima kutoka kwa mababu zetu na kuendeleza tamaduni zetu nyingi. Lakini wakati huo huo, baadhi ya mifumo yetu ya kitamaduni imevunjika na inawaweka watu kwenye mtego wa umaskini.

*Je, kama Wakristo, huu ni mfumo wa utamaduni wetu ambao tunapaswa kuukataa au kuuendeleza? Ikiwa mfumo husika ni mzuri na unapaswa kuendelezwa, je, tunahitaji kurekebisha chochote cha mfumo huo ili usitumiwe vibaya au usiwadhuru baadhi ya watu?*

*a. Ndoa za wake wengi*

*b. Adhabu za ukoo kwa uhalifu au kutotii*

*c. Mahari*

*d. Wajane kutorithi ardhi mume akifa*

Sio cha kuuzwa

*e. Viongozi wa kifalme wanaowakilisha, na kuongoza kila kabila*

---

*Je, unaweza kufikiria kuhusu mifumo yoyote ya kitamaduni iliyovunjika ambayo hatujaijadili bado?*

---

## Majadiliano ya Washirika

***Je, umewahi kuathiriwa na ufisadi? Je, tukio hilo lilikufanya uhisi vipi kuhusu mhusika huyo mwingine, kuhusu wewe mwenyewe, na kuhusu nchi yako?***

---

## Mhadhara wa Kiongozi: Ufisadi barani Afrika

Kati ya nchi kumi zinazochukuliwa kuwa fisadi zaidi duniani, sita ziko Kusini mwa Jangwa la Sahara, kwa mujibu wa shirika la Transparency International. Utafiti wa Umoja wa Afrika wa mwaka 2002 ulikadiria kuwa ufisadi unagharimu bara hili takriban dola bilioni 150 kwa mwaka. Linganisha hilo na kiasi cha misaada inayotolewa kwa bara la Afrika kila mwaka. Kwa mfano, dola bilioni 22.5 zilitolewa kama msaada kwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara katika mwaka wa 2008.[10]

***Hebu tuwe na ndoto pamoja. Je, ungeweza kufanya nini kwa ajili ya bara lako ukiwa na dola bilioni 150 za kukabiliana na umaskini na kuhamasisha maendeleo?***

---

Baadhi ya Waafrika wanasema kwamba tuna ugonjwa, na unaitwa "grabiosis (unyakuzi wa mali)". Tuna utamaduni wa kutaka kujinyakulia kila kitu tunachoweza.

---

Machoni pa Mungu wetu ufisadi ni dhambi mbaya ya tamaa na udanganyifu. Lakini kuna angalau sababu tatu zingine kwa nini ufisadi lazima upingwe na upunguzwe:[11]

1. Ufisadi husababisha uzembe. Pale ambapo huduma hutolewa tu baada ya malipo ya hongo au biashara inaweza tu kutekelezwa kwa kutoa malipo ya "chini ya meza", tunapoteza wakati, urasimu unazidi kuongezeka, gharama zinaongezeka, na ubora unaathiriwa.
2. Ufisadi hupelekea serikali kupoteza mapato kwa vile fedha zinazopatikana kwa njia za ufisadi hazitozwi kodi, na mara nyingi huelekezwa kwenye akaunti za benki za kigeni.
3. Ufisadi huwafadhaisha wawekezaji watarajiwa na kusababisha kukosa fursa za biashara na ajira.

Sio cha kuuzwa

Ni rahisi kwetu kuwakosoa wanasiasa na polisi wafisadi, lakini tunapaswa tujichunguze sisi wenyewe kwanza. Je, tumewahi kuiba chochote? Je, tumewahi kusema uongo?

> ***Je, ni dhambi gani kubwa zaidi, mwanasiasa kuiba shilingi milioni moja kutoka kwenye hazina ya umma, au mtu kuiba kuku kutoka kwa jirani yake?***

Wakati mwingine tunaanza tukiwa na uhakika kwamba kamwe hatutahusika katika ufisadi mahali petu pa kazi. Lakini hatua kwa hatua na kwa uhakika, tunabadilika hadi siku moja tunashangaa jinsi tulivyofanyika wafisadi. Na wakati mwingine tunahalalisha tabia zetu kwa kujiambia, "Kila mtu anafanya hivyo, kwa hivyo kuna ubaya gani mimi pia nikifanya hivyo?"

## Maswali ya Majadiliano:

> ***Je, tunatarajia kutendewa kwa upendeleo tunapokuwa na mtu wa ukoo katika cheo kikubwa, lakini wakati huo huo tunawakosoa wengine wanapopata upendeleo? Eleza.***
>
> ***Je, tunawakosoa wengine kwa kuwapigia kura watu wa kabila lao pekee, lakini sisi wenyewe tunafanya vivyo hivyo? Eleza.***
>
> ***Je, tunawakosoa wanasiasa kwa kutoa ahadi za uongo na kusema uongo kwa raia wa nchi yetu, lakini wakati huo huo tunawadanganya wanandoa wetu na marafiki zetu? Eleza.***

Ufisadi si dhambi tu ambayo Mungu anachukia, bali pia inaharibu ushuhuda wetu ulimwenguni. Huenda hongo ndiyo kikwazo kikubwa zaidi cha kueneza injili ulimwenguni leo hii. "Ikiwa watu hawahisi kuwa wanaweza kuamini kile tutakachofanya au kusema, ikiwa hawana uhakika kuwa tunafanya kazi kwa manufaa ya wote, au kwa manufaa yao binafsi, hawatachukua kwa uzito kile tunachosema kuhusu kitu chochote, ikiwa ni pamoja na habari njema ya Yesu Kristo."[12]

## Hongo na Unyang'anyi

**Hongo:** Kupitia hongo unatoa kitu ili upate manufaa fulani usiyostahili, kama vile kuomba fomu zako ziangaliwe kabla ya wengine wote waliowasilisha fomu zao mbele yako. Hongo pia inaweza kuwa kutoa kitu fulani ili usipate adhabu unayostahili, kama vile unapotoa pesa kwa polisi ili wasikuandikie taarifa ya kosa la barabarani kwa kuendesha gari kwa kasi. Kutoa hongo siku zote ni kosa na ni chukizo kwa Mungu.

**Unyang'anyi:** Unyang'anyi ni kitendo cha kupata pesa, mali au kitu kutoka kwa mtu mwingine kimakosa kwa kutumia nguvu, vitisho au vurugu. Kitendo hiki kwa kawaida hufanywa na watu walio madarakani au walio katika nyadhifa za mamlaka ambao hutumia vibaya nafasi zao kuwatisha na kuwanyang'anya wengine pesa au mali. Unyang'anyi ni wakati hujafanya kosa, lakini bado unaitishwa pesa.

Si cha Kuuzwa

*Tunakubaliana sote kuwa kutoa hongo ni makosa. Lakini je, ni dhambi kutoa pesa katika hali ya unyang'anyi?*

---

---

Ikiwa tutatoa pesa kila wakati kwa wale wanaotunyang'anya, wataendelea kufanya hivyo, na hata kuwanyang'anya wengine pia. Ni vyema tupinge unyang'anyi, kuwatangaza hadharani wale wanaowadhulumu wengine, na wakati mwingine tukubali kukabiliwa na adhabu kwa kufanya hivyo. Watu wanaowanyang'anya wengine hatimaye wanaweza kuacha kujaribu kufanya hivyo wakati badala ya kupata pesa, wanalazimika kupoteza wakati wao kuwapeleka watu jela. Huenda kufanya hivyo kutazua maswali kuhusu tabia zao.

---

## Kushinda Ufisadi na Mifumo Iliyovunjika

*Eleza hatua mahususi za kiutendaji tunazoweza kuchukua kibinafsi ili kupinga ufisadi na kile tunachoweza kufanya pia ili kushinda ufisadi nchini mwetu?*

---

---

Ikiwa sote tutashirikiana kwa ujasiri tukiwa na dhamira ya kuleta mabadiliko, kwanza kwa kufanya kazi ya kujibadilisha wenyewe, na kisha kushirikiana kubadilisha mifumo iliyovunjika, kunaweza kuwa na mabadiliko halisi. Mungu atatusaidia.

# Simulizi Kuhusu Ubaguzi wa Rangi nchini Afrika Kusini:

---

---

**Je, tunapaswa kuchukua hatua gani ili kushinda ufisadi na kuleta mabadiliko katika mifumo iliyovunjika?**

1. Tunahitaji kwanza kuzingatia kupatanisha mahusiano yaliyovunjika kati yetu na Mungu, nafsi zetu, watu wengine, na uumbaji.
2. Tunahitaji kuimarisha taasisi zetu na kuhakikisha kuwa watu wenye uwezo, uadilifu na ujuzi sahihi wanaajiriwa katika taasisi hizo. Tunahitaji kuhakikisha pia kuwa taasisi zinafadhiliwa ipasavyo na kwamba wafanyakazi wa serikali katika huduma ya polisi, hospitali na shule wanalipwa mishahara ya kutosha na wanalipwa kwa wakati unaofaa ili wasiweze kupata majaribu ya kushiriki kwenye ufisadi.
3. Tunahitaji sheria na sera nzuri zinazovutia uwekezaji na ukuaji na zinazobuni mazingira mazuri ya kazi, ili kuepuka urasimu mwingi usiohitajika.
4. Tunapaswa kuwahimiza viongozi wetu kutekeleza sheria kila wakati, na tunapaswa kuzungumza kila tunapoona sheria hazitekelezwi.



Sio cha kuuzwa

5. Tunapaswa kuwatuza wale walio uongozoni ambao ni waadilifu na wanajiepusha na ufisadi. Tuwapongeze hadharani na kuwaunga mkono katika kazi zao.
6. Tunahitaji kuripoti ufisadi hadharani popote tunapouona, iwe kanisani au serikalini au katika biashara.
7. Kama Waafrika, tunahitaji kutetea haki zetu katika vikao vya kimataifa, kuhusu sera za kimataifa, mashirika, miundo na mikataba ya kibiashara.
8. Tunahitaji kuomba neema na nguvu za Mungu ili tuwe na ujasiri wa kupitia mateso tunapopinga na kuripoti vitendo vya kutoa hongo, unyang'anyi, na ufisadi wa kila aina.

## Shughuli za Kufanya Baada ya Somo:

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisani au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi.

**1. Kwa viongozi wa kanisa:**

Pamoja na viongozi wa kanisa na washirika, tambueni mifumo iliyovunjika katika kanisa lenu na mjadili hatua za kiutendaji ambazo mnaweza kuchukua ili kuirekebisha. Andaeni mpango kazi unaojumuisha matatizo, masuluhisho, wahusika na muda uliopangwa wa utekelezaji. Wasilisheni mpango kazi wenu kwa washirika wa kanisa.

**2. Kwa wengine:**

Tambua mfumo mmoja uliovunjika katika jamii au nchi yenu ambao ungependa kuona ukibadilishwa. Jadili pamoja na wenzako na muandike mpango kazi pamoja ili kujaribu kuleta mabadiliko.

Sio cha kuuzwa

## Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

*1. Je, vifungu vilivyo hapa chini vinatufundisha nini kuhusu kupinga na kushinda ufisadi?*

---

*a. Kutoka 23:11*

---

*b. Kumbukumbu la Torati 1:17*

---

*c. Mithali 11:1*

---

*d. 1 Petro 2:12*

---

*(Maswali yanaendelea kwenye ukurasa wa 129)*

*2. Je, vifungu hivi vinatufundisha nini kuhusu kujaribu kubadilisha mifumo iliyovunjika na kuleta haki na usawa kwa wote?*

*a. Yakobo 2:1-7*

_______________

_______________

*b. Isaya 1:17*

_______________

_______________

*c. Isaya 58:3-7*

_______________

_______________

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Biashara au Misaada

Kuhusu mada ya mifumo ya kimataifa ya uchumi, kuna mjadala mkali kati ya viongozi wa dunia kuhusu kile ambacho kinaweza kuwasaidia Waafrika zaidi: sera bora za biashara au misaada zaidi kutoka nje au yote mawili?[13]

***Una maoni gani? Je, ingefaa zaidi kurekebisha baadhi ya mifumo ya kiuchumi iliyovunjika ya nchi yenu na kubadilisha sera za biashara ziwe zenye kufaa zaidi kwa Waafrika? Au ingekuwa vyema zaidi kupokea zawadi kubwa za msaada wa kifedha kwa ajili ya nchi yenu?***

_______________

_______________

Hakuna jibu rahisi kwa swali hili. Biashara na msaada yote ni muhimu sana katika kusaidia nchi kujiendeleza. Msaada kwa kawaida ni hatua ya uingiliaji kati ya muda mfupi ili kushughulikia haja ya dharura wakati biashara ni uhusiano wa muda mrefu unaochochea ukuaji wa uchumi wa nchi. Biashara ndiyo itakayosaidia nchi kujiendeleza kwa njia endelevu, ili zipate kile zinachohitaji wao wenyewe. Angalia faida na madhara ya msaada na biashara.

### Faida za Msaada

- Msaada ni muhimu katika kusaidia nchi kushughulikia masuala yao ya dharura kama vile njaa, majanga ya asili, magonjwa ya mlipuko, na mapungufu ya bajeti. Nchi nyingi za Kiafrika zinakabiliwa na hali kama hizo ambazo zinahitaji msaada wa kifedha kutoka nje kwani zinaweza kukosa uwezo na rasilimali za kuzishughulikia.
- Msaada unaweza kuipa nchi mtaji inayohitaji kujenga miundombinu kwa ajili ya maendeleo ya baadaye.

- Msaada unaweza kuwasaidia watu walio maskini sana na walio katika mazingira hatarishi, watu ambao hawatafaidika na sera mpya za biashara.

**Madhara ya Msaada**

- Msaada unaweza kwa urahisi kuwa chombo cha wafadhili wa kigeni kuwafanya viongozi wa Kiafrika kufanya wanavyotaka. Wakati mwingine masharti huambatanishwa na msaada ili kujaribu kuwahadaa Waafrika kubadili utamaduni na maadili yao.
- Nchi zinaweza kutegemea msaada na utegemezi huu unaweza kuzuia msukumo wa kubadilika na kujiendeleza.
- Msaada unaweza kukuza ukosefu wa usalama na ufisadi. Wale walio madarakani wakipokea msaada, hiyo inaweza kuwachochea wananchi wengine kuasi. Kuna ushindani katika suala la ni nani atakayedhibiti msaada huo na jinsi utakavyotumika.[14]
- Jambo la kusikitisha ni kuwa hapo awali viongozi wengi wa kiafrika wametumia msaada kujilimbikizia mali badala ya kutumia msaada huo kusaidia nchi zao.

**Faida za Biashara**

- Biashara ni muhimu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.
- Biashara husaidia nchi kujitegemea, na hivyo kuzisaidia kupunguza aibu na hali ya kujihisi duni.
- Biashara hukuza ushirikiano na kutegemeana kati ya nchi tofauti.
- Biashara huongeza ufikiaji wa rasilimali za kiuchumi ambazo nchi inayokua kiuchumi inahitaji, kupitia kubadilishana bidhaa na mawazo.
- Biashara hubuni ajira kwa watu kwani inavutia uwekezaji na kampuni za kigeni.

**Madhara ya Biashara**

- Si lazima biashara iwanufaishe watu ambao ni maskini sana wa mali, lakini huwanufaisha hasa watu wa tabaka la kati na la juu, walio na kazi nzuri na wanaoweza kufikia masoko.
- Biashara huria ni hatari kwa nchi zinazokua kiuchumi.
- Biashara inaweza kuhitaji uwekezaji wa awali kupitia msaada ili kuwa na faida.
- Baadhi ya nchi za Kiafrika hazina amani na utulivu wa kutosha kunufaika na sera mpya za biashara.

Nchi tofauti zinaweza kuwa na majibu tofauti kuhusu iwapo zinahitaji biashara au msaada. Lakini kwa jumla, jibu sahihi pengine ni kuwa tunahitaji biashara na msaada, lakini tunahitaji zifanyike kwa busara na haki. Hata hivyo, kwa sababu nchi nyingi barani Afrika zimetegemea msaada kwa muda mrefu, tunapendekeza kwamba leo hii tuzingatie zaidi biashara ili Afrika iweze kujiendeleza.

Zingatia maneno haya kutoka kwa Rais Wade wa Senegal katika mwaka wa 2002, "Sijawahi kuona nchi ikijiendeleza kupitia kwa misaada au mikopo. Nchi ambazo zimeendelea – barani Ulaya, Marekani, Japani, nchi za Asia kama Taiwan, Korea na Singapore – zote zinaamini mfumo wa masoko huria. Hakuna siri hapo. Afrika ilifuata mkondo usiokuwa sahihi baada ya kupata Uhuru."[15] Na kauli hii kutoka kwa Kofi Annan, katibu mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa, "Masoko wazi yanatoa tumaini pekee la kweli la kuwaondoa mabilioni ya watu katika nchi zinazokua kiuchumi kutoka katika umaskini uliokithiri, huku yakidumisha ustawi katika nchi zilizoendelea."[16]

Siyo cha kuuzwa

## Simulizi za kutia moyo kuhusu jinsi mifumo iliyovunjika na ufisadi unavyoweza kushindwa:

1. Simulizi hii ni nukuu kutoka katika kitabu cha, *The Bottom Billion*, kilichoandikwa na Paul Collier. Collier aliandika hivi:

   > Mashujaa hao ni Emmanuel Tumusiime-Mutebile, ambaye sasa ni gavana wa benki kuu ya Uganda, lakini katikati ya miaka ya 1990 alikuwa katibu mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, na Ritva Reinikka, mwanafunzi wangu wa zamani. Simulizi inaanza na Reinikka akiandaa utafiti wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma (utafiti uleule ambao ulifanywa nchini Chad). Hapo awali aliandaa utafiti huo kwa ajili ya Uganda, ambako uliibua matokeo ya kusikitisha: takriban asilimia 20 pekee ya fedha ambazo Wizara ya Fedha ilitoa kwa shule za msingi, kando na mishahara ya walimu, ndiyo iliyofikia shule hizo. Katika baadhi ya jamii serikali ingejaribu kuficha taarifa kama hiyo, lakini nchini Uganda, badala ya kuificha, Tumusiime-Mutebile aliitumia kama kichocheo cha kuchukua hatua. Bila shaka, hatua moja ingekuwa kuimarisha mfumo wa kutoka juu kwenda chini wa ukaguzi na uchunguzi, lakini walikuwa tayari wamejaribu hilo na ni dhahiri kwamba hawakufaulu sana. Kwa hivyo Tumusiime-Mutebile aliamua kujaribu mbinu tofauti kabisa: uchunguzi kutoka chini kwenda juu. Kila wakati Wizara ya Fedha ilipotoa pesa iliarifu vyombo vya habari vya kieneo, na pia ilituma bango kwa kila shule linaloeleza kiasi inachopaswa kupata. Tumusiime – Mutebile ni mtu wa vitendo ambaye alitaka kujua ikiwa hatua zilikuwa zikifua dafu, kwa hivyo miaka mitatu baadaye alirudia utafiti huo wa ufuatiliaji. Sasa, badala ya asilimia 20 tu kufika shuleni, asilimia 90 ndizo zilizokuwa zikifika shuleni. Katika utafiti wa takwimu wa hali ya juu ambao ulichanganua jaribio hili kwa kina, Reinikka na mwenzake Jakob Svensson waliweza kuonyesha kuwa vyombo vya habari vimeleta mabadiliko makubwa – katika hali hii kupitia ripoti katika magazeti. Kwa hivyo uchunguzi uligeuza asilimia 20 kuwa asilimia 90, hatua yenye ufanisi zaidi kuliko kuongeza msaada maradufu kisha kuuongeza maradufu tena.[17]

2. Simulizi hii ni nukuu kutoka kwenye kitabu cha, *The Challenge for Africa*, kilichoandikwa na Wangari Maathai. Aliandika hivi:

   > Nchini Kenya mnamo mwaka wa 2002, muungano wa vyama vya kisiasa hatimaye ulimwondoa mamlakani Rais Daniel arap Moi, na utawala mpya wa kwanza katika miaka ishirini na minne ukaingia madarakani. Roho mpya ya shauku ilienea nchini; kwa kweli, kulikuwa na nia njema wakati serikali mpya ilipoundwa kiasi kwamba kitu cha ajabu kilifanyika: kote nchini Kenya, "mashine ya kijamii" ilianza kusonga tena. Huu hapa mfano mmoja tu. Kwa miaka mingi, polisi walikuwa wanachukua hongo kutoka kwa madereva wa matatu, magari madogo ya kibinafsi ya bei nafuu, ambayo, kwa kuzingatia hali mbaya ya uchukuzi wa umma, ndiyo njia kuu ya usafiri kwa mamilioni ya Wakenya. Kwa madereva, hongo zilikuwa gharama inayokubalika ya kufanya biashara – ikiwaruhusu wao na si dereva mwingine kufanya kazi katika barabara fulani, au kuhakikisha kuwa maafisa wa polisi watapuuza ukiukaji wowote wa sheria unaohusiana na hali ya gari au uendeshaji wa gari. Matatu zilikuwa hatari sana: ajali zinazotokana na uendeshaji kwa mwendo wa kasi zilikuwa za kawaida, na maelfu ya watu walikuwa wakipoteza maisha kila mwaka. Licha ya hayo, watu hawakuwa na njia nyingi mbadala za usafiri hivyo walilazimika kuendelea kutumia matatu. Baada ya uchaguzi wa 2002, abiria wa matatu walianza kupinga polisi yeyote aliyedai hongo kutoka kwa dereva. Wakiwa wametiwa motisha na serikali mpya, iliyoapa kupatia kipaumbele vita dhidi ya ufisadi uliokithiri katika jamii kutoka ngazi za chini hadi za juu, wananchi wa kawaida walisimama kidete na kuwataka polisi na madereva wasifanye kazi kama kawaida. Ilifikia hatua ambapo polisi waliacha kuitisha hongo, iwe kwa sababu waliogopa hatua itakayochukuliwa na abiria wa matatu, au labda, kwa sababu hata wao walikumbatia roho hiyo mpya iliyokuwa imeibuka na kutekeleza wajibu wao wa kutoa huduma bila kudai hongo. Madereva wa Matatu pia walianza kutii vikomo vya mwendo kasi na kukubali kutii agizo jipya la serikali la kuweka mikanda ya usalama, hatua ya kiusalama ambayo pia inaweka kikomo katika idadi ya abiria kwenye gari. (Hapo awali, madereva wangebeba watu wengi kadiri walivyoweza, hata wakati abiria walikuwa wakining'inia nje ya milango.) Huu ulikuwa ushahidi wa "Kenya mpya" ambayo wananchi walitaka kuwa nayo na waliamini kuwa

> inawezekana, baada ya miongo kadhaa ya serikali kudharau matarajio yao ya kuwa na jamii iliyo na uadilifu na yenye haki zaidi. Lakini mara tu ilipodhihirika kuwa watu binafsi katika serikali mpya hawakuwa waaminifu na walikataa kuheshimu ahadi walizoahidiana wakati wa kampeni, roho mpya iliyokuwa imeibuka ilipotea ghafla; na Jambo la kusikitisha ni kuwa, baada ya muda usio mrefu sana watu wengi walirudi kwenye tabia mbaya za zamani.[18]

3. Simulizi hii inasimuliwa na mmishonari Mmarekani, Renita Reed, kuhusu mfanyabiashara mmoja nchini Ethiopia. (Jina lake limebadilishwa kwa ajili ya usiri). Moses alifanya kazi kama meneja katika kampuni ya samani kwa miaka kumi na minne. Alijulikana kama meneja ambaye hangekiuka maadili yake. Hatimaye alihisi Mungu akimwita aachane na biashara hiyo na kuanzisha yake. Moses alianza kuagiza samani za ofisi za ubora wa juu kutoka China, akifanya kazi hasa kupitia kandarasi (pia huitwa "zabuni") kutoka kwa ofisi mbalimbali za serikali, biashara, au taasisi. Biashara zinazoendeshwa kupitia kwa kandarasi au zabuni mara nyingi hukumbwa na uwezekano wa kutokea kwa ufisadi, kwani mara nyingi kandarasi hiyo hupewa yule aliye tayari kuwahonga watu wanaohusika na maamuzi. Walipofungua biashara hiyo, Moses na mkewe waliamua kwamba hawatatoa au kupokea hongo. Moses alisema: "Kila hongo ina wahusika wawili – mtoaji na mpokeaji. Ikiwa sote tutaacha kuwa watoaji, wapokeaji watafanya nini?" Huu haukuwa uamuzi rahisi kwao. Moses alipoteza kandarasi nyingi sana kwa sababu hakuwa tayari kutoa hongo. Lakini baada ya muda, na kwa sababu alisisitiza kuuza samani za ubora wa juu, alianza kujulikana kama mfanyabiashara mwenye uadilifu ambaye bidhaa zake zilidumu zaidi kuliko za washindani wake. Hatua hii imemfungulia milango ya kuwa na mazungumzo mengi, hasa na viongozi wa serikali (hata wale ambao ni Wakristo) kuhusu kufanya kazi kwa uaminifu. Lakini mojawapo ya mambo makuu ambayo yamemfanya awe mwadilifu kila wakati ni ukweli kuwa yeye na familia yake wameamua kuishi chini ya uwezo wao wa kifedha, ili siku zote wawe na chaguo la kukataa kandarasi zinazodai hongo. Moses alisema, "Furaha yangu haitokani na pesa katika biashara yangu, bali katika kuridhika kwa kufanya kazi vizuri." Moses ni mfano wa mtu mwenye ujasiri wa kuwa nuru katika mahali penye giza.[19]
4. Mji wa Gulu Kaskazini mwa Uganda una baadhi ya viwango vya juu zaidi vya unywaji pombe barani Afrika, na kuna visa vingi vya watu ambao maisha yao yameharibiwa na uraibu wa pombe. Ilikuwa maarufu kuuza pombe katika mifuko ya plastiki yenye rangi ya mililita 100. Watoto waliweza kuinunua na kuificha mifukoni mwao. Mnamo mapema 2015, kikundi cha eneo hilo, Wakonye Kenwa, kiliamua kuwa wakati wa mabadiliko umefika. Kwa miaka mingi, viongozi wa kidini, mashirika mbalimbali yasiyo ya serikali na vikundi vya jamii vilikuwa vimelalamikia tatizo la pombe. Juhudi za pamoja, za kimkakati zilihitajika. Kwa pamoja Wakristo walikusanya data na simulizi za kibinafsi kutoka kwa jamii kuhusu athari za pombe. Waliwasilisha ripoti kwa Serikali ya Wilaya, wakionyesha haja ya kuweka sheria mpya. Ombi lilitiwa saini na viongozi wakuu wa kidini wa Gulu wakitaka kupigwa marufuku kwa pombe inayouzwa kwenye mifuko. Zaidi ya saini 10,000 zilikusanywa. Wachungaji na viongozi wengine wa jamii waliandamana mjini ili kuwasilisha ombi hilo kwa maafisa husika. Viongozi wa wilaya walitangazia umati kuwa, "hatutawaangusha." Hatimaye, sheria hiyo ilipitishwa mnamo Oktoba 2016. Lakini ni rahisi kupitisha sheria mpya kuliko kuitekeleza. Baada ya matukio machache ya kukamatwa kwa pombe hiyo, wanasiasa wa kitaifa wenye ushawishi na viongozi wa polisi walikasirika. Juhudi zilifanywa kuhujumu sheria hiyo kupitia hongo na shinikizo la kisiasa. Lakini Wakonye Kenwa na viongozi wengine wa jamii hawakukata tamaa katika kujaribu kuleta mabadiliko. Hatimaye, waliweza kuwashawishi viongozi wa wilaya kubuni timu mahususi ili kuhakikisha sheria zinatekelezwa. Hii leo, mauzo ya pombe inayouzwa kwenye mifuko yamepungua sana na pombe hiyo inaweza kununuliwa tu kwa siri. Hivi sasa ulevi unaoonekana katika mitaa ya jiji umepungua sana. Ilichukua miaka mingi kuleta mabadiliko, lakini kwa uvumilivu, kushirikiana pamoja, na nguvu za Mungu, mabadiliko yanawezekana![20]
5. Sikiliza simulizi hii ya kweli ya Mary Crickmore katika mtaala wake uitwao "Shalom: Mwongozo kwa Wafanyakazi Wakristo". Majina yamebadilishwa. Crickmore aliandika hivi:

> Mary alikuwa mwanamke mwenye umri mdogo ambaye mume wake aliugua sana. Alifanya kazi kwa bidii ili kukimu mahitaji ya familia yake kwa kuwa mume wake hangeweza kufanya

Sio cha Kuuzwa

kazi. Baada ya muda, mumewe akafariki. Ndugu ya mume wake alikuja na kumwambia aondoke kwenye nyumba kwa sababu aliihitaji. Yeye na jamaa zake wengine walikuja na kuchukua samani zote. Kwa sababu hili lilikuwa kabila ambalo lilikuwa na mila ya kuwa mali yote ni ya jamaa za mume daima, hakuna aliyewazuia kufanya hivyo. Wajane wengine wengi walikuwa wamefanyiwa jambo hilo katika mji huo. Na kwa sababu watu wengi mahali hapo walikuwa na UKIMWI kulikuwa na wajane wengi. Dhehebu la kanisa la Mary liliamua kuwa wanataka kuwasaidia wajane. Walianzisha mpango wa kutoa mikopo midogo midogo, lakini waligundua kuwa walihitaji pia kushughulikia sababu kuu ya wajane wengi kuwa maskini. Waliweka sheria kwa makanisa yao yote kuwa mtu yeyote asichukue nyumba au samani kutoka kwa dada au binti-mkwe ambaye ni mjane. Na wakaanza mafundisho ya kuzuia UKIMWI makanisani mwao.[21]

6. Tembelea tovuti hii ili uone jinsi Kampala Pentecostal Church (Kanisa la Kipentekoste la Kampala) nchini Uganda lilivyoamua kuonyesha upendo kwa jeshi la polisi kupitia Siku ya Kuwashukuru Polisi – https://www.youtube.com/watch?v=S0lSAzqWp_8

Sio cha kuuzwa

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na Picha ya Adobe Stock.

[1] "Can Africa Afford Free Education?", *Global Education Monitoring Report*, (World Education Blog, Januari 27, 2017) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://gemreportunesco.wordpress.com/2016/01/27/can-africa-afford-free-education/.

[2] "State of education in Africa report 2015", (The Africa-America Institute, New York, NY 2015), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.aaiafrica.org/soe/2015?rq=soe%202015.

[3] Ibid.

[4] https://www.vocabulary.com/dictionary/bureaucracy.

[5] Dambisa Moyo, *Dead Aid: Why Aid is Not Working and How There Is a Better Way for Africa,* (New York, Farrar, Straus, and Giroux, 2009), Kindle ed., Location 1706-9.

[6] Ibid., Location 1717-20.

[7] Daniel J. Cantor, Juliet B. Schor, *Tunnel Vision: Labor, the World Economy, and Central America*, (South End Press, 1987), ukurasa wa 21.

[8] Carmody Pádraig, *The New Scramble for Africa*, toleo la 2., (Polity; 24 Octoba, 2016) Highlight Loc. 3069-72.

[9] Ibid., Highlight Loc. 1450-53.

[10] Stephanie Hanson, "Corruption in Sub-Saharan Africa", Transparency International (Council on Foreign Relations, 6 Agosti, 2009) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.cfr.org/backgrounder/corruption-sub-saharan-africa.

[11] A. S. Moreau et al., *Evangelical Dictionary of World Missions*, (Baker Books, Grand Rapids, MI; 2000), 233.

[12] https://www.lausanne.org/networks/issues/integrity-and-anti-corruption.

[13] "Aid vs. Trade", (EIIFF), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://web.archive.org/web/20181120102223/http://www.eiiff.com/aid/trade.html.

[14] Paul Collier, *The Bottom Billion: Why the Poorest Countries Are Failing and What Can Be Done about It,* (Oxford University Press, 2007), Kindle ed., Loc. 1716.

[15] Imenukuliwa na Dambisa Moyo, *Dead Aid: Why Aid is Not Working and How There Is a Better Way for Africa,* (New York, Farrar, Straus, and Giroux, 2009), Kindle ed., Loc. 2489-91.

[16] Kutoka kwa mahojiano na Kofi Annan na *The Globalist*, (Februari 6, 2001), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.theglobalist.com/kofi- annan-on-global-futures/.

[17] Paulo Collier, *The Bottom Billion*, Loc. 2502-13.

[18] Wangari Maathai, *The Challenge for Africa,* (New York: Pantheon Books, 2009). Kindle, ed., Loc. 1826-45.

[19] Renita Reed, mawasiliano ya kibinafsi na inaweza kufikiwa mtandaoni katika: http://reedsinthewind.blogspot.com/2016_05_30_archive.html.

[20] Mawasiliano ya kibinafsi kutoka kwa Tessa Laing.

[21] Mary Crickmore, "Shalom: A Manual for Christian Workers", (kuchapishwa binafsi, 2011), 15.

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



## Somo la 12: Injili ya Mafanikio

sio cha kuuzwa

# Swali la Majadiliano la Ufunguzi

*Eleza kwa ufupi jinsi unavyoweza kufafanua "injili ya mafanikio", inayojulikana pia kama "injili ya afya na utajiri".*

Injili ya mafanikio inawaumiza watu walio maskini wa mali.

Umaskini hauna suluhisho la haraka na rahisi, lakini bado kuna tumaini la mabadiliko kwa sababu ya Kristo.

Sio cha kuuzwa

# Majadiliano ya kikundi kikubwa

*1. Je, ni mafundisho gani ya injili ya mafanikio yanafunzwa nchini mwenu?*

*2. Je, umeona mafundisho gani ya injili ya mafanikio katika kanisa lako mwenyewe au miongoni mwa marafiki zako Wakristo?*

*3. Je, mafundisho haya yameathiri watu unaowajua vyema au vibaya?*

# Mhadhara: Kwa Nini Injili ya Mafanikio ni ya Uongo

1. Mafundisho ya mafanikio hufasiri vibaya vifungu vya Maandiko kwa kupuuza muktadha wao.[1]

**Yohana 8:32-32**

---

**a.** Wanafasiri vibaya **Yeremia 29:11.**

---

**Yeremia 29:10-14**

---

**Warumi 8:28**

---

**b. 2 Wakorintho 9:6-15**

---

***Je, wahubiri wa injili ya mafanikio hawaelewi nini kuhusu kifungu hiki?***

---

Kupanda na Kuvuna

---

Mungu hutoa ili tuwe wakarimu.

---

**2. Mafundisho ya mafanikio hukuza uhusiano wa hila na Mungu.**

---

Mungu si kifaa, bali ni Mungu aliye hai ambaye tunahitaji kumwabudu.

---

Hatupaswi kumhonga Mungu.

---

***Baadhi ya Wakristo wameona mfanano kati ya Dini za Jadi za Kiafrika na injili ya mafanikio. Je, ni kweli kuwa zote mbili hulenga kutumia matambiko na dhabihu ili kushawishi nguvu za kiroho kwa lengo la kukidhi mahitaji yetu? Eleza jibu lako.***

---

Sio cha kuuzwa

**Luka 1:37**

---

**3. Mafundisho ya mafanikio yanakosa kutambua kwa usahihi hitaji kuu zaidi la binadamu.**[2]

---

Hitaji letu kuu zaidi ni kuokolewa kutokana na dhambi zetu na kupatanishwa na Mungu.

---

**4. Mafundisho ya mafanikio hayaelewi asili halisi ya umaskini.**
Mafundisho ya mafanikio yanadai kuwa umaskini una uhusiano wa moja kwa moja na dhambi za watu. Ingawa ni kweli kuwa kisababishi kikuu cha umaskini wote ni dhambi kuingia katika ulimwengu huu na Uumbaji kulaaniwa wakati wa Adamu na Eva (angalia Somo la 3), hiyo ni tofauti sana na kusema kuwa umaskini wa mtu daima ni matokeo ya moja kwa moja ya dhambi zake wenyewe au maisha yake yasiyo ya kiroho.

---

Kuna visababishi vingi vya umaskini kando na maisha ya dhambi: kuabudu sanamu, mahusiano yaliyovunjika, majanga ya asili, nguvu za pepo, na mifumo ya serikali iliyovunjika tukitaja vichache.

Simulizi ya Ayubu

---

**5. Mafundisho ya mafanikio yanadai kwa uongo kuwa ukomavu wa kiroho unaweza kupimwa kwa mali na kwamba mali siku zote ni ishara ya baraka za Mungu.**[3]

Walimu wa mafundisho ya mafanikio huona mali kama ishara ya utakatifu na kusema kuwa mtu ambaye ni tajiri amebarikiwa na Mungu. Kinyume cha hilo, Biblia huonyesha wazi kuwa wakati mwingine wenye haki huteseka, na wakati mwingine waovu hufanikiwa. Afya njema na mali hazipaswi kuchukuliwa kuwa ishara za baraka za Mungu.

**Mithali 28:6**

---

**Kumbukumbu la Torati 32:15**

---

Injili ya mafanikio inahusisha utajiri, cheo, na afya ya mtu na kiwango chake cha imani. Kwa jumla, mtu anayempokea Kristo na kuacha tabia fulani za dhambi kama vile uvivu au uasherati, mara nyingi atapata uboreshaji wa hali yake ya afya na ya kifedha. Lakini kwa kuwa kuna visababishi vingine vya umaskini kando na dhambi ya mtu binafsi, hatuwezi kubaini utakatifu wa mtu au ukomavu wake wa kiroho kwa kuzingatia kiasi cha fedha alicho nacho.

*Unapomwona kiongozi wa kanisa au kiongozi wa jamii akiendesha gari, mtazamo wako wa kwanza ni upi kuhusu ukomavu wake wa kiroho? Unapomwona ombaomba akiwa ameketi chini, mtazamo wako wa kwanza ni upi kuhusu ukomavu wake wa kiroho? Je, tunaweza kufanya mambo gani mahususi ili kubadilisha mitazamo yetu?*

---

---

Sio cha kuuzwa

**6. Mafundisho ya mafanikio huwahimiza watu kutoa hasa ili kupokea manufaa ya mali.**

**2 Wakorintho 9:7**

Tunapaswa kutoa kwa uchangamfu kwa sababu tunampenda Mungu, tunawapenda maskini, na kama njia ya kumwabudu na kumshukuru Mungu.

Baraka huja kwa namna mbalimbali.

> ***Wachungaji wanapohubiri kuhusu kutoa katika kanisa lako, je, wanawaambia watu watoe kwa nia gani?***

**7. Mafundisho ya mafanikio hufanya pesa kuwa sanamu na huhimiza uchoyo.**

**Mathayo 6:24**

**Luka 12:15**

Mungu anapaswa kuwa zingatio letu kuu si pesa.

> ***Je, injili ya mafanikio inaweza kuchangia ufisadi barani Afrika au kuongezeka kwa pengo kati ya matajiri na maskini kwa njia gani?***

**8. Mafundisho ya mafanikio hayajumuishi ujumbe wa kujikana.**

Sio cha kuuzwa

Matajiri wanaweza kuhudhuria makanisa ya kuhubiri mafanikio ili wajihisi vizuri na maisha yao yenye anasa.

---

Injili ya mafanikio inatuhimiza kumkana Yesu na kufuata tamaa zetu za kimwili wakati Yesu anatuita tujikane wenyewe na kumfuata yeye.[4]

---

**9. Mafundisho ya mafanikio hayaelewi maana ya kuwa na imani yenye nguvu.[5]**

---

Theolojia ya "Neno la imani" inadai kuwa imani yetu inaweza kusababisha hali halisia.

---

Imani inahusu kuamini katika upendo na nguvu za Mungu, si kutumainia nguvu zetu wenyewe.
**Mathayo 9:28-29; Waefeso 2:8-9**

---

**10. Mafundisho ya mafanikio yanathamini mapenzi ya mwanadamu kuliko mapenzi ya Mungu.**

---

**Yohana 14:13-14** inasema kuwa Mungu atatufanyia lolote tutakalo.

---

Lakini katika Biblia, tunaona Wakristo wakiteseka. Na wakati mwingine hatupati tunachoomba katika maombi.
**2 Wakorintho 12:7-10**

---

Fasiri vifungu vya Biblia vinavyokanganya kwa kuangalia vifungu vingine.
**1 Yohana 5:14-15**

---

Kile tunachoomba kinapaswa kuendana na mapenzi ya Mungu na mpango wake kwa maisha yetu. Kuomba katika jina la Yesu hakuhusishi kutamka maneno ya kimazingaombwe bali kunaonyesha ulingano kati ya matamanio ya mtu na makusudi ya Mungu.[6]

**Luka 22:42**

---

**Mathayo 5:10**

---

Sio cha kuuzwa

**Warumi 8:28**

---

Mpango wa Mungu ni mzuri kwetu hata wakati hatupati kile tunachoomba na hata wakati hatuelewi mpango wake. Tunapaswa kumwamini yeye kama Baba yetu wa mbinguni.
**Mathayo 7:9-11**

---

*Je, umewahi kumwomba Mungu kitu ambacho hukupokea? Mungu alikufundisha nini kupitia hali hiyo?*

---

**11. Mafundisho ya mafanikio yanaahidi kwa uongo uponyaji kutokana na magonjwa yote katika maisha haya kwa Wakristo waaminifu.**
Waumini wa injili ya mafanikio wanasema kuwa kuna uhusiano kati ya afya njema na haki ya kiroho ya mtu.

---

**Isaya 53:5**

---

**1 Petro 2:24**

---

Wahubiri wa injili ya mafanikio wanasema kuwa tutaponywa kila tunapoomba ikiwa tuna imani ya kutosha. Hii inasababisha Wakristo kuwatuhumu wagonjwa kwa dhambi au imani dhaifu badala ya kuwajali. Hakika Mungu ana uwezo wa kuponya na sisi sote tunaweza kushuhudia uponyaji wa Mungu katika maisha yetu. Hata hivyo tunajua kuwa hatuponywi kila wakati tunapotaka. Tunaponywa kulingana na mpango wa Mungu na mapenzi ya Mungu kwa maisha yetu. Hata Paulo hakuponywa kila alipoomba.

**2 Wakorintho 12:7-10**

---

**1 Timotheo 5:23**

---

Wakati mwingine tunaponywa papo hapo, wakati mwingine inatubidi tusubiri uponyaji kwa muda mrefu, na wakati mwingine hatuponywi kabisa. Sote tutakufa hatimaye. Tunasubiri uponyaji wetu kamili wakati wa ufufuo wa wafu.

**12. Mafundisho ya mafanikio hayazingatii mafundisho ya Biblia kuhusu mateso katika maisha ya Kikristo.**

Sio cha kuuzwa

*1. Kulingana na Biblia, tunapaswa kutazamia kupata mateso ya aina gani kama Wakristo wakati mwingine maishani mwetu?*

___

*2. Fikiria kuhusu watu waliotajwa katika Biblia waliokuwa maskini. Orodhesha majina yao mengi kadri unavyoweza kufikiria.*

___

Wahubiri wa injili ya mafanikio hupuuza kwa kiasi kikubwa mada muhimu sana ya kibiblia ya mateso. Biblia inafundisha nini? Zifuatazo ni baadhi ya kanuni muhimu za kibiblia kuhusu mateso:

a. Kisababishi kikuu cha mateso na umaskini ulimwenguni ni dhambi. Tunateseka kwa sababu ya laana iliyokuja wakati Adamu na Eva walipotenda dhambi. Na kumbuka tulichojifunza katika Somo la 3 kuhusu mahusiano manne yaliyovunjika. Tunateseka kwa sababu tunamtenda Mungu dhambi na tunakoseana. Kwa sababu Yesu anafanya kazi katika ulimwengu huu, tunaweza kutumaini kuona mabadiliko na maendeleo katika maisha haya, lakini sote tutaendelea kupata mateso katika ulimwengu huu hadi Yesu atakaporudi.

b. Mungu ni mkuu na anatawala ulimwengu huu. Anajua yajayo. Hakuna kinachomshangaza. Yeye ni mweza yote na ni mkuu. Kwa hivyo, chochote kitakachotokea, hata mambo maovu yanapotokea, yote yanaendana kwa namna fulani na mpango wake wa jumla wa ulimwengu huu.

**Mithali 16:33**

___

**Mathayo 10:29-30**

___

Tunajua kuwa Mungu ana nguvu za kutosha kutumia uovu na mateso kuleta wema.
**Mwanzo 50:19-20 na Warumi 8:28**

___

Hatuelewi mpango wa Mungu siku zote, lakini tunajua kuwa mpango wake ni mzuri kwa sababu Mungu ni mwema, mwenye upendo, na mkamilifu. Na mateso yetu ni ya muda mfupi. Tutapata ufufuo na uzima wa milele usio na maumivu au umaskini tena.

c. Tunaweza kumweleza Mungu tunapoteseka.

**Zaburi 13**

___

Na ikiwa Mungu ataondoa mateso yetu au la, ni lazima tuendelee kumsifu na kumtii, tukitumainia mpango wake mzuri kwa maisha yetu.

d. Tunapaswa kutarajia kuteseka kwa sababu Bwana wetu Yesu aliteseka pia na tumeunganishwa naye.
**Warumi 8:17**

___

**Yakobo 1:2-4**

___

Si cha kuuzwa

**Warumi 5:3-5**

Mungu anaweza kutumia mateso katika maisha yetu:

- Ili kuwasaidia wengine.
- Ili kutuadhibu ili tukue katika utakatifu.
- Ili kutufundisha uvumilivu.
- Ili kujaribu imani yetu kama Ayubu.
- Ili kutufanya tusijaribiwe kutenda dhambi.
- Ili kutusaidia kujifunza kumtegemea na kumtumainia Mungu.
- Ili kuwavuta wengine kwa Kristo kupitia kwa ushuhuda wetu wa kumsifu Mungu hata katika mateso yetu.
- Ili kutusaidia kujua jinsi ya kuwa washauri bora kwa wengine wanaoteseka.

Angalia mfano wa msalaba.

## Usivunjike moyo

Tunaamini kuwa Yesu anafanya kazi katika maisha yetu na katika ulimwengu huu kuleta uponyaji na upatanisho.

Tatizo ni kuwa walimu wa injili ya mafanikio huahidi maisha bila mateso, umaskini, na magonjwa ikiwa mtu ana imani ya kutosha na anaishi maisha ya utiifu. Ingawa kuwa na imani katika Kristo na kuishi maisha ya utiifu mara nyingi kutapunguza umaskini wa mtu, si kweli siku zote katika kila hali. Wakati mwingine tunapitia umaskini kutokana na mifumo iliyovunjika, majanga ya asili, mateso, au sababu zinginezo zinazolingana na mpango wa Mungu kwa maisha yetu.

Kama wahubiri wa injili ya mafanikio tunataka kuona Wakristo wakipiga hatua za maendeleo na kuona kupungua kwa aina zote tano za umaskini. Lakini njia ya kufanya hilo ni kwa kuzingatia Mungu na kushiriki katika huduma ya upatanisho. Hatupaswi kuwapa watu ahadi za uongo au kuwatia moyo watu waabudu sanamu ya pesa kwa kiu ya kuwa matajiri. Badala yake, tunataka watu wafanye kazi kwa ajili ya maendeleo na uzalishaji wa utajiri kama njia ya kumtumikia Kristo na njia ya kuongeza uwezo wao wa kuwa wakarimu kwa wengine.

Si o cha kuuzwa

# Uigizaji

# Injili ya Mafanikio Inawaumiza Maskini

## Majadiliano ya Kikundi Kikubwa

*1. Je, injili ya mafanikio inawaumiza watu walio maskini wa mali kwa njia gani?*

---

*2. Ikiwa Wakristo katika kanisa la kieneo wameamini theolojia fulani ya mafanikio, wanawezaje kuwatendea vibaya watu maskini au wagonjwa katika kanisa lao bila kukusudia?*

---

Injili ya mafanikio huongeza umaskini wa nafsi. Inakuza hisia ya kujihukumu na aibu kati ya watu walio maskini wa mali na wagonjwa.

---

---

Injili ya mafanikio huongeza pia umaskini wa nafsi wa matajiri kwa kuzidisha hali yao ya kujiona kama Mungu.

---

Injili ya mafanikio inasisitiza utajiri wa mtu binafsi na mafanikio, bila kuzingatia hitaji la uwajibikaji wa jamii. Hilo limeharibu sifa nzuri ya utamaduni wa Kiafrika, kujitolea kuwajali wengine ndani ya familia kubwa na jamii pana.[7] Injili ya mafanikio husababisha watu kuonyesha upendeleo kwa matajiri, kwa kuwa hali ya kifedha inaonekana kama ishara ya ukomavu wa kiroho wa mtu.
**Yakobo 2:1-7**

---

*Je, kanisa lako linatii au halitii kanuni zilizo katika Yakobo 2:1-7 kwa njia gani?*

---

Injili ya mafanikio inakosa kuwatia moyo Wakristo kufanya kazi kwa bidii na kuwa wabunifu ili kushinda umaskini wa mali. Badala yake, mafundisho ya mafanikio yanawahimiza Wakristo kuomba, kuketi, na kungojea Mungu awatumie tu muujiza. Hii ndio maana Wakristo wengi siku hizi wanatumia muda wao mwingi kanisani kwa maombi, wakiwaomba wachungaji waombee upenyo na kumwomba Mungu mali, huku wakipuuza karama na uwezo ambao Mungu aliwabariki nao.

---

Injili ya mafanikio itasababisha baadhi ya watu kumkataa Mungu na Kanisa.

---

Sio cha kuuzwa

# Kushinda Injili ya Mafanikio

## Ili kushinda injili ya mafanikio barani Afrika lazima:

- Tutubu kwa jinsi tulivyokuwa tukiwatendea watu walio maskini wa mali, na kutubu ikiwa tumewahi kufundisha theolojia ya mafanikio.
- Tujitoe kuhubiri injili ya kweli hata kama haipendelewi.
- Soma, jifunze, na ufundishwe Neno la Mungu.
- Kutoa kwa ukarimu kwa watu walio maskini wa mali katika makanisa na jamii zetu badala ya kuwatumia vibaya kama wahubiri wa injili ya mafanikio wanavyofanya.
- Toa mafunzo ya uanafunzi na mafundisho hasa kwa wachungaji na viongozi wa kanisa.
- Hakikisha kuwa makanisa yana taratibu thabiti za uwajibikaji, ili viongozi wa kanisa na wamisionari waweze kuwajibika kwa kile wanachohubiri na jinsi wanavyoenenda. Katika hali zingine, serikali inaweza hata kufanya kazi na madhehebu ya kanisa kuweka sera nzuri ambazo zitawazuia wahubiri wa injili ya mafanikio kuwadanganya na kuwatumia vibaya maskini.

*Je, kuna taratibu gani mahususi za uwajibikaji kwa viongozi wa kanisa lako na kwa kanisa lako la kieneo? Je, zinafanya kazi vizuri?*

______________________________

______________________________

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya baada ya Somo:

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi:

**1. Kwa viongozi wa kanisa,** chagua mojawapo ya yafuatayo:
**a.** Hubiri na utangaze waziwazi habari njema kuhusu wokovu katika Kristo.
**b.** Ikiwa una darasa la shule ya Jumapili ya watu wazima, wafundishe washirika wa kanisa lako kuhusu makosa ya injili ya mafanikio kama ilivyoelezwa katika somo hili.
**c.** Hubiri kuhusu mojawapo ya vifungu kuhusu kuteseka kutokana na maswali ya majadiliano ya kikundi.

**2. Kwa wengine:**
Muulize mchungaji wako ikiwa unaweza kuanzisha mafundisho ya Biblia kanisani ambapo utaongoza kikundi kuchunguza na kujadili kile ambacho Biblia inafundisha tofauti na mafundisho ya injili ya mafanikio. Mnaweza kujifunza pamoja vifungu vya Biblia vilivyotajwa katika somo hili. Ikiwa huwezi kuongoza mafundisho ya Biblia kanisani, basi jaribu kuunda kikundi cha marafiki, familia, na majirani ili kujifunza na kujadili pamoja kuhusu mambo haya na vifungu hivi. Tuliangazia mengi katika somo hili kwa muda mfupi, lakini katika mafundisho yako ya Biblia unaweza kupanga kujadili vifungu vichache vya Biblia au mafundisho ya injili ya mafanikio kila mnapokutana.

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

*Someni vifungu vifuatavyo vya Maandiko. Jadilini pamoja kile ambacho kila kifungu kinafundisha tofauti na mafundisho ya uongo ya injili ya mafanikio. Hamtakuwa na muda wa kujadili kila kifungu. Someni nyumbani vifungu vyote ambavyo hamkujadili kwenye kikundi.*

*1 Timotheo 6:3-10*

---

*Yohana 9:1-3*

---

*Mathayo 5:44-45*

---

*2 Wakorintho 6:3-10*

---

*Mathayo 16:24-26*

---

*Habakuki 3:17-18*

---

*Luka 13:1-9*

---

*Methali 23:4-5*

---

*1 Petro 3:14-17*

---

*1 Petro 4:12-19*

---

*Mathayo 8:20*

---

*Luka 6:20-24*

---

*2 Wakorintho 11:23-30*

---

*1 Petro 1:6-7*

---

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa mafunzo zaidi)

## Kuangazia tena: *"Mafundisho ya mafanikio hufasiri vibaya vifungu vya Maandiko kwa kupuuza muktadha wao."*

**Mifano zaidi:**
**Soma 2 Wakorintho 8:9.** Wahubiri wa injili ya mafanikio wanaona kifungu hiki kama ushahidi wa wazi kuwa Yesu alikufa msalabani ili sisi kama wanafunzi wake tuwe matajiri wa mali. Lakini tukilinganisha kifungu hiki na yale tunayojua kutoka katika sehemu zingine za Biblia, tunajua kuwa Yesu hakufa msalabani ili tuwe matajiri katika maisha haya. Badala yake, alikufa msalabani ili kuchukua adhabu ya dhambi zetu na kushinda athari zote za Anguko. Kwa hivyo kifungu hiki kinamaanisha nini? Kristo aliacha utukufu wake wa mbinguni, akawa mwanadamu, akafa kwa ajili yetu, ili tupate kupatanishwa na Mungu na kukaa na yeye milele. Kristo atakapokuja tena, tutarejeshwa kikamilifu katika maana yote ya kuwa binadamu: miili na roho zetu zitaishi katika uhusiano mzuri na Mungu, nafsi zetu, watu wengine, na uumbaji. Karama hiyo ya kustawi kikamilifu kama wanadamu ndio hazina inayotufanya kuwa matajiri kweli.[8] Hebu tusome kifungu kingine ambapo Paulo anazungumzia kuhusu utajiri huu wa kweli wa kiroho, **2 Wakorintho 6:10.** Tukiangalia muktadha, tunaweza kuona kuwa Paulo anamtumia Kristo kama kielelezo ambacho tunapaswa kufuata. Paulo amemaliza tu kuzungumza kuhusu Wakristo wa Makedonia ambao walikuwa maskini na bado walitoa kwa ukarimu ili kuwasaidia wengine (kifungu cha 1-2). Walifuata mfano wa Kristo aliyejitoa kama dhabihu ili kuwasaidia wengine. Na Paulo anataka Wakorintho wafanye vivyo hivyo. Badala ya kufundisha kuwa Kristo atatufanya kuwa matajiri wa mali, kifungu hiki kinasisitiza hitaji letu la kujitoa kama dhabihu kama Kristo alivyofanya, kwa kutoa pesa zetu ili kuwasaidia wengine kwa ukarimu!

**Yakobo 4:2** inasema "Mmepungukiwa kwa sababu hammwombi Mungu." Katika makanisa mengi ya Afrika, ni jambo la kawaida sana kusikia viongozi wa makanisa wakihubiri kuhusu injili ya mafanikio na kuwaambia washirika wao "itaje, iguse na uidai na itakuwa yako!" Wanatumia kifungu hiki kimoja kuhalalisha ujumbe huu. Wazo ni kuwa watu hawana kile wanachotaka kwa sababu hawakuomba kwa imani ya kutosha. Lakini soma muktadha sasa. Soma **Yakobo 4:1-6.** Katika kifungu cha 3 tunasoma: "Mnapoomba hampati kwa sababu mnaomba kwa nia mbaya, ili mpate kuvitumia hivyo mtakavyopata kwa tamaa zenu." Tunaona kuwa si kwamba Wakristo hawaombi vya kutosha, lakini kwamba wanataka vitu kwa ajili yao wenyewe na raha zao pekee. Kwa hiyo kwa kweli Yakobo anaandika kinyume na kile ambacho wahubiri wa injili ya mafanikio wanavyowaambia watu wafanye. Zaidi ya hayo, ikiwa tutasoma sehemu iliyosalia ya waraka wa Yakobo, tunajua kuwa hatutapata kila kitu tunachotaka. Kwa mfano, mwanzoni mwa waraka katika **Yakobo 1:2-4**, tunajifunza kuwa tunapaswa kufurahi katika majaribu na mateso yetu. Ikiwa tunachopaswa kufanya ni kuitaja na kuidai, basi hatungeteseka kamwe. Na kisha Yakobo anawaambia watu kutarajia mateso tena katika **Yakobo 5:10-11.** Ni wazi kwamba Yakobo hakutarajia tuombe chochote tunachotaka na kukipata kila wakati. Badala yake, tunapaswa kuomba kwa imani kuwa Mungu atajibu maombi yetu lakini tukubali pia kuwa wakati mwingine tutapitia majaribu.

---

Uchoraji wa mistari ulifanywa na Lisa Brown kutokana na Picha ya Adobe Stock.

[1] Baadhi ya hoja zimetolewa kutoka: Michael Otieno Maura, Conrad Mbewe, Ken Mbugua, John Piper, Wayne Grudem, *Prosperity? Seeking the True Gospel*, (Africa Christian Textbooks Registered Trustees, Kenya, 2015) kilichapishwa kwa ushirikiano na Gospel Coalition, 3.

[2] ibid., 5-6.

[3] Kwabena Asamoah-Gyadu, "The Prosperity Gospel and its Challenge to Mission in our Time", (Lausanne Movement, Julai 2014) inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://www.lausanne.org/content/lga/2014-07/the-prosperity-gospel-and-its-challenge-to-mission-in-our-time.

[4] J. Lee Grady, "Five Ways Prosperity Gospel is Hurting Africa", (Charisma Magazine, Januari 2013), inaweza kufikiwa mtandaoni katika: https://mycharisma.com/blogs/fire-in-my-bones/5-ways-the-prosperity-gospel-is-hurting-africa/.

[5] Michael Otieno Maura, et al. *Prosperity? Seeking the True Gospel*, 29-31.

[6] Köstenberger, A. J. *John: Series Baker Exegetical Commentary on the New Testament* (Grand Rapids, MI: Baker Academic, 2004)., 433–434.

[7] The Africa Chapter of the Lausanne Theology Working Group's Statement on the Prosperity Gospel, access online: https://www.lausanne.org/content/a-statement-on-the-prosperity-gospel.

[8] Tazama Brian Fikkert and Kelly Kapic, *Becoming Whole,* (Chicago, Illinois, Moody, 2019).

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 13: Utamaduni wa Kiafrika na Pesa

Sio cha kuuzwa

# Majadiliano ya Ufunguzi

*1. Je, Afrika ina "utamaduni wa Kiafrika" wa jumla? Fafanua jibu lako.*

*2. Eleza kwa ufupi jinsi utamaduni wako unavyoona ukarimu na pesa kuhusiana na kudumisha uhusiano katika familia na jamii.*

*3. Kuhusiana na ukarimu na matumizi ya pesa, toa mifano mahususi ya mambo ambayo watu wanatarajiwa kufanya na mambo ambayo watu wanatarajiwa kutofanya.*

# Majadiliano ya Kikundi Kidogo

Jadilini katika vikundi vya watu watano kwa dakika kumi. Utapewa dakika mbili kuwasilisha majibu yako kwa vikundi vingine.

*Tumechambua mazoea na matarajio ya kitamaduni ya Kiafrika kuhusu ukarimu na pesa na jinsi zinavyotumika kudumisha uhusiano. Sasa fikiria juu ya kile ulichojifunza kutoka kwa masomo yote yaliyotangulia katika mtaala huu.*

*1. Andika orodha ya faida za mazoea haya ya kitamaduni na matarajio – njia ambazo zinakuza maendeleo halisi.*

*(Shughuli inaendelea kwenye ukurasa wa 151)*

Sio cha kuuzwa

*2. Andika orodha ya hasara za mazoea haya ya kitamaduni na matarajio – njia ambazo zinaweza kuhujumu au kuzuia maendeleo halisi.*

_______________
_______________
_______________
_______________
_______________
_______________
_______________
_______________
_______________
_______________

## Mhadhara wa Kiongozi: Urithi na Uongozi

Mgawanyo wa mali na urithi kwa kawaida huamuliwa na baba au kiongozi wa ukoo. Wake huenda wasipewe nafasi ya kutoa maoni yoyote. Wasichana huenda wasipokee urithi wowote. Wajane huenda wakapoteza mali zao kwa ukoo wakati waume zao wanapokufa.

*1. Kama Wakristo, tunapaswa kushughulikiaje masuala haya ya urithi kwa njia tofauti?*

_______________
_______________

*2. Soma Hesabu 27:1-11. Je, simulizi hii inatupa mwongozo kuhusu suala la urithi leo katika utamaduni wetu? Kwa nini iwe hivyo au kwa nini isiwe hivyo?*

_______________
_______________

Waafrika wengi wanamwamini Mungu kama mamlaka ya juu, na wa pili baada ya Mungu ni mwanaume, wa tatu ni mwanamke, na wa nne ni mtoto na mwishowe wanyama na ulimwengu wa asili. Wake wanapaswa kuwatii waume zao, watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao, na familia nzima inapaswa kumtii Mungu. Kama watu wenye mamlaka nyumbani, wanaume hudhibiti pesa, na wakati mwingine hawataki kuwajibishwa na wake zao. Fikiria methali hii ya jamii ya Bambara kutoka Mali: "Mtu muhimu anaweza kuwa amekosea lakini yuko sahihi kila wakati."[1]

*Je, unajua methali kama hizo katika utamaduni wako?*

_______________

Mafundisho ya kitamaduni kama haya yanaweza kuelezea kwa nini wanaume wengi hudhibiti rasilimali zote katika familia zao na pia huamua jinsi zitakavyogawanywa bila kujali kama walizifanyia kazi au ni mke ndiye aliyezifanyia kazi.

*1. Kwa mtazamo wa kibiblia, ni nini kilicho sahihi na kizuri kuhusu desturi hii ya kitamaduni ya ngazi za uongozi katika familia?*

---

Warumi 13:1-7, Wakolosai 3:18-21, 1 Wakorintho 11:3

---

*2. Kwa mtazamo wa kibiblia, ni sifa gani za desturi hii ya kitamaduni ya ngazi za uongozi katika familia si nzuri?*

---

Mwanzo 1:27-30, 1 Wakorintho 7:1-4, 1 Wakorintho 11:11

---

*3. Ni lipi kati ya machaguo haya manne linaloelezea desturi ya kawaida ya familia katika jamii yako? Ni chaguo gani unadhani linafaa zaidi kwa familia ya Kikristo?*

a. Mume anapaswa kuamua jinsi pesa zote zinavyotumika kama mkuu wa familia.

b. Mume anapaswa kuamua jinsi pesa zote zinavyotumika lakini anapaswa kuwa tayari kumwomba mkewe mapendekezo yake.

c. Mume na mke wanapaswa kujadili na kufanya maamuzi pamoja kuhusu jinsi pesa zinavyopaswa kutumiwa. Maoni ya kila mmoja yanachukuliwa kuwa na uzito sawa.

d. Mume anapaswa kuamua atafanyia nini pesa anazopata yeye ilhali mke akiamua atafanyia nini pesa anazopata yeye mwenyewe. Wote wawili wanapaswa kutumia sehemu ya pesa zao kwa mahitaji ya familia, na wote wawili wanaweza kutumia pesa kwa miradi mingine pia. Lakini wanasimamia pesa zao kila mtu kivyake na hawafanyi maamuzi pamoja.

---

---

---

Mathayo 19:4-6. *Je, inaonekanaje kwa mume na mke kuishi kana kwamba wao ni mwili mmoja?*

---

Mithali 31:10-31. *Hii inatufundisha nini kuhusu wanawake kutumia pesa?*

---

Sio cha kuuzwa

**Waefeso 5:21-33.** *Kuhusu matumizi ya pesa, ni jinsi gani wanawake wanapaswa kuwatii waume zao?*

---

**Mwanzo 2:18 na Waebrania 13:6.** Eva aliumbwa kuwa msaidizi wa Adamu. Hata hivyo katika Maandiko yote, lugha hiyo hiyo inatumiwa kumrejelea Mungu kama msaidizi wetu pia**.** ***Inamaanisha nini kuwa "msaidizi"? Ni maneno gani mengine katika Kiswahili au lugha yako yana maana sawa na "msaidizi"?***

---

**1 Petro 3:7.** *Inamaanisha nini kwa mume kumtendea mke wake kwa heshima kuhusu matumizi ya pesa ya familia?*

---

**Warumi 16:1-4. Paulo aliwasalimu wanawake wengi waliokuwa wafanyakazi wenzake huko Roma.** *Inamaanisha nini kuwa "mfanyakazi mwenza"? Ni neno gani lingine linalomaanisha "mfanyakazi mwenza" katika Kiswahili au lugha yako?*

---

## Kumtanguliza Kristo

Inaweza kuwa vigumu sana kwetu kutekeleza kile ambacho Mungu amekuwa akitufundisha katika Neno lake na kile ambacho tumejifunza katika masomo ya mtaala huu. Tunaweza kuogopa kwenda kinyume na matarajio ya utamaduni wetu au tuogope kuwafanya watu watudharau. Walakini tumeitwa kumtanguliza Kristo. Tunaweza kufahamu mema katika utamaduni wetu, lakini lazima tuwe tayari kumtii Kristo badala ya utamaduni wetu vitu hivyo viwili vinapokinzana.

*Unaweza kutoa ushauri gani kwa Mkristo mwingine anayeona ni vigumu kumtii Kristo badala ya utamaduni wake? Ni vifungu gani vya Biblia vinaweza kumsaidia mtu huyu?*

---

---

*Je, kuna mtu yeyote aliye tayari kushiriki simulizi kuhusu jinsi ulivyoenda kinyume na matarajio ya utamaduni wako ili kumtii Kristo?*

---

---

Sio cha kuuzwa

# Madeni na Mikopo

*Kwa nini mikopo ni njia bora ya kuwasaidia watu wenye mahitaji? Je, baadhi ya matokeo mazuri ya kuwapa watu mikopo ni yapi?*

*Je, hasara za mikopo ni zipi? Mikopo huharibu mahusiano kwa njia gani?*

*1. Tunapaswa kufanya nini wakati rafiki hawezi kulipa deni lake kwetu?*

*2. Tunapaswa kufanya nini wakati rafiki hataki kulipa deni lake kwetu?*

*3. Matokeo yanaweza kuwa nini ikiwa tunasamehe madeni mara nyingi sana?*

*4. Ni aina gani ya makubaliano ya kulipa madeni unayopendekeza wakati wa kukopesha marafiki au wanafamilia?*

*5. Wakati mtu anahisi kushinikizwa kusema "ndio" ili kumpa mtu mkopo, lakini anafikiri anapaswa kusema "hapana", anaweza kusema nini? Hali hiyo inapaswa kushughulikiwa vipi?*

*6. Mikopo hufanya kazi vizuri kwa ajili ya mahitaji gani? Tunapaswa kuepuka kutoa mkopo kwa mahitaji gani na badala yake kutoa zawadi?*

Sio cha kuuzwa

# Ongezeko la idadi ya watu na maendeleo

Hebu tuangalie uhalisia wa ongezeko la idadi ya watu ambao ulimwengu wetu unakabiliwa nao leo.

1. Mnamo mwaka 1500 BK idadi ya watu duniani ilikuwa milioni 425 tu. Mwaka 2000, ilikuwa bilioni 6. Leo ni bilioni 7.6. Ifikapo mwaka 2050 kutakuwa na takriban watu bilioni 9.2 katika ulimwengu wetu. Idadi ya watu inaongezeka kwa kasi zaidi.[2]

2. Idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kwa sababu watu wanaishi kwa muda mrefu kuliko hapo awali. Hii ni kutokana na huduma bora za afya, uzalishaji bora wa chakula, na teknolojia nyingine muhimu.[3]

3. Tumetumia rasilimali nyingi za asili za dunia katika miaka 50 iliyopita kuliko watu wote ambao wameishi ulimwenguni kabla yetu.[4]

4. Ikiwa kila mtu duniani angeishi kama Mmarekani wa tabaka la kati, basi sayari yetu ingeweza tu kukidhi mahitaji ya karibu watu bilioni mbili.[5] Idadi kubwa ya watu pamoja na jinsi tunavyoishi inaweka shinikizo kubwa kwa mazingira. Tunatumia kwa haraka mafuta, miti, maji ya ardhini, na samaki katika bahari zetu. Kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, ndivyo tunavyoweza kutarajia ushindani mkali zaidi juu ya rasilimali chache, hasa rasilimali za maji na ardhi kwa ajili ya makazi.

5. Wakati idadi ya watu inazidi kuongezeka katika baadhi ya nchi, katika mataifa tajiri kiwango cha kuzaliwa kinapungua. Kadiri umaskini wa mali wa watu unavyozidi kupungua, wataweza kukidhi mahitaji ya watoto wengi zaidi, lakini utafiti unaonyesha kwamba watu matajiri kwa ujumla wana watoto wachache.[6] Kadiri nchi inavyoendelea kiuchumi ndivyo kiwango cha kuzaliwa kinavyopungua. Hii inadhaniwa kuwa ni kwa sababu kadhaa:
   a. Kadiri nchi inavyoendelea kiuchumi, ndivyo wanawake wanavyokuwa huru zaidi na wanataka watoto wachache ili pia wawe na kazi.
   b. Taifa lililoendelea kiuchumi litakuwa na kiwango cha juu cha watu wanaotafuta elimu ya juu ambayo husababisha wengi kuhairisha kuanzisha familia zao hadi wanapofikia umri mkubwa.
   c. Watu wengi zaidi wanahamia mijini kwa ajili ya kazi badala ya kulima nyumbani. Aidha, mbinu za kisasa za kilimo zimepunguza kiwango cha kazi za binadamu zinazohitajika katika kilimo. Matokeo yake ni kwamba familia kubwa hazihitajiki mara nyingi kufanya kazi kwenye mashamba ya familia.
   d. Katika taifa tajiri kuna watoto wachache wanaokufa wakiwa na umri mdogo, kwa hivyo watu hawahisi kushinikizwa sana kuwa na watoto wengi.

Sio cha kuuzwa

## Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kikubwa

*1. Je, maadili yako ya kitamaduni kuhusu maisha ya familia na kuzaa watoto ni yapi?*

*2. Je, kuna faida na hasara gani za familia kuzaa watoto wengi?*

*3. Je, ongezeko la idadi ya watu katika nchi ni jambo zuri au baya kwa maendeleo? Eleza.*

*4. Je, upangaji uzazi unafaa kwa Wakristo? Ni aina gani ya mbinu za kupanga uzazi zinazokubalika na ni zipi hazikubaliki?*

Sio cha kuuzwa

## Mwanzo 1:28

*1. Je, hii ni amri kwa kila mtu binafsi kuijaza dunia, au wanadamu wote wanatakiwa kuijaza dunia pamoja?*

---

*2. Je, dunia imeshajaa? Tunajuaje kama tumetii amri hii kikamilifu?*

---

*3. Tunapaswa kuwaonaje na kuwaitikiaje wanandoa ambao hawana uwezo wa kuzaa?*

---

*4. Je, wanandoa watakuwa wanakosa kutii amri hii ikiwa watachagua kuwa na watoto wachache tu?*

---

# Shughuli za Kufanya baada ya Somo:

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Chagua mojawapo ya shughuli hizi **mbili** hapa chini.

1. Chambua uhusiano wako na wanafamilia na ndugu zako. Kwa sababu ya matarajio ya kitamaduni, je, unategemea sana mmoja wa jamaa zako? Au baadhi ya jamaa zako wanakutegemea kwa njia isiyo sahihi? Kuwa na mazungumzo ya wazi na watu wanaohusika na ujaribu kufanya mabadiliko. Kumbuka kuzingatia mahusiano manne muhimu – na Mungu, na nafsi, na wengine, na uumbaji.

2. Chukua muda zaidi kuchambua jinsi pesa zinavyoshughulikiwa katika familia yako. Ongea na mke wako au mume wako kuhusu majadiliano uliyofanya wakati wa mafunzo haya kuhusu njia tofauti ambazo wanandoa hushughulikia fedha. Ikiwa umesadikishwa kuwa mabadiliko yanahitajika, zungumza kwa upole na mwanandoa mwenzako na ujaribu kutekeleza mabadiliko hayo.

3. Fikiria juu ya mahusiano yako ambayo yamevunjika kwa sababu ya madeni ambayo hayajalipwa. Inaweza kuwa ni kwa sababu umeshindwa kulipa deni au kwa sababu mtu ameshindwa kukulipa deni. Mpigie simu mtu huyo na upange wakati wa kukutana pamoja na kufanya upatanisho kati yenu. Panga kumsamehe mkopo huo au fanya mpango wa kutatua hali hiyo. Lakini muhimu zaidi, ombeni pamoja na muombe msaada wa Mungu ili kurejesha uhusiano uliovunjika.

4. Ongea na mwanandoa mwenzako kuhusu kile ulichojifunza kuhusu kupanga uzazi. Muulize mwanandoa mwenzako maoni yake kisha msikilize vizuri. Jifunzeni vifungu husika vya Biblia pamoja. Ombeni pamoja kuhusu hilo. Jadilini na mfanye mpango pamoja kwa ajili ya familia yenu.

Sio cha kuuzwa

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

*Someni na kujadili vifungu hivi vya Biblia pamoja. Je, kuna vifungu vyovyote kati ya vifungu hivi ambavyo vinatusaidia kuelewa vizuri zaidi kile tunachopaswa kuamini kuhusu ongezeko la idadi ya watu au upangaji uzazi? Endeleeni kujadili pamoja mitazamo yenu tofauti kuhusu upangaji uzazi mnapojifunza vifungu hivi.*

*a. Zaburi 127:3-5*

___

*b. Mithali 14:28*

___

*c. 1 Timotheo 5:8*

___

*d. 1 Timotheo 3:1-5*

___

*e. Mithali 17:6*

___

*f. Mithali 11:29*

___

Sio cha kuuzwa

---

[1] David Maranz, *African Friends and Money Matters*, (SIL International, Dallas Texas, 2015), 25.

[2] Stephen Dovers and Colin Butler, "Population and Environment: A Global Challenge" (Australian Academy of Science), inapatikana mtandaoni kwenye: https://www.science.org.au/curious/earth-environment/population-environment.

[3] "Causes and Consequences of Overpopulation", (Acciona) inapatikana mtandano kwenye: https://www.activesustainability.com/sustainable- development/causes-consequences-overpopulation/.

[4] Stephen Dovers and Colin Butler, "Population and Environment".

[5] Ibid.

[6] Vandenbroucke Guillaume, "The Link between Fertility and Income", *Federal Reserve Bank of St. Louis* (Desemba 13, 2016, *Marekani)*, inapatikana mtandaoni kwenye: https://www.stlouisfed.org/on-the-economy/2016/december/link-fertility-income.

Kusaidia Bila

Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 14: Mabadiliko Katika Maisha ya Mtu Husababishwa na Nini?

Sampuli kwa Kuuzwa

# Zoezi la Ufunguzi na Majadiliano

*1. Kwa nini ni vigumu sana kwa watu kubadilisha tabia zao?*

________________________________________

________________________________________

*2. Ni aina gani za matukio husababisha watu kubadilisha tabia zao? Unaweza kutumia mfano katika maisha yako mwenyewe kuelezea.*

________________________________________

________________________________________

Tunapofanya kazi na watu maskini sana, wakati mwingine tunaweza kuona kwamba tabia fulani zinawafanya kuwa maskini wa mali, au zinawafanya waishi katika utegemezi na aibu. Tunawahimiza wabadilishe tabia zao, lakini tunafadhaika kwa urahisi wakati watu wanakataa kubadilika.

Katika masomo yetu ya awali, tulijifunza kwamba maendeleo ni mchakato wa mabadiliko ambapo watu husonga karibu na kuwa katika uhusiano sahihi na Mungu, nafsi, wengine na viumbe vyote. Mabadiliko muhimu zaidi katika maisha ya mtu ni kukutana na Kristo na kuwezeshwa na Roho Mtakatifu!

*Kwa ufupi, toa mfano mmoja mahususi wa jinsi mahusiano yako au tabia yako ilivyobadilika baada ya kumjua Yesu.*

________________________________________


Kama viongozi katika makanisa na jamii zetu, tunataka kuona watu wetu wakiendelea kubadilika ili waweze kuishi jinsi Mungu anavyotaka waishi, na kuwa watu ambao Mungu anataka wawe. Tunawezaje kuwahimiza zaidi wabadilike? Kazi ya kwanza ni kuomba.
Lakini tunaweza kufanya nini pamoja na kuomba? Katika somo hili, tutachunguza aina ya nguvu na hali ambazo watu wanapitia zinazosababisha watu binafsi na jamii kubadilika.

# Mhadhara: Mzunguko wa Mabadiliko

Katika mchoro kwenye ukurasa unaofuata tunaona kwamba mabadiliko huanza na kichocheo. Kichocheo ni kitu kinachoanzisha mwitikio. Kichocheo kinaweza kuwa mtu, kitu, au tukio. Kichocheo kinaweza kuwa maarifa mapya ambayo mtu amepata, au shida ambayo mtu amepitia.

Sio cha Kuuzwa

**Mduara wa mabadiliko kwa Watu Binafsi na Jumuiya**




## Aina za Vichocheo vinavyosababisha Mabadiliko

1. **Mgogoro wa hivi karibuni.** Hii inaweza kujumuisha ugonjwa, kupoteza kazi, kifo cha mwanafamilia, ajali, wizi, au janga la asili. Aina hii ya kichocheo huathiri watu binafsi na jamii. Biblia inafundisha kwamba mateso ni mojawapo ya zana ambazo Mungu hutumia kutusaidia kubadilika katika tabia zetu na kukua katika ukomavu.

---

**Mfano –** Jirani maskini katika jamii yako amekamatwa kama mwizi kwa kujaribu kuiba mbuzi wa mtu mwingine. Sasa yuko gerezani. Unaenda kumtembelea.

*Unaweza kumwambia nini jirani huyu ili imsaidie kutafakari maamuzi yake ili awe tayari kubadilika?*

---

2. **Kupitia matatizo madogo kwa muda mrefu.** Mwishowe, mtu huyo atafika mahali ambapo atahisi kufadhaika sana kuendelea kuwa katika hali fulani. Mtu anaweza kuwa amechoka kuhisi njaa mara kwa mara hivyo hatimaye anakuwa tayari kujaribu aina mpya ya kazi. Mtu anaweza kuwa amechoka kuona mazao yake yakinyauka kutokana na ukame mwaka baada ya mwaka, kwa hivyo hatimaye atakuwa tayari kulipa pesa zaidi ili kununua mbegu zinazoweza kustahimili ukame.

---

**Mfano –** Ali ni mpwa wako ambaye amekuwa akiomba msaada wa kifedha kutoka kwako mara kwa mara. Anatumia pesa hizi kusaidia kulipia simu yake ya mkononi na usafiri. Ana shahada ya uhasibu lakini bado hajapata kazi ya uhasibu. Umekuwa ukijaribu kumshawishi afanye kazi ya kibarua wakati bado anatafuta kazi za uhasibu, lakini amekataa.

*Unawezaje kuwezesha kichochezi katika maisha ya Ali ili abadilike na kuanza kufanya kazi?*

---

Sio cha Kuuzwa

**3. Kujifunza kitu kipya.** Hii inaweza kuwa kitu rahisi kama kuona aina mpya ya bidhaa au uvumbuzi. Au mtu anaweza kujifunza ujuzi mpya kutoka kwa rafiki.

---

**Mfano –** Kama mchungaji unaona kwamba washiriki wako wa kanisa wanalalamika kwamba aina fulani ya minyoo inaharibu mimea yao. Umewaombea na kutembelea nyumba zao na mashamba yao. Unataka kuwasaidia zaidi lakini huna uhakika jinsi ya kuwashauri.

*Unawezaje kusaidia kusanyiko kujifunza kitu kipya ili wajue jinsi ya kubadilisha mazoea yao ya kilimo kwa kukabiliana na shida ya minyoo?*

---

**4. Zawadi au adhabu.** Zawadi au adhabu ni kichocheo ambacho kinaweza kumfanya mtu kutafakari na kubadilika. Tunapaswa kuwa waangalifu na thawabu na adhabu tunapofanya kazi na watu maskini kwa kuwa tunataka kuepuka ubaba na hatutaki kuwatendea kama watoto walio chini ya mamlaka yetu. Lakini thawabu na adhabu zinaweza kufanya kazi vizuri wakati wa kujaribu kuwasaidia watoto wetu tuliowazaa kubadilisha tabia zao, au wakati wa kufanya kazi na watu tunaowaajiri katika biashara zetu.

---

**Mfano –** Wewe ni meneja wa duka ambalo linaajiri wafanyakazi 10. Umefadhaishwa na maadili ya kikazi ya wafanyakazi. Wengi ni wavivu. Hawana urafiki wa kutosha na wateja na hawana haraka ya kuwasaidia wateja kupata kile wanachohitaji. Wateja wamelalamika na unajua unapoteza mauzo.

*Je, unaweza kutekeleza kichochezi cha zawadi cha aina gani ili kuwatia moyo wafanyakazi wako kufanya kazi kwa bidii zaidi?*

---

---

**5. Uhusiano.** Mahusiano yamkini yamekuwa sababu muhimu zaidi ya kukufanya uwe vile ulivyo leo na kukufanya uwe na tabia ulizo nazo. Fikiria juu ya yote uliyojifunza kutoka kwa wazazi wako na jinsi uhusiano wako nao umeshawishi tabia yako. Na ukumbuke kwamba tulijadili jinsi maisha yetu yote yalivyobadilika sana tulipoanza uhusiano na Yesu. Lazima tuzingatie kujenga uhusiano na watu maskini.

---

**Mfano –** Samia ni mama mzazi mwenye watoto wawili wadogo. Anapata pesa kidogo kila siku kwa kufulia watu nguo wakati watoto wake wako shuleni. Lakini maisha yake ni magumu sana na ni vigumu kwake kupata pesa za kutosha kutunza familia yake. Anajihisi yuko peke yake, mwenye kupuuzwa na bila tumaini.

*Ikiwa wewe na familia yako mngeanza uhusiano na familia ya Samia, uhusiano huu mpya unawezaje kumbadilisha Samia na kumfaidi?*

---

---

Sio cha kuuzwa

# Kanuni za Kuhimiza Mabadiliko

**Kanuni ya 1 – Kukuza matukio ya kuchochea ambayo yatasababisha mtu kutafakari na kubadilika.**

**Kanuni ya 2 – Kuishi kwa mfano.**

**Kanuni ya 3 – Kuhamasisha Watu Wasaidizi.**

- Watu wanapojaribu kubadilika, wakati mwingine watu wanaowazunguka watawavunja moyo. Kwa sababu hii, watu wanahitaji kutiwa moyo sana wanapojaribu kubadilisha jinsi wanavyoishi. Tunapojaribu kuwasaidia watu maskini kufanya mabadiliko katika maisha yao, tunahitaji kuhamasisha watu ambao wanaweza kuwasaidia na kuwatia moyo.

- Wakati mwingine hii inaweza kufanywa kupitia kuunda vikundi rika vya watu ambao wote wanajaribu kufanya mabadiliko sawa pamoja. Kwa mfano, mnaweza kuunda kikundi cha walevi ambao wote wanataka kusaidiana kuacha kunywa pombe pamoja, pamoja na wengine ambao tayari wamepata uhuru kutokana na ulevi.

**Kanuni ya 4 – Anza Kidogo.**

- Ukijaribu kumsaidia mtu au jamii kufanya mabadiliko mengi katika mtindo wake wa maisha kwa wakati mmoja, anaweza kulemewa na kukata tamaa ya kufanya mabadiliko yoyote. Lakini ikiwa unaweza kuanza kwa kuwasaidia watu kufanya mabadiliko madogo, wataona faida ya mabadiliko watakapoona matokeo mazuri.

**Kanuni ya 5 – Anza na watu ambao wako tayari kubadilika.**

- Maendeleo yanaweza tu kutokea kwa watu ambao wako tayari kubadilika. Hata kama mtu yuko katika hali ngumu ambayo si matokeo ya kosa lake mwenyewe, ikiwa hayuko tayari kuchukua hatua yoyote mpya yeye mwenyewe ya kufanya mabadiliko chanya, basi itakuwa changamoto sana kuona maendeleo yoyote katika maisha yake.
- Ni muhimu pia kuanza na watu ambao wako tayari kubadilika kwa sababu watu hawa watakuwa mfano kwa wengine ambao wanapinga sana mabadiliko.

***Simulizi Kuhusu Chanjo ya Kuku***

Shirika la Kikristo lilikuwa likifanya kazi katika Afrika Magharibi likiwafunza watu kuhusu ufugaji wa kuku. Ilikuwa kawaida kwa wakulima kufuga kuku kwa ajili ya kuuza mayai na nyama. Lakini kuku wao walikuwa wanakabiliwa na magonjwa na mara nyingi walikufa. Wakati wa mafunzo, washiriki walijifunza jinsi ya kutunza kuku, jinsi ya kuwachanja, na kujifunza kuhusu baadhi ya magonjwa ya kawaida. Kama sehemu ya mafunzo kila mshiriki alipaswa kuleta kuku kutoka nyumbani kwake ili waweze kujifunza jinsi ya kumchanja. Mwanamke mmoja, Lydia, alikuja na kuku mdogo sana. Mumewe alikuwa na hakika kwamba chanjo hiyo ingemuua kuku huyo, kwa hivyo alimwambia alete kuku wao mdogo zaidi. Lydia alijifunza jinsi ya kumchanja kuku wake, kisha akaenda nyumbani kijijini kwake. Kwa sababu ya shaka

Sio cha kuuzwa

ya mumewe, huyo ndiye kuku pekee ambaye alimchanja. Miezi kadhaa baadaye janga lilienea kijijini, na kuku wote katika kijiji kizima walikufa. Kuku pekee aliyenusurika alikuwa kuku aliyekonda ambaye Lydia alikuwa amemleta kwenye mafunzo! Kila mtu kutoka kijiji chake alitaka kujua, "Ulimfanyia nini kuku huyo ulipomleta mjini miezi michache iliyopita?" Alielezea kuhusu mafunzo na chanjo. Cha kushangaza, watu hao wote walimwomba Lydia achanje kuku wao! Watu katika kijiji chake walipoanza kununua kuku wapya kuchukua nafasi ya wale waliokufa, Lydia alitoa chanjo kwa kila kuku.[1]

---

- Ikiwa watu hawako tayari kufanya mabadiliko yoyote katika maisha yao, basi tunaweza kufikiria kutowasaidia kabisa na badala yake kusubiri kwa subira hadi wawe tayari. Kuna sababu mbili ambazo tunapaswa kuzingatia kuhusiana na suala hili.

**Kwanza,** tuna kikomo katika muda na rasilimali zetu. Hatuwezi kumsaidia kila mtu. Kwa hivyo ni jambo la busara kuweka kipaumbele kuwasaidia wale watu ambao wako tayari kubadilika na ambao wataweka mfano mzuri kwa wengine.

---

**Pili,** ikiwa tutaacha kutoa msaada kama chakula na mavazi kwa watu ambao hawataki kufanya chochote kujaribu kubadilisha maisha yao, tunaweza kuwasaidia kupata mabadiliko. Wakati mwingine kutowapa watu pesa kwa kweli ni jambo la upendo la kufanya.

---

# Mafundisho ya Biblia kuhusu Kutoa

***Watu wanapoomba pesa au rasilimali kutoka kwetu, je, inakubalika kibiblia kwetu kusema "hapana" katika hali fulani mahususi? Tafadhali eleza jibu lako kwa mifano kutoka kwa maisha yako na kutoka kwa Maandiko.***

---

---

---

**Mathayo 5:42**

---

Tunahitaji kusoma mstari huu katika muktadha wake na kuzingatia mada zingine za kibiblia. **Mathayo 5:27-30.**

---

Mstari wa 42 haupaswi kuchukuliwa kama amri halisi kwa kila hali katika maisha yetu. Hoja kuu ambayo Yesu anawasilisha hapa ni kwamba tunapaswa kuwa watu wakarimu sana, na wenye kuwajali watu wa aina zote, hata adui zetu. Lakini kuna angalau sababu nne kwa nini mstari huu haupaswi kueleweka kama amri ya kutoa katika kila hali.

1. Kumbuka tulijifunza katika masomo ya awali kuhusu simulizi ya Biblia nzima na mada tunazoona katika Biblia yote. Lengo letu si tu kwamba watu wawe na pesa, bali ni **kuwasaidia watu kutimiza wito wao wa kumtukuza Mungu kwa kufanya kazi na kujikimu wao wenyewe na familia zao. Lengo letu ni**

Sio cha kuuzwa

**kwamba watu wapatanishwe na Mungu, wapatanishwe na nafsi zao, wapatanishwe na wengine, na wapatanishwe na uumbaji wote.**

2. Kuna vifungu vingine vya Biblia ambavyo vinatufundisha waziwazi "tusitoe" katika hali fulani.

**1 Timotheo 5:3-16**

**2 Wathesalonike 3:6-15**

3. Hakuna mtu anayeweza kutoa kwa kila mtu anayeomba, kwa sababu sisi sote tuna rasilimali chache.
**Matendo 3:2-6**

4. Hata katika hali ambapo hatumpi mtu kitu, haimaanishi kwamba tunamwacha. Ujumbe wetu unapaswa kuwa – "*Tunakupenda vya kutosha kukupa zaidi ya kile unachoomba kutoka kwetu hivi sasa. Tunataka kuwa sehemu ya maisha yako na kutembea nawe na kukusaidia kushinda hali uliyo nayo. Itakuwa rahisi kukupa pesa, lakini tutafanya jambo gumu la kushiriki maisha yetu na nguvu zetu na wewe ili kukusaidia kwa njia halisi, kwa sababu unastahili machoni pa Mungu.*"

# Haiba na Mabadiliko

Watu wanatofautiana katika mwitikio wao kwa mabadiliko kwa sababu ya haiba zao na asili zao. Tunaweza kuainisha watu katika vikundi vitano.[2]

1. **Wanaochukua hatua za hatari.**

2. **Watu wanaoheshimiwa.** Watu hawa wanachukuliwa kuwa wenye hekima na wanaheshimiwa na jamii. Watu huwafuata na wakati mwingine wana ushawishi zaidi kuliko viongozi rasmi.

3. **Watu Waangalifu**. Watu waangalifu wanapoamua kubadilika hiyo inaitwa "kichocheo", kwa sababu sasa watu wengi katika jamii watakubali mabadiliko pamoja.

Sio cha kuuzwa

4. **Watu wenye shaka**. Wanasubiri hadi watu wengi katika jamii wawe wamefanya mabadiliko, na wanaendelea kuyachunguza. Baada ya kuona mabadiliko na kuyazoea, wao pia watabadilika kwa sababu hawataki kuachwa nyuma.

---

5. **Watu wenye pingamizi**. Watu wachache hawapendi mabadiliko yoyote. Watashikilia njia za zamani hata wakati wanaenda kinyume na idadi kubwa ya jamii.

---

## Shughuli za kikundi kikubwa

Tambua ni kikundi gani kinakufaa zaidi. Simama pamoja na washiriki wengine ambao wanaendana na kikundi chako.

***Unataka kuona jamii ya vijijini ikitekeleza mabadiliko katika mazoea yao ya usafi. Unaenda kuwezesha mafunzo, lakini una pesa za kufundisha kikundi kimoja tu. Ni lipi kati ya makundi haya matano ambayo ungechagua kufundisha ikiwa ungeweza kuchagua moja tu? Je, faida na hasara za aina ya watu uliowachagua ni zipi?***

Si cha kuuzwa

## Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza.

**Kwa Kila mtu – jaribu kufanya yote matatu.**

1. Tambua watu wawili katika mahali pako pa kazi, kanisa, au jamii ambao umewaona wakifanya mabadiliko magumu lakini mazuri katika maisha yao. Waandikie kadi au barua ili kuwatia moyo na kuwashukuru kwa kuwawekea wengine mfano mzuri.

2. Amua badiliko moja ambalo Mungu anataka ufanye katika maisha yako mwenyewe. Inaweza kuwa kitu rahisi kama kufanya mazoezi zaidi au kusoma Biblia yako kila siku. Jaribu kuwahimiza marafiki kadhaa wajiunge nawe katika kufanya mabadiliko haya katika maisha yao pia. Kisha mkutane mara moja kwa mwezi ili kutiana moyo na kuwajibishana kuhusiana na mabadiliko hayo.

3. Kimojawapo cha vichocheo vya mabadiliko ni wakati watu wanajifunza kuhusu kitu kipya. Ni nani unaweza kumwalika kwenye hafla maalum ya kanisani ili kuwafundisha washiriki wako wa kanisa kitu kipya? (Kwa mfano: kufundisha kuhusu kilimo, huduma za afya, biashara, au kompyuta.) Fanya mpango wa kumwalika mtu huyo katika kipindi cha miezi michache ijayo.

## Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

*1. Je, kanisa lako linahamasisha watu walio tayari kusaidia kutembea na kuwatia moyo watu ambao kwa ujasiri wanajaribu kitu kipya ili kubadilisha maisha yao? Eleza. Ikiwa sivyo, kanisa lako linawezaje kufanya hivyo vizuri zaidi?*

________________________________________

________________________________________

*2. Kila mwanakikundi apewe fursa ya kushiriki na kikundi kuhusu mtu katika maisha yake ambaye amekuwa akijaribu kumsaidia lakini anapinga sana mabadiliko. Washiriki wa kikundi wakupe ushauri kuhusu kile unachoweza kufanya ili kumhimiza mtu huyo abadilike, na vichocheo vinavyoweza kumsaidia kutafakari na kuamua kufanya kitu tofauti. Ombeni pamoja kwamba Roho Mtakatifu awape watu hao ujasiri wa kubadilika.*

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

[1] Samuel na Brenda Soumalia Souleymane, mawasiliano binafsi. Imetumiwa kwa ruhusa.

[2] Mary Crickmore, "Shalom: A Manual for Christian Workers", (kuchapishwa binafsi, 2011), 22.

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 15: Ushiriki wa Jamii

Si kwa kuuzwa

# Majadiliano ya Ufunguzi

*Wageni muhimu wanakuja nyumbani kwako, utahitaji kufanya nini ili uhisi kwamba umeshiriki kikamilifu kuwakaribisha?*

# Simulizi kutoka Mashariki mwa Uganda

Shirika fulani la kimataifa lilitaka kusaidia kabila moja Mashariki mwa Uganda na likabaini kwamba watu katika eneo hilo hawakuwa na vyoo. Watu wengi walienda haja kubwa vichakani sehemu iliyo wazi. Shirika hilo lilipanga kuwapa watu vyoo vya shimo vyenye sehemu za kuingiza hewa safi ili kuboresha usafi wa mazingira katika mazingira yao. Vyoo vilijengwa na kukabidhiwa kwa watu. Baadaye, mfanyakazi wa maendeleo kutoka shirika tofauti alitembelea eneo hilo na kutumia kimoja kati ya vyoo hivyo. Cha kushangaza choo hicho kilikuwa safi kabisa ndani. Cha kusikitisha, mfanyakazi huyo wa maendeleo aligundua kuwa hali hiyo haikutokana na kusafishwa kwa choo hicho mara kwa mara na jamii. Ilitokana na ukweli kwamba hakuna mtu katika jamii aliyekuwa akitumia vyoo hivyo. Hawakuvitaka. Wote walipendelea kuenda haja kubwa vichakani. Kwa kweli, kwa kabila hilo, kutumia vyoo kulionekana kuwa mwiko. Kulikuwa hata na imani ya kitamaduni kwamba wanawake hawangezaa watoto ikiwa wangetumia vyoo hivyo.

*1. Ni sababu gani zilizofanya mradi huu usifaulu?*

*2. Je, unafikiri wenyeji walihusika katika kupanga, kuandaa, kutekeleza, na kutathmini mradi huu? Eleza jinsi ulivyoamua jibu lako kutokana na simulizi.*

*3. Katika eneo lenu, je, umeona hali kama hizo ambazo mashirika au makanisa hayakuwahusisha watu wa eneo hilo ambalo walikuwa wakijaribu kuwasaidia katika kupanga na kutekeleza miradi? Shiriki kwa ufupi mifano yako.*

Sio cha kuuzwa

# Mhadhara wa Kiongozi – Ushiriki wa Jamii a

## Matokeo chanya ya ushiriki wa jamii a:

1. **Umiliki.** Watu maskini na jamii ni kama watu wengine kwa vile wana uwezekano mkubwa wa kuthamini na kuwajibika kwa mradi ikiwa na wakati wanashiriki tangu mwanzo wa mradi hadi mwisho. Tukifanya kazi ***pamoja na*** jamii kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe, watahisi wanamiliki mchakato huo. Lakini tukifanya kazi ***kwa ajili yao,*** wanaweza kuwa wapokeaji tu.

2. **Uendelevu.** Ikiwa watu wanahisi umiliki wa maendeleo yao wenyewe, basi kunapaswa pia kuwa na uendelevu. Hata kama mtu au shirika ambalo linasaidia litaondoka, watu wataendelea kufanya mabadiliko peke yao, kwa vile sasa wamejifunza jukumu na furaha ya kusimamia maendeleo yao wenyewe.

3. **Kujistahi na kujiamini.** Ikiwa mtu binafsi au jamii imeshiriki kikamilifu, basi watajihisi vizuri wanapoona mabadiliko ambayo yametokea katika maisha yao. Wataona kwamba Mungu amewapa uwezo wa kuendelea kufanya mabadiliko katika maisha yao, na hii itawapa ujasiri wa siku zijazo. Kushiriki katika mradi, hata kama mradi hautafanikiwa kikamilifu, kutapunguza umaskini wa nafsi katika jamiina kuwapa uwezo wa kujistahi zaidi.

4. **Kushiriki maarifa.** Watu maskini na jamii mara nyingi hawaeleweki vizuri na watu wanaokusudia kuwasaidia. Kwa mfano, ombaomba anaelewa changamoto za kuwa ombaomba vyema zaidi kuliko kanisa la kieneo! Haitakuwa jambo la busara kwa kanisa kupanga jinsi ya kuwasaidia ombaomba katika mtaa wao bila kwanza kuzungumza na ombaomba hao. Lazima tuwasikilize kwa makini watu ambao ni maskini wa mali, tujifunze kuhusu mazingira na utamaduni wao, na tushiriki maarifa. Kushiriki maarifa kutatusaidia kupanga mipango yenye mafanikio pamoja.

5. **Mgao Sawa.** Wakati mwingine makanisa au mashirika yanapojaribu kusaidia jamii maskini, ni vikundi fulani tu ndani ya jamii ndivyo vinavyofaidika, na watu wanaohitaji msaada zaidi wanaweza kupuuzwa. Ushiriki wa jamii nzima utasaidia kuhakikisha rasilimali zinasambazwa kwa wale wanaozihitaji zaidi. Kupitia ushiriki kamili wa jamii, fursa za ufisadi na upendeleo zitapunguzwa.

6. **Uhamasishaji wa rasilimali.** Wakati watu ambao wanasaidiwa wanashiriki, wanakuwa na uwezo wa kujitolea kama wafanyakazi na kutoa vifaa na pesa kwa ajili ya mradi husika. Hii inapunguza sana gharama kwa kanisa au shirika ambalo linajaribu kusaidia na huwezesha jamii kumiliki mradi husika.

7. **Kufanya Kazi Kama Timu na Uwajibikaji.** Wakati kila mtu katika jamii anashiriki ili kuona mabadiliko yakitokea, kunaweza kuwa na roho kubwa ya ushirikiano wa pamoja na maelewano kati ya wanajamii, maafisa wa serikali, makanisa, na mashirika. Kwa sababu kila mtu anajua kinachoendelea, kila mshiriki anaweza kuwajibika kwa wengine. Shirika linalosaidia na jamii yenyewe vinaweza kuwajibishana katika kufanya kazi nzuri inayomtukuza Mungu.[1]

Sio cha kuuzwa

*Je, umewahi kusikia kuhusu jamii inayowajibisha maafisa wa serikali au mashirika kuhusu jinsi walivyojaribu kuisaidia jamii hiyo? Shiriki simulizi yako kwa ufupi.*

________________________________________

________________________________________

Ushiriki wa jamii ni muhimu ili kuwasaidia watu bila kuwaumiza. Mojawapo ya makosa ya kawaida ambayo makanisa, wamishonari, serikali, na mashirika ya maendeleo hufanya ni kwamba wanajaribu kuwasaidia watu bila ushiriki kamili wa watu wanaojaribu kuwasaidia.

## Matokeo ya kutoshirikisha jamii:

1. **Mtazamo wa kujiona kama Mungu.** Ikiwa tunajaribu kuwasaidia watu bila kuwapa fursa ya kupanga na kushiriki pamoja nasi, hii inaonyesha kwamba hatuwaheshimu. Tutakuwa tunawaonyesha kwamba sisi ni bora kuliko wao na tuna mawazo yote sahihi. Hii inamaanisha tunajiona kama Mungu. Mwishoni mwa mradi, mtazmao wetu wa kujiona kama Mungu utaimarishwa zaidi na watu tunaowasaidia wanaweza kujiona duni zaidi na kuwa na aibu zaidi.

2. **Utegemezi.** Ikiwa tutawasaidia watu bila ushiriki wao, hawatahisi umiliki wowote wa mchakato huo. Wataona mali mpya kama jengo la kanisa, shule, au kisima kama mali ya wale walioijenga. Hawatahisi wana jukumu kubwa katika kusimamia na kukarabati mali hizo. Wanaweza kusema: "Lakini wewe ndiye uliyejenga kitu hiki. Ni chako. Tunakusubiri ukirekebishe." Kwa kuwa hawakushiriki katika maendeleo yao wenyewe, wataendelea kusubiri watu kutoka nje wawaletee zawadi zaidi.

3. **Mradi Ulioshindwa.** Viongozi na mashirika ya nje ya kanisa yanapojaribu kusaidia jamii zingine, mara nyingi hufanya kosa la kufikiria kwamba kile kilichokuwa cha manufaa katika jamii moja waliyosaidia kitakuwa cha manufaa katika jamii zingine. Lakini hiyo si kweli wakati wote. Kila jamii ina haiba, mahitaji, mali, ardhi, na tamaduni tofauti. Tunapoingia katika jamii tukiwa na mtazamo wa kwamba tunajua kila kitu au mtazamo wa kusema kwamba tumeshawahi kufanya mradi kama huo hapo awali, kuna uwezekano mkubwa kwamba jitihada zetu za kusaidia zitaishia kushindwa. Tunahitaji kufahamu mchakato wa kujadiliana na kupanga pamoja na watu tunaowasaidia, badala ya kuharikisha kutekeleza mipango yetu tuliyoamua awali.

---

# Uchunguzi Kifani

### 1. Ishara za Mradi.

Katika jamii zingine, ni kawaida kuona ishara ambazo zinasema – "Mradi huu ulitolewa na shirika la ABC" au "Darasa hili lilijengwa na shirika la ABC."

*Je, unaweza kufikiria mifano kama hiyo katika eneo lako? Ishara kama hizi zinatuambia nini kuhusu ushiriki wa jamii? Je, miradi hii bado inafanya kazi?*

________________________________________

________________________________________

## Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

Fikiria aina tofauti ya ishara ambazo zinasema, "Sisi, kanisa la ABC, tulijenga jengo hili kwa msaada wa shirika la DEF."

***Je, aina hii ya ishara inatuambia nini kuhusu ushiriki wa jamii?***

---

**2. Simulizi ya kweli: Kituo cha kusoma na kuandika kilichojengwa na Waislamu na Wakristo pamoja.**
Katika eneo la Afrika Magharibi ambapo watu ni mchanganyiko wa Wakatoliki, Waprotestanti, na Waislamu, shirika fulani la kanisa lilipokea maombi mengi ya kufundisha watu kusoma na kuandika katika vijiji. Mkurugenzi wa shirika hilo alijua shirika la maendeleo la Kikristo kutoka Canada na akaomba msaada. Shirika hilo kutoka Canada liliwapa fedha za kuwalipa walimu katika vijiji vitano tu kama mradi wa majaribio. Vijiji vililazimika kujenga vituo vyao vya kusoma na kuandika na kulipa ada fulani kwa ajili ya vitabu. Madarasa ya kusoma na kuandika katika vijiji hivyo vitano yalipokaribia kukamilika, shirika hilo kutoka Canada lilituma wataalamu wawili ambao walikuwa na uzoefu wa kufanya kazi katika mipango ya kusoma na kuandika katika nchi jirani. Walitembelea vijiji vitano, na kupendekeza njia nyingi za kufanya ufundishaji na madarasa kuwa bora zaidi. Pia waliandika ripoti. Wakitumia ripoti hiyo, shirika hilo kutoka Canada lilisaidia shirika la kanisa kuandikia mfadhili pendekezo la ruzuku. Mfadhili alikubali pendekezo hilo na akafanya makubaliano kwa maandishi ya kufadhili walimu na wasimamizi wa kutosha kufanya kazi katika vijiji 30 kwa zaidi ya miaka mitatu. Takriban watu elfu moja, Wakatoliki,Waprotestanti na Waislamu, walijifunza kusoma pamoja, na walifurahia sana ujuzi wao mpya.[2]

***Je, una maoni gani kuhusu simulizi hii?***

---

***Inatufundisha nini kuhusu ushiriki wa jamii?***

---

**3. Simulizi ya kweli: Jenereta iliyoharibika.**
Shirika fulani la maendeleo huko Afrika Magharibi lilitaka kuwasaidia wanawake kwa kurahisisha kazi zao. Waliamua kutoa majenereta kwa vijiji ambayo yanaweza kutumika kusaga nafaka na pia kupiga maji ili kuyapandisha kwenye minara ya maji. Walikwenda katika vijiji vingi na kutoa majenereta, na wakasema litakuwa jukumu la wanavijiji kuyafanyia ukarabati. Kulikuwa na kijiji ambapo shirika hilo lilitoa jenereta na kujenga mnara wa maji. Watu walichangia kwa kufanya kazi kama shirika lilivyowataka wafanye. Lakini baada ya kufanya kazi kwa muda mfupi, jenereta hilo lilihitaji ukarabati. Kila lilipoharibika walilazimika kukusanya pesa na kumtuma mtu jijini kununua vipuri. Baada ya kukarabati jenereta hilo mara nne, lilipoharibika mara ya tano, waliamua kuwa hakuna faida kulirekebisha na wakaliacha likiwa limeharibika. Mnara wa maji wa gharama kubwa umesimama kijijini ukiwa mtupu.[3]

***Je, una maoni gani kuhusu simulizi hii?***

---

***Inatufundisha nini kuhusu ushiriki wa jamii?***

---

**4. Mipango ya VSLA – Vyama vya akiba na mikopo vya vijijini.**[4]

Sio cha kuuza

*1. Je, kuna mtu anayeweza kutueleza kwa ufupi chama cha akiba na mikopo cha kijijini ni nini?*

*2. Kwa nini vyama vya Akiba na Mikopo vya Vijijini vinaenea kwa kasi katika jamii masikini kote Afrika? Ni nini kinachofanya vifanikiwe sana?*

# Kuwasikiliza Wasio na Sauti

## Shughuli ya kikundi kidogo

*Ikiwa mfadhili alitoa dola 1,000 za Marekani kwa kikundi chetu cha mafunzo leo, pesa hizo zinapaswa kutumiwaje ili kunufaisha kikundi chetu na kuboresha eneo letu la mafunzo?*

Shughuli hii inatuonyesha kwa nini ni muhimu kusikiliza na kuhusisha watu wa aina zote katika jamii, iwe ni jamii yetu wenyewe au jamii katika eneo lingine tunalojaribu kusaidia.

Wakati wa kujaribu kusaidia jamii, ni muhimu sana kuwa na watu wanaoshiriki bila kujali jinsia, elimu, rangi, umri, dini, au ulemavu wao.

Tunahitaji kuwa waangalifu sana ili tusizungumze tu na watu walio madarakani, bali pia tuzungumze na wale ambao ni maskini na wasio na sauti. Tunaposema watu wasio na sauti, hatumaanishi watu ambao hawawezi kuzungumza. Tunamaanisha watu ambao hawasikilizwi na watu wengine, hasa watu wenye mamlaka na pesa. Watu wasio na sauti hawana mamlaka na ushawishi mkubwa kwa sababu ya kutengwa na jamii, kuhisi wao ni duni, au kutendewa isivyo haki na jamii.

*Ni watu wa aina gani ambao mara nyingi hawana sauti katika jamii zetu?*

Lazima tuwasikilize wasio na sauti wenyewe, lakini pia tujaribu kuwapa fursa za kuzungumza ili wengine wawasikilize pia. Hii ni "kuwapa sauti wasio na sauti".

Sio cha kuuzwa

**Mithali 31:8-9**

**Mithali 21:13**

*1. Vifungu hivi vinatufundisha nini kuhusu jinsi ya kuwasaidia wasio na sauti?*

*2. Jadili jinsi wewe binafsi au kanisa lako, shirika, au serikali inavyoweza kuwapa sauti wasio na sauti? Eleza kwa umahususi.*

# Ramani ya Nyenzo

Zana moja bora ya kukuza ushiriki wa jamii inaitwa **ramani ya nyenzo**.

Ramani ya nyenzo itaonyesha mali za jamii na maeneo ambapo zinapatikana.

Baada ya kutengeneza ramani ya nyenzo na jamii yetu wenyewe au na jamii nyingine tunayojaribu kusaidia, tunaweza kupanga pamoja na wanajamii jinsi ya kushughulikia mahitaji muhimu tukianza na nyenzo zinazopatikana. Ni hatua nzuri ya kwanza katika kupanga na kushirikiana ili kuleta mabadiliko katika maisha yao na jamii yao.

## Unatengenezaje ramani ya nyenzo?

1. Hakikisha kuwa kuna uwakilishaji wa vikundi vyenye mahitaji maalum na watu wa aina tofauti kutoka kwa jamii wanaohudhuria mkutano, hasa wale ambao mara nyingi hawana sauti.
2. Gawanya wanajamii katika vikundi vidogo kulingana na umri, jinsia, au kazi.
3. Inasaidia kila kikundi kidogo kikichora ramani tofauti ya rasilimali. Kila kikundi kitachora ramani ya eneo lilelile lakini kila kikundi kitaangazia mali tofauti na changamoto tofauti kwenye ramani zao.
4. Ambia vikundi vichore jamii yao, wakionyesha mali, rasilimali asilia, vyanzo vya maji, miti, barabara, taasisi, na vifaa vya jamii na maeneo ambapo mali hizo zinapatikana. Kuna aina nyingi tofauti za mali ambazo unaweza kuwakumbusha (kumbuka Somo la 7). Ramani inapaswa kuchorwa ardhini kwa kutumia vifaa vinavyopatikana kwa urahisi kama vile mawe, vijiti, majani, matunda, chupa za maji, n.k. Wanapaswa pia kuashiria maeneo yenye changamoto na mahitaji na maeneo ambayo yanatoa suluhisho zinazowezekana. Kwa mfano, wanaweza kuweka alama kwenye chanzo cha maji ambacho

Sio cha Kuuzwa

kimechafuliwa. Ikiwa wewe ni mgeni anayejadili suala hili na jamii, sikiliza kwa subira na uruhusu muda kwa washiriki kujadili. Uliza maswali ya uchunguzi ili kuchochea mawazo yao kuhusu aina mbalimbali za mali, na uulize maswali kuhusu vitu ambavyo wameweka kwenye ramani yao.

5. Baada ya kuchora ramani ya nyenzo, vikundi vidogo vinapaswa kujadili mahitaji matano muhimu ya jamii yao. Wanapaswa kuyapanga kulingana na vipaumbele. Ikiwezekana, wanapaswa kutambua mali walizochora ambazo zinaweza kutumika kwa njia fulani kuleta suluhisho kwa hitaji husika. Kwa mfano, ramani ya rasilimali inaweza kuonyesha kuwa kuna miti michache sana ya kutumia kama kuni. Lakini ramani hiyo hiyo inaweza kuonyesha vyanzo vingi vya maji, na maeneo makubwa yaliyo wazi ya kupanda miti.
6. Kila kikundi kidogo kinapaswa kuwasilisha ramani yake kwa wanajamii wengine. Wanaweza kuelezea kila kitu kilicho kwenye ramani hiyo, wakisisitiza mali zao muhimu zaidi, na pia kuelezea changamoto au mahitaji muhimu.
7. Ramani ya rasilimali inapaswa kutia jamii moyo na kuiwezesha kuwa na uhakika kwamba wana rasilimali wanazoweza kutumia kuleta mabadiliko. Habari hiyo sasa inaweza kutumiwa na jamii na wasaidizi wengine wa nje wanapopanga pamoja miradi na mipango ya baadaye.

## Shughuli ya kikundi kikubwa – Kuunda Ramani ya Nyenzo

## Shughuli za Kufanya Baada ya Somo:

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza.

1. Kwa Kila Mtu – Nenda nyumbani na ufanye mazoezi ya kutumia zana ya ramani ya nyenzo. Anza kwa kukusanya wanafamilia wako na kisha mtafakari pamoja juu ya mali za familia yenu. Fikirieni kuhusu ardhi, majengo, mali za nyumbani, na mali nyinginezo za familia yenu. Lakini pia mnaweza kuzingatia fursa mahususi na ujuzi ambao ni wa kipekee wa kila mwanafamilia. Pia, chukua muda wa kusikia kutoka kwa kila mtu kuhusu mahitaji na changamoto muhimu. Kisha fanyeni mpango pamoja kama familia kushughulikia changamoto muhimu zaidi kwa kutumia mali na fursa ambazo mmezitambua. Hakikisha unazingatia masilahi ya kila mwanafamilia mnapofanya mpango pamoja.
2. Kwa Viongozi wa Kanisa – Jaribu kukusanya viongozi wa kanisa na washiriki wa kanisa kutoka makanisa na mashirika mengine kadhaa yaliyo karibu nawe katika mtaa au eneo lako. Waongoze katika kutumia nyenzo ya ramani ili kutafakari juu ya mali, fursa, na mahitaji katika mtaa au eneo lako. Jadilini pamoja ikiwa kuna njia ambayo mnaweza kufanya kazi pamoja ili kutumia mali zenu kujaribu kushughulikia mojawapo ya mahitaji muhimu. Jaribuni kufanya mpango mahususi wa utekelezaji, mkihakikisha kwamba mnaamua watu watakaowajibika kwa kila kazi, na muda ambao kazi zitafanywa. Wasilisha hitimisho la kikundi kwa kanisa lako, ombeeni mpango wenu, na mtekeleze mpango mlioandaa.

Sio cha kuuzwa

[1] Kwa mawazo zaidi kuhusu jinsi jamii na mashirika yanavyoweza kuwajibishana na kuwa na ushirikiano bora, soma kuhusu Core Humanitarian Standard – https://corehumanitarianstandard.org/the-standard.

[2] Mary Crickmore, "Shalom: A Manual for Christian Workers", (kuchapishwa binafsi, 2011), 54.

[3] Ibid., 55.

[4] Ikiwa unahitaji mtaala mzuri wa akiba, tazama nyenzo hii ya bure inayopatikana kutoka kwa Kituo cha Chalmers inayoitwa Restore: *Akiba*. https://chalmers.org/restore-savings/.

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



## Somo la 16: Huduma ya Ukarimu ya Kanisa

# Majadiliano ya Ufunguzi[1]

*Je, kuna mtu yeyote anayetaka kujaribu kutoa ufafanuzi wa huduma ya ukarimu?*

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

Yakobo 1: 27

________________________________________________________________________

1 Yohana 3:16-18

________________________________________________________________________

Makanisa yetu ya kieneo yanahitaji huduma ya ukarimu iliyopangwa yenye sera za wazi ili yajue yanapaswa kumpa pesa nani na ni nani hayapaswi kumpa pesa. Na ukumbuke, hata tunapokataa kumpa mtu pesa, bado tunapaswa kuendelea kuwa na uhusiano naye na kushirikiana naye kwa njia nyingine.

*1. Je, kanisa lako lina huduma ya ukarimu?*

________________________________________________________________________

*2. Ikiwa ndio, kanisa lako linaamuaje nani wa kumpa pesa na nani wa kutompa pesa?*

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

*3. Ikiwa hapana, je, kanisa lako linawasaidia watu wenye mahitaji ya kimwili kwa njia nyingine?*

________________________________________________________________________

# Mhadhara wa Kiongozi: Kusudi la Ukarimu Huduma

Kusudi la huduma ya ukarimu ni kuwapenda watu kama mwitikio wa upendo wa Mungu kwetu. Tunapaswa kuwatumikia watu ili wasaidiwe na mahitaji ya kimwili na wakue katika mahusiano yao manne ya msingi – na Mungu, nafsi, wengine, na Uumbaji.

________________________________________________________________________

Nani anapaswa kufaidika na huduma zetu za ukarimu? Biblia iko wazi kwamba jukumu letu la kwanza ni kwa wale walio pamoja nasi katika kanisa la kieneo. Kumbuka miduara ya kipaumbele kutoka Somo la 6.

Sio cha kuuzwa

**Wagalatia 6:2** na **6:10.**

Ingawa huduma ya ukarimu inaweza kutanguliza mahitaji ya washirika wa kanisa, lazima tuwe waangalifu tusijizingatie sana. Lazima tuhakikishe kwamba kwa makusudi tunatenga sehemu ya rasilimali zetu ili kuwasaidia wale walio katika jamii ambao si washirika wa kanisa.

Huduma nzuri ya ukarimu pia inaweza kuwa sifa kuu ya utume wa kanisa.

Huduma nzuri ya ukarimu inaweza kuleta changamoto. Unaweza kupokea washirika wengi wapya ambao ni maskini sana. Kuwa tayari kwa hali hiyo na usiruhusu ikuvunje moyo.
**Yakobo 2:5**

**1 Wakorintho 1:26-29**

*1. Vifungu hivi vya Biblia vinatufundisha nini?*

*2. Viongozi wengine wa kanisa hawataki makanisa yao yajulikane kwa kuwa na washirika wengi maskini. Unafikiri kwa nini wanahisi hivi?*

Sio cha kuuzwa

# Majadiliano ya kikundi kikubwa

*1. Katika huduma ya ukarimu, kwa nini kwa kawaida tunapaswa kuepuka kutoa pesa taslimu kwa mtu anayehitaji msaada?*

*2. Kanisa la kieneo hupata faida gani kwa kutoa mikopo kwa washirika wa kanisa wenye mahitaji? Je, ni matatizo na changamoto gani zinaweza kutokea kutokana na kufanya hivyo?*

## Taratibu na Sera za Huduma ya Ukarimu

Sera za huduma ya ukarimu[2] ni kauli fupi zinazoeleza miongozo na taratibu za jumla ambazo zitatumika wakati wa kutoa msaada kwa watu wenye mahitaji. Sera pia zinaweza kuchukuliwa kama sheria zinazosimamia huduma.

***Toa baadhi ya mifano ya sera ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya huduma ya ukarimu ya kanisa. Kila kauli ya sera inapaswa kuwa na urefu wa sentensi moja.***

Ni muhimu kuwa na sera wazi na zilizofikiriwa vizuri kwa ajili ya huduma zetu za ukarimu kwa sababu kadhaa:

1. Sera zinatuzuia kutoa na kusaidia kwa njia zisizofuata utaratibu mahususi.
2. Sera zinatuzuia kutoa kwa upendeleo. Katika makanisa mengine, ni familia zinazojulikana kanisani pekee ndizo zinazopokea msaada wakati wa mahitaji. Katika makanisa mengine, ni watu matajiri tu au wenye ushawishi ndio wanaoamua ni nani wa kumsaidia na jinsi ya kumsaidia.
3. Sera zitatusaidia kuwa mawakili wazuri wa rasilimali chache tulizonazo. Tunaweza kutoa kwa njia ambazo zitakuwa bora zaidi.
4. Sera zinaweza kuhakikisha kwamba tunazingatia mahusiano yote manne ya msingi tunapojaribu kusaidia. Sera zitatusaidia kuepuka makosa ambayo tumejifunza kuhusu *Kusaidia Bila Kuumiza barani Afrika*.
5. Sera zitaruhusu huduma kufanya kazi vizuri na haraka, bila kuhitaji mkutano wa ziada wa kanisa na viongozi wote wa kanisa kila wakati hitaji jipya linapotokea.
6. Sera zitawalinda wafanyakazi wa huduma ya ukarimu kutokana na kushambuliwa au kukosolewa wanapokataa kutoa pesa kwa mtu anayeomba. Mwakilishi wa timu ya ukarimu anaweza kusema: "Kulingana na sera yetu, hatuwezi kukupa pesa kwa wakati huu kwa ombi lako mahususi. Hii si tu sera yangu mwenyewe, bali ni sera iliyokubaliwa na kanisa lote pamoja."

Siyo cha kuuzwa

***Je, umeona matatizo yoyote kama hayo katika huduma ya kanisa lako kwa vile hamkuwa na sera? Eleza.***

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Lengo kuu la sera za ukarimu ni kutoa msingi thabiti wa kufanya maamuzi kwa wale ambao wako mstari wa mbele katika huduma yako ya ukarimu.[3]

## Sera Mahususi

Mojawapo ya taratibu au sera muhimu zaidi za huduma ya ukarimu kanisani ni matumizi ya fomu za usajili. Fomu ya usajili itajazwa na mwanachama wa timu ya huduma ya ukarimu wakati anamhoji mtu anayeomba msaada. Fomu ya usajili inamruhusu mhoji kukusanya taarifa zaidi kuhusu watu wanaoomba msaada na mahitaji yao mahususi.

Fomu hiyo inahakikisha kuwa mahojiano hayaharakishwi na timu ya huduma ya ukarimu haitasahau kukusanya aina zote za habari muhimu kwa ajili ya kufanya uamuzi mzuri. Baada ya kujazwa kwa fomu ya usajili, wanachama wa huduma ya ukarimu wanaweza kukutana pamoja na kuamua cha kufanya.

Sio cha kuuzwa

## FOMU YA USAJILI YA HUDUMA YA UKARIMU[4]

Tarehe ya Mahojiano ya Kwanza _________________________ Tarehe Fomu ya Usajili Ilipojazwa _____________
Tarehe Timu ya Ukarimu Ilipoarifiwa ______________________ Tarehe ya Kujibu Ombi ______________________
Ukweli wa Taarifa Umekaguliwa na _________________________ Tarehe ___________________________________

**SEHEMU YA 1: Taarifa ya Utambulisho**

Jina: ____________________________________________________________________________
Umri _____ Mwanaume _____ Mwanamke _____ Wanandoa _____
Anwani: __________________________________________________________________________
Simu ya Kazini: ___________________ Simu ya Mkononi: ______________________
Barua pepe: _______________________________________________________________
Jina la Mwanandoa Mwenzako: ______________________________________________________
Majina na umri wa watoto:
__________________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________________
Wanafamilia wengine wanaoishi na mtu husika:
__________________________________________________________________________________
Mshirika wa kanisa? ____ ndio ____ hapana Ikiwa Ndio, Kwa Muda Gani? _____
Ikiwa hapana, unahudhuria mara kwa mara? ____ ndio ____ hapana Ikiwa Ndio, Kwa Muda Gani? _____
Ikiwa hahudhurii mara kwa mara, je, mtu huyu ameunganishwa na kanisa kwa njia yoyote?
__________________________________________________________________________________

Je, mtu huyu amesaidiwa na kanisa hapo awali? ____ ndio ____ hapana
Ikiwa ndio, lini? _________________________________________________________________
Msaada ulikuwa wa nini?
__________________________________________________________________________________
Msaada gani ulitolewa na kwa kiwango gani?
__________________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________________
Je, mtu huyu alipokea msaada wa kifedha? ____ ndio ____ hapana

Je, mtu huyu amepokea msaada kutoka kwa makanisa/mashirika mengine katika mwaka uliopita?
____ ndio ____ hapana
Ikiwa ndio, msaada ulikuwa wa nini na msaada ulikuwa wa aina gani? _________________________
__________________________________________________________________________________
Orodhesha majina na nambari za simu za watu binafsi au wachungaji ambao wanaweza kupigiwa simu kwa ajili ya kupata habari zaidi kuhusu mtu huyu (omba ruhusa ya mdomo ili kuwasiliana na watu hao):
__________________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________________

**SEHEMU YA 2: Hali ya Sasa na Sababu ya Ombi**

Tatizo linalojitokeza ni lipi kama ilivyoelezwa na mtu huyu?
__________________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________________
__________________________________________________________________________________
_______________________________________________________________

Sio cha kuuzwa

Tatizo hili limeendelea kwa muda gani?
___________________________________________________________________________

Je, mtu huyu hivi karibuni amedhulumiwa na watu wanyanyasaji au mafisadi kwa njia ambazo zimesababisha au kuchangia tatizo hilo?
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Je, mtu huyo amefanya au hajafanya kitu chochote ambacho kimesababisha au kuchangia tatizo hilo?
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Maelezo mengine muhimu kuhusu hali hiyo:
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Je, mtu huyu amechukua hatua gani kurekebisha hali hiyo?
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Ombi mahususi la mtu huyu kwa kanisa ni lipi?
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Je, mtu huyu anafikiri ni nini kinahitaji kubadilishwa katika hali hiyo na/au katika yeye wenyewe?
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Je, mtu huyu yuko tayari kufanya kazi na kanisa ili kuunda mpango kazi unaolenga kutatua matatizo yake ya sasa na pia kuchukua hatua ili kusaidia kuzuia tatizo hili lisitokee tena?
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Fomu hii ilianzishwa na: ______________________ mnamo (tarehe) _________________
Mtu aliyepewa jukumu la ufuatiliaji: __________________________

**SEHEMU YA 3: Muktadha wa Kina na Historia**
(Unaweza kusubiri hadi mikutano ya baadaye ili kupata baadhi au taarifa zote zifuatazo)

***Elimu/Historia ya Kazi***
Kazi anayofanya sasa: _______________ Kazi anayofanya sasa ameifanya kwa muda gani? _________
Historia ya kazi:
___________________________________________________________________________
___________________________________________________________________________

Kiwango cha juu zaidi cha elimu na shahada alizo nazo:
___________________________________________________________________________

Vyeti vingine vya mafunzo au programu alizokamilisha:
___________________________________________________________________________

***Hali ya Kifedha***
**Mali**
Akiba ya Sasa kwenye benki ________________________________________________
Pesa taslimu mkononi na kwenye Simu __________________________________________
Hifadhi za chakula nyumbani ________________________________________________
Mali ya gari ____________________________________________________________
Mali ya mifugo __________________________________________________________
Mali ya ardhi ___________________________________________________________

Sio cha kuuzwa

Mali nyingin ______________________________
JUMLA YA THAMANI YA MALI = ______________________________

**Kipato**

Mapato ya kila mwezi ______________________________
Zawadi za kila mwezi kutoka kwa jamaa, marafiki ______________________________
Msaada kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali ______________________________
Mipango ya msaada wa serikali ______________________________
JUMLA YA MAPATO YA KILA MWEZI = ______________________________

**Gharama za Kila Mwezi**

Chakula ______________________________
Maji ______________________________
Makazi ______________________________
Umeme ______________________________
Gesi ya Kupikia/Mkaa/kuni ______________________________
Muda wa maongezi ya simu ______________________________
Gharama za usafirishaji ______________________________
Dawa na matibabu yanayoendelea ______________________________
Gharama za maduka makubwa kama vile sabuni, dawa ya meno, sukari, karatasi ya chooni, n.k.
______________________________
Chakula na matibabu ya mifugo ______________________________
Karo ya Shule ______________________________
Nguo/Viatu ______________________________
Ada za ATM/Ada za Benki/Ada za mashirika au klabu ______________________________
Kutoa kwa kanisa na misaada mingine ______________________________
Bima ______________________________
JUMLA YA GHARAMA = ______________________________

***Hali ya Makazi***

Je, mtu huyu anakodisha au anamiliki nyumba? ________________
Anaishi na nani? ______________________________
Je, mtu huyu ana wategemezi wowote wanaoishi naye? Ikiwa ndiyo, ni kina nani?
______________________________
Je, mtu huyu hana makazi? _____ ndio _____ hapana

***Afya ya Kiroho, Kijamii, na Kihisia/Kiakili***

Eleza uzoefu wa Kikristo/safari ya kiroho ya mtu huyu, ikiwa inafaa:
______________________________
______________________________

Mtu huyu ana aina gani ya msaada wa kijamii?
______________________________
Je, mtu huyu ana wanafamilia wowote wanaoishikaribu? _____ ndio _____ hapana
Ikiwa ndio, ni kina nani? ______________________________
Je, mtu huyu ana kikundi kidogo cha kanisa? _____ ndio _____ hapana
Ikiwa ndio, jina na nambari ya simu ya kiongozi wa kikundi hicho
______________________________
Je, kuna rafiki mmoja au wawili wa karibu wanaojua hali ya mtu huyu? _____ ndio _____ hapana
Je, Mtu huyu huenda kwa mshauri? _____ ndio _____ hapana
Ikiwa ndio, ni nani? ______________________________

Sio cha kuuzwa

Je, mtu huyu amewahi kugunduliwa na/au kutibiwa kwa ugonjwa wa akili?
_____ ndio _____ hapana
Ikiwa ndio, eleza: ______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________________________
Je, mtu huyu kwa sasa anatumia dawa zozote alizoagizwa na daktari? _____ ndio _____ hapana
Je, mtu huyu amepata kiwewe wakati fulani maishani mwake? Ikiwa ndio, eleza:
______________________________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________________________

**SEHEMU YA 4: Tathmini na Jibu la Kanisa kwa Ombi hili**

*- Kumbuka kwamba umaskini una sababu nyingi: tabia ya mtu binafsi, watu wanaodhulumu au wanaonyonya wengine, mifumo ya ukandamizaji, na nguvu za kipepo. Katika hali nyingi, umaskini unasababishwa na zaidi ya moja ya sababu hizi.*
*- Hata hivyo, kwa kiwango ambacho tabia ya mtu mwenyewe ndio imechangia umaskini wake, unapaswa kujaribu kupima utayari wake wa kuchukua hatua za kuleta mabadiliko chanya katika maisha yake. Katika hali kama hizo, chagua hatua inayofaa zaidi:*

Mtu/familia hii inaamini:
1. _______ Hakuna tatizo la kina ambalo mimi/sisi tunahitaji kushughulikia.
2. _______ Kunaweza kuwa na tatizo, lakini si mimi/si sisi ndio tunaohitaji kubadilika.
3. _______ Ndio kuna shida, lakini nina shaka kwamba inaweza kubadilishwa.
4. _______ Ndio kuna tatizo, na mimi/sisi tunaweza kuwa sehemu ya kufanya mabadiliko.
5. _______ Ndio kuna tatizo, na mimi/sisi tuko tayari sana kuchukua hatua za kufanya mabadiliko.

*Kategoria ya 1 au 2:* Mtu huyu/familia haiko tayari kufanya kazi ngumu ya: (1) kutambua mambo ambayo wanahitaji kubadilisha, na (2) kufanya mabadiliko hayo kwa msaada wa kanisa lako. Hawako tayari kuunda mpango kazi. Ukosefu wao wa kuwa tayari kubadilika unaweza kuwafanya wasistahili kupokea msaada kutoka kwa kanisa wakati huu. Lakini hiyo haimaanishi wanapaswa kupuuzwa. Kupitia kuendelea kuwasiliana na kuzungumza nao, huenda wakawa wazi zaidi kufanya mabadiliko.

*Kategoria ya 3–5:* Mtu huyu yuko tayari kuunda mpango kazi.
Unaweza kugundua kuwa watu walio katika kategoria ya 3 au 4 wanakamilisha mpango kazi wao lakini hawafuatilii ili kufikia malengo yao. *Usikate tamaa*! Yamkini watahitaji kutiwa moyo na usaidizi wa ziada, na malengo na muda wao wa utekelezaji unaweza kuhitaji kurekebishwa. Ikiwa hawafanyi maendeleo ya kutosha kwenye malengo yao hata kwa kutiwa moyo mara kwa mara au kupewa msaada, basi wewe na kanisa lako mnaweza kuhitaji kuacha kutoa nyenzo na rasilimali za kibinadamu zinazowezekana ambazo mmejitolea kutoa katika mpango kazi. Lakini mtaendelea kuwatia moyo na kujenga uhusiano.

**Tathmini ya awali ya kanisa ya masuala ambayo yanahitaji kushughulikiwa yaliyochangia tatizo la sasa:**

______________________________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________________________

Sio ya Kuuzwa

1. Je, kushindwa kutoa msaada wa haraka kunaweza kusababisha madhara makubwa kwa mtu h u yu?
_______________________________________________
_______________________________________________

2. Je, mtu huyo anawajibika kwa kiasi kikubwa kwa hali yake?_______________________
_______________________________________________

3. Je, kutoa msaada wa haraka wa kifedha kutasaidia au kuzuia uwezeshaji huo (katika mahusiano 4)?_____
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**Mbali na kupokea msaada, je, mtu huyo yuko tayari kujadili mpango kazi na njia ya kusonga mbele ili kufanya mabadiliko katika hali yake kwa msaada wa kanisa?**

_______________________________________________
_______________________________________________

**Uamuzi wa awali uliofanywa na huduma ya ukarimu:**

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**Ripoti juu ya mwitikio uliotolewa na huduma ya ukarimu na athari yake:**

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**Ripoti kutoka kwa ziara ya ufuatiliaji wa siku zijazo na mazungumzo:**

_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________
_______________________________________________

**Fomu ya usajili iliwasilishwa katika rekodi na ____________________ Tarehe ____________________**

Sio cha kuuzwa

**Mpango Kazi:** Mpango kazi ni mpango ulioandikwa ulioandaliwa na mtu anayesaidiwa pamoja na timu ya ukarimu. Mpango kazi unajumuisha malengo ambayo ni mabadiliko ambayo mtu huyo anataka kuona katika maisha yake, pamoja na shughuli ambazo atafanya ili kuona malengo yake yametimizwa. Kuna sampuli ya fomu ya mpango kazi katika sehemu ya "Tafakari Zaidi" mwishoni mwa somo.

**Kukagua Ukweli:** Ni muhimu kufanya angalau ukaguzi wa ukweli kidogo ili kujua ikiwa simulizi ya mtu huyo ni ya kweli. Wakati mwingine hii inaweza kuwa rahisi kama kupiga simu kwa shule au hospitali ili kujua kwamba mtu huyo kweli ana bili ambayo inahitaji kulipwa. Wakati mwingine inaweza kuhitaji kutembelea nyumba na familia ya mtu huyo. Ziara zinapaswa kufanywa kama timu ikiwezekana.

***Kama mwanatimu wa ukarimu, kwa nini ni muhimu kutembelea nyumba ya mtu husika na angalau mwanatimu mwingine mmoja?***

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## Sera Zingine

Unapoenda nyumbani, unapaswa kuwauliza washiriki wa timu yako ya huduma ya ukarimu ya kanisa maswali haya ili kubuni kauli zako za sera.5

1. Kauli yetu ya kusudi kwa ajili ya huduma ya ukarimu ya kanisa letu ni ipi?
2. Ufafanuzi wetu wa umaskini ni upi?
3. Nani ataongoza na kushiriki katika huduma ya ukarimu? Je, watakuwa viongozi wa kanisa au watu wa kujitolea au wote wawili?
4. Je, pesa zinazotumika katika huduma ya ukarimu zitakusanywaje? Ni asilimia ngapi ya bajeti au matoleo ya kanisa yatakwenda kwa huduma ya ukarimu?
5. Ni asilimia ngapi ya bajeti ya huduma ya ukarimu itatumika kwa washiriki wa kanisa na ni asilimia ngapi itatumika kwa wengine katika jamii?
6. Mchakato wetu wa usajili utakuwa vipi watu wanapokuja na maombi?
7. Je, tutamhitaji kila wakati mtu tunayemsaidia kuandaa mpango kazi kwa ajili ya kufanya mabadiliko? Au kuna baadhi ya hali ambapo mpango kazi si lazima?
8. Kanisa letu linahisi limeitwa kusaidia makundi gani ya walengwa?
9. Je, tutatoa msaada kwa wale ambao si Wakristo, kama Waislamu, Wahindu, na wale wanaofuata Dini za Jadi za Kiafrika?
10. Ni katika hali gani tutachukua hatua ya kutoa msaada wa kifedha au wa vifaa?
11. Je, ni mara ngapi tutamsaidia mtu yule yule au familia ile ile kwa msaada wa kifedha au wa vifaa?
12. Je, tutazingatia usaidizi, urekebisahji, au maendeleo, au kiwango kidogo cha kila moja?
13. Huduma yetu itasaidiaje watu kukua katika uhusiano wao na Mungu? Na wengine? Na nafsi zao wenyewe? Na uumbaji?

Sio cha kuuzwa

14. Watu wanapoomba msaada wetu lakini hawana kazi, tutachukua hatua gani kuwasaidia kupata kazi yenye maana?
15. Tutawaitikiaje watu ambao wana uwezo wa kufanya kazi lakini hawako tayari kufanya kazi?
16. Tutatangazaje sera zetu kwa kanisa letu na kuzijadili pamoja ili kuhakikisha wanakubaliana nazo?
17. Je, tutatangazaje huduma yetu kwa jamii? Je, tutaijulisha jamii hadharani kuhusu sera zetu?
18. Je, msaada wetu utakuwa wa aina gani? (pesa taslimu, chakula, kulipa bili moja kwa moja, n.k.)
19. Je, tutawasaidia washirika wa kanisa kwa gharama za harusi au mazishi?
20. Je, tutaweka kipaumbele cha juu zaidi katika kuwasaidia viongozi wa kanisa wenye mahitaji ikilinganishwa na washirika wengine wa kanisa?
21. Tutatoaje taarifa na ripoti za mara kwa mara kwa kanisa?
22. Tunapokataa kutoa msaada wa kifedha, ni aina gani ya shughuli ambazo bado tunaweza kufanya na watu ili kujaribu kuwasaidia?
23. Tutachukua hatua gani kuthibitisha ukweli wa simulizi za watu kabla ya kuwasaidia? Nani anawajibika kufanya ukaguzi huu wa ukweli?
24. Ni wakati gani na kwa jinsi gani tutatumia huduma zingine, makanisa, mipango ya serikali, na mashirika? Tutajaribu kukidhi mahitaji gani, na tutatuma watu kwenye mashirika mengine kwa ajili ya mahitaji gani?

***Je, kuna maswali mengine muhimu ambayo unafikiri yanapaswa kuzingatiwa wakati wa kubuni sera za kanisa za huduma ya ukarimu?***

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

Sio cha kuuzwa

Sikiliza mfano huu kutoka kwa kanisa fulani la Nairobi, Kenya linaloitwa Huduma ya Huruma ya Kristo. Hizi hapa ni sera zao chache kutoka kwa huduma yao ya ukarimu. Wanaiita “Sera yao ya Ustawi wa Kanisa”.

- Sera moja inasema kwamba fedha zinakusanywa kwa ajili ya mfuko huo kwa kumfanya kila mshirika wa kanisa alipe shilingi 100 za Kenya (dola 1) kwa mfuko huo kila mwezi. Wanatoa kwa washirika wa kanisa wakati wa shida kama vile wakati wa kifo cha mpendwa na kulazwa hospitalini kwa sababu ya ugonjwa.
- Sera nyingine inasema kuwa kiasi cha msaada wa kifedha kinachotolewa kwa familia ambayo imepoteza mwanandoa, watoto, au wazazi kitakuwa shilingi 20,000 za Kenya.
- Sera nyingine inasema kuwa kiasi kinachotolewa kwa familia ambayo imepoteza kaka au dada kitakuwa shilingi 14,000 za Kenya.
- Wakati wa magonjwa na kulazwa hospitalini, sera zinasema kwamba pamoja na msaada wa kifedha, washirika wa kanisa watamtembelea mgonjwa hospitalini na kumwombea ili apate uponyaji.

- Sera nyingine inasema kwamba washirika wote wa kanisa watahimizwa kujiandikisha katika bima ya afya mara kwa mara. Jumla ya sera zilizoandikwa za kanisa hili zina urefu wa kurasa 6.

---

Kila kanisa litakuwa na sera tofauti kulingana na muktadha wake na jinsi Mungu anavyowaongoza kwa Neno lake na Roho wake. Jambo muhimu ni kwamba urudi na kujadili pamoja na washirika wako wa kanisa huku mkiliombea jambo hili na mbuni sera kwa ajili ya huduma yenu ya ukarimu.

---

## Ushauri wa Kuhitimisha

- Kumbuka kujaribu kuwasaidia watu kutambua vipawa na rasilimali ambazo Mungu amewapa.
- Toa kwa watu kwa njia ambayo itaepuka kuwafanywa wawe wategemezi.
- Kumbuka kusaidia kwa ujumla. Hata katika hali ambapo hutoi pesa, bado unaweza kuwafundisha watu ujuzi wa kazi, kuwaangalilia watoto wao wakati wanafanya kazi, kuwaalika kwenye kikundi kidogo kanisani, kuwaombea, kuwasaidia kuwa na upatanisho na watu ambao wamewaumiza, kuwasaidia kupanda bustani zao, kuwaalika nyumbani kwako kwa chakula, n.k.
- Sherehekea mabadiliko, na uwatie moyo watu ambao wametekeleza mipango kazi yao.
- Wakati mwingine, hata baada ya yote ambayo tumejifunza *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika*, bado ni vigumu sana kujua cha kufanya katika hali fulani. Je, tunapaswa kutoa au hatupaswi kutoa? Katika hali ngumu kama hizo, ni bora kufanya makosa ya kutoa kuliko kufanya makosa ya kutotoa. Kama Wakristo, Mungu anatuita tuwapende watu na kutoa kwa ukarimu hata kwa watu ambao hawastahili, kama vile Mungu anavyotupenda na hutoa kwa ukarimu kwetu ingawa hatustahili. Ni bora kufanya makosa upande wa ukarimu.
- Kumbuka jambo muhimu zaidi ni kuwaelekeza watu kwa Yesu Kristo. Usipuuze jambo hilo wakati wa kukidhi mahitaji ya kimwili ya watu. Chukua muda wa kuomba na watu na kuwaambia kuhusu injili.

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza.

**1. Ikiwa kanisa lako lina huduma ya ukarimu:**
Fahamu ikiwa kuna sera zozote zilizoandikwa. Ikiwa unaweza, jiunge na timu ya huduma ya ukarimu na uwasaidie kuandika sera zenye kina kwa kutumia somo hili kama mwongozo, au kuboresha sera ambazo tayari zipo. Weka mfano mzuri kwa kuchangia kifedha kwenye mfuko wa ukarimu wewe mwenyewe.

**2. Ikiwa kanisa lako bado halina huduma ya ukarimu:**
Wasiliana na viongozi wa kanisa lako na washirika wa kanisa, na upendekeze wazo la kuanzisha huduma ya ukarimu ya kanisa. Ikiwa kanisa linakubali kuanzisha huduma ya ukarimu, jitolee kuiongoza kwa kujiunga na timu na kuisaidia timu kuandika sera za kina kwa kutumia somo hili kama mwongozo. Weka mfano mzuri kwa kuchangia kifedha kwenye mfuko wa ukarimu wewe mwenyewe.

Sio cha Kuuzwa

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

*Jadili hali zifuatazo. Ni njia gani bora zaidi ya kuitikia na kusaidia kama timu ya ukarimu ya kanisa? Je, ni sera gani za ukarimu ambazo zingesaidia kujitayarisha kwa hali kama hizo?*

*A. Michael ni mshirika wa kanisa lako mwenye umri wa miaka 20. Alipoteza wazazi wake wote wawili kutokana na Virusi Vya Ukimwi alipokuwa na umri wa miaka mitano na alilelewa na babu na nyanya yake. Siku zote wamekuwa wakitatizika katika kuweza kukidhi mahitaji yake. Michael amekubaliwa kujiunga na chuo kikuu kusomea uhandisi. Anauliza timu ya ukarimu ya kanisa ikiwa inaweza kumsaidia kumlipia karo ya chuo kikuu. Ingawa amekuwa akifanya kazi kama kibarua katika kazi ya ujenzi mjini, pesa kidogo anazopata anatumia kujinunulia chakula yeye na babu na nyanya yake.*

*B. Amit na Geeta ni wanandoa katika kanisa lako. Wanahusika katika mzozo wa ardhi na jirani ambaye wanasema anajaribu kubadilisha mipaka ya ardhi yao. Hawana pesa za wakili, kwa hivyo wanaomba kanisa kuwapa msaada wa kifedha kwa ada ya wakili. Jirani yao katika mzozo wa ardhi ni mshirika wa kanisa lingine katika eneo hilo.*

*C. Grace ana umri wa miaka 35 na si mshirika wa kanisa lako. Siku moja anajitokeza kanisani kwako kuzungumza na mchungaji, akilia na kuonyesha hofu. Anaomba kanisa kumtunza. Hana pesa. Mumewe amekuwa akimdhulumu, na unaweza kuona majeraha kwenye mwili wake. Ana wasiwasi kwamba akirudi nyumbani, mumewe atamuua. Grace anakiri kuwa ana tatizo la kunywa pombe na mumewe anamkasirikia kwa kutumia pesa kwa ajili ya pombe.*

*D. Francis na Rose ni wanandoa, na washirika waaminifu wa kanisa lako ambao huhudumu katika huduma mbalimbali. Wanaheshimiwa sana. Ndugu ya Rose na shemeji yake wana binti ambaye alizaliwa kiziwi. Kupitia shirikia lisilo la kiserikali, binti huyo amepata fursa ya kufanyiwa upandikizaji wa kifaa cha sehemu ya ndani ya sikio ambacho kitamawezesha kusikia kwa kiwango kidogo. Bei ya shughuli hiyo iliyopunguzwa kwa kiasi kikubwa ni dola 5,000. Francis na Rose wanauliza ikiwa kanisa lako linaweza kuchangia msaada wa kifedha kupitia mfuko wa ukarimu au toleo maalum la hiari kwa familia yao.*

*E. Roland na Divine ni wapenzi ambao hawajafunga ndoa ambao walianza kuhudhuria kanisa lako miezi sita iliyopita. Roland anazungumza na mchungaji wako na kuomba ikiwa kanisa linaweza kumsaidia yeye na familia yake katika miezi michache ijayo. Anasema hivi karibuni alipoteza kazi yake katika kampuni ya simu wakati alimripoti mwenzake aliyehusika na ufisadi, lakini suala hilo lilifunikwa. Anasema anatafuta kazi nyingine, lakini kwa sasa, hajui jinsi ya kulisha familia yake au kulipia karo ya shule ya watoto wake.*

Si cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(Soma sehemu hii nyumbani kwa ajili ya kujifunza zaidi)

Hii hapa chini ni sampuli ya “Fomu ya Mpango Kazi”. Hii ndio fomu unayoweza kutumia na mtu ambaye atasaidiwa na huduma ya ukarimu, lakini awe ni mtu ambaye amekubali kuandaa mpango kazi wa kuchukua hatua za kubadilisha hali yake. Unaruhusiwa kurekebisha fomu hii kama inavyohitajika.

Sio cha kuuzwa

# MPANGO KAZI WA HUDUMA YA UKARIMU[6]

**SEHEMU YA 1: Tafakari**

**A. Mustakabali Wako**

Ni jinsi gani ungependa hali yako ya maisha iwe tofauti au iboreshwe miezi minne hadi sita kutoka sasa?
Lengo la 1:

_______________________________________________

Lengo la 2:

_______________________________________________

**B. Uwezo na Rasilimali:**
Je, una uwezo na rasilimali gani ambazo zinaweza kukusaidia kufika mahali unapotaka kuwa miezi minne hadi sita kutoka sasa?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

**C. Vikwazo:**
Ni vizuri kufahamu mambo ambayo yanaweza kukuzuia kufika mahali unapotaka kuwa miezi minne hadi sita kutoka sasa. Inaweza kusaidia kuorodhesha kwa umahususi vikwazo muhimu vinavyoweza kuibuka. Kufanya hivyo kunaweza kutusaidia sote kuvifahamu na kuandaa mipango ya kuvishinda au angalau kupunguza athari za vikwazo hivyo.

Vikwazo vya ndani (mambo yanayohusu haiba yako au tabia ambazo zinaweza kuzuia au kupunguza kasi ya maendeleo)

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Vikwazo vya nje (watu au hali ambazo zinaweza kuzuia au kupunguza kasi ya maendeleo)

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

**SEHEMU YA 2: Kufanya Mipango ya Siku Zijazo Pamoja**

**A. Mambo Unayotaka Kufanya:**
Hatua ambazo zitakupeleka mahali unapotaka kuwa ndani ya miezi minne hadi sita:

Sio cha kuuzwa

**Lengo la 1**

_______________________________________________

Ni mambo gani mahususi unayoweza kufanya? Utayafanya lini?

(a) ______________________ ______________

(b) ______________________ ______________

(c) ______________________ ______________

Ni mambo gani mahususi ambayo kanisa linaweza kufanya? Litayafanya lini?

(a) ______________________ ______________

(b) ______________________ ______________

(c) ______________________ ______________

**Lengo la 2**

_______________________________________________

Ni mambo gani mahususi unayoweza kufanya? Utazifanya lini?

(a) ______________________ ______________

(b) ______________________ ______________

(c) ______________________ ______________

Ni mambo gani mahususi ambayo kanisa linaweza kufanya? Lini?

(a) ______________________ ______________

(b) ______________________ ______________

(c) ______________________ ______________

**SEHEMU YA 3: Kutia Watu Moyo na Uwajibikaji**

**A. Watu Wasaidizi**

Ni vigumu kwa wengi wetu kufanya mabadiliko peke yetu. Kwa hivyo, kama sehemu ya kukusaidia kufikia malengo yako, tuna mtu/timu ambayo ingependa kukusaidia kupitia maombi na kukutia moyo. Wameahidi:

☐ Kukuombea kila siku.

☐ Kuongea na wewe angalau mara moja kwa wiki. Hilo litafanywa ili kuona jinsi unavyoendelea na kukupa maoni kama unavyotaka.

☐ Kuweka habari siri kama inavyostahili.

Je, ungependa kuwa na mtu/timu inayokusaidia katika malengo yako?

______________

Jina la mtu msaidizi Nambari ya simu ya kiongozi wa timu simu

______________________ ______________________________

**B. Ufuatiliaji**

Mipango hushindwa ikiwa itapotea katika hali ya maisha yenye shughuli nyingi, kwa hivyo kuendelea kuwasiliana na kila mmoja ni muhimu sana. Kwa kawaida mawasiliano yatakuwa ya mara kwa mara mwanzoni mwa utekelezaji wa mpango kazi ili kuhakikisha kuwa kasi inapatikana.

Si cha kuuzwa

Ni lini na wapi tunaweza kukusanyika tena ili kukagua jinsi mambo yanavyoendelea?

_______________________________________________________________________________

Masharti mengine ya makubaliano:

_______________________________________________________________________________

Sahihi ya mtu husika:

_______________________________________________________________________________

Tarehe ____________________________________________

Sahihi ya mwakilishi wa kanisa: Tarehe

_______________________________________________________________________________

Tarehe ____________________________________________

Sio cha kuuzwa

[1] Mawazo mengi katika sehemu hii yamechukuliwa kutoka kwenye Steve Corbett and Brian Fikkert with Katie Casselberry, *Helping Without Hurting in Church Benevolence* (Chicago: Moody Publishers, 2015), 52-53, 57. Used by permission of Moody Publishers.

[2] Imehaririwa kutoka katika *Kusaidia bila Kuumiza katika Ukarimu wa Kanisa,* 53.

[3] Ibid., 57.

[4] Fomu hii imebadilishwa kwa ruhusa kutoka kwenye tovuti ya Kituo cha Chalmers: https://chalmers.org/wp-content/uploads/2021/01/tool-2-benevolence-intake-form.pdf.

[5] Maswali haya yamebadilishwa kutka katika *Kusaidia bila Kuumiza katika Ukarimu wa Kanisa,* 52-53.

[6] Fomu hii imebadilishwa kutoka kwenye tovuti ya Kituo cha Chalmers, iliyopatikana hapa: https://chalmers.org/wp- maudhui/upakiaji/2018/09/HWH_Benev_Tool_3_Action_Plan.pdf.

Sio cha kuuzwa

## Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa mshiriki



# Somo la 17: Huduma ya Mijini: Fursa na Changamoto

# Majadiliano ya Ufunguzi

*Inakufanya uhisije kuishi katika jiji kubwa au kusafiri kwenda katika jiji kubwa? Tuambie jibu lako kwa kutumia neno moja tu.*

______________________________

**Jadili na mwenzako:**

*1. Unaishi katika jiji gani au ni jiji gani lililo karibu na mahali unapoishi?*

______________________________

*2. Ni nini kinachokufurahisha kuhusu jiji lako?*

______________________________

*3. Ni nini kinachokufanya uhuzunike kuhusu jiji lako?*

______________________________

# Ukuaji wa Miji barani Afrika

"Jiji" au "eneo la mijini" ni mahali ambapo idadi kubwa ya watu wanaishi kwa karibu.[1] Kimahususi, katika somo hili tutaangazia jinsi ya kueneza habari njema ya Yesu Kristo kupitia maneno yetu na matendo yetu mijini, na tutazingatia sana jinsi ya kuwafikia kwa upendo watu walio maskini wa mali mijini.

______________________________

Miji barani Afrika inakua kwa kasi kwa sababu ya harakati zinazoendelea za watu wengi kuhama kutoka vijijini hadi mijini.

______________________________

**Takwimu:**

- Mnamo 1980, ni asilimia 20 tu ya idadi ya watu wa Afrika waliishi mijini.[2] Kufikia 2014, idadi hiyo ilikuwa imeongezeka hadi asilimia 40.[3] Kufikia 2050 inakadiriwa kuwa asilimia 55 ya Waafrika wataishi mijini.[4]
- Katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa asilimia 60 ya wakazi wa mijini wanaishi katika makazi duni.[5]
- Ni asilimia 16 tu ya kaya za mijini barani Afrika zina paa la kudumu.[6]
- Asilimia ya wakazi katika miji ya Afrika ambao wanapata maji safi kutoka kwa mabomba imekuwa ikipungua huku ukuaji wa miji ukiendelea. Ni asilimia 34 tu ndio walioweza kupata maji safi kufikia 2010.[7]
- Usafiri wa mijini katika miji ya Afrika ni ghali zaidi kwa asilimia 42 kuliko miji katika maeneo mengine ya dunia, kwa kiasi kikubwa kutokana na njia zisizofaa za uchukuzi wa umma kama vile pikipiki na mabasi madogo au teksi ambazo hubeba idadi ndogo ya watu.[8]



Sio cha kuuzwa

- Katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, inakadiriwa kuwa asilimia 60 ya wafanyakazi wa mijini wameajiriwa katika kazi zisizo rasmi kama vile uuzaji wa kiwango cha chini, huduma ndogo ndogo, au kufanya kazi katika viwanda ambavyo havijasajiliwa, kwa kipato cha chini sana.[9]

# Mhadhara: Je, Wakristo Wanapaswa Kujali Miji?

Biblia inafundisha nini?
**Mwanzo 11:1-9** na **Mwanzo 13:11-13.**

_______________

*Kutoka kwenye vifungu hivi viwili katika kitabu cha Mwanzo, tunajifunza nini kuhusu baadhi ya miji ya kwanza?*

_______________

Baada ya Mungu kuwaokoa Waisraeli kutoka Misri, aliwapa maagizo kuhusu jinsi wanavyopaswa kuishi katika Nchi ya Ahadi.
**Yoshua 20:1-3**

_______________

*Miji katika kifungu hiki inaonyeshwaje kwa namna tofauti na miji katika kitabu cha Mwanzo?*

_______________

Watu wa Israeli wakawa ufalme na taifa.
**1 Wafalme 14:21**

_______________

Yerusalemu ikawa makao ya Jina la Mungu. Huko Babeli, watu walijenga mji ili kujitukuza wenyewe, lakini Yerusalemu ulikuwa mji ambao Mungu alichagua kwa ajili ya utukufu wake.[10]

_______________

_______________

Kwa kuangalia manabii, tunakumbuka kwamba Mungu alimwita Yona kuhubiri hukumu kwa Waninawi ili watubu na kuokolewa kutokana na adhabu ya Mungu. Ninawi ilikuwa imejaa watu waovu sana.
**Yona 3:10** na **4:10-11.**

_______________

*Unawezaje kuelezea hisia za Mungu kwa mji mwovu wa Ninawi?*

_______________

_______________

Sio cha kuuzwa

Mara tu baada ya Ufalme wa Israeli kuundwa, wafalme na watu mara nyingi walishindwa kumwabudu Mungu ipasavyo. Waisraeli waliendelea kuabudu sanamu, kuwatendea vibaya maskini, na kushiriki katika uasherati na ufisadi. Hatimaye, hukumu ya Mungu iliwajia Israeli kwa ajili ya dhambi zao. Kwanza Mungu aliruhusu taifa la Ashuru, na baadaye taifa la Babeli, kuja na kushinda Israeli na Yuda yote. Watu wengi walipelekwa uhamishoni Babeli. Dola la Babeli lilikuwa adui mkubwa wa Israeli, na mji mkuu wa Babeli ulikuwa mji uliojaa ibada ya sanamu na dhambi.
**Yeremia 29:4-14**

---

*Ni amri gani mahususi ambazo Mungu anawapa Waisraeli walio uhamishoni katika kifungu hiki?*

---

---

---

---

## Nukuu kutoka kwa Timothy Keller:

> Mungu bado anajali kimsingi mpango wake wa wokovu. Lazima awastawishe watu wake; injili lazima itangazwe; wanadamu lazima wapatanishwe naye. "Hata hivyo anawahakikishia watu wake kwamba kutumikia ustawi wa mji huu wa kipagani ni sehemu ya mpango huu: 'Mwombeni Bwana kwa ajili ya mji huo, kwa sababu ukistawi, ninyi pia mtastawi.'" (Yer. 29:7). Kupenda na kutumikia mji huo hakuonyeshi tu upendo na huruma; kufanya hivyo pia kunaimarisha mikono ya watu wa Mungu, ambao wamebeba ujumbe wa injili kwa ulimwengu. Kwa sababu Wayahudi waliokuwa uhamishoni walitii amri hiyo, walipata ushawishi na nguvu zinazohitajika ili hatimaye kurudi na kurejesha nchi yao. Mungu anafungamanisha, kwa namna fulani, baraka za watu wake na ufanisi wa huduma yao ya mijini.[11]

Lazima tuzingatie kwamba leo tuko katika hali sawa na ya Wayahudi waliokuwa huko Babeli. Uraia wetu uko Mbinguni, lakini bado tuko katika ulimwengu huu uliovunjika ambao unamuasi Mungu. Lakini badala ya kukimbia ulimwengu kwa kukimbia miji, tunapaswa kupenda miji ya mataifa yetu.

---

Katika kitabu cha Matendo, injili kwa kiasi kikubwa ilipelekwa katika maeneo mapya kupitia kwa miji. Paulo na wamisionari wengine walisafiri kutoka jiji moja hadi lingine ili kuanzisha makanisa. Paulo alichukulia miji kama maeneo muhimu ambayo yalihitaji kufikiwa ili injili iweze kwenda vijijini pia.
**Warumi 15:18-24**

---

*Katika eneo lako, ni miji gani muhimu ambayo inahitaji makanisa zaidi ili tuweze kufikia eneo lote na injili?*

---

Sio cha kuuzwa

Fikiria juu ya mwisho wa Biblia katika Ufunuo sura ya 21 na 22.

Katika Ufunuo, tunaona kwamba makao makamilifu kwa watu wa Mungu ni mji, mji ambapo Mungu anakaa. Katika simulizi ya Biblia, watu wa Mungu wanaanza kuishi katika bustani, lakini wanaishia katika mji.

## Muhtasari

Kutokana na simulizi ya Bibilia, tumeona kwamba miji mingine imeanzishwa katika uasi dhidi ya Mungu na inaweza kuwa mahali pa maovu makubwa. Lakini pia tumeona kwamba miji inaweza kuwa mahali pa kukimbilia au kumwabudu Mungu wakati watu wa Mungu wanafanya kazi katika miji hiyo. Katika miji mingi, kutakuwa na uovu mkubwa na mema makubwa yanayotokea kwa wakati mmoja. Na tumeona kwamba Mungu anatuita tupende miji ambapo tunajikuta ndani yake. Hatupaswi kuwa kama Yona ambaye alihubiri kama njia ya kutelekeza jukumu, bali badala yake lazima tuhubiri kwa moyo wa upendo kwa ajili ya miji yetu. Lazima tuombee miji yetu, tutafute mema katika miji yetu, tujishughulishe na maisha ya miji yetu, tuitumikie miji yetu, na tulete maendeleo katika miji yetu ili ifanikiwe na ili tufanikiwe. Hatupaswi kuanguka katika dhambi tunazoziona karibu nasi katika miji yetu, bali tuhifadhi utambulisho wetu wa Kikristo na kuhubiri injili bila hofu. Na tunapofanya hivyo, tunatekeleza jukumu katika harakati ya jumla ya mpango wa ukombozi wa Mungu, ambao unahama kutoka kwenye bustani hadi kwenye mji. Haya yote yanatupa msingi wa kitheolojia ambao tunahitaji ili kufanya huduma ya mijini. Huduma ya mijini inahusu kuwapenda watu wa miji yetu kwa maneno yetu na matendo yetu kama sehemu ya mpango wa Mungu wa ukombozi.

*1. Ingeonekan aje hususan kwa kanisa lako kutafuta amani na ustawi wa jiji lako (au jiji lililo karibu nawe)?*

*2. Ikiwa kanisa lako lingetoweka ghafla kutoka kwa jiji lako, je, mtu yeyote angegundua? Je, mtu yeyote anaweza kusema, "Jamii yetu itawezaje kuishi bila kanisa hili?"*[12]

# Huduma ya Mijini: Fursa na Changamoto

*1. Ni changamoto gani mahususi ambazo makanisa ya mijini na viongozi wake wanakabiliana nazo katika huduma kwa sababu ya kuwa mjini?*

Sio cha kuuzwa

*2. Ni zipi baadhi ya fursa na faida za kipekee za huduma ambazo makanisa ya mijini na viongozi wake hupata kwa sababu ya kuwa mjini?*

Sio cha kuuzwa

## Kukabiliana na Changamoto na Kutumia Fursa

Kwa baadhi yetu, kufanya kazi jijini kunaonekana kuwa jambo la kutisha, lisilofurahisha na gumu. Tunahitaji kumtazama Kristo kama mfano wetu.

**1 Wakorintho 9:19-23**

Ikiwa hatuishi na watu walio maskini wa mali mijini, tutawajuaje na kujenga uhusiano? Hatuwezi kutatua matatizo ya jiji tukiwa mbali. Tunahitaji kuwahimiza waanzishaji wengi zaidi wa makanisa wahamie mijini. Na kwa sisi ambao ni viongozi wa kanisa la mijini, tunapaswa kuzingatia fursa za kimkakati za huduma ya mijini.

# Watoto Yatima na Walio Hatarini

Kuna watoto yatima zaidi ya milioni 52 barani Afrika kufikia mwaka 2017.[13] Wengi wao wako katika miji yetu. Wengine hawana makazi, wengine huomba msaada kutoka kwa madereva waliokwama katika msongamano wa magari, na wengine wanaiba ili kuishi. Kuishi katika miji kwa njia hii kumewaweka hawa watoto yatima na walio hatarini (pia inajulikana kama OVCs) katika hatari nyingi.

*1. Eleza kwa ufupi hatari zinazowakabili yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi jijini?*

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

*2. Ni njia gani bora kwa makanisa ya eneo husika kusaidia yatima na watoto walio katika mazingira hatari jijini?*

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Sio cha kuuzwa

## Vituo vya watoto yatima

Kumekuwa na ukosoaji mwingi wa hivi karibuni dhidi ya vituo vya yatima. Baadhi ya nchi za Afrika zinajitahidi kupunguza idadi ya vituo vya kulelea watoto yatima katika nchi zao na kuwatunza yatima kwa njia nyingine. Kwa mfano, Rwanda imeahidi kwamba itakuwa nchi ya kwanza ya Afrika ambayo haina vituo vya kulelea watoto yatima.[14] Tangu mwaka 2012, Rwanda imefunga vituo 25 kati ya 39 vya kulelea watoto yatima.[15] Wanafanya kazi ya kuwaweka yatima ndani ya familia za jamaa zao au katika familia za kulea watoto.

______________________________

## Hoja dhidi ya Vituo vya Yatima

1. Wengine wanasema kuwa vituo vya watoto yatima ni wazo la kigeni ambalo haliendani vizuri na utamaduni wa Kiafrika na mifumo ya familia. Kwa kawaida, katika tamaduni nyingi za Kiafrika, jamaa wangewachukua na kuwatunza yatima ikiwa wazazi wao wangekufa. Mtoto anachukuliwa kuwa na mama na baba wengi na nyumba nyingi za kuishi ndani ya jamii yao.[16] Kisha watoto hawa yatima hukua katika mifumya kifamilia na hubaki kuwa sehemu ya ukoo wao. Badala yake vituo vya watoto yatima huondoa watoto kutoka kwa jamaa zao na ukoo wao, na ikiwa watachukuliwa na watu wa kigeni, watoto hao wanaweza kupotea kutoka kwa jamii milele. Baada ya muda, vituo vya yatima vinaweza kusababisha jamii kupuuza majukumu yao ya kuwatunza yatima wao na kutegemea watu wa nje kuwalea watoto hao.

2. Vituo vya yatima vinahitaji pesa nyingi zaidi ili kumlea kila mtoto ikilinganishwa na gharama ya familia kuchukua watoto yatima ili kuwalea pamoja na watoto wao wengine.

3. Baadhi ya watu wanasema kuwa vituo vya watoto yatima huleta mgawanyiko na migogoro katika jamii kwa sababu yatima wanaweza kulelewa katika kiwango tofauti cha maisha ikilinganishwa na jamii inayowazunguka. Vituo vya yatima ambavyo havina wafanyakazi wa kutosha na havina fedha nyingi vinaweza kuwapuuza watoto na kutowatunza vizuri. Vituo vingine vya yatima ambavyo vimefadhiliwa vizuri vinaweza kuwapa yatima kiwango bora cha maisha kuliko watoto katika jamii. Hii inaweza kusababisha jamii kuhisi wivu. Ni kawaida pia kwa wazazi waliostawi kuwaacha watoto wao katika vituo vya yatima kwa sababu wanataka maisha bora kwa watoto wao au wanataka watoto wao wapate elimu ya bure ambayo vituo vya yatima vinatoa. Katika hali hizi, vituo vya yatima vinaleta migawanyiko katika familia badala ya kuzijenga. Badala ya kujenga vituo zaidi vya watoto yatima, tunahitaji kutumia rasilimali na muda wetu kuwatunza wazazi ili wawe na kazi bora na waweze kuwatunza watoto wao vizuri. Kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya jamii kutasaidia watoto zaidi kuliko kujenga vituo vya yatima.

4. Kukulia katika kituo cha yatima kunaweza kuwa tatizo sana kwa ukuaji wa mtoto.[17] Watoto wanaweza kukua na matatizo mbalimbali ya kisaikolojia kutokana na kutelekezwa, dhuluma ya kimwili, au dhuluma ya kingono. Inakadiriwa kuwa watoto wanaolelewa katika taasisi wana uwezekano mara sita wa kukabiliwa na vurugu kuliko watoto wanaolelewa katika mazingira ya familia.[18] Kwa wastani, watoto wanaokulia katika vituo vya yatima wana hisa ya akili iliyo chini kwa alama 20 ikilinganishwa na ya wale walio katika familia za kulea watoto, na wana uwezekano mdogo wa kupata ajira kama vijana wazima. Watoto wanapoondoka vituo vya yatima, wana uwezekano mara 10 zaidi wa kuingia katika ukahaba na mara 40 zaidi ya kupata rekodi ya uhalifu.[19] Watoto wengi katika vituo vya yatima wanakabiliwa na matatizo ya kushikamana na wengine kwani mara nyingi hawawezi kujenga mahusiano ya muda mrefu na watu wazima wanaowatunza. Hii ni kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya wafanyakazi wa kituo cha watoto yatima, pamoja na ukweli kwamba vituo vingi vya watoto yatima hufanya kazi kwa kutumia watu wa kujitolea wa kitaifa au wa kigeni ambao wanaweza kuhudumu kwa wiki kadhaa au miezi michache tu kwa wakati mmoja.

5. Baadhi ya watu wanadai kwamba serikali zinaweza kutegemea vituo vya yatima vinavyofadhiliwa na makanisa na mashirika yasiyo ya kiserikali na kupuuza kazi ngumu ya kuunganisha watoto waliopotea na familia zao au kutafuta nyumba na maeneo salama kwa ajili ya watoto wa mitaani.

6. Baadhi ya vituo vya yatima na mashirika ya kupanga watoto huwafanya watoto wawe katika hatari zaidi ya usafirishaji haramu wa binadamu. Wafanyabiashara wanaweza kuwahadaa kihisia watoto wapweke na kuwalazimisha kuondoka kwenye kituo hicho. Baadhi ya vituo visivyosimamiwa vizuri hushirikiana kwa makusudi na wasafirishaji haramu wa binadamu. Baadhi ya vituo vya yatima "huwezesha vikundi vya usafirishaji haramu wa watoto kwa kutumia ahadi za uwongo kuajiri watoto na kuwatumia ili kupata faida kutokana na michango."[20]

## Hoja za Kupendelea Vituo vya Yatima

1. Watu wengi wanakubali kwamba jamaa ndio wanaopaswa kuwatunza yatima, lakini ukweli ni kwamba hilo halifanyiki kila wakati. Watoto wa mitaani kwa kweli tayari wametengwa na jamii zao. Baadhi ya watoto wa mitaani na yatima wanapuuzwa na kutelekezwa na jamaa zao. Katika hali nyingine, watoto wanaishi mitaani jijini kwa sababu walikimbia mbali na vurugu au dhuluma ya kingono nyumbani kwao. Watoto wengine yatima hawana familia zinazoweza kufuatiliwa. Vituo vya watoto yatima vinatoa suluhu kwa ajili ya watoto walio katika hali hizi.[21]

2. Watu wengine wanakubali kwamba vituo vingi vya yatima vinatoa kiwango bora cha maisha kuliko kiwango kile ambacho watoto katika jamii wanapata, lakini wanasema kwamba yatima wanastahili uangalizi wetu maalum. Katika maeneo mengi, Biblia inataja hitaji la kutoa huduma maalum kwa yatima. Yatima tayari wamekuwa na mateso na shida za kutosha, na maisha yao ya baadaye kama watu wazima yatabaki kuwa magumu bila msaada kutoka kwa wazazi. Tunapaswa kufanya kadiri tuwezavyo kwa ajili yao wakati wako katika kituo cha yatima.

3. Vituo vya yatima vya Kikristo huwapa watoto yatima na watoto wa mitaani nafasi ya kusikia injili na kupata upendo wa Kristo. Yatima wengi wanatoka katika jamii ambazo watu hawamjui Yesu.[22]

4. Vituo vya watoto yatima hutoa ulinzi, utunzaji, makazi, elimu, na chakula kwa watoto walio katika mazingira magumu ambao wanaweza kuwa hawana mahali pengine pa kwenda katika jamii.

5. Vituo vya watoto yatima huokoa maisha ya watoto wengi ambao mama zao wangetoa mimba au kuwaua baada ya kuwazaa. Ni kawaida sana barani Afrika kwa watoto wachanga wanaozaliwa kupelekwa kwenye vituo vya watoto yatima na akina mama waliofadhaika ambao wanahisi hawana uwezo wa kuwatunza watoto hao, au wanaona aibu kwa kupata mtoto nje ya ndoa.

6. Vituo vya yatima kama taasisi husaidia kuwezesha mchakato wa kupanga watoto ili watoto yatima waweze kuwekwa ndani ya familia zenye upendo.

***Je, unaonaje? Tunapaswa kufanya juhudi za kufunga vituo vya yatima na kuwatunza yatima kwa njia mbadala? Au je, vituo vya yatima ni njia muhimu na bora ya kuwatunza yatima?***

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Sio cha kuuzwa

# Jukumu la Kanisa la Mjini katika Kupambana na Umaskini

- Hubiri injili kwa maneno na matendo. Kanisa ni kitovu cha mabadiliko katika jamii yoyote. Yesu huleta mabadiliko katika maisha ya watu na mahusiano ya watu ambayo hayawezi kufanikishwa na mpango wowote wala pesa. Wafundishe watu mtazamo wa kibiblia. Wafundishe na utembee nao wanapokua katika Kristo.

- Tia juhudi katika kuleta upatanisho. Wasaidie watu kukua katika uhusiano wao na Mungu, nafsi, wengine, na uumbaji wote.

- Wasaidie watu kugundua mali na ujuzi wao na kuvitumia kufanya kazi ya maana ili kujikimu wao wenyewe na familia zao.

- Toa kwa ukarimu kwa watu wenye mahitaji katika jamii yako kupitia huduma ya ukarimu ya kanisa lako.

- Jitahidi kushinda na kubadilisha mifumo iliyovunjika katika jiji lako. Tetea haki kwa niaba ya wale wanaodhulumiwa. Kanisa linapaswa kuwa sauti kwa wasio na sauti. Wawajibishe viongozi ili watu katika mtaa wako wapokee utawala bora na utoaji bora wa huduma.

- Unda ushirikiano na makanisa na mashirika mengine ya karibu na mfanye kazi pamoja ili kukabiliana na umaskini na changamoto katika jamii. Kwa mfano, makanisa yanaweza kufanya kazi pamoja na maafisa wa serikali au mashirika kujenga shule au kituo cha matibabu.

- Anzisha makanisa mapya katika maeneo mengine ya jiji, hasa maeneo masikini ambayo makanisa mengine yanaweza kuyaepuka. Epuka kushindana na makanisa mengine katika kupata washirika, bali tanguliza mahubiri kwa wale ambao bado hawamjui Yesu.

- Makanisa ya mijini yanapaswa kuongoza kwa mfano. Yanapaswa kuwa vielelezo vya uwazi na uadilifu katika jamii. Yanapaswa kuongoza katika kuwapenda na kuwakumbatia watu wa tamaduni na asili nyingine.

- Lenga kuleta manufaa katika jiji lako na mtaa wako. Safisha takataka na upande miti katika mtaa wako. Rekebisha mashimo katika barabara zilizo karibu. Jitolee kusaidia katika shule na kliniki. Tafuta njia za kuwahudumia watu katika jamii yako. Hata matendo madogo ya huduma yanaweza kuleta mabadiliko makubwa na kuwapa watu matumaini.

# Makanisa ya Mjini Yanaleta Mabadiliko

***Je, unaweza kutaja kanisa mahususi la mjini katika nchi yako ambalo linaleta matokeo chanya katika jiji lake? Eleza kile kanisa hilo linafanya na kwa nini unafikiri linafanikiwa kuleta mabadiliko.***

________________________________________

________________________________________

Sio cha kuuzwa

## Simulizi Zingine

1. Kulikuwa na kanisa la watu wapatao 20 huko Kagishu, jamii iliyoishi katika kitongoji duni jijini Nairobi, Kenya. Meshack, kijana kutoka kanisa hilo, alihudhuria mkutano wa Kikristo kuhusu maendeleo, na akarudi nyumbani kutoa changamoto kwa mchungaji wake kwamba kanisa lao linapaswa kufanya huduma kamili zaidi katika jamii yao. Mchungaji alishangaa jinsi wangeweza kukidhi mahitaji ya wengine wakati washirika wake wa kanisa walikuwa tayari maskini sana. Kulikuwa na watoto katika jamii ambao hawakuwa na uwezo wa kwenda shule. Kwa hivyo mke wa mchungaji na Meshack walianza kufundisha watoto hao bila malipo na baadaye wakafungua shule ambayo ilianza na wanafunzi 30. Ndani ya mwaka mmoja tu idadi ya watoto waliosajiliwa katika shule hiyo ilikua hadi kufikia wanafunzi 313, na wafanyakazi sita. Kwa sababu jamii iliona jinsi

kanisa lilivyowatunza watu wenye mahitaji, kanisa lilikua na washirika wake wakaongezeka mara dufu. Leo shule hiyo ina wanafunzi wapatao 450 na wafanyakazi 20 wanaolipwa, na shule nyingine tatu za msingi pamoja na shule ya sekondari zimeanzishwa.[23]

2. Kanisa la "God Bless Nigeria", huko Lagos, Nigeria, limekuwa likijaribu kwa makusudi kuwasiliana na makahaba. Viongozi wa kanisa huenda mitaani na kuwaalika wasichana wadogo waje kanisani. Kanisa lilianzisha nyumba ya makazi yenye vitanda 42 iitwayo Genesis House ili kuwasaidia wanawake kukaa mbali na masoko ya ngono. Wakati mwingine, kanisa huwasaidia makahaba hao wa zamani kuwalipa wanaume waliowasimamia na hata hoteli ambapo walikuwa wamekodisha vyumba. Makahaba wanaoacha biashara hiyo wanashauriwa na kupewa mafunzo ya stadi mbalimbali. Mchungaji Akinnola anaripoti kwamba karibu asilimia 40 ya wanawake wanaopitia mpango huo huepuka ukahaba kwa muda mrefu. Wengine wameolewa. Wengine wametumia ujuzi wao mpya kufanya kazi za kusuka nywele, upishi, ushonaji na taaluma zingine halali.[24]

## Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Washiriki wote wanapaswa kujaribu kufanya shughuli zote mbili hapa chini.

1. Ongoza kikao cha kujifunza Biblia na familia yako au kikundi kidogo kutoka kanisani ili kujifunza kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu miji. Jifunzeni pamoja vifungu ambavyo vinajadiliwa katika somo hili. Aidha, jaribu kupata vifungu vingine muhimu vya Biblia ambavyo pia vinahusiana na miji. Tumia konkodansi ili ikusaidie. Lenga kujifunza mengi zaidi kuhusu jinsi Mungu anavyotaka Wakristo waone na kuhusiana na miji.
2. Fanya utafiti kuhusu mtaa ulio karibu na kanisa lako la mjini. Ongea na wakazi wa eneo hilo na ujue kile wanachoamini kuwa fursa, mali, changamoto, na mahitaji ya jamii. Iwe pamoja na washiriki wengine wachache wa kujitolea kutoka kanisani au pamoja na uongozi rasmi wa kanisa, weka mpango kazi wa kuhudumia mtaa wako wa mijini. Anza na kitu kidogo. Inaweza kuwa rahisi kama kuanza mchezo wa soka wa kila wiki na kuwafundisha watoto Biblia, kupanda miti, kupaka rangi upya nyumba na ishara ambazo zimefutika, kuanza ziara za hospitali za kila wiki ili kuwatia moyo madaktari na wagonjwa, au kuzungumza na afisa wa serikali kuhusu ukarabati unaohitajika mtaani. Jaribu kufanya angalau badiliko moja zuri na mahususi katika jamii yako.

Sio cha kuuzwa

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

## Kuonyesha Ukarimu

Mbali na kuhudumia jamii zetu za mijini kwa upendo, tunapaswa pia kuhakikisha kuwa makanisa yetu ni maeneo ya kuvutia ambapo watu watahisi kukaribishwa. Makanisa yetu yanapaswa kuwa mahali ambapo watu wanaweza kutembelea na kupata upendo wa Kristo na kusikia habari njema ya injili.

*Tunaweza kufanya nini ili kufanya makanisa yetu ya mijini yawe na ukarimu zaidi kwa ajili ya:*

*1. Watu walio maskini wa mali?*

*2. Watu kutoka jamii na makabila mengine?*

*3. Watu wenye ulemavu wa kimwili au kisaikolojia?*

*4. Wageni wa mara ya kwanza?*

Sio cha kuuzwa

---

[1] City, (2019), In Vocabulary.com, inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://www.vocabulary.com/dictionary/city.

[2] Marian Starkey, "African Urbanization", (Population Connection, Januari 28, 2015), inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://populationconnection.org/blog/african-urbanization/

[3] See *World Urbanization Prospects: the 2014 Revision* (United Nations, New York, 2014), 1, inaweza kufikiwa mtandoano kwenye: https://web.archive.org/web/20160320085121/https://esa.un.org/unpd/wup/publications/files/wup2014-highlights.pdf.

[4] Mariama Sow, "Foresight Africa 2016: Urbanization in the African Context", (Brookings Institution, Washington DC, Desemba 30 2015), inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://www.brookings.edu/blog/africa-in-focus/2015/12/30/foresight-africa-2016-urbanization-in-the-african-context/.

[5] Somik Vinay Lall, J. Vernon Henderson, Anthony J. Venables, *African Cities: Opening Doors to the World,* (the World Bank, Washington DC, 2017), 38, inaweza kufikiwa mtandano kwenye: http://documents.worldbank.org/curated/en/854221490781543956/122290272_201711346052345/additional/113851-PUB-PUBLIC-PUBDATE-2-9-2017.pdf.

[6] Ibid., 48.

[7] Ibid., 140.

[8] Ibid., 88.

[9] "Unemployment Threatens World Cities; Jobs are Needed to Check Growth in Urban Poverty", International Labour Office, 29 Mei, 1996, inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://www.ilo.org/global/about-the-ilo/newsroom/news/WCMS_008055/lang--en/index.htm.

[10] Timothy Keller, *Center Church: Doing Balanced, Gospel-Centered Ministry in Your City,* (Zondervan, Grand Rapids, Michigan, Septemba 4, 2012), Loc. 3865-67.

[11] Ibid., Mahali. 3938-43.

[12] Timothy Keller, Twitter Post, 9 Januari 2014, 7:31AM. Inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://twitter.com/dailykeller/status/421257802854592512?lang=en.

[13] *On Orphans*, (Unicef, Juni 16, 2017), inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://web.archive.org/web/20180319141756/https://www.unicef.org/media/media_45279.html.

[14] Jack Graham, "Rwanda Wants to Become Africa's First Orphanage-free Country-Here's How", (Apolitical, Mei 24, 2018) inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://apolitical.co/solution-articles/en/rwanda-wants-to-become-africas-first-orphanage-free-country-heres-how.

[15] Ibid.

[16] Conrad Mbewe, "Orphans, Adoption and the African Extended Family", (The Gospel Coalition, Desemba 31, 2018) inaweza kufikiwa mtandani kwenye: https://africa.thegospelcoalition.org/article/orphans-adoption-african-extended-family/.

[17] Kwa muhtasari wa utafiti, tazama yafuatayo:
Save the Children Policy Brief, *Institutional Care: the Last Resort,* (Mei 2014) inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: http://www.thinkchildsafe.org/thinkbeforedonating/wp-content/uploads/Institutional-Care-The-Last-Resort-Save-The-Children.pdf.

Sio cha kuuzwa

Faith to Action Initiative, *Children, Orphanges, and Families,* (2014), inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: http://www.faithtoaction.org/wp- content/uploads/2014/03/Summary-of-Research4.pdf.

[18] Camaleo, "Orphanages Need to be Closed and Here is Why", (Julai 17, 2017), inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: http://camaleoproject.org/en/orphanages-need-to-be-closed-here-is-why/.

[19] Jack Graham, "Rwanda Wants…"

[20] US Department of State fact sheet: "Child Institutionalization and Human Trafficking" (Juni 28, 2018) inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://2017-2021.state.gov/wp-content/uploads/2019/02/283784.pdf.

[21] Kwa mtazamo huu, baadhi ya watu wanajaribu kukuza desturi bora kwa ajili ya vituo vya yatima. Tazama Philip Darke and Keith McFarland, *In Pursuit of Orphan Excellence,* (Credo House Publishers, Grand Rapids, Michigan, 2014).

[22] Conrad Mbewe, "Orphans, Adoption…"

[23] Scott Allen, Darrow L. Miller, and the African working group of Samaritan Strategy Africa, *Against All Hope: Hope for Africa* (Phoenix, Ariz., Disciple Nations Alliance, 2005), 50, inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://disciplenations.org/resources/against-all-hope-hope-for-africa/.

[24] Danny McCain, "Addressing Urban Problems Through Kingdom Theology: The 'Apostles in the Market Place' Model in Lagos, Nigeria", (Africa Journal of Evangelical Theology 32.1 ukurasa 61-80, 2013), 68 Tazama katika mfumo wa PDF [Imetolewa tena kwa idhini ya mwenye hakimiliki wa sasa]: https://www.biblicalstudies.org.uk/pdf/ajet/32-1_061.pdf.

Sio cha kuuzwa

## Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 18: Safari za Misheni ndani ya Afrika

Si ya kuuzwa

# Utafiti wa Ufunguzi [1]

*Warumi 10:14-15*

Ufafanuzi wa SMMM =

## Utafiti wa Kikundi

*1. Ni wangapi kati yenu wamewahi kwenda kwenye SMMM katika jamii au eneo lingine?*

*2. Ni wangapi kati yenu mlifanya uinjilisti katika safari zenu? Ni wangapi kati yenu mlijaribu kuwahudumia au kuwasaidia watu maskini katika safari zenu?*

*3. Ni wangapi kati yenu mlitoa rasilimali au pesa kwenye safari zenu?*

*4. Ni nini hasa ulichowapa watu?*

*5. Ni wangapi kati yenu mlishauriana na watu, jamii, au eneo kabla ya kwenda?*

Sio cha kuuzwa

## Faida za SMMM

*Je, ni zipi faida au manufaa yanayoweza kupatikana katika safari za misheni za muda mfupi?*

## Changamoto na Makosa katika SMMM

*1. Je, baadhi ya changamoto au mapungufu ya SMMM ni yapi?*

*2. Ni makosa gani umefanya kwenye SMMM ambayo yalisababisha madhara kwa watu katika jamii ya wenyeji au kwa washiriki wa SMMM?*

Sio cha kuuzwa

# Shughuli ya Kikundi Kuhusu Tofauti za Kitamaduni

*1. Je, wamisionari walifanya chochote kilichokanganya au kuudhi jamii ya wenyeji?*

---

*2. Je, jamii ya wenyeji ilifanya chochote kilichokanganya au kuwaudhi wamisionari?*

---

*3. Je, ulipogundua tofauti zenu za kitamaduni, uliweza kubadilika ili kukabiliana na hali hiyo?*

---

*4. Ulishughulikiaje suala la utoaji zawadi?*

---

*5. Soma 1 Wakorintho 9:19-23. Kifungu hiki kinaweza kutusaidiaje kufikiria juu ya tofauti za kitamaduni tukiwa kwenye SMMM?*

---

---

Sio cha kuuzwa

# Kupanga SMMM Zenye Manufaa

Kanuni za mwisho za kutafakari:

1. Jifunze kadiri uwezavyo kuhusu utamaduni, desturi za kijamii, lugha, na mazingira ya eneo unalokusudia kutembelea. Usiruhusu washirika wa kanisa kwenda kwenye safari isipokuwa waonyeshe kujitolea kujifunza na kutumia muda katika maandalizi.

---

2. Hakikisha kwamba SMMM yako ina kusudi la wazi na mahususi.

---

3. Kumbuka kutangaza habari njema ya ufalme wa Mungu. Kuwahudumia watu kwa njia kamili kwa kufanya kazi kwa ajili ya upatanisho katika mahusiano yao na Mungu, nafsi zao, watu wengine, na uumbaji.

---

4. Mwakilishi wa kanisa lako anapaswa kujaribu kutembelea eneo hilo kwanza peke yake.

---

5. Baada ya kupanga kwa uangalifu safari yako, ikiwa utagundua kuwa ni ghali sana, au kwamba hatari zinazidi faida zinazowez kupatikana, basi uwe tayari kusema "hapana" kwa wazo la SMMM, na utumie pesa hizo kusaidia wamisionari wa muda mrefu katika eneo hilo, au kuwekeza zaidi katika kusaidia watu

walio maskini wa mali katika jamii yako mwenyewe.

6. Kumbuka kwamba SMMM yako inapaswa kumletea Mungu utukufu. Si nafasi ya kufanya mwonekane wazuri, au kujenga sifa ya kanisa lenu, au kumtukuza mwinjilisti au mchungaji.

7. Kumbuka kuomba. Maombi kwa ajili ya SMMM yako pia yatakusaidia kukabiliana na kutubu kwa ajili ya mtazamo wowote wa kujiona kama mungu ambao unaweza kuwa nao kabla ya kuenda kwenye safari yako.

8. Zingatia maendeleo ya muda mrefu.

9. Kwa kadiri inavyowezekana jaribu kuwasaidia watu kugundua mali, ujuzi, na fursa zao. Zingatia kuwatia moyo na kuwajenga watu.

10. Uwe mnyumbufu na uwe tayari kubadilika.

11. Omba washiriki kwenye SMMM wawekeze rasilimali zao wenyewe kwenye safari.

12. Fikiria kwa makini kuhusu ni nani anayepaswa kuongoza SMMM. Ni vyema kwamba viongozi wa SMMM wawe tayari wanahusika katika misheni na wawe ni watu ambao wanawapenda na kuwajua watu walio maskini wa mali.

13. Kuwa tayari kujifunza.

14. Uwe mwangalifu kuhusu jinsi unavyozungumza kuhusu watu walio maskini wa mali unapozungumza na kanisa lako kuhusu safari yako na unapozungumza na watu katika jamii ya wenyeji. Hatutaki kila wakati kuita watu ambao tutatembelea "maskini". Umaskini wao wa mali haupaswi kufafanua utambulisho wao wote. Kumbuka kwamba wao ni watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu.

15. Tumia vipawa mbalimbali vya wanatimu wako. Uwe mbunifu katika kupanga safari. Kila mtu ana njia tofauti ambazo anaweza kufundisha, kuhudumu, au kutia moyo. Soma **1 Petro 4:10.**

Sio cha kuuzwa

16. Kwa ujumla, ni sera nzuri kuepuka kuenda na rasilimali za kuwapa watu isipokuwa watu wawe wanahitaji msaada kwa sababu ya shida.

17. Unapotembelea jamii ya wenyeji, tafuta njia za kushirikiana na makanisa ya eneo husika, mashirika ya maendeleo ya eneo husika, na viongozi wengine katika serikali na jamii.

18. Baada ya safari, chukua muda wa kutathmini pamoja na timu nzima yale mliyoshuhudia:

- Tafuta kujua kile ambacho kila mwanatimu alijifunza kuhusu kuvunjika kwake katika uhusiano wake na Mungu, watu wengine, nafsi yake, au uumbaji.
- Walijifunza nini kutoka kwa watu? Ni mambo gani mazuri waliyoyaona katika uhusiano wa watu wa eneo hilo na Mungu, nafsi zao, watu wengine, na uumbaji?
- Unafikiri mliimarishaje makanisa na huduma zilizo katika eneo hilo kwa muda mrefu?
- Je, kuna njia ambazo mlifanya mambo kuwa magumu zaidi kwa makanisa na huduma zilizo katika eneo hilo kwa muda mrefu?
- Jadilini ikiwa safari hiyo imewafanya muwe wakarimu zaidi, muwe tayari zaidi kuwasaidia wamisionari, au muwe tayari zaidi kufanya urafiki na watu maskini katika eneo lenu.
- Ili mabadiliko haya yatendeke, lazima myatekeleze badala ya kuyazungumzia tu. Kwa hivyo andikeni hatua ambazo mtachukua ili mbadilike kama kanisa la kieneo au kama watu binafsi.
- Jadili ikiwa safari ya siku zijazo inaweza kusaidia kuendeleza uhusiano na jamii ya wenyeji kwa muda mrefu.
- Muhimu zaidi, usisahau kuwauliza wanajamii wenyeji walichofikiria kuhusu safari hiyo na ikiwa ilikuwa na manufaa kwao. Jaribu kutafuta zaidi ya shukrani zao za kiungwana na ujaribu kubaini uwezo wa muda mrefu wa jamii ya wenyeji katika kutafuta mabadiliko ya kudumu.
- Jitoleeni kuendelea kuomba pamoja kwa ajili ya jamii ya wenyeji. Furahia fursa ya kushiriki katika utume wa Mungu wa kuhubiri mema mapya.

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza. Washiriki wote wanapaswa kujaribu kufanya shughuli zote mbili hapa chini.

1. Fikiria kuhusu wamisionari wa muda mrefu ambao kanisa lako limetuma kwa jamii au nchi nyingine. Wasiliana nao na uone jinsi wanavyoendelea na ujue ikiwa wanahitaji kutiwa moyo au kupewa usaidizi wa aina yoyote. Waulize ikiwa itasaidia huduma yao na itafaa kwa jamii iwapo kanisa litatuma timu ya muda mfupi kuwatembelea au ikiwa kuna njia nyingine ambayo unaweza kuwapa msaada zaidi.

2. Kanisa lako litakapopanga SMMM tena, jifunze kanuni katika somo hili pamoja na viongozi na timu ya mipango ya STM. Tumia miongozo uliyojifunza katika somo hili kuandaa SMMM yako kwa busara.

---

[1] Dhana nyingi katika sura hii zinatokana na mawazo yaliyo katika kitabu cha Brian Fikkert and Steve Corbett, *Helping Without Hurting in Short-Term Missions,* (Moody Publishers, Chicago, IL, 2014).

Sio cha kuuzwa

# Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki



# Somo la 19: Wageni, Wamisionari, na Wafadhili

Sio cha kuuzwa

# Majadiliano ya Ufunguzi

## Aina 4 za Wageni:

1. ______________________
2. ______________________
3. ______________________
4. ______________________

Katika somo hili, tutakuwa na majadiliano nyeti.
**1 Wakorintho 13:1-3**

______________________

**Waefeso 4:2**

______________________

**Waefeso 4:29**

______________________

Sio cha kuuzwa

*Katika vikundi vya watu watatu au wanne, kila mtu anapaswa kujadili kwa ufupi uzoefu wake wa kufanya kazi na wageni kutoka kwenye mojawapo ya makundi haya manne.*

*1. Eleza uhusiano bora zaidi uliokuwa nao na mgeni.*

______________________

______________________

*2. Eleza uhusiano mgumu uliokuwa nao na mgeni.*

______________________

______________________

*3. Ikiwa umefanya kazi pamoja na mgeni, ni nani aliyechukua jukumu la uongozi na kufanya maamuzi mengi?*

______________________

*4. Je, unamjua mgeni ambaye unamwona kuwa rafiki wa kweli? Eleza.*

______________________

______________________

Serikali nyingi za kigeni, kampuni, mashirika, wamisionari, na wadhamini wamechangia sana katika maendeleo ya hatua kwa hatua na uboreshaji wa maisha barani Afrika. Hata hivyo, wageni pia wamesababisha madhara katika mchakato huo, hata kama wakati mwingine madhara hayo yanasababishwa bila kukusudia.

______________________

Jambo la kushukuru ni kwamba baadhi ya wageni wamebadilishwa katika mawazo yao, wamebadilisha mtazamo wao na kutubu kwa makosa ambayo walifanya hapo awali. Baadhi yao wanajaribu kusaidia kwa njia bora zaidi na inayozingatia zaidi ufalme, na hilo kwa kiasi fulani ni kwa sababu ya vitabu kama vile *Wakati Kusaidia Kunaumiza*, ambacho ndio msingi wa mtaala huu.

Tutajadili jinsi tunavyoweza kufanya kazi vizuri zaidi pamoja na wageni barani Afrika, ili kwa pamoja tuweze kuwasaidia watu maskini katika nchi zetu bila kusababisha madhara. Tunahitaji kusaidiana kushinda mivutano inayotokea wakati mwingine kati yetu kama Waafrika na wageni wanaofanya kazi barani Afrika.

# Kutoelewana na Migogoro Kwa Sababu za Kitamaduni

Watu wengi hupatwa na "mshtuko wa kitamaduni" wanapohamia nchi ya kigeni na kujaribu kuzoea tofauti za kitamaduni.

______________________________

Wageni wanahitaji kuwa tayari kuzoea tamaduni zetu wanapofanya kazi barani Afrika, lakini pia tunahitaji kuwa na subira na wao na kuwafundisha kwa upole.

______________________________

Kumbuka kwamba tamaduni ni tofauti sana na ni changamano.

______________________________

______________________________

***Je, ni yapi baadhi ya matukio ya kawaida ya kutoelewana na migogoro kwa sababu za kitamaduni kati ya wageni na Waafrika ambayo huleta mafadhaiko katika mahusiano yetu au kusababisha matatizo katika jitihada zetu za kuwasaidia watu maskini pamoja?***

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Sio cha kuuzwa

## Uchunguzi kifani kuhusu kutoelewana kwa sababu za kitamaduni

*Mmishonari wa kigeni alikuwa akiongoza warsha ya viongozi wa kanisa la kitaifa wanaohusika katika kutafsiri Biblia. Mmishonari huyo hakujua kwamba katika utamaduni huo mtu mzee zaidi ndiye wa kwanza kuzungumza, kisha mtu wa pili kwa umri anazungumza, kisha mtu wa tatu kwa umri anzungumza, na kadhalika hadi mwishowe, mtu mwenye umri mdogo zaidi anaweza kuzungumza. Mmishonari huyo alipendekeza swali la majadiliano kwa kikundi kizima. Kila mtu alikuwa kimya. Mmishonari huyo aliuliza swali hilo tena. Kikundi kilikuwa bado kimenyamaza. Mmishonari huyo hakujua kwamba mtu mzee zaidi katika kikundi hicho hakuwa na uhakika kuhusu maana ya swali hilo, na hakuna mtu mwingine aliyethubutu kuzungumza. Mmishonari huyo hakujua kilichokuwa kikiendelea, kwa hivyo aliacha kutumia njia shirikishi na kikundi hicho na akawasilisha habari mwenyewe.*[1]

***1. Tunajifunza nini kutokana na simulizi hii?***

____________________________________________________________

____________________________________________________________

***2. Viongozi wa kanisa wangeweza kufanya nini kumsaidia mmishonari huyo?***

____________________________________________________________

____________________________________________________________

# Migogoro Juu ya Pesa

Kumbuka kile tulichojifunza katika Somo la 13 – "Utamaduni wa Kiafrika na Pesa". Sifa za tamaduni za Kiafrika ambazo tulijadili katika somo hilo ni sifa zile zile ambazo wageni wanaweza kupata shida kuzielewa na kuzizoea.

***Ni vipengele gani vya matumizi ya fedha katika utamaduni wetu ambavyo unaweza kukumbuka kutokana na somo hilo ambavyo vingekuwa vigumu kwa wageni kuzoea?***

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

## Mifano mahususi ya migogoro kati ya Waafrika na wageni kwa sababu ya mitazamo tofauti juu ya urafiki na pesa:

1. Waafrika wengine wanaweza kuvunjika moyo wakati marafiki wa kigeni hawawapi msaada wowote wa kifedha au wa vifaa. Rafiki wa kweli barani Afrika anachukuliwa kuwa yule anayemsaidia mwenzake wakati wa mahitaji. Waafrika wengine wanaweza kuangalia maisha ya kitajiri ya wageni na wanyama vipenzi wao na magari yao ya bei ghali na kudhani kwamba wao ni matajiri sana, na hivyo wanakuwa na hisia kwamba wageni ni wabinafsi na wanajijali wao tu wakati watu wanaoishi karibu nao wako katika dhiki ya umaskini wa mali.

Sio cha kuuzwa

2. Wageni wanaweza kufadhaika wanapokuwa na marafiki wengi wa Kiafrika, lakini hawajui ni marafiki gani wanaowajali kikweli, na ni marafiki gani wanatafuta tu mtu wa kuwapa pesa.

3. Waafrika wanaweza kuudhika wakati mgeni au rafiki wa kigeni anakataa zawadi. Hii inaweza kuwafanya baadhi yao wajihisi duni au kudhani kwamba mgeni huyo ana kiburi. Mgeni anaweza kutaka kukataa zawadi hiyo kwa sababu anaona kwamba mtu anayetoa zawadi hiyo anaihitaji zaidi na hataki kuwa mzigo kwa watu walio maskini wa mali. Kosa hili linaweza kutoka kwenye moyo wa huruma, lakini lina madhara sana kwani linawanyima Waafrika heshima, baraka, na furaha ya kuweza kutoa kwa wengine.

4. Wageni wanaweza kujaribu kutoa kwa ukarimu ili kuwasaidia marafiki na majirani zao wa Kiafrika, lakini wakati mwingine wana upungufu wa kifedha na kwa hivyo hawawezi kumsaidia kila mtu. Hii inaweza kuwasababishia msongo mkubwa wa mawazo wanapojaribu kuamua ni nani wa kumsaidia na kwa njia gani.

5. Waafrika mara nyingi hufadhaishwa na wageni ambao hawawezi kukiri wakati wanapokuwa na mahitaji au wakati wanahitaji msaada. Waafrika wanataka kuwatunza marafiki zao ambao ni wageni, lakini ni vigumu kujua jinsi ya kusaidia ikiwa wageni wanajaribu kuishi kwa kujitegemea, kuwa na kiburi, na hawakubali kwamba wao pia wanahitaji msaada wakati mwingine.

6. Baadhi ya wageni wamejitolea kwa kujinyima ili kuja Afrika na hawana pesa nyingi. Wengine wanaweza hata kuwa watu wa kujitolea ambao hawalipwi. Wanaweza kufadhaika wakati Waafrika wanachukulia kwamba wao ni matajiri kwa sababu tu ya nchi yao ya asili. Wakati mwingine Waafrika hawaelewi jinsi wageni walivyojitolea kwa kujinyima na wanaweza kufikiria kwamba wageni wanatafuta fursa za ajira barani Afrika ambazo hawangeweza kupata katika nchi zao.

***Ni migogoro gani mingine ya kawaida kati ya Waafrika na wageni ambayo inahusu pesa? Unapojibu, jaribu kutoa suluhisho yenye manufaa ili kuzuia au kutatua mgogoro huo.***

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

## Kuzungumza Kuhusu Migogoro

Masuala haya yanaweza kuonekana kuwa madogo lakini baada ya muda yanaweza kusababisha kuvunjika kwa mahusiano kati ya Waafrika na wageni. Masuala haya yanapoanza kusababisha mafadhaiko, mara nyingi tunajaribiwa kuyapuuza kwa ajili ya "kulinda amani". Tunachukua hatua ya kuwa na subira na hatuzungumzi hadi tukasirike kiasi kwamba uchungu wetu ujitokeze wazi. Hali hiyo ya uchungu kujitokeza wazi inaweza inaweza kusababisha uhusiano kuvunjika kabisa, kupigiana, au kujiuzulu kutoka kwenye wadhifa.

Sio cha kuuzwa

Badala ya kupuuza suala husika, lazima tuendelee kujitahidi kusema ukweli kwa upendo. Tafakari **Warumi 12:18** na **Mathayo 18:15-17.**

*Amri hizi zinatuongozaje katika jinsi ya kushughulikia migogoro kati ya Waafrika na wageni, hasa wageni ambao ni Wakristo?*

## Kujenga Mahusiano Bora

*Shiriki kwa ufupi ni hatua gani tunaweza kuchukua ili kujenga mahusiano bora na yenye manufaa kati ya Waafrika na wageni.*

### Maombi ya Kufunga

Sio cha kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza.

1. **Kwa Waafrika ambao wanajua wageni –** Mwalike rafiki au mwenzako wa kigeni ili akutembelee nyumbani kwako kwa chakula. Chukueni muda kujadili tamaduni zenu tofauti ili kila mmoja aweze kujifunza kutoka kwa mwenzake. Mwambie rafiki yako wa kigeni baadhi ya mambo uliyojifunza katika somo hili. Muulize rafiki yako kile unachoweza kufanya kwa namna tofauti katika uhusiano wenu ili kuzoea utamaduni wa rafiki yako na muwe na uhusiano wenye manufaa zaidi. Ikiwa rafiki yuko tayari, ombeni pamoja baada ya mazungumzo haya.

2. **Kwa Waafrika ambao hawajui wageni wowote –** Fikiria ikiwa kuna mmishonari yeyote wa kigeni au shirika ambalo limefanya kazi katika jamii yako. Ikiwa unafikiri mmepata faida yoyote ya kibinafsi kutokana na kazi ya mmishonari huyo au shirika hilo katika jamii yenu, chukua hatua ya kuonyesha shukrani kwa kazi yao. Unaweza kuwasiliana na mmishonari huyo au shirika hilo ana kwa ana ili kuwashukuru kwa kazi waliyofanya, au unaweza kuwaandikia barua ya kibinafsi ili kuwashukuru kwa kile walichofanya na kuwatumia kwa njia ya posta au barua pepe.

3. **Kwa wageni –** Alika rafiki au mwenzako wa Kiafrika nyumbani kwako kwa chakula. Ikiwa uko Afrika kwa ziara fupi tu, mnaweza kupanga kukutana pamoja katika eneo tofauti. Chukueni muda kujadili tamaduni zenu tofauti ili kila mmoja aweze kujifunza kutoka kwa mwenzake. Mwambie rafiki yako baadhi ya mambo uliyojifunza katika somo hili. Mwambie rafiki yako wa Kiafrika awe mkweli kwako na akuambie mambo unayoweza kubadilisha ili ujizoeshe vizuri utamaduni na jamii ya eneo husika ili uweze kuwa na uhusiano bora na wenye mahufaa zaidi. Uliza ikiwa kuna kitu chochote unachofanya ambacho kinaonekana kuwa cha kukera au cha kufadhaisha kwa rafiki yako au wengine. Ikiwa rafiki yuko tayari, ombeni pamoja baada ya mazungumzo haya.

# Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kidogo

*1. Ulishangaa zaidi kujifunza nini katika somo hili?*

___

___

*2. Je, kuna kitu chochote katika somo hili ambacho hukukubaliana nacho, au ambacho uliona ni vigumu kukielewa? Acha wenzako wa kikundi wakufafanulie mada zozote ambazo zilikuwa ngumu kwako kuzielewa kikamilifu.*

___

___

*3. Je, umewahi kumwomba mgeni akupe pesa au rasilimali za vifaa? Kwa nini iwe hivyo au kwa nini isiwe hivyo? Ikiwa wewe ni mgeni, je, umewahi kuwaomba Waafrika wakupe pesa au rasilimali za vifaa?*
*Kwa nini iwe hivyo au kwa nini isiwe hivyo?*

*(Maswali yanaendelea kwenye ukurasa wa 224)*

Sio cha kuuzwa

*4. Je, mgeni amewahi kukusaidia kwa kukufundisha kitu kipya kuhusu Mungu, au maarifa au ujuzi mpya wa kiutendaji? Je, alikuwa tayari pia kujifunza mambo kutoka kwako? Ikiwa wewe ni mgeni, umejifunza nini kutoka kwa Waafrika?*

*5. Je, umeona wageni wakisababisha madhara gani barani Afrika?*

*6. Je, ungependa mmishonari wa kigeni aje kuishi katika jamii yako kwa miaka michache au kikundi tofauti cha kanisa la kigeni kije kila baada ya miezi michache kwa wiki moja tu kwa wakati mmoja? Kwa nini?*

*7. Wageni wanaweza kufanya nini kwa namna tofauti ili kuboresha uhusiano wao na wewe kama Waafrika?*

*8. Waafrika wanaweza kufanya nini kwa namna tofauti ili kuboresha uhusiano wao na nyinyi kama wageni?*

Sio cha kuuzwa

# Tafakari Zaidi

(*Soma sehemu hii nyumbani kwa ajili ya kujifunza zaidi*).

Tunaposhirikiana na kila moja ya makundi manne ya wageni ambayo yalitajwa mwanzoni mwa somo hili, kuna kanuni za kuzingatia ambazo zitatusaidia tunapoingiliana na kila kikundi.

### A. Wamisionari wa muda mfupi na wa muda mrefu

Wageni hawa ni ndugu na dada zetu katika Kristo. Wako Afrika kuhubiri injili na kutusaidia katika vita vyetu dhidi ya umaskini. Unaposhirikiana na wamisionari hawa wa kigeni, kumbuka kufuata mafundisho ya Biblia kuhusu jinsi ya kuhusiana na ndugu na dada. Tunapaswa kufanya kazi nao kama sehemu ya timu moja, mwili wa Kristo. Wanapofanya makosa au kuanguka dhambini, tunapaswa kuwakabili kwa upole na kujaribu kuwarejesha.

Kanuni za kutafakari:

1. Usiwahukumu wamisionari wote wa kigeni kwa msingi wa kile ulichopitia wewe binafsi na mmishonari mmoja. Wamisionari wa kigeni wanatoka nchi mbalimbali kote ulimwenguni. Wako tofauti sana si tu katika suala la utamaduni bali pia katika suala la kanuni za imani, desturi za kanisa, na desturi za mtindo wa maisha. Na uwe mwangalifu usihukumu jinsi watu kutoka nchi fulani walivyo kulingana na jinsi mmishonari mmoja alivyo. Mmishonari wa kigeni kutoka Kanada yamkini ni tofauti sana kwa njia nyingi muhimu na raia wa kawaida wa Kanada.

2. Wamisionari wengi wa kigeni wanajaribu kusaidia barani Afrika. Wanajali kuhusu shida za hapa na wanataka kuona mabadiliko yakitokea. Lakini wanaweza kuja wakiwa na mtazamo wa kujiona kama mungu, au ufahamu mdogo wa asili halisi ya umaskini na sababu zake. Wengi wao huishia kuumia barani Afrika huku wakijaribu kusaidia. Kama Waafrika, lazima tuwe tayari kuwapa changamoto kwa upole ili waboreshe mbinu zao za kupambana na umaskini, na kuwapa changamoto kwa upole ili kuwasaidia kuona mtazamo wao wa kujiona kama mungu na kiburi chao. Wakati wowote inapowezekana, tunapaswa kuwahimiza kushiriki katika mafunzo ya siku zijazo ya *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrka*.

3. Kuna vikundi vingi vya wamisionari wa muda mfupi ambavyo hutembelea Afrika kutoka nchi nyingine za kigeni. Mengi ya makundi haya yanaweza kufaidika sana na kanuni tulizoangazia katika Somo la 18 – "Safari za Misheni Ndani ya Afrika". Kanuni zile zile ambazo tulijifunza kuhusu safari ndani ya Afrika pia zinatumika kwa safari za kwenda Afrika kutoka nchi za kigeni. Usikubali kukaribisha kila mwanafunzi, mgeni, au timu ya muda mfupi ambayo inataka kuja kutoka nchi ya kigeni. Hakikisha kwamba timu kama hiyo itapanga safari yake vizuri na kulinufaisha kanisa au jamii yako. Kuwa tayari kuwaambia "hapana, hupaswi kuja", inapobidi. Hili linaweza kuwa jambo gumu sana, hasa ikiwa kusema "hapana" inamaanisha tutapoteza msaada wa kifedha au zawadi ambazo zitaletwa na watu hao katika safari yao. Kumbuka kile tulichojifunza katika mtaala huu, kwamba suluhisho la umaskini si rahisi kama kutoa tu pesa. Ikiwa safari hiyo itasababisha madhara zaidi kuliko mema, kuwa na ujasiri wa kusema "hapana" au kuwa mkweli kwao kuhusu jinsi wanavyoweza kubadilisha mipango yao ili safari yao iwe na manufaa zaidi. Fikiria kuambia timu za kigeni kwamba zinahitajika kufanya mafunzo ya *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika* kabla ya kukutembelea. Au unaweza kuwaambia kwamba wanahitaji kusoma kitabu cha Kimarekani kinachoitwa, *Kusaidia Bila Kuumiza katika Mmisheni za Muda Mfupi* kabla ya kukutembelea.

4. Wamisionari wa kigeni huja Afrika kwa sababu tofauti. Wengine wanakuja kujifunza, na wengine wanakuja kuhudumu, na tunatumaini kwamba hata wale wanaokuja kuhudumu pia watakuwa tayari kujifunza. Kwa wale wamisionari wanaokuja kuhudumu na kufanya kazi barani Afrika, tunapaswa kuwahimiza waje wakati wamepata ujuzi na mafunzo. Inasababishia jamii za Kiafrika mafadhaiko makubwa wakati wamisionari wa kigeni wanapokuja Afrika na hamu ya kubadilisha ulimwengu haraka ingawa hawana mafunzo wanayohitaji. Hii inaonekana sana hasa kwa vijana wa kigeni ambao wamemaliza shule ya sekondari au chuo kikuu. Wanataka kuleta mabadiliko ulimwenguni. Hamu hiyo ni nzuri, lakini tunapaswa kuwahimiza kujiandaa kikamilifu kwa kazi ambayo wanataka kufanya. Wahimize wamisionari wa kigeni kwamba ikiwa wanataka kuwafundisha wachungaji, wanapaswa kuwa wamepata mafunzo ya kitheolojia. Ikiwa wanataka kufanya kazi na watu wasio na makazi barani Afrika, wanapaswa kuwa na uzoefu wa kufanya kazi na watu wasio na makazi katika nchi yao ya asili. Ikiwa wanataka kuja Afrika kuwasaidia wagonjwa, wanapaswa kuwa walisomea utabibu katika nchi yao ya asili. Wawajibishe wamisionari kwa kazi wanayofanya, na usisitize kwamba wawe watu waliofunzwa vizuri na wenye ujuzi.

5. Chukua muda wa kuwashukuru wamisionari kwa ajili ya huduma yao. Wameacha nyumba na familia zao za asili ili kuhubiri injili au kuwasaidia watu maskini barani Afrika. Wamejitolea kwa kujinyima. Na baadhi yao pia wameacha mitindo ya maisha yenye utajiri wa mali katika nchi zao ili kuishi barani Afrika. Unapoona wamisionari wakisaidia bila kuumiza, washukuru kwa huduma yao.

### B. Mashirika ya maendeleo na ya kibinadamu

Mashirika ya maendeleo, mashirika ya kibinadamu, na mashirika ya misaada yanatofautiana sana katika shughuli zao barani Afrika. Mashirika husambaza misaada baada ya majanga, kuchimba visima, kufadhili watoto katika elimu yao, kuwaokoa watu kutokana na usafirishaji haramu wa binadamu, kuandaa vikundi vya akiba, kushauri na kutibu watu wenye VVU, kufundisha njia mpya za kilimo, kufundisha desturi za usafi, n.k. Orodha ya shughuli za mashirika hayo ni ndefu sana. Mashirika mengi yanafanya kazi nzuri ambayo nchi na jamii za Kiafrika zimefaidika nayo. Lakini pia kuna mashirika mengi ambayo yanafanya makosa ambayo tumeyaangazia katika mtaala huu wote.

Kanuni za kutafakari:

1. Yawajibishe mashirika katika kufanya kazi bora kwa uadilifu katika nchi na jamii za Afrika. Unapogundua kuwa kuna wafanyakazi wafisadi, wawe ni wageni au Waafrika, hakikisha unaripoti ufisadi huo kwa ngazi za juu zaidi za shirika, na wakati mwingine inaweza kuwa muhimu kuripoti ufisadi huo kwa viongozi wako wa serikali pia.

2. Jaribu kuwahimiza wafanyakazi wa Kikristo katika mashirika ya maendeleo kupitia mtaala huu, *Kusaidia Bila Kuumiza Barani Afrika*. Hii itasaidia mashirika kufanya kazi bora zaidi katika kupambana na umaskini kwa kuwa na mtazamo mkamilifu zaidi, na kuzingatia asili ya kina ya umaskini na sababu zake, pamoja na makosa ya kawaida yanayofanywa. Hata iwapo wafanyakazi na shirika si Wakristo, bado unaweza kujaribu kuwawajibisha katika kusaidia bila kuumiza, kwa kushiriki nao baadhi ya kanuni ambazo umejifunza katika mtaala huu na kuwaonyesha kile kinachotokea katika jamii yako.

3. Kuhimiza mashirika kufanya kazi na jamii za wenyeji ili watu wa eneo hilo waweze kumiliki maendeleo yao wenyewe. Kuhimiza ushiriki wa wanainchi katika kila ngazi ya kufanya mipango, utekelezaji na tathmini. Kuhimiza mashirika kuwajibika si tu kwa wafadhili bali pia kwa makanisa ya eneo husika, vikundi vya jamii, na kwa ujumla kwa watu wote wa jamii katika eneo ambapo mashirikia hayo yanafanya kazi.

4. Ikiwa shirika linatoa zawadi za bure kwa jamii yako kwa njia ambayo unajua itasababisha utegemezi au aina nyingine za madhara, kuwa tayari kuliambia shirika hilo kwamba hutaki zawadi za bure, na kwamba njia yao haitasaidia jamii. Weka mfano kwa kurudishia shirika hilo zawadi za bure ulizopokea wewe binafsi. Usichukue vitu kwa sababu tu ni vya bure ikiwa unajua kwamba mbinu mbaya inatumiwa.

5. Jaribu kushawishi udhibiti wa serikali yako wa mashirika katika nchi yako. Itasaidia ikiwa serikali zitahitaji mashirika yote kutii viwango fulani vya uadilifu katika kazi zao. Unaweza pia kuhimiza mashirika kuzingatia viwango fulani vya kimataifa katika shughuli na kazi zao. Kwa mfano, kiwango kimoja kinachoweza kutumiwa kinaitwa Kiwango cha Kimsingi cha Kibinadamu. Kiwango cha Kimsingi cha Kibinadamu kinazingatia ahadi tisa za ubora kwa mashirika. Ahadi hizi ni pamoja na kuhakikisha kuwa mashirika yanahusisha jamii katika kufanya maamuzi, kwamba kuna njia za wafanyakazi na wanajamii kutoa malalamiko, na kwamba pesa zinatumiwa kwa kuwajibika kama ilivyokusudiwa.[2] Unapoungana na mashirika tofauti yanayofanya kazi barani Afrika, unaweza pia kushauriana na watathmini wa misaada wanaofuatilia kazi za mashirika ya misaada na mashirika mengine. Nchini Marekani, mifano michache ni Evangelical Council for Financial Accountability (Baraza la Kiinjilisti la Uwajibikaji wa Kifedha na Charity Navigator (Mtathmini wa Mashirika ya Misaada).[3]

6. Unapoona mashirika yakifanya kazi nzuri katika jamii yako katika kuwatunza watu walio maskini wa mali, tafuta njia za kusaidia shirika hilo kifedha, hata kama mchango wako ni mdogo. Usiwe na mtazamo kwamba kazi zote za maendeleo zinazofanywa kupitia kwa mashirika katika jamii yako zinapaswa kufadhiliwa na wafadhili wa kigeni. Hamasisha rasilimali za eneo husika ili kuchangia katika kazi ya mashirika hayo mazuri.

## C. Kampuni na serikali za kigeni

Kuna nchi nyingi za kigeni ambazo zina maafisa wa serikali wanaoishi barani Afrika pamoja na wafanyakazi wa kampuni za kibinafsi. Baadhi ya nchi zilizo na uwepo mkubwa zaidi barani Afrika leo ni pamoja na Uchina, Marekani, na Umoja wa nchi za Ulaya. Lakini kuna nchi nyingine nyingi za kigeni zinazofanya kazi katika nchi za Afrika pia.

Serikali na kampuni za kigeni mara nyingi hujaribu kusaidia nchi za Afrika, lakini wakati huo huo pia zinalenga kunufaisha kampuni na serikali zao wenyewe. Hatupaswi kuwa wajinga na kufikiri kwamba wote wako Afrika ili tu kuwasaidia watu walio maskini wa mali. Wako hapa kujitafutia faida pia. Mahusiano kati ya serikali za kigeni na serikali za Afrika yanaweza kuwa changamano sana. Kwa njia hiyo hiyo, ushirikiano kati ya kampuni za kigeni, serikali za Kiafrika na wafanyakazi wa Kiafrika pia unaweza kuwa changamano sana. Kwa upande mmoja, Afrika imenufaika sana na ushirikiano huu katika suala la maendeleo ya miundombinu, mikopo, misaada wakati wa shida au majanga, na uzalishaji wa ajira.

Hata hivyo, wakati huo huo, baadhi ya kampuni na serikali za kigeni zimesababisha madhara makubwa, mateso, na ukosefu wa utulivu barani Afrika, tangu nyakati za ukoloni hadi leo. Labda jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba Waafrika wengi na watu wengi ulimwenguni kote hawajui unyanyasaji unaoendelea sasa barani Afrika. Kiasi kikubwa cha rasilimali za Afrika kinasafirishwa kwenda nchi zingine na mara nyingi kuna faida ndogo sana kwa watu wa kawaida wa Afrika.

<u>Vipengele vya kutafakari</u>:

1. Tumia ruzuku zinazotolewa na kampuni za kigeni na serikali kwa busara. Kuwa mwangalifu kusoma makubaliano kwa uangalifu na uone ni masharti gani yamejumuishwa humo. Fanya makubaliano na kampuni na serikali za kigeni ambayo hayatakufaidi wewe binafsi tu, bali pia jamii yako na nchi yako pia.

2. Kuwa mwangalifu kuhusu kuchukua mikopo kutoka kwa serikali za kigeni ambayo inaweza kuifanya jamii au nchi yako kuwa mtumwa wa deni lisiloweza kulipwa. Zingatia athari za mikopo kwa vizazi vijavyo au kwa watu watakaochukua wadhifa wako baadaye. Ni rahisi kufikiria kwamba mikopo inasaidia sana na ni mizuri wakati malipo yanaruhusiwa kuhairishwa. Lakini fikiria ni madhara gani unayowasababishia wale watakaokuja baada yako ambao watalazimika kulipa mikopo hiyo.

3. Punguza urasimu, fanya kazi kwa ajili ya utulivu na usalama, jenga miundombinu, na utekeleze utawala wa sheria ili kufanya nchi yako iwe mazingira mazuri kwa kampuni za kigeni ambazo zinataka kuwekeza katika nchi yako.

4. Kumbuka kuwatunza wafanyakazi wa serikali za kigeni na makampuni kama watu. Wote wako tofauti. Wengine ni Wakristo na wengine si Wakristo. Baadhi yao wanajaribu kuleta mabadiliko chanya sana barani Afrika na wengine hawalengi kufanya hivyo. Wajue kama watu binafsi na ujenge urafiki nao. Wasaidie kukaa vizuri katika jamii wanazoishi kwani wakati mwingine mtu anaweza kuwa mpweke anapoishi katika nchi ya kigeni. Waalike kwenye makanisa yenu.

5. Wawajibishe viongozi wa Kiafrika ambao wanafanya makubaliano na serikali na nchi za nje ili kupata faida za kibinafsi au hata rushwa. Mara nyingi, viongozi hawa hunufaika kibinafsi wakati nchi yao inapoporwa na serikali na kampuni za kigeni. Vitendo hivi viovu lazima vikome. Hatupaswi kupuuza kile kinachofanyika. Aidha, tunahitaji kuwa tayari kuripoti maafisa wafisadi wa kigeni na kuwawajibisha. Hakuna mtu anayepaswa kuwa juu ya sheria. Wakati mwingine inaweza kuwa na manufaa kuomba msaada wa wamisionari wa kigeni katika kuwawajibisha viongozi wa kigeni. Wakati wa ukoloni, kulikuwa na wamisionari wengi wa Kikristo wa kigeni ambao walisimama dhidi ya serikali zao kupinga utumwa na kulinda haki za ardhi za Waafrika.

Sio cha kuuzwa

Mifano michache ya kile kinachofanyika leo barani Afrika kinachohusisha serikali na kampuni za kigeni:

- "Nigeria katika Afrika Magharibi imezalisha mafuta yenye thamani ya zaidi ya dola bilioni 400 tangu yalipogunduliwa huko katika miaka ya 1950 – fedha zinazotosha kufuta deni lote la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, zaidi ya asilimia 80 ya mapato ya mafuta yamefikia asilimia 1 tu ya idadi ya watu, wakati idadi kubwa ya watu imezidi kuwa maskini, na imesababisha uasi wa kivita katika eneo la Niger Delta lenye utajiri wa mafuta."[4] Niger Delta "ndilo eneo masikini zaidi nchini na kuna shule 1 tu ya sekondari kwa watu 14,000."[5]

- "Takriban asilimia 70 ya mbao kutoka nchi ya Gabon husafirishwa hadi nchini Uchina kinyume cha sheria, wakati takwimu ya Guinea ya Ikweta inadhaniwa kuwa asilimia 90."[6]

- "Katika miaka ya 2000, tuna, uduvi na kamba wa thamani ya hadi Dola milioni 300 kwa mwaka, walikuwa wakiibwa na mashua kubwa za kigeni za kuvulia samaki katika maji ya Somalia kila mwaka… Uporaji wa maji ya eneo la Somalia na meli za wavuvi wa kigeni ulisababisha mwitikio wa silaha kutoka kwa wavuvi wa eneo hilo. 'Uharamia huu wa matajiri' ndio uliosababisha 'uharamia wa maskini' kama itikio."[7]

### D. Wadhamini, wafadhili, na washirika wanaoishi nje ya Afrika
Fedha zinazotumiwa barani Afrika na mashirika ya kigeni na wamisionari zinatokana na michango inayotolewa na watu wa kawaida katika nchi za kigeni. Watu hutoa pesa ambazo wangeweza kutumia kwa ajili yao wenyewe. Wanachagua kutoa ili waweze kuona injili ikienea barani Afrika, au wanatoa ili kusaidia jumuiya maskini za Kiafrika. Hawa ni wageni ambao hatuwezi kukutana nao ana kwa ana, lakini wana mchango mkubwa katika maisha yetu barani Afrika, kwa njia nzuri lakini wakati mwingine pia kwa njia hasi.

Vipengele vya kutafakari:

1. Acha kutumia neno *wafadhili*, kwa sababu linaimarisha mtazamo wa kujiona kama mungu na hisia za kujiona duni kwa kuainisha kila mtu kama mtoaji au mpokeaji. Ni bora kuwarejelea watu kama *washirika katika huduma* au *washirika wa rasilimali za fedha*.[8]

2. Ikiwezekana, wasiliana na washirika hao wa rasilimali za kifedha na uwashukuru kwa kutoa kwao kwa kujinyima. Unaweza kufanya hivyo kupitia barua pepe au mitandao ya kijamii au simu, lakini hiyo pia inaweza kufanywa kwa kuwasiliana na wamisionari au wafanyakazi wa shirika ambao wako barani Afrika. Kumbuka kwamba kuna umaskini katika kila nchi ya ulimwengu. Kila dola au shilingi inayotolewa kwa Afrika ni pesa ambazo zingeweza kutumiwa kupambana na umaskini katika nchi ya mgeni. Wakati mwingine ni kusikia tu mtu akisema "asante" ndilo jambo litakalowatia watu moyo kuendelea kutoa kwa ukarimu.

3. Wawajibishe washirika wa rasilimali za kifedha. Ni kawaida kwa wale ambao wanatoa pesa kuamuru kile kitakachofanywa kupitia mashirika na wamisionari. Wana mpango na ajenda yao na wakati mwingine mipango na ajenda hizo zinalazimishwa kwa jamii na makanisa ya Kiafrika. Kuwa tayari kuzungumza na washirika hao moja kwa moja, au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia wafanyakazi wa maendeleo na wamisionari. Tetea ushiriki wa jamii katika kila kipengele cha mradi au mpango wowote wa huduma. Wakumbushe washirika wa rasilimali za kifedha kwamba hawajui kikamilifu mambo yalivyo katika maeneo lengwa, na kwa hivyo ni muhimu sana kwa washirika wa kigeni, jamii ya Kiafrika na washirika wa kanisa kusikilizana vizuri na kujifunza kutoka kwa kila mmoja. Wahimize wajifunze kuhusu utamaduni wa Kiafrika na kuzingatia suluhu za Kiafrika kwa matatizo ya Kiafrika.

4. Wasiliana na washirika kwa uwazi na mara kwa mara ili kuepuka kutoelewana. Shiriki na washirika wa kigeni simulizi sahihi na ambazo hazijatiwa chumvi. Sema ukweli kila wakati. Unaweza kujaribiwa kufanya hali ionekane mbaya ili kuwafanya watu waone huruma na watoe zaidi.

Pia unaweza kujaribiwa kutia chumvi kwenye simulizi za za mafanikio ili kuwafanya watu watoe zaidi. Hiyo ni kudanganya.

5. Lazima tuwe watu wanaosema ukweli. Kumbuka kile tulichojifunza katika Somo la 11 kuhusu ufisadi. Tunaposema ukweli, sisi na washirika wa kigeni tunaweza kufanya kazi pamoja ili kushinda changamoto mpya ili huduma na miradi iweze kufanikiwa.
6. Wasilisha matarajio yako wazi kwa washirika wa kigeni, na uwaombe wao pia wawasilishe matarajio yao wazi kwako. Jaribu kukumbuka kwamba kanisa au huduma yako ni mojawapo ya maelfu ya huduma ambazo Mungu anatumia kuendeleza ufalme wake barani Afrika. Huduma nyingine hazishindani nasi. Wao ni sehemu ya familia yetu katika mwili wa Kristo. Ikiwa Mungu amemwita mshirika wa kigeni kuhusika katika shughuli A, na huduma yako inafanya shughuli B, msaidie mshirika huyo wa kigeni apate kuungana na shirika lingine karibu nawe ambalo linajihusisha na shughuli A badala ya kujaribu kufanya huduma yako ionekane kana kwamba inahusu shughuli A.[9]
7. Wahimize washirika wa kigeni kuja kutembelea nchi yako mara kwa mara. Hii itawasaidia kujifunza kuhusu maisha na utamaduni wa Kiafrika na kujifunza zaidi kuhusu huduma zinazoendelea katika jamii zenu. Hii pia ni muhimu ili kujenga uhusiano imara na washirika hao wa kigeni. Washirika wa kigeni wanahitaji kukumbushwa kwamba kupambana na umaskini kunahusu kupatanisha mahusiano, si tu kutoa pesa. Ziara huwaleta washirika wa kigeni uso kwa uso na watu wanaojaribu kuwasaidia. Na ziara hizi pia ni muhimu kwa uwajibikaji. Kuna mashirika fisadi barani Afrika ambayo yanapokea fedha za wafadhili na kudanganya kuhusu mipango yao. Siku zote tunapaswa kuwahimiza washirika wa kigeni kututembelea ili waweze kuona kile kinachofanyika, na kwa upande wao ili waweze kusaidia mashirika ambayo ni maaminifu na yanafanya kazi nzuri.

---

[1] Mary Crickmore, "Shalom: A Manual for Christian Workers", (kuchapishwa binafsi, 2011), 45-46.

[2] Kwa taarifa zaidi kuhusu Kiwango cha Kimsingi cha Kibinadamu (CHS) nenda kwenye https://corehumanitarianstandard.org/the-standard.

[3] Kwa taarifa zaidi kuhusu ECFA nenda kwenye https://www.ecfa.org/. Kwa taarifa zaidi kuhusu Charity Navigator nenda kwenye https://www.charitynavigator.org/.

[4] Carmody Pádraig, *The New Scramble for Africa*, 2nd ed., (Polity; Octoba 24, 2016) Highlight Loc. 3069-72.

[5] Ibid., Highlight Loc. 3077-81.

[6] Ibid., Highlight Loc. 4412-13.

[7] Ibid., Highlight Loc. 4535-39.

[8] Brian Fikkert and Kelly Kapic, A Field Guide to Becoming Whole, (Chicago, Moody Pub., 2019), 86.

[9] Ibid., 87.


Sio cha Kuuzwa

Kusaidia Bila

Kuumiza Barani Afrika

# Mwongozo wa Mshiriki

Sio cha Kuuzwa



# Somo la 20: Miradi ya Mbegu na Rasilimali Zaidi

# Majadiliano ya Ufunguzi

## Mawazo mengi katika masomo haya ishirini yanaweza kurahisishwa kuwa kanuni chache za msingi ambazo zinaweza kutusaidia katika maisha yetu ya kila siku:

1. Mungu ametuita tuwe na huruma kwa watu walio maskini wa mali. Kama vile Mungu anavyotupenda sisi na akawa mkarimu kwetu, tunapaswa pia kuwapenda watu walio maskini wa mali na kutoa kwa ukarimu wakati wetu na rasilimali zetu.

2. Unapotaka kuwasaidia watu walio maskini wa mali, fikiria ikiwa kitendo chako kitakusogeza wewe na watu wengine karibu zaidi na kuwa na uhusiano sahihi na Mungu, nafsi, wengine, na uumbaji.

3. Kwa kadiri iwezekanavyo, fanya kazi *na* watu walio maskini wa mali, si *kwa ajili* yao. Usiwafanyie watu kile wanachoweza kujifanyia.

4. Wahimize watu kutumia mali na ujuzi wao kufanya kazi kwa bidii ili kujikimu wao wenyewe na familia zao na kushiriki na wengine wenye mahitaji.

5. Omba kila wakati na utafute mwongozo wa Mungu unapoenda kujaribu kuwasaidia maskini. Usijaribu kufanya kazi hiyo peke yako. Mtegemee Bwana akuwezeshe kupitia Roho wake Mtakatifu.

Tutafanya makosa fulani.

______________________________________________

Hatutakubaliana wakati mwingine.

______________________________________________

Tunapaswa kuwa wanyenyekevu na si wenye kuhukumu.

______________________________________________

Usiondoke hapa ukihisi umelemazwa na hofu.

______________________________________________

**2 Timotheo 1:7**

______________________________________________

Kuwa na imani katika Mungu wetu aliye hai kwamba anaweza kufanya kazi kupitia wewe leo, wiki hii, na mwaka huu. Unaweza kuona mabadiliko ya kweli katika jamii yako. Tunakubaliana na maneno ya Obiageli Ezekwesili, raia wa Nigeria ambaye ni mwanzilishi mwenza wa shirika la Transparency International,[1] "Hakuna kitu chochote ambacho Mungu ninayemwamini hawezi kufanya!"

***Sasa kwa kuwa tumemaliza mafunzo haya, toa mifano mahususi ya hatua zinazofuata unazoweza kuchukua kama mtu binafsi kufuatilia kile ulichojifunza na kuwasaidia watu walio maskini wa mali.***

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

1. Tafakari juu ya vipawa, ujuzi, maarifa, na rasilimali ulizopewa na Mungu.
2. Fikiria kuandaa ramani ya nyenzo au ramani ya mali na familia yako au jumuiya yako kama tulivyojadili katika Somo la 15.
3. Jaribu kufanya shughuli zozote za kufanya baada ya somo ambazo bado hujakamilisha.

Sio cha kuuzwa

4. Kusudia kutumia muda zaidi kujenga uhusiano thabiti na watu walio maskini wa mali katika familia, kanisa, na jamii yako.
5. Anza kuhubiri na kufundisha katika kanisa lako kile ulichojifunza katika mtaala huu.
6. Toa kwa ukarimu zaidi kuliko ulivyokuwa ukitoa hapo awali, lakini tumia busara na ubunifu katika kutoa kwako kufuatia kile ulichojifunza katika mtaala huu. Hapa kuna maoni kadhaa:
   - Saidia kanisa lako kwa kutoa kwa ukarimu zaidi kifedha au vifaa.
   - Epuka kuwapa watu vitu vya bure mara kwa mara isipokuwa kama ni zawadi ya kibinafsi kwa rafiki yako. Badala yake, toa vitu kwa bei iliyopunguzwa. Kisha watu watahisi kumiliki kile wanachonunua kutoka kwako, na utajua ikiwa kweli wanathamini kile unachowapa. Zaidi ya hayo, utaweza kuokoa pesa na kuwasaidia watu wengi zaidi. Kwa mfano, badala ya kusambaza vichujio vya maji kwa jamii nzima bila malipo, toza watu angalau asilimia 10 ya bei halisi ya vichujio hivyo.
   - Wekeza katika maendeleo ya watu wengine kwa kuwasaidia kulipia elimu.
   - Unapompa mtu au shirika zawadi, fikiria kuifanya iwe zawadi inayolingana na mchango wa watu. Kwa mfano, unaweza kusema kwamba kanisa lako litachangia shilingi moja kwa ajili ya mradi katika jamii nyingine kwa kila shilingi moja inayotolewa na wenyeji wa jamii hiyo.
   - Wasaidie watu kuanzisha biashara mpya kupitia msaada wa kifedha unaotolewa wa mara moja, au kwa kuwapa mkopo.
   - Toa misaada ya kifedha kwa mashirika ya kieneo ambayo yanafanya kazi nzuri ya maendeleo katika jamii yako.

# Miradi ya Mbegu

Miradi ya mbegu ni mipango midogo ambayo makanisa au jamii zinaweza kufanya katika eneo lao ili kupambana na umaskini. Vitendo hivi vinapaswa kuonyesha upendo wa Mungu na kuwasaidia watu walio maskini wa mali.[2] Miradi ya mbegu ni kama mbegu iliyopandwa ardhini. Lengo ni kwamba mbegu ndogo inakua na kuzaa matunda makubwa. Mradi wa mbegu ni mwanzo mdogo wa huduma ya kanisa lako ya kusaidia maskini na kupambana na umaskini katika jamii yako.

Miradi ya mbegu inapaswa kufanywa kwa kutumia rasilimali za kieneo za kifedha na nyenzo. Na siku zote makanisa yanapaswa kujaribu kufanya kazi pamoja na wanajamii wengine katika miradi yao ya mbegu ili kuwe na ushiriki wa jamii.

## Mifano ya Miradi ya Mbegu

*Ni miradi gani mingine inayowezekana ya mbegu ambayo makanisa au jamii za kieneo zinaweza kufanya?*

Sio cha kuuzwa

Zingatia maneno ya Desmond Tutu, Askofu Mkuu wa zamani nchini Afrika Kusini: "Fanya kitendo chako kidogo cha wema mahali ulipo; ni vitendo hivyo vidogo vya wema ndivyo vitakavyobadilisha ulimwengu."[3]

# Upangaji wa Hatua

***Ni nini kinachofanyika kwa nia zetu nyingi nzuri?***

________________________________________________________

Mpango Kazi – Ni hati inayoangazia hatua ambazo lazima zichukuliwe ili kufikia lengo fulani mahususi.

________________________________________________________

Mpango kazi rahisi unaweza kuwa na sehemu mbili: lengo moja na shughuli kadhaa.[4]

1. Lengo ni kile unachotaka kuona kikifanyika, au mabadiliko mazuri unayotaka kuona.
2. Shughuli ni mambo ambayo tunahitaji kufanya ili kuona mabadiliko hayo yakitokea.

Ni muhimu kwamba kila shughuli ijumuishe mtu anayehusika na hatua na muda ambao shughuli lazima ikamilike.

## Mifano ya Malengo

1. Watu watatu wasio na ajira katika kanisa langu watapata kazi ya kila siku ambayo itawawezesha kujikimu wenyewe na familia zao ifikapo tarehe 28 Machi.
2. Miti minne itapandwa kanisani kwangu ifikapo tarehe 5 Juni.
3. Jamii yangu itakuwa na kisima kipya cha kupata maji safi ya kunywa ifikapo tarehe 1 Agosti.

## Mifano ya Shughuli (Mifano hii mitatu ya shughuli inaweza kuendana na lengo #3 hapo juu.)

1. Siku ya Jumapili tarehe 10, nitaandaa mkutano kwa ajili ya viongozi wengine wa kanisa na viongozi wa jamii katika eneo letu ili kujadili kuhusu wazo letu la kutengeneza kisima kipya. Wakikubali, tutachagua wanachama wa kamati ambao wanaweza kuongoza mradi huu.
2. Siku ya Alhamisi, tarehe 14, kamati iliyochaguliwa itazungumza na viongozi wetu wa serikali za mitaa na kuona kama wanaweza kuturuhusu kujenga kisima au kushiriki katika mradi pamoja nasi.
3. Jumapili ijayo, kila kanisa la kieneo linalohusika katika mradi huu wa kisima litakuwa na hafla ya kuchangisha fedha katika makanisa yao. Mchungaji wa kila kanisa anawajibika kuona kwamba hili linafanyika.

________________________________________________________

________________________________________________________

***Je, kuna mtu yeyote ambaye amewahi kuandaa mpango kazi kwa ajili yake mweyewe au pamoja na familia yake? Ikiwa ndio, tafadhali shiriki kuhusu tukio lako na faida za mpango wako.***

________________________________________________________

________________________________________________________

Si kwa kuuzwa

# Zoezi – Andaa Mpango Kazi

Kama mtu binafsi, kanisa lako, au jamii:

**Mpango Kazi Wangu:**

**Lengo:**

______________________________

______________________________

**Shughuli ya 1**

______________________________

______________________________

**Shughuli ya 2**

______________________________

______________________________

**Shughuli ya 3**

______________________________

______________________________

**Shughuli ya 4**

______________________________

______________________________

**Shughuli ya 5**

______________________________

______________________________

Sio cha kuuzwa

# Rasilimali, Mafunzo, na Vitabu

*Ni nyenzo gani nyingine, mafunzo, na vitabu unavyoweza kupendekeza kwa kikundi kama hatua muhimu zinazofuata baada ya kukamilisha mafunzo haya? Ni zana au mipango gani inaweza kusaidia makanisa na jamii za eneo husika wanapojaribu kupambana na umaskini na kuona maendeleo?*

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

## Mafunzo katika Huduma za Mikopo Midogo

Mikopo midogo huwezesha kaya zenye kipato cha chini kupata huduma za kifedha kama vile akiba, mikopo, na bima. Kaya masikini hutumia huduma hizi kukidhi mahitaji mbalimbali ya kiuchumi, na ikiunganishwa na shughuli za uinjilisti na uanafunzi, utoaji wa mikopo midogo unaweza kuwa zana yenye nguvu ya huduma kamili, ikishughulikia mahitaji ya watu ya kiuchumi, kijamii, na kiroho.

Jambo la kusikitisha ni kwamba mipango ya mikopo midogo iliyoandaliwa vibaya inaweza kuleta madhara makubwa:

______________________________

Hasa, ni hatari sana kwa makanisa na huduma ndogo kuendesha mipango ya kutoa mikopo midogo, **kwani tamaduni zao hazitoi mazingira ya kuhakikisha ulipaji wa mkopo.** Njia mbadala ambayo imefanikiwa sana ni kwa makanisa na huduma ndogo kukuza vyama vya akiba na mikopo ambapo watu maskini wanaweka akiba na kukopeshana pesa zao wenyewe.

**Rasilimali kwa ajili ya Huduma za Mikopo Midogo**

- Kabla ya kujaribu kuzindua huduma ya mikopo midogo, soma kitabu kifuatacho kilichoandikwa na Kituo cha Chalmers: Brian Fikkert and Russel Mask, ***From Dependence to Dignity: How to Alleviate Poverty Through Church-Centered Microfinance*** (Grand Rapids, Michigan: Zondervan, 2015).
- Kwa msaada katika kukuza vyama vya akiba na mikopo vinavyohusishwa na kanisa, mtaala wa Kituo cha Chalmers wa ***Restore: Savings*** unaweza kupakuliwa kutoka kwenye tovuti ya Kituo cha Chalmers kwenye https://chalmers.org/restore-savings/
- Mtaala wa ***Business, Home, and Health*** wa Kituo cha Chalmers unaweza kutumiwa kutoa mafunzo ya ziada katika muktadha wa huduma za mikopo midogo. Pakua kutoka kwenye tovuti ya Kituo cha Chalmers kwenye https://chalmers.org/bhh/

## Mafunzo ya Kuhamasisha Makanisa na Jamii

- **Rejesha: Ubunifu –** Mchakato wa kufundisha makanisa kuwa mabalozi wa upatanisho. Washiriki wa kanisa wanaongozwa katika mchakato unaoweza kurudiwa wa kubuni na kutekeleza mipango ya kushiriki upendo wa Kristo katika jamii zao. Inapatikana kwenye www.chalmers.org.
- **Mafunzo ya Uongozi ya Timotheo –** Mafunzo ya kiutendaji ya huduma yaliyobuniwa na *Raise Up Global Ministries* ili kuwaandaa viongozi wa kanisa kuandaa mipango kazi kwa ajili ya mabadiliko ya kanisa na jamii. https://www.resonateglobalmission.org/timothy-leadership-training
- **Mabadiliko Yanayozingatia Ukweli –** Programu ya Ulimwengu Uliopatanishwa iliyoundwa kuandaa makanisa ya vijijini kutumia ukweli wa Mungu katika maisha yao, kufikia na kutumikia jamii zao na kujifunza stadi za msingi za maisha. https://tctprogram.org/

- **Mchakato wa Uhamasishaji wa Kanisa na Jamii –** Mwongozo kamili ulioandaliwa na *Tearfund* ambao unaandaa makanisa kuhamasisha jamii zao kutekeleza maendeleo ya jamii yanayotegemea mali. https://learn.tearfund.org/en/resources/series/church-and-community-mobilisation-process-ccmp/ccmp-facilitators-manual
- **Mwongozo wa Shalom: Mwongozo kwa Wafanyakazi wa Kikristo –** Warsha ya wiki moja kwa kutumia kanuni shirikishi za elimu ya watu wazima ili kuwafundisha viongozi wa Kikristo jinsi ya kushiriki katika mabadiliko ya jamii zao. Wasiliana na Mary Crickmore kupitia barua pepe info@worldrenew.net.
- **Uinjilisti wa Afya ya Jamii –** Mpango wa *Medical Ambassadors International* (*Mabalozi wa Matibabu wa Kimataifa)* ambao unajumuisha uanafunzi na uanzishaji wa makanisa kwa urahisi na uzuiaji wa magonjwa na maendeleo ya jamii. Tovuti https://www.chenetwork.org/.
- **Mikutano ya Maono –** Hafla hizi, zinazoandaliwa na *Disciple Nations Alliance* (Muungano wa Kufanya Mataifa Kuwa Wanafunzi), hutoa fursa ya kuunganisha mwili wa Kristo kwa msingi wa maono ya kibiblia ya mabadiliko ya kijamii yanayotegemea kanisa na kupokea mafunzo ya kiutendaji na zana za matumizi ya haraka. https://disciplenations.org/

## Mafunzo katika Biashara

- **Biashara ya Kiufalme: Elimu ya Biashara ya Kikristo** – Nyenzo inayozalishwa *na Kushangazwa na Matumaini* ambayo inashughulikia misingi ya kuanzisha biashara. https://programs.surprisedbyhope.org/
- **Biashara, Nyumbani, na Afya –** Mfululizo wa kozi za *Kituo cha Chalmers* ili kuandaa biashara ndogo ndogo na kaya za kipato cha chini ambazo zimejumuishwa. https://chalmers.org/bhh/

## Vitabu vya Kujisomea Binafsi

- *When Helping Hurts* by Steve Corbett and Brian Fikkert (Moody, 2012)
- *The Challenge for Africa* by Wangari Maathai (Pantheon Books, 2009)
- *Prosperity? Seeking the True Gospel* by Michael Otieno Maura, Conrad Mbewe, and Ken Mbugua (Africa Christian Textbooks – Registered Trustees, 2015)
- *Walking with the Poor* by Bryant Myers (Orbis Books, 1999)
- *Dead Aid* by Dambisa Moyo and Niall Ferguson (Farrar, Straus, and Giroux, 2009)
- *African Friends and Money Matters* by David E. Maranz (SIL International)
- *The New Scramble for Africa* by Pádraig Carmody (Polity, 2016)
- *Against all Hope: Hope for Africa* by Darrow L. Miller with Scott Allen (Disciple Nations Alliance, 2005)

Sio kwa kuuzwa

# Shughuli za Kufanya Baada ya Somo

Shughuli za kufanya baada ya somo zinajumuisha kazi au shughuli za kufanya katika jamii zenu, kanisa au mahali pa kazi, kwa kutumia masomo uliyojifunza.

1. Endelea kukamilisha mpango kazi wako huku ukijadiliana na familia, kanisa, na jamii yako. Mara baada ya mpango kazi huo kukamilika, tia bidii katika kutekeleza shughuli ulizopanga. Hakikisha unaombea mpango wako mara kwa mara.
2. Amua na viongozi wa kanisa na viongozi wa jamii kuhusu mitaala au mipango mingine inayoweza kusaidia kanisa au jamii yako (kama zile zilizojadiliwa katika somo hili), na ufanye mpango wa jinsi utakavyopata rasilimali hizo.

# Maoni, Shuhuda, Tathmini, na Maombi

## Shuhuda

___

___

## Maswali ya Tathmini

**1)** *Je, kuna kitu chochote ambacho tumejadili ambacho kimekukanganya? Je, kuna chochote ninachoweza kukusaidia kuelewa vizuri?*

___

___

**2)** *Ni masomo au shughuli gani ulizothamini zaidi?*

___

**3)** *Utafanya mabadiliko gani katika huduma yako kulingana na kile ulichojifunza?*

___

**4)** *Ni nini kinachoweza kuboreshwa katika mafunzo haya au katika uwezeshaji wangu?*

___

**5)** *Je, ungependekeza mafunzo haya kwa rafiki? Kwa nini au kwa nini sivyo?*

___

Sio cha kuuzwa

***Tafadhali kuwa huru pia kutuma barua pepe moja kwa moja kwa waandishi ikiwa una maswali na ushuhuda:**
Jonny: jonny.kabiswa@chalmers.org Anthony: anthony.sytsma@chalmers.org

---

[1] Nukuu imechukuliwa kutoka kwa hotuba iliyotolewa na Obiageli Ezekwesili katika Time 100 Gala, Aprilii 21, 2015. Hotuba inaweza kusikizwa hapa: https://praisephilly.com/2669383/bring-back-our-girls-founder-obiageli-ezekwesili-gives-emotional-speech-at-time-100-gala/.

[2] Imebadilishwa kutoka *If Jesus Were Meior* na Bob Moffitt (2006, Monarch Books), sura ya 13: "Kupanga Mradi wa Mbegu", ukurasa wa 1, Mabadilisho yalifanywa na la Disciple Nation na inaweza kupatikana hapa: https://disciplenations.org/resources/seed-projects-overview-and-planning-guide/.

[3] Desmond Tutu, Nukuu iliyochapishwa tena na Desmond Tutu Peace Foundation, (Oktoba 7, 2015). Inaweza kufikiwa mtandaoni kwenye: https://thewisdomdaily.com/10-pieces-wisdom-desmond-tutu/#:~:text=%E2%80%9CDo%20your%20little%20bit%20of,into%20the%20world%20fully%20formed.

[4] Timothy Leadership Training, *Caring for God's People* 6e, (Timothy Leadership Training Institute, 2016), 13.

# *LA HIARI* Ushuhuda na Tathmini iliyoandikwa

(Mpe kiongozi wako ukurasa huu baada ya mafunzo
au mtumie kupitia barua pepe HWHAfrica@chalmers.org)

Ushuhuda

Tathmini

1) *Ni masomo au shughuli gani ulizothamini zaidi katika masomo haya?*

2) *Utafanya mabadiliko gani katika huduma yako kulingana na kile ulichojifunza?*

3) *Ni nini kinachoweza kuboreshwa katika mafunzo haya au katika uwezeshaji wangu?*

4) *Je, ungependekeza mafunzo haya kwa rafiki? Kwa nini au kwa nini sivyo?*

Maoni ya ziada

Sio cha kuuzwa